# UTAMADUNI, ITIKADI NA UTAMBULISHO KATIKA RIWAYA YA *CAITAANI MUTHARABA-INI* NA TAFSIRI ZAKE *SHETANI MSALABANI* NA *DEVIL ON THE CROSS*

**NA**

**MAGUGU VINCENT NJERU**

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI (TAFSIRI)

**KITIVO CHA FANI NA SAYANSI JAMII**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2022**

# IKIRARI

**MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya utahini katika chuo kikuu kingine chochote. Haki zote zimehifadhiwa na hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi na Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi............................................................................ Tarehe: ...............................

**Magugu Vincent Njeru**

**SASS/DPHIL/KIS/01/14**

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama washauri walioteuliwa na Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi............................................................................ Tarehe: ...............................

**Profesa. Robert Wilton Oduori**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi............................................................................ Tarehe: ...............................

**Profesa. Mosol Mark Kandagor**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

## TABARUKU

Kwa Baba na Mama,

Kwa Mke na Wana,

Kwa Ndugu na Jamaa,

Na

Kwa Wasomi wa Tafsiri.

# SHUKURANI

Natanguliza shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwa neema zake na kwa kunijaalia afya, na kunitunukia akili razini kuniwezesha kuendesha na kukamilisha utafiti huu. Pili, natoa shukurani za dhati kwa wasimamizi wangu, Prof. Robert Wilton Oduori na Prof. Mosol Mark Kandagor, kwa ushauri, nasaha na kunihimiza katika mchakato mzima wa kuendesha utafiti huu na kuandaa tasnifu hii. Namshukuru Mwalimu Collins Kenga Mumbo kwa kunipa wosia pale nilipohitaji msaada wake.

Kwa walimu wangu wote katika masomo haya ya uzamifu, kwa pamoja mlichangia ufahamu wangu na kunipa msingi kama msomi; nasema asante. Aidha, natoa shukurani kwa wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika – Chuo Kikuu cha Moi, kwa kunihimiza katika utafiti wangu na kwa kushirikiana nami katika majukumu mengine idarani ambayo yangetinga kukamilika kwa kazi hii.

Kwa mke wangu mpendwa, siku nyingi nilijifungia kubukua vitabu, ulinielewa na kunipa nafasi ya kukamilisha masomo haya. Nasema asante. Kwa mama yangu, hatimaye tumefika kileleni. Asante kwa kunitia hamasa kila mara kukamilisha kazi hii. Kwa ndugu zangu, nawashukuru kwa msaada wenu wakati wote huu.

Mwisho, natoa shukurani kwa wanafunzi wenzangu tuliojiunga nao masomo haya ya uzamifu. Tulishauriana na kuhimizana. Safari ilichukua mikondo tofauti lakini sifa kwa Maulana hatimaye imekamilika.

# IKISIRI

Katika kusoma riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* iliyoandikwa na Ngũgĩ wa Thiong'o na tafsiri yake kwa Kiswahili, *Shetani Msalabani* na kwa Kiingereza, *Devil on the Cross,* inabainika kwamba kuna tofauti zinazojitokeza katika jinsi ujumbe umesimbwa na kuwasilishwa. Kando na kwamba tafsiri iliyotekelezwa imekiuka ubia wa kimapokeo katika utekelezaji na uhawilishaji wa maana, matini za Kiswahili na za Kiingereza zilizoangaziwa ni mazao ya tafsiri binafsi. Kwa jinsi hii, utafiti huu kwanza ulichanganua udhihirikaji wa utamaduni, itikadi na utambulisho katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*. Utafiti aidha uliangazia jinsi dhana hizi zilishughulikiwa katika tafsiri za *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross.* Uchanganuzi uliangazia lugha hasa uteuzi wa kiisimu, vipengele vya fasihi simulizi na matumizi ya dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi. Utafiti huu vilevile ulichunguza namna itikadi ilidhihirika kupitia kwa lugha katika riwaya hii na jinsi dhana hii ilihawilishwa katika tafsiri za Kiswahili na Kiingereza. Dhana ya utambulisho ilishughulikiwa kwa kuchunguza jinsi ilivyobainishwa katika *Caitaani Mutharaba-ini* na ilivyotafsiriwa kwa Kiswahili na Kiingereza. Utafiti uliongozwa na nadharia mbili: nadharia ya Baadaukoloni katika tafsiri na nadharia ya Uchanganuzi wa Diskosi. Data ya utafiti ilikusanywa kwa kutumia usampulishaji wa kimakusudi ambapo usomaji hakikifu ulitekelezwa kwa matini husika kuambatana na azma na upeo wa utafiti huu. Data ilipangwa kwa utaratibu wa vigeu vilivyokuwa vikijadiliwa na uchanganuzi ukafanywa kwa njia ya maelezo. Uchanganuzi ulidhihirisha matumizi ya vipera vya fasihi simulizi pamoja na dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi katika kuumba matini chanzi. Hali hii ilihusishwa na uteuzi wa kimakusudi ambao unabainika katika fasihi ya baadaukoloni. Katika kuchunguza tafsiri, ilibainika kuwa mtafsiri alichanganya baina ya mbinu ya uibuaji ugeni na ile ya ubinafsishaji katika kuhawilisha dhana hizi za kitamaduni. Aidha, uteuzi wa kiisimu aliofanya mtafsiri katika tafsiri ya Kiswahili na ile ya Kiingereza pakubwa ulibainishwa kuwa ulikuwa wa kimakusudi na uliongozwa na msukumo wa kiitikadi. Utambulisho ulibainishwa kuwa dhana ya kimsingi katika fasihi ya baadaukoloni na tafsiri yake ambapo mtafsiri anatumia lugha kwa njia ya kimakusudi kuumba utambulisho maalum na kuuhawilisha kadri ya dhima ya tafsiri yake. Kutokana na utafiti huu, ilidhihirishwa kwamba, tafsiri aghalabu ni mchakato changamano wa mawasiliano. Vilevile, tafsiri ni jukwaa ambapo mahusiano ya kiuwezo baina ya lugha na tamaduni tofauti hudhihirika. Hitimisho la utafiti ni kwamba lugha katika tafsiri za baadaukoloni hutumiwa makusudi kwa lengo la kukinza ubabe wa lugha na tamaduni za kibepari huku ikikweza tamaduni na lugha za waliowahi kutawaliwa. Utafiti huu umependekeza haja ya kitaaluma ya kutambua nafasi ya mtafsiri na athari yake katika mchakato wa tafsiri. Aidha, pana haja ya kutalii dhana ya itikadi kama kipengele cha kimsingi katika utekelezaji na katika taaluma ya tafsiri. Isitoshe, utafiti unapendekeza kwamba ni muhimu kuimarisha mwelekeo wa nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri kwa kujumuisha ndani mwake vipengele vya uchanganuzi wa diskosi ili kuwezesha uchanganuzi wa kina. Mwisho, pana haja ya kuzidi kupanua upeo wa utafiti katika taaluma ya tafsiri kwa Kiswahili kwa kuchunguza vipengele zaidi vya ulinganifu katika tafsiri na ubora wa tafsiri.

# ABSTRACT

A reading of the novel *Caitaani Mutharaba-ini* by Ngũgĩ wa Thiong'o and its translations in Kiswahili, *Shetani Msalabani* and in English, *Devil on the Cross*, manifests a difference in the manner in which the message is encoded and presented. Other than the fact that there is evident negation of the universal classical approach in execution and in transference of meaning, the Kiswahili and English versions are Self-translated. It is on this premise that this research analyzed the manifestation of culture, ideology and identity in the novel *Caitaani Mutharaba-ini*. This research also analyzed how these concepts have been handled in the translations *Shetani Msalabani* and *Devil on the Cross.* The analysis was based on linguistic choices, aspects of oral literature and the use of culturally specific concepts attributed the source culture. In addition, the research analyzed how ideology is manifest through language in this novel as well as how this concept is transferred in the Kiswahili and English translations. Identity as a concept was handled by analyzing how it is created in *Caitaani Mutharaba-ini* and how it is rendered in the Kiswahili and English translation. The study employed two theories: post-colonial theory in translation and discourse analysis theory. Data for this research was purposively sampled where critical reading of the select texts was undertaken guided by the purpose and scope of the study. The data was presented in accordance with the variables being discussed and the analysis was conducted in a descriptive approach. The analysis showed the utilization of aspects of oral literature as well as culturally specifics concepts tied to the source culture. This was attributed to the intentional choices which are manifest in post-colonial literature. In analyzing the translation, it came out that the translator employed both the domestication and foreignization strategies in handling these cultural concepts. In addition, it became evident that the linguistic choice made by the translator in Kiswahili and in English was largely deliberate and was hinged on an ideological agenda. It was established that identity was a fundamental aspect in post-colonial literature and its translation whereby the translator employs language in a deliberate manner to create a particular identity and render it in accordance with the purpose of the translation being carried out. From this research, it was evident that translation is often a complex process of communication. In addition, translation is a platform where power relations between different languages and cultures is manifest. This study concluded that language in post-colonial translations in used deliberately with an aim of resisting the hitherto dominance of the imperialist language and culture while uplifting the culture and language of the communities that were colonized. This advocates for the need to recognize the place of the translator and his influence in the process of translation. There is need to explore the concept of ideology as a fundamental concept in any translation endeavor and within the discipline of translation studies. Further, the research proposes that there is need to rework the post-colonial approach to translation theory by incorporating aspects of discourse analysis to enable a more detailed analysis. In conclusion, the study recognizes the need to broaden the scope of research in the discipline of translation studies in Kiswahili by analyzing aspects beyond equivalence and the quality of translations.

# YALIYOMO


IKIRARI ....................................................................................................ii

TABARUKU .................................................................................................. iii

SHUKURANI ..............................................................................................iv

IKISIRI ......................................................................................................v

ABSTRACT..................................................................................................vi

YALIYOMO..................................................................................................vii

ORODHA YA MICHORO.................................................................................xi

ORODHA YA PICHA......................................................................................xii

MAELEZO YA AKRONIMU............................................................................. xiii

MAELEZO YA ISTILAHI.................................................................................xiv

**SURA YA KWANZA ........................................................................................1**

**MISINGI YA UTAFITI ......................................................................................1**

1.0 Utangulizi....................................................................................................1

1.1 Usuli wa Utafiti............................................................................................1

1.1.1 Taaluma ya tafsiri.......................................................................................1

1.1.2 Mwingiliano taaluma katika tafsiri ...............................................................5

1.1.3 Utafiti katika Taaluma ya Tafsiri kwa na katika Kiswahili ..............................9

1.1.4 Lugha na Tafsiri .........................................................................................12

1.1.5 Ngũgĩ wa Thiong’o na Fasihi.......................................................................14

1.1.6 Matini zilizoangaziwa ..................................................................................18

1.1.6.1 Riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* (MC)................................................18

1.1.6.2 Riwaya za *Shetani Msalabani* (MT1) na *Devil on the Cross* (MT2) .......20

1.2 Suala la Utafiti ............................................................................................21

1.3 Malengo ya Utafiti ........................................................................................22

1.4 Maswali ya Utafiti..........................................................................................22

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti...............................................................................23

1.6 Azma ya Utafiti..............................................................................................24

1.7 Mbinu za Utafiti ........ 26
1.7.1 Muundo wa Utafiti ........ 26
1.7.2 Uteuzi wa Sampuli ........ 26
1.7.3 Ukusanyaji wa Data ........ 27
1.7.4 Uchanganuzi wa Data ........ 29
1.7.5 Uwasilishaji wa Matokeo ya Uchanganuzi ........ 31
1.8 Hitimisho ........ 31
**SURA YA PILI ........ 32**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA ........ 32**
2.0 Utangulizi ........ 32
2.1 Uandishi wa Baadaukoloni ........ 32
2.2 Tafsiri Binafsi katika Muktadha wa Baadaukoloni ........ 37
2.3 Utamaduni na Tafsiri ........ 39
2.3.1 Utamaduni na tafsiri za fasihi ya Afrika ........ 41
2.4 Dhana ya Itikadi ........ 44
2.4.1 Itikadi katika tafsiri ........ 48
2.5 Dhana ya Utambulisho ........ 57
2.5.1 Utambulisho katika Tafsiri ........ 60
2.6 Misingi ya Kinadharia ........ 62
2.6.1 Nadharia ya Baadaukoloni ........ 62
2.6.1.1 Baadaukoloni ........ 63
2.6.1.2 Baadaukoloni katika Tafsiri ........ 64
2.6.2 Uchanganuzi wa Diskosi ........ 68
2.7 Hitimisho ........ 74
**SURA YA TATU ........ 75**
**UTAMADUNI KATIKA RIWAYA YA *CAITAANI MUTHARABA-INI* NA TAFSIRI ZAKE ........ 75**
3.0 Utangulizi ........ 75
3.1 Utamaduni katika Tafsiri ........ 75

3.2 Udhihirikaji wa Tamaduni mbalimbali Kupitia kwa Lugha Husika ...................... 77
3.2.1 Tafsiri za Mitindo ya Ufunguzi na Utekelezaji ............................................. 77
3.2.2 Tafsiri za Methali ......................................................................................... 89
3.2.3 Tafsiri za Maneno Yanayofungamana na Utamaduni .................................... 99
3.2.4 Tafsiri ya Misemo ....................................................................................... 117
3.2.5 Tafsiri ya Nyimbo ....................................................................................... 126
3.2.6 Tafsiri ya Misimu ........................................................................................ 131
3.2.7 Tafsiri ya Majazi ......................................................................................... 138
3.3 Mwingiliano baina ya tamaduni: Ithibati za Kiisimu katika MC ........................ 150
3.4 Athari za Utamaduni katika Ubora wa Tafsiri; MT1 na MT2 ............................. 157
3.5 Hitimisho ............................................................................................................ 159
**SURA YA NNE ...................................................................................................... 161**
**ITIKADI NA UTAMBULISHO KATIKA *CAITAANI MUTHARABA-INI* NA TAFSIRI ZAKE ..................................................................................................... 161**
4.0 Utangulizi ........................................................................................................... 161
4.1 Dhima ya Utamaduni na Lugha katika Kubainisha Itikadi na Utambulisho ....... 161
4.2 Itikadi katika Caitaani Mutharaba-ini ................................................................. 163
4.2.1 Lugha katika MC na Udhihirikaji wa Itikadi ............................................... 164
4.3 Itikadi katika Uteuzi wa Lugha katika MC na Tafsiri za MT1 na MT2 .............. 185
4.4 Utambulisho katika *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake MT1 na MT2 ........ 196
4.5 Hitimisho ............................................................................................................ 211
**SURA YA TANO ................................................................................................... 212**
**MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........... 212**
5.0 Utangulizi ........................................................................................................... 212
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ......................................................................................... 212
5.2 Matokeo ya Utafiti .............................................................................................. 214
5.2.1 Utamaduni katika MC, MT1 na MT2 .......................................................... 214
5.2.2 Itikadi katika MC, MT1 na MT2 ................................................................. 219
5.2.3 Utambulisho katika MC, MT1 na MT2 ....................................................... 224

5.3 Mahitimisho ya Utafiti....................228
5.4 Mchango wa Utafiti....................233
5.5 Mapendekezo ya Utafiti....................234
MAREJELEO....................236

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1 – Mwingiliano Taaluma katika Tafsiri ............................................................ 6

Mchoro 2 – Kielelezo cha Mawasiliano Sahili ........................................................... 157

Mchoro 3 – Kielelezo cha Mawasiliano katika Tafsiri ................................................ 158

# ORODHA YA PICHA

Picha 1 – Gicaandi ........................................................................................................ 103

Picha 2 – Michoro kwenye Gicaandi ............................................................................ 104

## MAELEZO YA AKRONIMU

| | | |
|---|---|---|
| **LC** | - | Lugha Chanzi |
| **LP** | - | Lugha Pokezi |
| **MC** | - | Matini Chanzi |
| **MT** | - | Matini Tafsiri |
| **MT1** | - | Matini Tafsiri ya Kiswahili |
| **MT2** | - | Matini Tafsiri ya Kiingereza |
| **Ty** | - | Tafsiri Yangu |

## MAELEZO YA ISTILAHI

Itikadi - Ni imani, msimamo, mtazamo wa mtu binafsi au wa jamii fulani kwa ujumla kuhusu jambo, mtu, kikundi cha watu au hali fulani ambao aghalabu unadhihirika kupitia kwa matumizi ya lugha.

Utamaduni - Mila, desturi na mipangilio ya kijamii pamoja na vipengele vya matumizi ya lugha kama vile fasihi simulizi ambayo hufungamana na maisha ya jamii husika.

Ubinafsishaji – Ni hali ambapo mtafsiri anatumia lugha na uteuzi wa kiisimu kumleta mwandishi wa matini chanzi (MC) karibu na msomaji wa matini tafsiri (MT) kwa jinsi ambavyo msomaji anahisi kana kwamba matini anayosoma iliandaliwa mahususi kwa usomaji wake. MT inasomeka kama matini asilia katika lugha na utamaduni wa wapokeaji.

Ugeni - Ni hali ambapo mtafsiri anatumia usanii kiisimu kumleta msomaji wa MT karibu na lugha na utamaduni wa mwandishi wa MC kwa jinsi inayomfahamisha msomaji wa MT moja kwa moja kuwa matini anayoisoma ni tafsiri. Mkakati huu aghalabu unajumuisha uhawilishaji wa dhana za kigeni jinsi zilizvyo pamoja na ubunaji wa dhana mseto kueleza dhana zilizotumika katika MC.

Tafsiri Binafsi – Ni hali ambapo mwandishi wa MC pia ndiye mtafsiri.

Tafsiri ya Utatulugha - Ni matini iliyotafsiriwa kwa lugha mbili tofauti.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeeleza misingi iliyozingatiwa katika utekelezaji wa utafiti huu. Katika kufanya hivi, sura hii imetoa maelezo ya kiusuli ili kuwekea msingi suala la utafiti lililoshughulikiwa katika utafiti huu. Malengo ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na upeo na azma ya utafiti ni miongoni mwa vipengele vilivyoangaziwa katika sura hii. Sura hii imekamilika kwa kueleza misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti pamoja na mbinu za utafiti zilizotumika katika kutekeleza utafiti huu.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

### 1.1.1 Taaluma ya tafsiri

Taaluma ya tafsiri, kama ilivyo kwa fani nyingine za usomi, imekua na kubadilika kadri ya mpito wa maisha. Taaluma hii kama uwanja maalum wa usomi iliimarika pakubwa hasa katika karne ya ishirini kinadharia na kiutafiti. Miongoni mwa michango muhimu iliyotokea katika karne hii ya ishirini ni pamoja na mchango wa Holmes (1972) ambaye katika ramani yake ya tafsiri, zaidi ya kuipa taaluma ya tafsiri kitambulisho rasmi, alibainisha upeo wa taaluma hii na kuweka bayana maeneo anuwai ya kushughulikiwa katika usomi na utafiti wa tafsiri. Mojawapo ya maeneo aliyobainisha kama tawi la taaluma ya tafsiri ni uhakiki wa tafsiri mbalimbali.

Mawazo haya ya Holmes yamekuwa msingi kwa wataalamu wa tafsiri wa baadaye ambao wamezidi kupanua upeo wa ramani aliyoipendekeza ili kuweza kuakisi uhalisia wa sasa wa utafiti na usomi katika tafsiri. Toury (1985), kwa mfano, anasifu ramani ya Holmes na kueleza kwamba ilikusudia kuweka msingi wa taaluma kamili ya kisayansi. Msingi huu unadhihirika tunapoangazia kwa mfano Williams na Chesterman (2002) ambao katika kitabu chao *The Map: A beginner's guide to doing research in translation studies,* wanatumia istilahi za kimsingi pamoja na baadhi ya mihimili aliyobainisha Holmes kama vile anwani ya taaluma ya tafsiri pamoja na tanzu za taaluma hii. Upeo wa maeneo ya utafiti ambao wameangazia katika kitabu hiki, japo umetoa taarifa za utondoti, pakubwa umejikita kwa upeo mpana uliobainishwa katika ramani ya Holmes.

Tunapotalii taaluma ya tafsiri kimapokeo, inabainika kwamba uhakiki wa tafsiri ulijikita katika uchanganuzi linganifu wa vipengele vya kiisimu, hasa vya kisemantiki, baina ya Matini Chanzi (MC) na Matini Tafsiri (MT). Hali hii inadhihirika tunapochunguza mielekeo ya kinadharia kama vile nadharia ya ulinganifu wa kiisimu ya Catford (1965), ambapo anahimiza haja ya nadharia yoyote ya tafsiri kujikita katika vipengele vya usayansi wa lugha. Hata hivyo, katika awamu hii pia, paliibuka wataalamu kama vile Nida (1964) ambaye licha ya kutambua umuhimu wa isimu katika tafsiri, alibainisha kwamba pana haja ya kuzingatia ulinganifu katika ngazi ya kimawasiliano. Utambuzi huu ulikuwa hatua muhimu ambayo iliweka msingi wa kupanua mielekeo ya kuhakiki tafsiri kinyume na

kuzingatia vipengele vya kiisimu pekee. Hii ndiyo maana utafiti wa maendeleo katika taaluma ya tafsiri hasa kuanzia mwishoni mwa miaka ya sitini na mwanzoni mwa miaka ya sabini, unadhihrisha kuwa msisitizo katika uhakiki wa tafsiri unaelekezwa kwa vipengele visivyo vya kiisimu. Kwa mfano, kufikia mwishoni mwa karne ya ishirini, paliibuka wataalamu walioandama mtazamo wa kiuamilifu hasa wasomi wa Kijerumani kama vile Reiss na Vermeer (1984) na Nord (1997), kupitia kwa mapendekezo ya kinadharia almaarufu *Skopostheorie*. Wataalamu wanaoandama mielekeo ya kiuamilifu na kiuchanganuzi makinifu katika tafsiri wanahoji kuwa, kwa sasa hatuwezi kutafitia tafsiri pasi na kujumuisha vipengele vya kijamii, kitamaduni pamoja na muktadha kwa ujumla unaozalisha MC na MT.

Kupanuliwa kwa vipengele vya kuhakikiwa pamoja na mielekeo ya kinadharia katika uchanganuzi wa tafsiri kumeipanua taaluma ya tafsiri pakubwa. Licha ya hivyo, kupanuka huku kumeangaziwa zaidi katika mataifa ya kaskazini mwa ulimwengu na wasomi kama vile Venuti (1995), Tymoczko na Gentzler (2002), Cronin (2003, 2006) na Snell-Hornby (2006) miongoni mwa wengine kuliko ilivyo kwa mataifa ya kusini mwa ulimwengu. Barani Afrika hata hivyo, kumekuwa na juhudi za kutafitia vipengele mbalimbali kama inavyodhihirika kutokana na kazi za wasomi kama vile Marais (2014, 2018) ambaye amezamia mwelekeo wa kisemiotiki katika tafsiri pamoja na Bandia (2008, 2010, 2014) ambaye amezamia suala la baadaukoloni katika tafsiri na fasihi ya Afrika miongoni mwa wengine. Nchini Kenya, tafiti zimeanza kuendeshwa na wasomi tofauti kuambatana na upeo mpya

katika taaluma ya tafsiri na wasomi tofauti. Mfano bora kwa mwelekeo huu nchini Kenya ni utafiti wa uzamifu wa Zaja (2011) ambaye aliangazia tafsiri ya fasihi ya Kiswahili kwa kujikita kwa uamilifu wa vipengele vya muktadha na utamaduni.

Katika usanjari huu wa kuendeleza taaluma ya tafsiri kiupeo na kupanua kongoo ya tafiti zilizoendeshwa hasa katika mazingira ya Bara la Afrika, utafiti huu ulichanganua matini zilizoteuliwa ili kuibuka na data kamilifu ya kisayansi inayotalii dhana za utamaduni, utambulisho na ile ya itikadi katika matini tafsiri za kifasihi. Dhana hizi ni za kimsingi kwa mielekeo ya uamilifu na uchanganuzi makinifu katika taaluma ya tafsiri na zina umuhimu katika kubuni na kuendeleza mielekeo ya kinadharia katika taaluma ya tafsiri, ufundishaji wa tafsiri pamoja na uhakiki wa tafsiri.

Wananadharia katika taaluma ya tafsiri katika juhudi za kuendeleza taaluma ya tafsiri kinadharia na kiupeo wamezidi kuibuka na ramani mbalimbali zilizoimarishwa na zinazolenga kueleza upeo na kiini cha taaluma ya tafsiri. Miongoni mwa maendeleo muhimu katika taaluma ya tafsiri ni kubainishwa kwa mielekeo ya mwingiliano-taaluma hasa katika kutalii mielekeo ya kinadharia baina ya taaluma ya tafsiri na taaluma nyinginezo. Tafiti za tafsiri katika miaka ya karibuni zimevuka misingi ya kiisimu iliyosisitizwa na wasomi mwanzoni mwa karne ya ishirini na kuingia katika awamu muhimu inayopanua sio tu upeo wa kitaaluma bali pia kuibua namna mbadala za kuitafakari na kuangazia dhana ya tafsiri, uamilifu wake na dhima yake katika jamii ya kisasa.


Mojawapo ya vipengele vya kimsingi katika uhakiki wa tafsiri imekuwa ni dhana ya ulinganifu. Japo dhana hii ingali muhimu, mielekeo ya kuishughulikia na kuichunguza imebadilika na kupanuka. Aidha, ulinganifu ulivyodhukuriwa kimapokeo hauzingatiwi tena kuwa ndio uti wa mgongo wa nadharia, taaluma na utekelezaji wa tafsiri. Ulinganisho wa MT na MC sio tena kigezo cha kipekee cha kushughulikia uhakiki wa tafsiri. Mitazamo inayotumiwa sasa katika kushughulikia dhana ya ulinganifu katika tafsiri imebadilika kutoka kwa maelezo yanayojikita kwa dhana za kiisimu na kwa sasa, ulinganifu unaangaziwa kwa njia pana inayojumuisha aina ya matini, muktadha pamoja na matumizi kama anavyoeleza Baker (1992).

### 1.1.2 Mwingiliano taaluma katika tafsiri

Taaluma ya tafsiri vilevile imepanuliwa kujumuisha dhana kando na MC na MT kutokana na mageuzi yaliyoshuhudiwa katika kipindi cha miaka ya tisini. Mageuzi haya yalitokana na mawazo kuwa tafsiri ni zaidi ya mchakato sahili wa uhawilishaji wa dhana kutoka lugha moja hadi nyingine bali hujumuisha michakato ya ubunifu kwa upande wa mtafsiri na uandishi upya kuafiki uamilifu na matarajio ya hadhira lengwa. Mtafsiri haangaziwi kama daraja lisiloathiri matini anazoshughulikia ila wataalamu wametambua kuwa mtafsiri huathiri matini anazotafsiri ama kimakusudi au kwa njia isiyokuwa ya kimakusudi. Athari hizi aghalabu zinachangiwa na masuala mbalimbali ikiwemo itikadi ya mtafsiri, mageuzi yanayotokana na mifumo ya lugha, lengo la tafsiri, tamaduni zinazohusika, udhibiti wa mamlaka mbalimbali kama vile serikali na wachapishaji miongoni mwa masuala mengine. Utambuzi huu

ni wa kimsingi katika utafiti huu hasa katika uchanganuzi wa uteuzi wa kiisimu uliofanywa kwa kuwa ni kupitia kwa uteuzi huu ambapo athari za mtafsiri na mamlaka nyinginezo zinaweza kubainishwa kwa kuziweka katika muktadha wake wa kiisimu, kitamaduni na kihali.

Hatim na Munday (2004) katika kufafanua sura ya taaluma ya tafsiri katika karne ya ishirini na moja, wanatoa kiunzi kifuatacho kama taswira wakilishi ya mwingiliano taaluma katika taaluma na katika utekelezaji wa tafsiri.




**Mchoro 1 – Mwingiliano Taaluma katika Tafsiri**

**Kiunzi cha Mwingiliano-taaluma katika Taaluma ya Tafsiri (Hatim & Munday, 2004:8)**

Kutokana na kiunzi hiki, Hatim na Munday (kshj) wanaonyesha jinsi taaluma ya tafsiri inavyojumuisha ndani mwake na kuhusiana na vipengele vya taaluma nyinginezo. Mwingiliano-taaluma unaobainishwa haudhihiriki tu katika ngazi za kidhahania bali ni tukio la kihalisia katika kutafitia uwanja huu, utekelezaji wa tafsiri na ubunaji wa nadharia. Kiunzi wanachotoa Hatim na Munday (kshj) kinapanua namna ya kutalii tafsiri kama mchakato, kama taaluma na kama zao. Aidha, kinatoa nafasi kwa tafiti kuendeshwa ili kutalii na kuchunguza dhana, michakato, mageuzi na athari mbalimbali za tafsiri kiutekelezaji na kiusomi na kwa jinsi hiyo, kuweza kubainisha dhima mbalimbali za tafsiri katika ulimwengu wa sasa. Isitoshe, kinatoa fursa kwa watafiti kudadisi tafsiri kama mchakato na kama zao kwa kuvuka mipaka ya kimapokeo ya ulinganifu finyu wa kiisimu-semantiki. Kiunzi hiki kinashadidia hoja kuwa pana haja ya kuelewa vichocheo vya uteuzi unaofanywa katika tafsiri maalum pamoja na kudadisi athari za uteuzi huo. Hoja hii inatarajiwa kupanua mtazamo wa kuchunguza dhana za ubora na ufaafu wa tafsiri kwa kuvuka mipaka ya kiisimu ya matini husika. Vilevile, upanuzi huu unadadisi ufaafu wa ‘kanuni bia’ zilizopendekezwa kimapokeo kwa tafsiri za matini za tanzu anuwai. Inaelekea kuwa mikakati inayotumiwa inategemea sio tu mapendekezo ya kinadharia, bali pia mahitaji maalum kulingana na mradi wa tafsiri katika ngazi za dhima, uamilifu pamoja na matarajio ya hadhira lengwa.

Taaluma ya tafsiri pamoja na tafiti zinazoendeshwa kuangazia masuala anuwai katika taaluma hii zimepata kupanuka na kubadilika hasa baada ya mageuzi

yaliyopinga msisitizo wa kuitazama MT kama kimelea cha MC, na badala yake kuipa hadhi yake kama zao la michakato mbalimbali ikiwemo; mageuzi, ubunifu na uandishi upya (Tazama Baker, 1992). Tafiti zimeangazia dhana anuwai zinazoathiri tafsiri na kudhihirika kupitia kwa tafsiri. Kwa mfano, Alvarez na Vidal (1996) katika kujadili tafsiri kama tendo la kisiasa, anaeleza kuwa kinyume na mielekeo ya awali ambapo mtafsiri alikuwa "amefungwa" na MC, maendeleo ya kitaaluma yamedhihirisha kuwa mtafsiri ana uhuru wa kuifinyanga MC ili iafiki mfumo fulani wa imani na matarajio ya hadhira lengwa na utamaduni pokezi. Mageuzi yanayotokea yanaathiriwa na vipengele vinavyovuka sifa za MC, LC kiisimu na kujumuisha dhana zilizo nje ya upeo wa isimu kama vile upendeleo wa kiitikadi, mahusiano ya kiuwezo yanayojengeka, matarajio ya kitamaduni pamoja na uamilifu uliokusudiwa wa tafsiri husika.

Umuhimu wa mtafsiri na athari yake katika matini anazoshughulikia ni dhana inayopata umuhimu zaidi tunapozingatia tafsiri binafsi. Matukio ya tafsiri binafsi hasa barani Afrika ni dhana ambayo si ngeni. Kwa mfano, kufikia miaka ya themanini na tisini, paliibuka waandishi wa Kiafrika ambao walitunga kazi za fasihi na kuzitafsiri wenyewe. Mifano ya waandishi kama hawa ni pamoja na: Kunene Mazisi (Kizulu-Kiingereza), Archivald Jordan Campbell (Kixhosa-Kiingereza), Okot p'Bitek (Acholi-Kiingereza), Van Hereden Ernst (Kiafrikaans-Kiingereza) na Ngũgĩ wa Thiong'o (Kikuyu-Kiingereza-Kiswahili) miongoni mwa wengine. Tafiti zimebainisha kuwa inaelekea kwamba mtindo huu wa mwandishi kutunga kazi kisha

kuitafsiri mwenyewe umetumiwa zaidi katika mataifa yaliyowahi kutawaliwa na wakoloni. Bandin (1993) katika makala yake, *The Role of Self-Translation in the Decolonization Process of African Countries,* anaeleza kuwa mtindo huu aghalabu umetumiwa kama njia mojawapo ya ukombozi. Kwamba waandishi hawa hutumia mbinu hii kujikomboa wao binafsi kutokana na ukoloni pamoja na kuzikomboa lugha zao na tamaduni zao mtawalia kutokana na lugha na utamaduni babe wa kibepari. Dhana anazoangazia Bandin (kshj) kuwa ndizo vichocheo vya tafsiri binafsi ni dhana zilizo nje ya vipengele vya kiisimu na zinaeleweka kwa kuchanganua matini husika katika muktadha wake wa kitamaduni na kihali. Hata hivyo, uwakilishi na uhawilishaji wa dhana hizi huweza kubainika kupitia kwa lugha. Hivyo basi, hata katika kuchanganua tafsiri katika misingi pana isiyojikita kwa vipengele vya isimu peke tu, lugha ingali na umuhimu mkubwa.

### 1.1.3 Utafiti katika Taaluma ya Tafsiri kwa na katika Kiswahili

Taaluma ya tafsiri kwa, na katika Kiswahili sio kongwe ikilinganishwa na taaluma hii ulimwenguni hasa kwa, na katika Kiingereza. Hii ni licha ya kuwepo kwa utendaji wa tafsiri kama sehemu ya kimsingi ya mawasiliano kutokana na mtagusano wa jamii ya Waswahili na wageni. Tunaweza kukisia kutokana na historia iliyorekodiwa kuhusu maendeleo ya Kiswahili kwamba zoezi la tafsiri, ikiwemo ukalimani, lilikuwa la kimsingi katika mahusiano na wageni. Kama uwanja maalum wa usomi, tafsiri kwa na katika Kiswahili inaweza kuhusishwa na Mwansoko (1996) alipoandika kitabu chake *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Kitabu hiki

kilijikita kwa dhana na nadharia za kimapokeo kama vile mikakati ya tafsiri na suala la ulinganifu huku mchango wake mkuu ukiwa ufasili wa dhana hizi kwa msingi wa Kiswahili. Katika karne ya ishirini na moja, ndipo taaluma hii ya tafsiri kwa, na katika Kiswahili imeshuhudia ongezeko la tafiti. Hata hivyo, kama anavyoeleza Zaja (2011), bado asilimia kubwa ya utafiti imefungwa katika misingi finyu ya kulinganisha leksimu na maana kisemantiki. Suala la tafsiri binafsi ambalo ni miongoni mwa dhana za kimsingi katika utafiti huu halijatiliwa mkazo sana. Isitoshe, lengo kuu la tafiti nyingi zilizoendeshwa kwa, na katika Kiswahili, aghalabu limekuwa ni kutathmini ubora katika tafsiri husika. Mielekeo hii ya ulinganisho kiisimu na kutathmini ubora wa tafsiri ni ya kimapokeo na ipo haja ya kupanua upeo wa tafiti hizi.

Tafiti nyingi za awali katika tafsiri kwenye eneo la Afrika Mashariki, vilevile zimejikita katika kutafitia tafsiri za ujozilugha na aghalabu ambazo mwandishi wa MC na mtafsiri ni watu wawili tofauti. Kwa mfano, tafiti nyingi za uzamili na uzamifu na hata makala ya kitaaluma nchini Kenya zimeandama mkondo huu. Shitemi (1997) katika tasnifu yake ya uzamifu, aliangazia uaminifu katika tafsiri za mashairi ya jadi katika Kiswahili kwa kulinganisha MC za Kiswahili na tafsiri zake katika Kiingereza. Japo kimwelekeo alipanua mtazamo wa kimapokeo, msingi wa uaminifu umehusishwa kwa karibu na dhana za kimapokeo kama vile ulinganifu. Utafiti wake ulitoa mchango hasa kwa kuangazia utanzu wa ushairi japo mwelekeo wa kinadharia uliotumika wakati huo kwa sasa unafasiliwa kuwa wa kimapokeo.

Muigai (2005) katika tasnifu yake ya uzamili, alishughulikia ubunifu wa mtafsiri kwa kuangazia tafsiri ya *The Trials of Brother Jero* (MC) na *Masaibu ya Ndugu Jero* (MT). Suala hili la ubunifu liliangaziwa ili kuelezea uteuzi uliofanywa na mtafsiri. Uchunguzi pakubwa ulijikita katika kigezo cha uteuzi wa kileksia huku dhana ya ubunifu ikichunguzwa kwa msingi wa kuibua matini bora.

Mwingine aliyeendesha utafiti ambao tunauainisha kuwa wa kimapokeo kutokana na upeo na mwelekeo aliotumia ni Mugambi (2001). Yeye alichanganua dhana za kiisimu zilivyoshughulikiwa katika tafsiri ya *Betrayal in The City - Usaliti Mjini.* Katika uchanganuzi wake, suala la ulinganifu na suala la ubora lilikuwa la kimsingi. Aliweza hata kutoa vibadala ambavyo vingekuwa faafu zaidi kwa baadhi ya tafsiri zilizotolewa. Licha ya kuwa aliangazia vipengele vya utamaduni, upeo wa uchunguzi pamoja na mwelekeo uliotumiwa ni tofauti na ule ulioazimiwa katika utafiti huu. Badala ya kuhakiki uteuzi na kutoa hukumu za iwapo ni faafu au la, kama alivyofanya Mugambi, utafiti huu umejikita katika kujadili sababu ambazo huenda zilichangia uteuzi uliofanywa kwa kuhusisha dhana za itikadi na utambulisho.

Hata hivyo, kuna watafiti ambao wamepiga hatua katika kutafitia uwanja huu na kupanua mwelekeo pamoja na upeo wa tafiti zao kama vile Zaja (2011), ambaye katika tasnifu ya uzamifu, ameangazia ufundishaji wa tafsiri kwa kupanua mwelekeo unaotumiwa ili kujumuisha utamaduni na muktadha kwa kujikita katika matini za fasihi ya Kiswahili.

Serem (2018) ameangazia kiulinganishi vipengele vya fani katika tafsiri ya za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Utafiti huu unapanua mtindo wa uhakiki wa hapo awali kwa kuangazia tafsiri mbili za tamthilia moja zilizofanywa na watafsiri wawili tofauti na katika vipindi tofauti vya kihistoria. Uchanganuzi wa vipengele vya fani aidha unapanua upeo wa uchunguzi japo unajikita kwa vipengele vya kimtindo na kiisimu.

Watafiti wengi katika uwanja wa tafsiri wamejikita katika uhakiki na uchanganuzi wa tafsiri za kifasihi kwa kuangazia hasa matini zilizotafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine na/au ambazo mwandishi na mtafsiri ni watu wawili tofauti. Hivyo basi, utafiti huu ni tofauti kwa kuwa zaidi ya kuvuka mipaka ya kileksia katika uchanganuzi, aidha umepanua upeo kwa kuangazia tafsiri katika lugha mbili tofauti ambapo mwandishi pia ndiye mtafsiri; yaani tafsiri binafsi katika lugha mbili tofauti. Isitoshe, dhana zinazochunguzwa pamoja na mwelekeo uliotumiwa unatazamiwa kuibua ufahamu mpya katika taaluma ya tafsiri kwa na katika Kiswahili na kwa ujumla.

### 1.1.4 Lugha na Tafsiri

Parikh (2001) anahoji kwamba binadamu kama anavyobuni vifaa mbalimbali vya kutendea kazi tofauti tofauti, vivyo hivyo alibuni lugha kama kifaa cha kutekelezea wajibu wa kimsingi ambao ni kuwasiliana. Wakati wowote tunapoitumia lugha; iwe ni katika maandishi au mazungumzo, uteuzi wetu hufanywa kwa njia ya makusudi kimsingi ili kuwasilisha maana iliyokusudiwa. Hata hivyo, uteuzi huu vilevile

hutawaliwa na imani zetu, kaida za jamii, utamaduni husika pamoja na itikadi za mtu binafsi na za jumuia ambamo mtu anashiriki. Kama anavyoeleza Verschueren (2011), matumizi ya lugha hayawezi kujitenga na mitazamo ya kiitikadi japo itikadi hii haidhihiriki moja kwa moja ila hudokezwa kupitia kwa misimamo, maoni, mawazo na nadharia za jinsi hali ilivyo na vile inastahili kuwa.

Kando na kuwezesha mawasiliano, lugha pia hutekeleza wajibu wa uwakilishi. Wajibu huu kama anavyoeleza Joseph (2004), unahusiana na kile ambacho Aristotle alibainisha kuwa dhima ya lugha ya kutofautisha vitu. Baina ya matumizi ya lugha kuwasiliana na matumizi ya lugha kama kiwakilishi, ndipo suala la utambulisho linatokea. Joseph (kshj) anazidi kueleza kwamba lugha kama kitambulisho, huweza kuelekeza kwa utambulisho wa mtu binafsi au hata kwa utambulisho wa kikundi. Hivyo basi, lugha zetu na uteuzi wetu katika matumizi ya lugha hunuia kujenga uhusiano na utambulisho maalum katika miktadha mbalimbali na watu au makundi tofauti tofauti. Hali hii katika uandishi wa fasihi hudhihirika ambapo, licha ya usanii uliomo, mwandishi aghalabu hujihusisha katika mchakato wa uteuzi wa lugha kimakusudi kwa ajili ya kutimiza lengo maalum. Uteuzi huu hudhibitiwa na kuongozwa na utamaduni, imani na itikadi pamoja na matazamio ya hadhira. Hali hii pia ni sawa tunapodhukuru matumizi ya lugha katika utekelezaji wa tafsiri ambapo mtafsiri husimbua ujumbe kisha kuusimba katika mfumo mwingine wa lugha na utamaduni kwa kuongozwa na mila, desturi, imani na itikadi zake na za hadhira lengwa.

Tunapochunguza uteuzi wa lugha katika misingi ya diskosi, masuala kadhaa yanaweza kubainika ikiwemo matumizi ya lugha ama kwa lengo la kudumisha mahusiano ya kiuwezo au kwa lengo la kukiusha mahusiano yaliyopo tayari. Hili hudhihirika katika ngazi za utambulisho na msimamo wa kiitikadi iwe ni kijamii, kisiasa ua hata kiuchumi. Uteuzi huu wa kiisimu na athari zake vilevile huwepo katika utekelezaji wa tafsiri pamoja na matini zinazozalishwa kutokana na mchakato wa tafsiri. Upekee huu wa uteuzi wa kiisimu na athari zake kwa matini katika ngazi mbalimbali ni msingi muhimu katika utafiti huu. Uchanganuzi ulilenga kutalii athari ya mtafsiri katika tafsiri binafsi ya utatulugha. Hii ni kwa kujikita kwa riwaya ya Ngũgĩ wa Thiong'o *Caitaani Mutharaba-ini* iliyoandikwa kwanza kwa Kikuyu (1980), kisha kufanyiwa tafsiri na Ngũgĩ wa Thiong’o kwa Kiswahili (1982) kuwa *Shetani Msalabani* na baadaye kwa Kiingereza kuwa *Devil on the Cross* (1982).

### 1.1.5 Ngũgĩ wa Thiong’o na Fasihi

Ngũgĩ wa Thiong’o ni mmojawapo wa watunzi wa fasihi na wasomi maarufu wa fasihi kutoka nchini Kenya na Bara la Afrika. Umahiri wake katika fasihi umemfikisha katika kiwango cha kuwa mmojawapo wa wawaniaji waliopigiwa upatu kushinda tuzo ya *Nobel* ya fasihi mwaka wa 2014, 2015, 2016 na mwaka wa 2017 japo hakuishinda. Kazi zake, kama anavyoeleza Williams (1999) zinajihusisha zaidi na masuala ya historia, utamaduni na siasa. Katika juhudi za kuwakomboa Waafrika na utamaduni wa Kiafrika, Ngũgĩ (1986) katika kitabu chake *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature* anatetea na kuhimiza

matumizi ya lugha za kiasili katika ubunaji na uandishi wa kazi za fasihi. Kwa mujibu wake, uteuzi wa lugha ipi itumike na jamii fulani ni wa kimsingi kwa jamii husika katika kujitambulisha, kujenga na kudumisha mahusiano kijamii pamoja na uhusiano na ulimwengu mzima kwa jumla. Kwa mfano, tukiangazia nukuu ifuatayo kutoka *Decolonizing the Mind,* anaeleza ifuatavyo:

> Hakuna nchi ambayo inaweza kujiita huru kisiasa iwapo uchumi wake na *utamaduni* wake unatawaliwa na mahitaji ya kigeni.
>
> Ngũgĩ (1981: xv)

Kutokana na nukuu hii ni wazi kwamba Ngũgĩ anaamini katika ukombozi wa kiutamaduni na kisaikolojia kama nyenzo muhimu ya kuhakikisha uhuru wa taifa lolote lile. Uhuru huu unaangaziwa sio tu katika misingi ya kisiasa na kiuchumi, bali pia kitamaduni na kijamii. Utamaduni katika muktadha huu ni dhana pana inayojumuisha lugha, maadili, mifumo ya imani pamoja na kaida na itikadi za jamii mahususi. Imani katika lugha za Kiafrika na falsafa ya kuuenzi utamaduni asili wa Mwafrika ndiyo iliyomchochea Ngũgĩ kusisitiza matumizi ya lugha za kiasili katika utunzi wa fasihi ili "kuikomboa" fasihi na lugha za kiasili na kwa jinsi hiyo kuhakikisha uhuru kutokana na ubepari wa kiisimu na kitamaduni.

Kutokana na mawazo haya, kwa Ngũgĩ, lugha sio tu chombo cha mawasiliano bali ni kipengele muhimu cha utamaduni, ukombozi na utambulisho wa jamii yoyote na huiwezesha jamii husika kuhusiana na jamii nyinginezo pamoja na ulimwengu mzima kwa jumla.

Ngũgĩ wa Thiong'o ameweza kuandika kazi mbalimbali za sanaa zikiwemo riwaya, tamthilia na hata hadithi fupi. Awali, alipoanza kuandika, Ngũgĩ aliandika kwa Kiingereza. Baadhi ya kazi za kifasihi za wakati huo ni pamoja na: *Weep Not Child*[1] (1964) *The River Between* (1965*), A Grain of Wheat* (1967), tamthilia ya *The Black Hermit* (1963) na diwani ya hadithi fupi *A Meeting in the Dark* (1974) na *Secret Lives and Other Stories* (1975). Machapisho mengine ni kama vile tamthilia ya *The Trial of Dedan Kimathi* (1976) na Riwaya *Petals of Blood* (1977). Katika kipindi hiki, aliandika pia machapisho yasiyokuwa ya kifasihi kama vile *Homecoming* (1972), na *Decolonising the Mind* (1986). Riwaya ya *Petals of Blood* ilikuwa kazi ya mwisho ya fasihi aliyoiandika kwa Kiingereza.

Mnamo 1978, Ngũgĩ alifungwa jela kuu ya *Kamiti* kwa madai ya uchochezi. Akizungumzia kufungwa kwake katika *Detained: A Writer's Prison Diary* (1981: i) anaeleza kuwa; kwa kuwa hafahamiani kijamii wala kiuchumi na watu waliomfunga, tofauti baina yake nao sio jambo la siri wala la kibinafsi. Ilikuwa ni tofauti za *kiitikadi*.

Alipigania uhuru wa wananchi kiuchumi na kijamii kupitia kwa fasihi yake iliyoazimia kuwazindua wananchi kama ilivyokuwa katika mradi wa *Kamiirithu.* Madai kuwa alifungwa kutokana na msimamo wake kiitikadi yanashadidiwa na Mazrui anayeeleza kuwa kufungwa kwa Ngũgĩ kulichangiwa zaidi na msimamo wake kiitikadi. Alionekana kama mtetezi wa ujamaa katika taifa la kibepari.

---

[1] Ni riwaya yake ya kwanza kuchapishwa bali *The River Between* ndiyo ya kwanza kuandikwa.

Akiwa jela, ndiko alikoandika mswada wa riwaya yake ya kwanza; *Caitaani Mutharaba-ini* (1980) katika lugha ya Kikuyu. Hii ilikuwa riwaya ya kwanza kuandika kwa Kikuyu. Hata hivyo kazi ya kwanza ya kifasihi aliyoiandika katika lugha ya Kikuyu ilikuwa ni mchezo wa kuigiza wa *Ngahika Ndeenda* alioandika na Ngũgĩ wa Mirii (1977) kisha akautafsiri na kuuchapisha kwa Kiingereza kama *I Will Marry When I Want*. Riwaya hii ilifuatiwa na kazi nyingine za kifasihi katika lugha ya Kikuyu zikiwemo: *Njamba Nene na Mbaathi I Mathagu* (1982), *Bathitoora ya Njamba Nene* (1984) riwaya ya *Matigari na Njiruungi* (1987) pamoja na riwaya ya *Murogi wa Kagogo (2006).* Hivi majuzi ameandika hadithi fupi *Ituĩka Rĩa Mũrũngarũ: Kana Kĩrĩa Gĩtũmaga Andũ Mathiĩ Marũngiĩ (2016)* na riwaya ya *Kenda Muiyuru*: *Runago rwa Gĩkũyũ na Muumbi* (2018).

Wasomi mbalimbali wamechanganua msisitizo wake wa kuandika katika lugha yake ya mama na anapata sifa na uhakiki hasi kwa viwango sawa. Kuna wale wanaosifu juhudi hizi kwa kuwa zililenga kufikia hadhira pana zaidi kuliko ile ingefikiwa iwapo angeandika katika Kiingereza (Cook na Okenimkpe; 1997) huku wengine wakitilia shaka uzalendo wake kitaifa na badala yake kumhusisha na uzalendo wa kikabila kama inavyoelezwa katika *Detained: A Writers' Prison Diary* (1981: xxi-xxiii).

Katika utafiti huu, tunatambua msisitizo anaotia kwenye uandishi katika lugha yake ya mama pamoja na kutalii uteuzi unaofanywa katika kuzitafsiri kazi husika kwa kujikita kwa tafsiri ya *Caitaani Mutharaba-ini* kwa kuuhusisha na dhana za

utamaduni, itikadi na utambulisho. Utafiti ulizitalii dhana hizi kama msingi wa tafsiri za kibaadaukoloni, na kwa upana wake kama vigezo vya kimsingi katika tafsiri za fasihi yoyote ile.

### 1.1.6 Matini zilizoangaziwa

#### 1.1.6.1 Riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* (MC)

*Caitaani Mutharaba-ini* ni riwaya ambayo kama anavyoeleza mwandishi, kwanza aliiandika kwenye karatasi shashi akiwa jela na katika lugha ya Kikuyu. Inaangazia matatizo ya kisiasa na kijamii yaliyomkumba mwananchi wa Kenya wakati ule. Kama wanavyoeleza Cook na Okenimkpe (1997) kwa kumnukuu mwandishi mwenyewe;

> Mawazo huru kwenye karatasi shashi! Nilikuwa nimeamua kutumia lugha ambayo haikuwa imeandikiwa riwaya ya kisasa, changamoto kwangu binafsi, na njia ya kuhimiza imani yangu katika uwezo wa lugha zote za jamii za Kenya…Maudhui? Juhudi za jamii za Kenya za kupinga na kukabiliana na ukoloni mamboleo na ubepari!
>
> Cook na Okenimkpe (1997:114) Ty

Riwaya hii ni mojawapo ya riwaya maarufu zaidi za Ngũgĩ japo umaarufu wake zaidi unatokana na tafsiri ya Kiingereza; *Devil on the Cross*. Umaarufu wake unashadidiwa tunapozingatia kuwa pamoja na riwaya ya *A Grain of Wheat,* zilikuwa zimeteuliwa kuwa miongoni mwa fasihi bora zaidi ya Kiafrika katika karne ya ishirini. Kama wanavyoeleza Cook & Okenimkpe (kshj), riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* japo ilitungwa kwa lugha ya Kikuyu, ilikuwa na ukomavu wa kimaudhui na kimtindo kuambatana na riwaya za awali zilizoandikwa kwa

Kiingereza. Kama ilivyo kwa riwaya nyingine za Kiafrika, riwaya hii ilitumia mandhari ya Kiafrika pamoja na fasihi simulizi ya Kiafrika katika uwasilishaji wake. Riwaya hii imetumia dhana zinazofungamana na utamaduni wa jamii ya Gikuyu pamoja na jazanda zinazofasirika tu katika muktadha wa utamaduni huu. Utafiti huu ulikisia kuwa dhana hizi ndizo jukwaa ambamo utambulisho na itikadi hudhihirika. Mtindo uliotumiwa, hasa matumizi ya lugha, unasheheni vipengele vya fasihi simulizi ya Wakikuyu ikiwemo matumizi ya nyimbo, mashairi (*Marebeta),* balagha (*Gĩcaandĩ*), misemo na methali. Uteuzi huu umechukuliwa kuwa umefanywa kimakusudi na unaeleweka kwa kuieleza matini hii katika muktadha wake wa kihistoria. Uhawilishaji na uwakilishaji wa dhana hizi katika MT1 na MT2 ndio kiini cha tasnifu hii katika misingi ya utambulisho, utamaduni na itikadi.

Aidha, kuna baadhi ya sehemu za riwaya hii ambazo zinaelezea mtazamo wa Mwafrika; kupitia kwa wahusika mbalimbali au mwandishi mwenyewe, kwa utamaduni wa kigeni na lugha ya kigeni. Lugha ya Kikuyu iliyotumiwa kuelezea baadhi ya vipengele hivi ina ukali wa maneno ambayo ama yamepunguziwa ukalia katika tafsiri au kudondoshwa katika tafsiri kwenye MT1 na MT2. Utafiti huu ulifasili kwamba uteuzi unaofanywa katika mazingira haya ni wa kimakusudi, ulioongozwa na sababu za kitikadi kama ilivyojadiliwa katika sura ya nne kwenye tasnifu hii au ni kutokana na tofauti za kitamaduni kama ilivyojadiliwa katika sura ya tatu.

### 1.1.6.2 Riwaya za *Shetani Msalabani* (MT1) na *Devil on the Cross* (MT2)

Tafsiri hizi za Kiingereza, *Devil on the Cross* na ile ya Kiswahili, *Shetani Msalabani*, sio mazao ya mchakato wa tafsiri pekee ila zina vichocheo vya kujenga utambulisho pamoja na vichocheo vya kitamaduni na kiitikadi vilivyompa mtafsiri msukumo wa kuzifanya. Zote ni tafsiri-binafsi na zilichapishwa mnamo 1982. Ubainishaji wa ni tafsiri ipi iliyotangulia ni mgumu ila katika muktadha wa utafiti huu, tunachukulia kuwa nakala ya Kiswahili ndiyo tafsiri ya kwanza (MT1) huku ile ya Kiingereza ikiwa tafsiri ya pili (MT2).

Ufahamu wa hadhira lengwa pamoja na utambuzi wa lengo kuu la tafsiri ni muhimu katika tafsiri hasa kwa mtazamo wa kiuamilifu kama unavyopambanuliwa na wasomi kama vile Newmark (1981/1988), Nord (1990), Reiss na Vermeer (1984) miongoni mwa wengine. Uteuzi anaoufanya mtafsiri aghalabu hulenga kudumisha dhima ya utekelezwaji wa tafsiri husika pamoja na kutimiza mahitaji ya hadhira lengwa kwa kuzingatia muktadha wake kijamii na kiisimu.

Katika muktadha wa tafsiri hizi, mwandishi ndiye mtafsiri hivyo anaelewa vyema lengo la MC. Malengo ya MT zote mbili huenda yakafanana au kutofautiana na kwa jinsi hiyo kuathiri mikakati na mbinu alizotumia. Hii ni kutegemea hadhira inayolengwa. Tofauti kama hizi hazitokani tu na utamaduni wa hadhira lengwa bali pia Zinaweza kueleweka pia kwa kutalii imani na itikadi za mwandishi na mtafsiri pamoja na uchanganuzi wa lengo la tafsiri hizi.

Katika utafiti huu, tulikisia kuwa MC na MT1 na MT2 zilidhihirisha tofauti katika ngazi ya tafsiri hasa katika kigezo cha uibuaji wa athari sawa kwa kujikita kwa dhana za kitamaduni na zinazofungamana na utamaduni. Hali hii ilichukuliwa kuwa ilizalishwa na, miongoni mwa vichocheo vingine, juhudi za kimakusudi zilizoongozwa na uamilifu wa tafsiri zilizotekelezwa. Utafiti uliazimia kuchanganua tofauti zilizopo kwa kuhusisha dhana za utambulisho na itikadi.

**1.2 Suala la Utafiti**

Katika kusoma riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* (MC) iliyoandikwa na Ngũgĩ wa Thiong'o na tafsiri yake kwa Kiswahili, *Shetani Msalabani* (MT1), na tafsiri ya Kiingereza, *Devil on the Cross* (MT2), inaelekea kwamba kuna tofauti zinazojitokeza katika jinsi ujumbe umefumbwa na kuwasilishwa. Kuna upekee wa uandishi katika MC ambapo matini hii imeumbwa kwa kuiweka katika mazingira ya utamaduni wa lugha chanzi. Hata hivyo, upekee huu umeshughulikiwa kwa njia tofauti katika tafsiri hasa uhawilishaji wa dhana zinazofungamana na utamaduni wa MC katika MT1 na katika MT2. Dhana za kitamaduni zinazobainika moja kwa moja ni; vipengele vya fasihi simulizi na maneno yanayofungamana na utamaduni maalum. Tofauti hizi zinakiuka ubia wa kimapokeo katika utekelezaji wa tafsiri na ndipo utafiti huu ulilenga kueleza tukio hili. Isitoshe, riwaya hii ina upekee kutokana na hoja kwamba ni tafsiri binafsi ambapo mwandishi wa MC ndiye mtafsiri wa MT1 na MT2 mtawalia. Hivyo basi, utafiti utalii mchakato wa uumbaji wa MC na uzalishaji wa tafsiri zake kwa kuangazia athari ya mwandishi aliye pia mtafsiri

katika uzalishaji wa matini zilizorejelewa. Athari hii iliangaziwa kwa kujikita kwa dhana za itikadi na utambulisho kupitia kwa utalii wa uteuzi wa kiisimu uliofanywa katika MC, MT1 na MT2 kwa kuzingatia muktadha maalum wa utunzi na tafsiri kihistoria na kihali.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutalii na kuchanganua dhana za utamaduni, itikadi na utambulisho katika tafsiri kwa kujikita katika tafsiri za riwaya *Caitaani Mutharaba-ini*. Katika kufikia lengo hili, utafiti uliongozwa na malengo mahususi yafuatayo:

i. Kuchanganua utamaduni unavyodhihirika katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, na katika tafsiri zake; *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross*.
ii. Kuchunguza itikadi inavyodhihirika kupitia kwa lugha katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na jinsi inavyowakilishwa katika tafsiri za *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross.*
iii. Kupambanua jinsi utambulisho umeumbwa katika MC na jinsi mtafsiri wa *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross* alivyoshughulikia utambulisho huu.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Katika kufikia malengo ya utafiti huu, nilichochewa na maswali yafuatayo:

i. Je, dhana za kitamaduni zimesanifiwa vipi katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, na zimehawilishwa vipi katika *Shetani Msalabani* na katika

*Devil on the Cross*?

ii. Je, itikadi imeumbwa vipi kupitia kwa lugha ya mwandishi wa *Caitaani Mutharaba-ini* na imewakilishwa vipi katika tafsiri ya *Shetani Msalabani* na tafsiri ya *Devil on the Cross*?

iii. Mtafsiri ametumia mikakati na mbinu zipi katika kudumisha au kuujenga upya utambulisho uliopo katika *Caitaani Mutharaba-ini* kwenye tafsiri za *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross*?

**1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kuchanganua tafsiri za riyawa ya Ngũgĩ wa Thiong'o *Caitaani Mutharaba-ini* iliyoandikwa katika lugha ya Kikuyu. Katika muktadha wa utafiti huu riwaya hii ilichukuliwa kuwa ndiyo MC Kikuyu kikiwa LC mtawalia. Tafsiri hii ni ya utatulugha kwa kuwa imehusisha Kikuyu, Kiingereza na Kiswahili. Tafsiri ya Kiswahili inafasiliwa kuwa matini tafsiri ya kwanza (MT1) huku ile ya Kiingereza ikifasiriwa kuwa matini tafsiri ya pili (MT2) kulingana na kipindi cha kuchapishwa na kutokana na maelezo ya mwandishi aliye pia mtafsiri katika kitabu chake *Decolonizing the Mind* (1981). Utafiti ulijikita katika uchanganuzi wa utamaduni kwa kuzingatia uteuzi uliofanywa katika kutafsiri dhana zinazofungamana na mila na desturi pamoja na vipengele vya fasihi simulizi vinavyofungamana na utamaduni chanzi na vinavyojitokeza katika MC kama vile semi, nyimbo na mafumbo. Aidha, uchanganuzi ulijikita kwa jinsi dhana hizi zilivyohawilishwa katika tafsiri ya Kiswahili (MT1) na ya Kiingereza (MT2).

Isitoshe, utafiti ulishughulikia uteuzi wa mikakati na mbinu za tafsiri alizotumia mtafsiri huku ukihusisha uteuzi huu na harakati za kudumisha au kujenga upya utambulisho wa MC katika MT1 na MT2. Mwisho utafiti umejikita katika suala la ukamilifu wa tafsiri za MT1 na MT2 kwa kuangazia ubora wake na ukubalifu wake kimaana na kimawasiliano. Maana za maneno na vifungu zilichunguzwa katika misingi ya uchanganuzi makinifu wa diskosi.

## 1.6 Azma ya Utafiti

Maendeleo katika taaluma ya tafsiri yamepanua upeo wa taaluma hii kujumuisha dhana zisizo za kiisimu kinyume na mielekeo ya awali iliyojikita kwa masuala ya kiisimu katika MC na MT pekee. Mielekeo kama vile ya kutalii mwingiliano baina ya uchanganuzi matini na dhana kama vile utamaduni na itikadi imepata msukumo na uamilifu mpya katika taaluma ya tafsiri. Hii ni kutokana na ufahamu kuwa taaluma ya tafsiri inaathiriwa na masuala mengine kando na lugha kama ilivyo kwa michakato yoyote mingine ya matumizi ya lugha. Venuti (1992) kwa mfano, ameangazia uamilifu wa itikadi katika taaluma ya tafsiri japo kwa njia tofauti. Anadadisi suala la kupuuzwa kwa athari ya mtafsiri katika mchakato wa tafsiri pamoja na athari yake katika matini tafsiri. Kupitia kile anachokiita; kudhihirika kwa mtafsiri, anaeleza kuwa mtafsiri daima huiathiri matini anayoishughulikia kutokana na upendeleo wake binafsi, imani zake, utamaduni wake kati ya vichocheo vingine. Utafiti huu uliazimia kuchunguza jinsi dhana za utamaduni na itikadi zinavyofungamana na kujalizana katika kuibua utambulisho maalum. Kwa jinsi hiyo,

utafiti uliazimia kuzibainisha dhana hizi tatu kama vidhibiti muhimu vinavyoongoza uteuzi katika tafsiri na utekelezaji wa tafsiri kwa ujumla. Isitoshe, utafiti uliazimia kuchanganua athari ya mtafsiri kwa mchakato wa tafsiri pamoja na kwa MT1 na MT2 hasa kiitikadi.

Matumizi ya misingi ya uchanganuzi wa matini na ya baadaukoloni yanapanua mielekeo ya kinadharia katika taaluma ya tafsiri, jambo ambalo ni muhimu katika enzi ya usomi na utafiti wa kimwingiliano-taaluma. Aidha, utambuzi wa utamaduni, utambulisho na itikadi kama dhana zenye umuhimu katika tafsiri unapanua uamilifu wa tafsiri na kubainisha athari zake na nafasi yake katika nyanja nyinginezo kama vile siasa na hata dini. Hali hii inatoa mwao kuhusu vipengele vinavyoathiri tendo na zao la tafsiri.

Isitoshe, tafiti zilizoangazia tafsiri binafsi za baadaukoloni hazijaangazia suala la utambulisho kwa kina hasa barani Afrika. Fuertes (2004) amejadili dhima ya tafsiri-binafsi katika juhudi za ukombozi kwa waliotawaliwa na wakoloni. Anatambua kwamba tafsiri-binafsi barani Afrika ni mkakati unaotumiwa na wengi hasa kutokana na utata na mjadala uliopo kuhusu suala la lugha ya fasihi ya Kiafrika. Baadhi ya waandishi huandika katika lugha zao asilia kisha kuzitafsiri kazi hizo katika lugha nyingine za kigeni ikiwemo Kiingereza. Hali kama hii inabainika katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini.* Japo Fuertes (kshj) hajahusisha dhana hii na utambulisho, utafiti huu uliazimia kupambanua hoja kuwa zaidi ya kuandika kwa lugha za kiasili kama mbinu ya kuzikomboa lugha hizi na utamaduni wa Mwafrika, waandishi

wanaozitafsiri kazi zao binafsi aidha hulenga kujinasibisha na ndugu zao wa Kiafrika katika maandishi yao. Utafiti huu vilevile uliazimia kuchangia kongoo ya tafiti zinazoangazia utambulisho katika miktadha ya baadaukoloni pamoja na kupanua mitazamo ya kinadharia na vipengele vya kuzingatiwa katika utekelezaji wa tafsiri, ufundishaji pamoja na ubunaji wa mielekeo ya kinadharia katika taaluma ya tafsiri.

## 1.7 Mbinu za Utafiti

### 1.7.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na ulifuata mwelekeo wa utafiti wa kithamano katika utekelezaji. Mwelekeo huu ulipendelewa kwa kuwa ulimwezesha mtafiti kutalii data changamano kwa kujenga uhusiano na kwa kukamilishana katika azma ya kutimiza malengo ya utafiti huu. Aidha, ulitusaidia kufanya makisio ya kitaaluma kwa hali au matukio maalum jambo ambalo lilituwezesha kufikia mahitimisho ya kisayansi katika utafiti huu. Sehemu ifuatayo imeangazia jinsi sampuli ya utafiti iliteuliwa, mbinu zilizotumika katika kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya uchanganuzi.

### 1.7.2 Uteuzi wa Sampuli

Licha ya kuwa kuna tafsiri nyingi zilizofanywa zikilenga uwanja wa fasihi, hususan riwaya, matini za kuchanganuliwa katika utafiti huu; riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, na tafsiri zake *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross* ziliteuliwa kimakusudi kutokana na upekee wake kwamba:

i. *Caitaani Mutharaba-ini* ni riwaya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiafrika;

Kikuyu.

ii. Hii ni riwaya ya baadaukoloni kimaudhui na katika muktadha wa utunzi kihistoria.

iii. *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross* ni tafsiri-binafsi.

iv. Mwandishi wa riwaya hii aliye pia mtafsiri, amebainisha msimamo wake kuhusu lugha ya maandishi ya kazi zake na suala la tafsiri kuwezesha mawasiliano na lugha nyinginezo. (Taz. *Decolonising the Mind, 1986)*

Sifa hizi zilikuwa muhimu katika kufikia malengo ya utafiti huu na upeo uliowekwa. Sampuli ya data iliteuliwa kimakusudi kuambatana na vigeu vilivyobainishwa katika utafiti huu pamoja na mihimili ya kinadharia iliyouongoza utafiti huu.

Ijapokuwa riwaya hii siyo kazi ya pekee ambayo iliandikwa na Ngũgĩ ambayo imetafsiriwa na ambayo inatimiza baadhi ya matakwa ya uteuzi kwa utafiti huu, mtafiti alihisi kwamba upeo wa utafiti uliokusudiwa ungebainika vyema kwa kuzingatia riwaya ambayo ina mawanda mapana na aghalabu inatoa maelezo ya dhati. Aidha, upekee wa kazi hii kwa mwandishi mwenyewe, hasa katika vigezo vilivyolengwa katika utafiti huu, ni bayana kutokana na maelezo ambayo mwandishi ametoa katika [2]machapisho yake mengine kuihusu.

### 1.7.3 Ukusanyaji wa Data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutokana na usomaji na uchanganuzi wa MC, MT1 na MT2 mtawalia. Usomaji ulimsaidia mtafiti kuweza kubaini taswira za uandishi na

---

[2] Tazama *Decolonizing the Mind* na *Detained: A Writers Prison Diary.*

uteuzi wa kiisimu ambao uliainishwa kama data ya kuwezesha kutimiza malengo ya utafiti huu. Vipengele vya lugha hasa uteuzi wa kiisimu unaodhihirisha utamaduni, itikadi na utambulisho uliangaziwa kwa kuzingatia ngazi ya; leksimu, methali na vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile nyimbo, ngano na misimu. Aidha, matumizi ya lugha kisanii hasa matumizi ya jazanda zinazofungamana na utamaduni wa Gĩkũyũ yaliangaziwa. Isitoshe, vipengele hivi vilitumiwa kuchanganua jinsi ujengaji wa utambulisho katika tafsiri husika umedhihirika.

Ili kuepuka uradidi wa mifano inayotolewa kutokana na data iliyokusanywa, sampuli ya leksimu, methali, vipera mbalimbali vya fasihi simulizi pamoja na jazanda zinazofungamana na utamaduni wa MC ziliteuliwa kinasibu na kuorodheshwa kutoka kwenye riwaya chanzi; *Caitaani Mutharaba-ini* na kuorodheshwa kwenye daftari chini ya mada za ama; ugeni, ubinafsishaji au mwelekeo mseto katika jinsi zilivyoshughulikiwa katika MT1 na MT2. Ubainishaji huu ulikuwa muhimu tukizingatia sifa za lugha za fasihi ya Kiafrika na fasihi ya baadaukoloni kwa ujumla pamoja na machukulio ya utafiti huu kwamba itikadi na utambulisho, kama anavyopendekeza Venuti (1992) huweza kudhihirika vyema zaidi kupitia kwa mikakati ama ya ujengaji wa ugeni katika tafsiri au ubinafsishaji wa dhana. Chini ya uorodheshaji huu, mtafiti alibainisha dhana za kitamaduni, zilizolenga kujenga utambulisho na zile zilizohusika na uwasilishaji wa itikadi. Aidha, aliweka kategoria maalum ya dhana zilizowasilisha itikadi na kwa wakati huo huo kujenga utambulisho wa ama kibinafsi au kijamii.

### 1.7.4 Uchanganuzi wa Data

Kwa kuzingatia mihimili ya baadaukoloni, mikakati ya ubinafsishaji na uibuaji wa ugeni pamoja na mihimili ya nadharia ya uchanganuzi wa diskosi iliyotumiwa katika utafiti huu, mtafiti alichanganua ubainikaji wa utamaduni katika MC, udhihirikaji wa itikadi pamoja na taswira za utambulisho katika MC. Uchanganuzi sawia ulifanywa kwa MT1 na MT2 kwa kuchanganua kiulinganishi jinsi vipengele vya kitamaduni, kiitikadi na kiutambulisho vilivyobainishwa katika MC vimehawilishwa katika tafsiri.

Katika kuchanganua ubainikaji wa dhana za utamaduni, itikadi na utambulisho katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, tulijikita kwa vipengele vya fasihi simulizi pamoja na maneno na dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi wa Gĩkũyũ. Aidha, kwa kuwa utafiti uliazimia kuchunguza jinsi vipengele hivi vimehawilishwa katika tafsiri ya riwaya hii kwa Kiswahili na kwa Kiingereza, tulijikita kwenye uteuzi wa kiisimu uliofanywa kwenye matini tafsiri na kujadili vichocheo vya uteuzi huu. Katika kutekeleza uchanganuzi huu, utafiti pia uliangazia jinsi uteuzi wa kiisimu uliathiri uwakilishi wa maana na mawasiliano katika tafsiri ya Kiswahili na ya Kiingereza kwa kujikita katika muktadha wa baadaukoloni.

Uchanganuzi wa dhana ya utamaduni ulijikita kwa vipengele viwili vikuu. Kipengele cha kwanza, ni cha fasihi simulizi ambapo tuliangazia semi, nyimbo na mafumbo ambayo yanafungamana na utamaduni chanzi. Pili, tulijikita kwa maneno yanayorejelea dhana mahususi katika mila na desturi za utamaduni chanzi. Utafiti

ulichunguza uamilifu wa dhana hizi na dhima ambazo dhana hizi zilitekeleza katika uumbaji na ukamilifu wa MC. Aidha, utafiti uliangazia jinsi dhana hizi zilivyohawilishwa katika MT1 na katika MT2 na athari za uwakilishi uliotumika katika ukamilifu na ufaafu wa tafsiri husika katika kuwezesha mawasiliano na kutimiza dhima ya tafsiri husika katika muktadha wa baadaukoloni.

Dhana za itikadi na utambulisho zilichanganuliwa kwa kuangazia jinsi vipengele vya imani, misimamo kuhusu hali na mambo mbalimbali, majina, mila na desturi zilivyoumbwa katika MC, pamoja na jinsi zilivyoendelezwa na kuwasilishwa katika MT1 na MT2 kwa kuchanganua lugha iliyotumiwa. Dhana hizi mbili; itikadi na utambulisho, zilishughulikiwa kwa pamoja kwa kutambua kuwa kutokana na jinsi zilivyofafanuliwa katika utafiti huu zinachangiana na kujengana. Uchanganuzi ulifafanua jinsi vipengele vya kiitikadi vimeathiri uandishi wa MC, pamoja na mchakato wa tafsiri hasa katika ngazi ya uteuzi wa mikakati ya tafsiri iliyotumiwa na uteuzi wa kiisimu unaobainika katika matini zilizochunguzwa.

Uchanganuzi ulidhihirisha uteuzi wa kiisimu unavyotawaliwa na utamaduni pamoja na unavyosheheni na kudhihirisha utamaduni na itikadi. Aidha, uchanganuzi ulibainisha athari za itikadi katika utekelezaji wa tafsiri kupitia ama kwa ujengaji wa ugeni au mbinu ya ubinafsishaji. Isitoshe, uchanganuzi ulisaidia kubainisha jinsi dhana za utamaduni na itikadi zinaathiri na kuingiliana na dhana ya utambulisho. Dhana hii ya utambulisho ilishughulikiwa katika misingi ya baadaukoloni ambapo lugha na utamaduni vilikuwa vigezo vya kimsingi vya kuubainisha.

### 1.7.5 Uwasilishaji wa Matokeo ya Uchanganuzi

Matokeo ya uchanganuzi ulioendeshwa katika utafiti huu yamewasilishwa kinathari. Kila seti ya data imetolewa maelezo kamilifu kwa kuihusisha na vigeu husika katika upeo wa utafiti huu. Maelezo haya yamepangwa katika vijimada kwa mfuatano wenye mantiki na mshikamano na unaoambatana na malengo mahususi ya utafiti huu.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imejadili vipengele mbalimbali ambavyo vinaweka msingi kwa utafiti huu. Imetoa maelezo msingi ya matini zilizochunguzwa, mwandishi na kueleza japo kimuhtasari masuala ya kimsingi yaliyouchochea utafiti huu. Suala la utafiti pamoja na malengo mahususi ambayo yaliuongoza utafiti huu yamebainishwa katika sura hii. Isitoshe, mipaka ya utafiti huu imewekwa bayana na vigeugeu kubainishwa. Sura hii aidha, imeeleza mwelekeo na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti ulioendeshwa.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia mapitio muhimu ya maandishi kuhusu dhana za kimsingi katika utafiti huu. Imeangazia baadaukoloni, tafsiri binafsi, utamaduni, itikadi na utambulisho. Dhana hizi zimejadiliwa kwa kuzihusisha na kipengele cha lugha na tafsiri. Katika sura hii pia tumejadili dhana za utamaduni na lugha kama vigezo vya kimsingi katika utalii wa fasihi ya baadaukoloni. Katika kutalii vipengele vya lugha, utamaduni na itikadi, utafiti umejiegemeza kwa maoni ya wataalamu mbalimbali na kuyahusisha na mwelekeo wa kinadharia na upeo wa utafiti huu. Uhusisho wa maoni haya ni wa kimsingi katika kuweka bayana muktadha ambao kazi zilizoshughulikiwa zimezalishwa na kuweka msingi wa uchanganuzi wa data katika sura ya tatu na ya nne mtawalia.

## 2.1 Uandishi wa Baadaukoloni

Dhana baadaukoloni ni pana na yenye fasili mbalimbali kulingana na muktadha na uwanja wa matumizi. Dhana hii inakisiwa kuwa iliibuka mnamo miaka ya sitini ambapo waandishi kama vile Fanon katika vitabu vyake *Black Skin, White Masks (1967)* na *Wretched of the Earth (1963)* anaangazia jinsi ukoloni ulivyoharibu mipangilio ya kijamii, kitamaduni na kuzitiisha jumuia zilizotawalia kwa ujumla. Japo machapisho haya yalitokea kabla ya nadharia ya baadaukoloni, masuala yaliyoangaziwa katika vitabu hivi yalikuwa msingi thabiti kwa nadharia hii baadaye.

Baadaukoloni kama mwelekeo wa kinadharia na mtindo wa uhakiki unahusishwa na Edward Said ambaye katika kitabu chake *Orientalism* (1978) anabainisha mahusiano na kiuwezo baina ya sisi na wao; watawaliwa na watawala. Mahusiano haya ya kiuwezo ni sehemu ya msingi katika baadaukoloni hasa katika kuchunguza vipengele vya utamaduni, utambulisho na itikadi.

Maandishi ya kifasihi ya baadaukoloni yamejadiliwa na Boehmer (2005) kuwa ni fasihi ambayo imeangazia kiuhakiki masuala ya uhusiano wa kikoloni. Ni uandishi ambao hulenga kwa njia moja au nyingine kukinza mitazamo ya kikoloni pamoja na kubadili mahusiano ya kiuwezo. Kwa jinsi hii, fasihi ya baadaukoloni pakubwa husheheni dhana za kitamaduni zinazosawiri jinsi tamaduni za watawaliwa zilivyotwezwa huku za watawala zikikwezwa katika mahusiano ya kikoloni. Kwa mintarafu hii, uchanganuzi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake kwa Kiswahili na Kiingereza umechukua mwelekeo wa baadaukoloni makusudi ili kuweza kuhakiki vipengele hivi vya utamaduni na dhima zake katika ukiushi wa mahusiano ya kikoloni.

Tunapoangazia usawiri wa kitamaduni katika mazingira ya fasihi ya baadaukoloni, tunatambua kwamba lugha aghalabu hutekeleza dhima muhimu katika kuumba na kuwasilisha taswira husika. Hivyo basi, uhakiki wa fasihi ya baadaukoloni hauna budi kuangazia suala la lugha na jinsi ilivyotumiwa ama kukiusha au kudumisha mahusiano ya kikoloni.

Lugha vilevile, kando na kutekeleza dhima ya kuumba na kuwasilisha taswira katika fasihi ya kikoloni, imetumika kama kigezo cha kuainisha fasihi barani Afrika. Katika utafiti huu, kuna umuhimu wa kuangazia dhana Fasihi ya Afrika hasa kwa kujikita katika kipengele cha lugha. Katika kufanya hivi ni tunatambua kwamba ujelezi unaotolewa na wataalamu mbalimbali unaweza kufungamanishwa na dhana ya baadaukoloni kwa kuzingatia kwamba mataifa mengi ya Afrika yaliwahi kutawaliwa na mkoloni na fasihi ambayo aghalabu huainishwa kuwa fasihi ya Kiafrika ilizalishwa katika kipindi baada ya mataifa haya kujinyakulia uhuru, yaani kipindi cha baadaukoloni.

Tukiangazia fasihi ya Afrika, tunapata kuwa vipengele anuwai vimeweza kutumiwa kama vigezo vya kuainisha. Kuna mtazamo unaoangazia fasihi ya Afrika kuwa na maana ya fasihi iliyozalishwa na Afrika au kuhusu Afrika. Kuna ujelezi unaoiangazia fasihi ya Afrika katika misingi ya mtunzi; Mwafrika, mandhari ya utunzi, uhusika, mtindo, msuko wa matukio na maudhui yaliyoangaziwa yahusiane na Afrika. Aidha, fasihi inayozingatia lugha inayoakisi sifa za matumizi ya lugha katika muktadha wa Kiafrika; matumizi ya methali na mafumbo katika kuwasiliana. Kigezo hiki cha lugha ndicho muhimu katika muktadha wa utafiti huu. Lengo letu hapa ni kutambua dhima ya lugha na upekee wake katika mjadala mzima wa dhana ya Fasihi ya Afrika. Tunatambua mielekeo miwili mikuu: ulioshabikiwa na Ngũgĩ wa Thiong’o na ulioshabikiwa na Chinua Achebe tangu kongamano la fasihi kule Makerere (1962).

Ngũgĩ wa Thiong'o alipendekeza matumizi ya lugha za Kiafrika kusimulia tajriba za Kiafrika katika fasihi huku Achebe akitambua nafasi ya Kiingereza katika uandishi wa fasihi ya Kiafrika;

> "Je, ni halali kwa mtu kuitelekeza lugha yake na kuipendelea ya mwingine? Kufanya hivi kunaonekana kama usaliti mkuu na kunaibua hisia za hatia. Hata hivyo, kwangu sina jingine. Nimepewa lugha na ninanuia kuitumia."
>
> (Achebe 1975:62) Ty (Msisitizo wangu)

ila, akapendekeza matumizi ya lugha hizi za kigeni kwa njia ambayo itaafikia uwasilishaji wa tajriba za Mwafrika:

> Badala yake, mwandishi wa Kiafrika anapaswa kujizatiti kuibuka na Kiingereza ambacho kitawasiliana na hadhira pana na kitaweza kuwasilisha tajriba za kipekee za Mwafrika.
>
> (Achebe 1975:82) Ty

Maoni haya yote yana uamilifu muhimu katika utafiti huu kutokana na hali kuwa tafsiri iliyoangaziwa inaanzia kwa mapendekezo ya Ngũgĩ wa Thiong'o; MC imeandikwa kwa lugha ya Kiafrika (Kikuyu) na kuishia kwa mawazo ya Achebe ambapo MT2 inasheheni lugha (Kiingereza) ambayo inaakisi tajriba za Mwafrika na haijizatiti kuwa na uasilia wa Kiingereza bali ni chombo tu cha kusimulia tajriba za Kiafrika kwa Kiingereza. Isitoshe, lugha inapata umuhimu zaidi katika utafiti huu tunapodhukuru mawazo ya Ngũgĩ wa Thiong'o kuwa;

> Lugha ni jukwaa ambamo utamaduni wa jamii hudhihirika, utamaduni wa jamii unajumuisha maadili na imani ambazo huisaidia jamii kutambua nafasi yake ulimwenguni. Maadili ndiyo msingi wa utambulisho wa jamii…yote haya yanajumuishwa katika lugha.
>
> Ngũgĩ (1986:15) Ty

Mawazo haya ni muhimu katika kutambua dhima na uamilifu wa lugha katika uchanganuzi uliofanywa utafiti huu katika ngazi ya itikadi na utambulisho.

Kwamba lugha ilitumiwa kama chombo cha kumdhalilisha Mwafrika na utamaduni wake ni bayana (Fanon, 1963; Ashcroft, 2002). Hata hivyo, baada ya kujinyakulia uhuru, mataifa mengi ya Afrika yalikabiliwa na mtanziko wa lugha ipi itumike, lugha ya mkoloni kama vile Kiingereza na Kifaransa, au lugha za kiasili. Suala la uteuzi wa lugha halikuwa la kimawasiliano tu bali la kusisitiza uhuru wa Mwafrika, kumwezesha Mwafrika kisiasa na kiuchumi na hata kumpa Mwafrika utambulisho. Hata hivyo, mataifa mengi yalipendelea lugha za kigeni katika mifumo mbalimbali ikiwemo wa elimu, jambo lililodumaza ubunifu na fasihi katika lugha za kiasilia. Achebe aliamua kutumia Kiingereza katika maandishi yake, kinyume na Ngũgĩ aliyependelea matumizi ya lugha za kiasili. Hata hivyo, Achebe anasisitiza haja ya kuifinyanga lugha hii ya Kiingereza ili iweze kutumiwa kuwasilisha na kueleza tajriba za Mwafrika. Ufinyanzi huu unajumuisha miongoni mwa mambo mengine tafsiri sisisi ya dhana za kitamaduni pamoja na matumizi ya taswira za Kiafrika.

Licha ya kuwa mjadala kuhusu lugha katika fasihi ya Kiafrika ni mkongwe na changamano, katika utafiti huu tumetambua dhima ya mielekeo hii miwili kuhusu lugha za Kiafrika; matumizi ya lugha za kiasili na matumizi ya lugha za kigeni kwa “mtindo wa Kiafrika” katika uandishi wa fasihi. Uandishi katika lugha za kiasili kwa upande wake katika muktadha wa Kiafrika unachochewa na imani na haja ya kujenga na kudumisha utambulisho na jamii na utamaduni husika kama ilivyo katika

*Caitaani Mutharaba-ini* na *Shetani Msalabani*. Kwa upande mwingine, matumizi ya lugha za kigeni kwa "mtindo wa Kiafrika" ni mwelekeo ulioshamiri zaidi miongoni mwa waandishi wa Kiafrika wanaotumia lugha za kigeni kama inavyodhihirika katika tafsiri ya *Devil on the Cross*. Hili tunaweza kulihusisha na haja ya kukinza ubabe wa lugha na utamaduni wa kibepari huku fasihi husika ikitumiwa kama jukwaa la kuwasilisha tajriba, utamaduni, itikadi na utambulisho wa mtawaliwa kwa hadhira ya kilimwengu kwa njia inayokiuka mikatale ya kibepari kilugha na kitamaduni. Hali hizi mbili ndizo msingi wa utafiti huu.

## 2.2 Tafsiri Binafsi katika Muktadha wa Baadaukoloni

Katika taaluma ya tafsiri, dhana ya tafsiri binafsi ni miongoni mwa dhana ambazo zimechochea mwamko mpya miongoni mwa watafiti. Tafsiri binafsi hutumiwa kwa maana ya hali ambapo mwandishi wa matini chanzi huifanyia matini hii tafsiri kwa lugha nyingine ya pili. Kwa mfano, katika Kiswahili, mwandishi Ben Mtobwa aliandika riwaya yake *Dar es Salaam Usiku* (1998) kwa Kiswahili kisha yeye mwenyewe akaifanyia tafsiri kwa Kiingereza kuwa *Dar es Salaam by Night* (1999). Licha ya matumizi ya dhana hii katika utafiti huu, ni muhimu kutambua kama anavyofanya Bassnett (2013) kwamba dhana hii ni tata. Utata huu unatokana na suala la madai ya matini asilia ambayo, aghalabu, ni vigumu kuibainisha hasa tukizingatia kwamba waandishi wanaozitafsiri kazi zao wenyewe wana umilisi katika lugha mbili au zaidi. Hali hii ni kweli tunapodhukuru mwandishi Ngũgĩ wa Thiong'o ambaye licha ya kuwa ameandika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* kwa

lugha ya Kikuyu, ni bayana kuwa awali alikuwa ametunga fasihi katika lugha ya Kiingereza. Isitoshe, machapisho yake ya riwaya na tamthilia yamefanyiwa tafsiri za Kiswahili ambazo yeye ametafsiri. Katika hali kama hii, inakuwa vigumu kutambua matini asilia kwa uyakinifu hasa tukihusisha mawazo ya Bandia (2014) kwamba waandishi wengi wa fasihi ya Kiafrika huwasilisha yaliyomo akilini mwao, masimulizi, katika maandishi. Ni vigumu kueleza lugha ya masimulizi haya ya akilini. Hii ndiyo sababu katika utafiti huu tukapendelea dhana ya matini chanzi badala ya matini asilia.

Suala hili la tafsiri binafsi limeshamiri sana kwa wandishi wa Kiafrika ambao awali hutunga kwa lugha zao za kiasili au za kitaifa kisha kuzitafsiri kazi zao kwa lugha nyingine za kigeni. Kwa msingi wa taaluma ya tafsiri, ni muhimu kutambua kwamba, tafsiri binafsi, hasa katika muktadha wa baadaukoloni, zinaweza kuelezewa kwa misingi ya kudhihirika na kutodhihirika kwa mtafsiri kama anavyoeleza Venuti (1995). Katika enzi ya ukoloni, tafsiri zilitarajiwa kuwa na uasilia kiasi cha kutobainika kuwa ni tafsiri. Yaani tukio la tafsiri na mchango wa mtafsiri haukutazamiwa kudhihirika bayana. Hata hivyo, katika kipindi cha baadaukoloni, tafsiri, zikiwemo tafsiri binafsi, zimesheheni udhihirikaji wa tukio la tafsiri na mchango wa mtafsiri. Udhihirikaji huu ni tukio la kimakusudi ambalo linalenga kubaini umahuluti wa kitamaduni, kiutambulisho hasa kwa msingi wa itikadi ya mtafsiri. Hivyo basi, tafsiri inakuwa sio tu mchakato wa uhawilishaji na wa mawasiliano, bali inakuwa jukwaa ambamo mahusiano ya kiuwezo baina ya

tamaduni husika; imani, mila na desturi, pamoja na lugha zinazohusika yanadhihirika. Mahusiano haya ama yanadumishwa au kunatokea ukinzani wa kubadili mahusiano hayo. Katika muktadha wa utafiti huu, suala hili la udhihirikaji wa tafsiri ni la kimsingi na limehusishwa kwa karibu na juhudi za kukinza ubepari wa kikoloni; kitamaduni na kilugha. Ni juhudi za makusudi za kupinga ubabe wa utamaduni na lugha ya kipebari.

## 2.3 Utamaduni na Tafsiri

Utamaduni katika tafsiri umebainishwa kuwa kipengele cha kimsingi kama ilivyo lugha.

Mchakato wa tafsiri sio tu tukio la uhawilishaji wa dhana za kisiimu kutoka lugha moja hadi nyingine bali ni mchakato wa mawasiliano baina ya jamiilugha mbili tofauti. Ukamilifu wa mawasiliano haya pakubwa hutegemea uteuzi wa kiisimu na wa mikakati inayotumiwa katika kuwakilisha sio tu maana za kisemantiki bali pia dhana za kitamaduni na maana kimatumizi katika matini husika. Kwa jinsi hii tafsiri inaweza kunafasiliwa kuwa uhawilishaji wa dhana za kiisimu na kitamaduni baina ya lugha na tamaduni mbili au zaidi kwa njia inayoibua athari sawa kimawasiliano kwa hadhira lengwa.

Katika historia ya taaluma ya tafsiri na maendeleo ya kinadharia katika tafsiri, dhana ya utamaduni huenda ndiyo imepanua zaidi upeo na mielekeo ya kuchunguza na kutalii mchakato wa tafsiri na tafsiri zinazozalishwa. “Mageuzi ya Kitamaduni”[3]

---

[3](Lefevere na Bassnett’s, 1990) - ni dhana iliyopendekezwa kurejelea mabadiliko yaliyotokea tangu

yaliyotokea mwanzoni mwa miaka ya tisini yalikuwa na athari kuu kwa mustakabali wa taaluma ya tafsiri. Wasomi waliacha kuangazia mchakato wa tafsiri kama tukio la kiisimu pekee linalojishughulisha na maana msingi za maneno pekee na badala yake wakatambua dhima na nafasi ya utamaduni katika tafsiri. Utambuzi huu pakubwa ulitokana na hoja kuwa tafsiri ni mchakato wa kimawasiliano baina ya lugha na tamaduni mbalimbali zaidi ya ulivyo mchakato finyu wa kiisimu unaojishughulisha na uhawilishaji wa maana na utafutaji wa visawe kwa dhana za kiisimu (Lefevere na Bassnett, 1990). Utambuzi huu ulipanua upeo wa uchunguzi katika taaluma ya tafsiri na kukaibuka wataalamu kama vile Venuti (1995) ambao walijumuisha masuala ya itikadi na mahusiano ya kijamii. Dhana nyingine ambazo zimejumuishwa katika vipengele vya kuchunguzwa na taaluma ya tafsiri ni pamoja na masuala ya kijinsia, sosholojia na utalii wa dhana ya baadaukoloni.

Kwa mujibu wa Vermeer (1992) tafsiri inahusisha michakato ya kiisimu na dhana za kitamaduni na kwa jinsi hiyo, tafsiri ni dhana ya kiisimu kama ilivyo ya kitamaduni. Aidha, kwa kuwa lugha yoyote ile ni sehemu ya utamaduni maalum, tafsiri inaeleweka kama dhana ya kitamaduni. Yaani, ni mchakato unaovuka mipaka ya kiisimu. Kutokana na maelezo haya, lugha na utamaduni ni dhana pacha na katika tafsiri utamaduni na isimu ni vipengele vya kimsingi ambavyo haviwezi kutenganishwa katika kuhakiki, kuchanganua ama hata kutekeleza tafsiri.

Mwansoko (1996) katika kujadili utamaduni na tafsiri, anashughulikia dhana ya

katikati ya miaka ya 1970 hasa ikiathiriwa na mawazo ya André Lefevere kuhusu mchakato mzima wa tafsiri kama dhana ya kitamaduni zaidi ya ilivyo ya kiisimu.

utamaduni kwa kuangazia vijenzi vyake ikiwemo mila, desturi na mipangilio ya kijamii. Katika utafiti huu, dhana utamaduni imetumika kwa maana pana inayojumuisha sio tu mila, desturi na mipangilio ya kijamii, bali pia vipengele vya matumizi ya lugha kama vile fasihi simulizi ambayo daima hufungamana na maisha ya jamii husika. Katika kuchanganua tafsiri zilizoangaziwa katika utafiti huu hivyo basi, kipengele cha utamaduni kimetiliwa mkazo kama kiunzi cha kimsingi kinachoangaziwa na kuchangia ufaafu ukamilifu na ukubalifu wa tafsiri yoyote ile.

Katika utafiti huu, tunatambua kwamba, miongoni mwa dhana ambazo ni changamano zaidi kutafsiri ni utamaduni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba vipengele vinavyofungamana na utamaduni maalum wakati mwingi huwa havina viwakilishi linganifu katika lugha na utamaduni lengwa. Hali hii kimapokeo ilifasiliwa kuchangia suala la upoteaji wa maana. Hata hivyo katika muktadha wa baadaukoloni, ni maoni yetu kuwa uwasilishaji wa utamaduni katika tafsiri kando na kwamba aghalabu hauna ulinganifu kamili, pakubwa hukiushwa makusudi kwa malengo mawili makuu: kukinza ubabe wa lugha na utamaduni lengwa hasa wa kibepari na kukweza lugha na utamaduni chanzi wa mtawaliwa. Huu ndio msingi wa uchanganuzi wa dhana hii katika utafiti huu.

### 2.3.1 Utamaduni na tafsiri za fasihi ya Afrika

p'Bitek (1986) anaeleza kuwa, fasihi andishi ya Kiafrika imefungamana kwa karibu sana na utamaduni wa Kiafrika kwa kuwa licha ya kuwa inaandama mtindo wa kimagharibi, pakubwa imetokana na fasihi simulizi ya jamii mbalimbali za Kiafrika.

Anazidi kueleza kuwa utafiti katika fasihi hii sio tu tukio la uhakiki wa fasihi bali unahitaji pia maarifa ya kianthropolojia kuielewa. Madai haya yanashadidia uhusiano wa kufungamana uliopo baina ya fasihi andishi ya Kiafrika, fasihi simulizi na utamaduni. Hali hii hufanya tafsiri ya fasihi ya Kiafrika kuwa mchakato changamano hasa katika kuhawilisha dhana za fasihi simulizi zinazofungamana na utamaduni. Uhawilishaji wa dhana hizi katika MT1 na MT2 za utafiti huu ni wa kimsingi katika kubainisha dhana za itikadi na utambulisho.

Bandia (2002) katika kujadili fasihi tafsiri ya Kiafrika anatambua kuwa, japo ni vigumu kutafsiri fasihi yoyote ile, kutafsiri fasihi ya Kiafrika ni mchakato changamano zaidi. Kwa ujumla, tafsiri ya fasihi huhitaji sio tu umilisi wa kiujozilugha, bali pia umilisi wa kiujozimila, umilisi wa utanzu na ubunifu wa hali ya juu. Kutokana na mwingiliano-taaluma uliopo kwa sasa katika tafsiri, Hermas (2002) anaeleza kuwa tafsiri ya fasihi ya Kiafrika inamhitaji mtafsiri kuunganisha mielekeo ya kimapokeo katika tafsiri na maarifa ya kitamaduni, kimtindo na kifasihi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa fasihi ya Kiafrika ina upekee wa kitamaduni ikilinganishwa na fasihi kutoka maeneo mengine kama vile fasihi ya Ulaya. Hali hii inasababishwa na ukweli kuwa, waandishi wengi wa fasihi ya Kiafrika “hutafsiri” mawazo kutoka kwa masimulizi yaliyoshamiri katika muktadha wa Kiafrika na kuyawasilisha kimaandishi kwa kuyaunda upya ili kuafiki tanzu mbalimbali. Hali hii imezungumziwa na waandishi wa kiafrika kama vile Okara (1963:15) ambaye anaeleza kuwa:

> Kama mwandishi anayeamini katika matumizi ya mawazo ya Kiafrika, falsafa ya Kiafrika, fasihi simulizi na taswira za kiafrika kadri iwezekanavyo, ni maoni yangu kuwa njia pekee ya kutumia vipengele hivi kikamilifu ni kuvitafsiri sisisi kutoka lugha asili ya Kiafrika ya mwandishi hadi lugha yoyote ya Ulaya anayoitumia kama mbinu ya kujieleza ... kuanzia kwa neno, kikundi cha maneno, sentensi au hata jina katika lugha yoyote ya Kiafrika mtu anapata kuona maadili ya kijamii, mitazamo na mila za jamii.
>
> (Ty)

Maoni haya yanaoana na yale ya wasomi na waandishi maarufu wa Kiafrika kama vile Chinua Achebe, ambaye licha ya kutumia lugha ya Ulaya, Kiingereza, kama mbinu ya kujieleza, kazi zake zinasheheni fasihi simulizi na taswira ya Kiafrika kwa undani. Isitoshe, mawazo haya yanaoana na ya Ngũgĩ wa Thiong'o kipindi baada ya kuandika *Decolonising the Mind* ambapo anaandika fasihi kwanza kwa lugha ya Kikuyu, kisha anaitafsiri ama inatafsiriwa hadi Kiingereza, Kiswahili na lugha nyinginezo. Kwa kuzichunguza tafsiri za kazi mbalimbali tunaweza kuthibitisha kuwa mawazo ya Okara yanaafikiwa.

Japo kuna mbinu mbalimbali za tafsiri kama anavyoeleza Mwansoko (1996), tafsiri ya dhana za kitamaduni hutekelezwa vyema zaidi mtafsiri anapotumia tafsiri ya kimawasiliano. Mbinu hii humhitaji mtafsiri kutafuta vibadala mwafaka kwa dhana iliyomo katika MC ili kuiwasilisha katika LP kwa njia itakayowasiliana na kuibua athari sawa kwa hadhira ya MT. Licha ya hayo, mtindo ulioshamiri katika fasihi ya Kiafrika ni wa matumizi ya tafsiri sisisi. Mtindo huu hudumisha ulinganifu kiisimu lakini tafsiri inayozalishwa inakuwa na upungufu kimawasiliano hasa kwa kurejelea dhana zinazofungamana na utamaduni wa MC. Hata hivyo katika msingi wa

baadaukoloni, tafsiri hizi zinafanikiwa kiuamilifu, yaani kuzikomboa tamaduni na lugha za Mwafrika dhidi ya lugha na utamaduni wa kibepari. Hili linatokana na kuzivusha tamaduni hizi kutoka mipaka yake asilia na kuzikweza kuwa na hadhi sawa na ile ya tamaduni za kibepari.

Matumizi ya tafsiri sisisi katika fasihi ya Kiafrika ni ya kimakusudi. Tafsiri sisisi inatumika kwa lengo la kuwasilisha dhana za kitamaduni, tajriba na taswira za Kiafrika kwa ukaribu iwezekanavyo katika mfumo pokezi kiisimu na kitamaduni. Hii hufanywa wakati ambapo lugha inatumiwa kama mbinu ila sio katika kuhawilisha dhana katika mfumo wa LP na utamaduni pokezi. Hivyo basi, ili kuzielewa tafsiri hizi, ni muhimu kuzingatia tamaduni, imani na itikadi pamoja na mitindo iliyotumiwa katika MC na jinsi ilivyowasilishwa katika MT.

**2.4 Dhana ya Itikadi**

Hii ni miongoni mwa dhana ambazo ni changamano na tata zaidi kueleza. Ufafanuzi tofauti umetolewa kutegemea uwanja na muktadha ambapo dhana hii imetumika. Van Djik (1998) anafafanua itikadi kuwa na maana jumuishi ya; jumla ya imani za kimsingi za kikundi fulani na watu wanaojumuika katika kikundi hicho. Itikadi aghalabu hutokana na utambuzi unaotokana na fikra na huathiriwa na mawazo yaliyopo katika jamii husika. Hivyo, itikadi ni kipengele dhanifu ambacho kinategemea zaidi fikra na mawazo. Hata hivyo kipengele hiki kinapata uyakinifu kupitia kwa lugha na matumizi yake hasa katika kueleza mawazo na fikra za m(wa)tumiaji.

Kwa mujibu wa Eagleton (1991) licha ya kuwepo na ujelezi tofauti tofauti wa dhana ya itikadi, aghalabu inatumiwa kurejelea utalii wa jinsi maana (na ishara zinazoifumbata) zinavyotumiwa kuwasilisha na kudumisha mahusiano ya kiuwezo. Katika kutalii mahusiano haya, tunaangazia wahusika wenye mamlaka kwa kuwalinganisha na wasio na mamlaka, kwa mfano; uhusiano baina ya lugha, tamaduni, uchumi na mifumo ya kisiasa. Uwasilishwaji huu hutegemea matumizi ya lugha, yaani uteuzi wa kiisimu; leksimu na miundo ya tungo, na hivyo ni kupitia kwa lugha ndipo tunaweza kuifasili na kuielewa dhana ya itikadi. Uchunguzi wa itikadi katika utafiti huu umo katika kuchanganua uteuzi wa kiisimu hasa ukijikita kwa vipengele vya utamaduni. Kutokana na uteuzi huu, utafiti unaweza kutalii dhana ya itikadi ilivyoumbwa katika MC na kwa wakati huo huo kuchunguza jinsi ilivyohawilishwa katika tafsiri za MT1 na MT2.

Fairclough (1995) anaeleza kuwa itikadi daima ni kipengele ambacho huwepo katika lugha. Aidha, lugha ndilo jukwaa ambamo itikadi hubainishwa na kuwasilishwa. Utalii wa itikadi hivyo basi hauna budi kushughulikia vipengele vya lugha kama msingi wa udhihirikaji na ubainishwaji wake. Mielekeo ya kiitikadi inadhihirika kupitia uteuzi wa lugha kileksia na hata jinsi matini inavyosawidiwa kutegemea dhana zinazopewa uzito na zile zinazodidimizwa. Katika utafiti huu, mawazo haya yanasaidia hasa katika kuchanganua uteuzi unaofanywa katika uhawilishaji wa dhana kwa kuchanganua dhana zinazodumishwa kama zilivyo katika MC – nazifasiri kuwa zilizotiliwa uzito, pamoja na zile zinazoumbwa upya - hizi nazifasili kuwa

zilizodidimizwa. Hatim na Mason (1997) wanafafanua itikadi kuwa dhana yenye maana ya; machukulio, imani na mfumo wa kimaadili ambao kikundi fulani cha kijamii kinashiriki.

Kutokana na maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya itikadi, utafiti huu uliifasili dhana hii kwa upana wake kurejelea imani, msimamo, mtazamo wa mtu binafsi au wa jamii fulani kwa ujumla kuhusu jambo mtu au kikundi cha watu au hali fulani ambao aghalabu unadhihirika kupitia kwa matumizi ya lugha. Kwa kuzingatia maelezo ya Puurtinen (2003) kuwa uteuzi wa kiisimu anaofanya mwandishi wa matini au hata mtafsiri aghalabu huunda mtazamo fulani kwa hali au tukio linalowasilishwa, itikadi katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa kuchunguza uteuzi wa kiisimu wa mtafsiri katika MT1 na MT2 kwa kuulinganisha na uteuzi katika MC. Wakati mwingine uteuzi huu huwasilisha hisia, mitazamo na misimamo ya mwandishi au mtafsiri na kwa jinsi hiyo, huenda ukaathiri mtazamo na msimamo wa hadhira lengwa.

Kutokana na uamilifu wa dhana ya itikadi katika utafiti huu, tuliichunguza kwa upana wa upeo wake hasa mawazo ya Van Djik (1998) ambaye amebainisha mihimili mitatu mikuu ya udhihirikaji na uchanganuzi wa dhana hii. Katika ufasili wake wa dhana itikadi, Van Djik ameifafanua kuwa ni msingi wa uwakilishi wa kijamii ambao ni sawa kwa washiriki katika kikundi maalum. Hivyo, itikadi huwawezesha watu, wakiwa washiriki wa kikundi, kupanga imani zao za kijamii kuhusu hali mbalimbali zinazowaathiri na kwa jinsi hiyo kutenda ipasavyo.

Van Djik (1998) amesisitiza mihimili mitatu ya kimsingi katika kutalii na kuchunguza dhana ya itikadi:

a. Jamii (hapa anarejelea matakwa ya kikundi au jumuia, uwezo na mahusiano ya kiuwezo) - Katika utafiti huu, dhana hii ni muhimu katika kuelewa jinsi mwandishi anashughulikia matakwa ya kijamii pamoja na jinsi alivyoyasawiri mahusiaano ya kiuwezo katika MC pamoja na kuchunguza jinsi dhana hizi zilivyoshughulikiwa katika tafsiri ya MT1 na MT2 mtawalia.
b. Diskosi (anaifafanua kama matumizi ya lugha ambayo huwasilisha itikadi ya jamii na ambayo aghalabu huhusisha juhudi za [4]usitiri au [5]ufaraguzi. Katika utafiti huu, dhana hii ni ya kimsingi katika kuelewa jinsi uteuzi wa lugha uliofanywa katika MC umechangia ubainishaji wa itikadi ya kijamii na ya mwandishi mwenyewe. Aidha, suala la usitiri na ufinyanzi ni muhimu katika kuchunguza uteuzi unaofanywa katika MT1 na katika MT2 katika msingi wa tafsiri za baadaukoloni.
c. Utambuzi (anauhusisha na mawazo na imani ambazo kwa pamoja hushirikiana katika kubuni mawazo) – Dhana hii tumeihusisha na suala la tafsiri ya kiakili ambayo tumeipa nafasi maalum katika kueleza uchakataji wa taarifa akilini mwa mwandishi na hata mtafsiri kama inavyodhihirika na uteuzi aliofanya katika uzalishaji wa matini yake. Tumeiangazia kwa

---

[4] Tafsiri yangu ya dhana ya *Concealment* aliyotumia Van Djik (1998).

[5] Tafsiri yangu ya dhana ya *Manipulation* aliyotumia Van Djik (1998).

njia ya kipekee huku tukizingatia hoja kuwa, uandishi wa baadaukoloni umehusishwa na zoezi la tafsiri katika kiwango cha kiakili. Tafsiri hii inachangia pakubwa jinsi matini inasanifiwa kwa kutumia lugha teule kimakusudi.

### 2.4.1 Itikadi katika tafsiri

Schaffner (2007) anaeleza kuwa tafiti na tafsiri nyingi za baadaukoloni huangazia dhana za uwezo, harakati za ukombozi, utambulisho na itikadi. Maoni haya japo yanatofautiana na utafiti huu, msingi wake unaingiliana na utafiti huu kiupeo na kimalengo. Hata hivyo, utafiti wa aina hii ni muhimu hasa katika kujadili dhana za utamaduni, itikadi na utambulisho tukizingatia kwamba matini hizi ni tafsiri binafsi.

Goduwala (2007) katika kujadili suala la wigo katika fasihi ya baadaukoloni, anaeleza kuwa wigo hudhihirika katika ngazi mbili kuu, kiisimu-kijamii na kiitikadi-kijamii. Kwa mujibu wake, waandishi wa mataifa yaliyotawaliwa hutumia dhana hizi mbili ama kujikomboa au kuendeleza kasumba za kuwa utamaduni wa kikoloni ndio babe katika fasihi zao. Kutokana na maelezo haya ni bayana kuwa katika kuchanganua fasihi tafsiri ya kibaadaukoloni, hatuna budi kuangazia dhana za kiisimu-kijamii na za kiitikadi-kijamii mtawalia. Ni maoni ya utafii huu kuwa ngazi hizi mbili ni za kimsingi katika kudadisi dhana ya itikadi pamoja na ile ya utambulisho katika tafsiri za *Caitaani Mutharaba-ini*. Utafitihuu hivyo basi, uliazimia kuchunguza dhana hizi ili kubainisha zinavyodhihirika na zinavyoathiri mchakato wa tafsiri na MT1 na MT2.

Fawcett (1998) anaeleza kuwa, kazi nyingi za kwanza kushughulikia dhana ya itikadi katika tafsiri hazikuwa na uzito wa kiufafanuzi ulioegemezwa kwenye data mahususi ila zilitoa kauli jumuishi (Tazama; Venuti, 1992a na Niranjana, 1992). Utafiti huu unaazimia kupiga hatua kwa kubainisha dhana ya itikadi katika tafsiri kwa kutoa mifano mahususi na kuijadili kwa kuiegemeza kwa mawazo ya kinadharia.

Ben-Ari (2008) anaeleza dhana ya itikadi kuwa kipengele cha kimsingi katika ufinyanzi na ubadilishaji unaodhihirika katika tafsiri. Kwa kuangazia hali ya fasihi tafsiri nchini Israeli, anaeleza kuwa wafadhili wa miradi ya kutafsiri matini mbalimbali walihitaji tafsiri husika kudhihirisha mitazamo ya kiitikadi. Kwamba anaibua suala la waanzilishi wa miradi ya tafsiri na wafadhili kama vyanzo mojawapo vya itikadi zinazoathiri na kutawala tafsiri mbalimbali ni dhana muhimu katika utafiti huu. Hii hasa ni kutokana na hoja kuwa, mwanzilishi wa mradi wa kutafsiri MT1 na MT2, Ngũgĩ wa Thiong’o, pia ndiye mwandishi wa MC. Kutokana na hali hii, tunaweka matini hizi katika muktadha halisi wa utunzi na tafsiri ili kutuwezesha kutalii udhihirikaji wa dhana ya itikadi na jinsi ilivyoshughulikiwa katika tafsiri za Kiswahili na Kiingereza.

Ben-Ari (kshj) anazidi kueleza kuwa udhihirikaji wa itikadi katika fasihi ulikuwa sehemu ya kimsingi katika ubainishwaji wa taifa jipya la Israeli pamoja na utamaduni wake, yaani kulipa taifa hili utambulisho. Kutokana na mawazo haya, muumano unabainishwa baina ya dhana ya itikadi na ile ya utambulisho kama

zinazojitokeza, kuchangiana na kuathiriana katika tafsiri. Hivyo basi, utafiti huu ulizitalii dhana hizi mbili, itikadi na utambulisho, kwa pamoja ukitambua kwamba tafsiri za jamii zinazojaribu kujikomboa kama ilivyokuwa kwa Israeli pakubwa zilitekeleza dhima zaidi ya kuwezesha mawasiliano.

Mawazo sawa kuhusu athari za waanzilishi wa mradi wa tafsiri kwa zao a tafsiri yanaelezwa na Lefevere & Bassnet (1995). Hawa wanadokeza kuwa itikadi katika tafsiri aghalabu huhimizwa na waanzilishi wa mradi au hata wachapishaji wa tafsiri inayozalishwa. Kutokana na haya, tukiangazia tafsiri inayoshughulikiwa katika utafiti huu, mwandishi ndiye mtafsiri na kwa jinsi hiyo, ndiye mwanzilishi wa mradi. Hivyo imani zake na mitazamo yake kuhusu dhana mbalimbali zinazodhihirika katika maudhui, mtindo na vipengele vinginevyo vya kifani vya riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* ndivyo vinavyotawala uzalishaji wa MT1 na MT2 mtawalia. Ni dhahiri kutokana na utafiti wa Ben-Ari (2008) kuwa tafsiri inayosheheni mageuzi imetumika kuendeleza mifumo maalum ya kimawazo. Aidha, msisitizo wa kuangazia utamaduni maalum hasa kwa misingi ya kiitikadi ni muhimu katika ujengaji wa utambulisho. Hali hizi ndizo zilizochunguzwa jinsi zinavyobainika katika tafsiri za riwaya iliyoteuliwa na tafsiri zake.

Hatim & Mason (1990, 1997) na Venuti (1995) wanaihusisha tafsiri na dhana za uchanganuzi wa diskosi na kujumuisha itikadi kama kipengele muhimu kinachoathiri mchakato wa tafsiri. Usomi wa tafsiri, kitaaluma kwa sasa hauwezi kupuuza hali za kijamii, na muktadha ambamo MC na MT zinazalishwa. Jamii, na

utamaduni wake pamoja na muktadha zinapata umuhimu katika ubunaji wa nadharia katika tafsiri, ufundishaji, utekelezaji na hata uhakiki wa tafsiri. Katika utafiti huu, vipengele hivi vilitumiwa kudhihirirsha jinsi itikadi inavyoathiri uzalishaji wa matini yoyote ile pamoja na jinsi itikadi ya mwandishi/mtafsiri inaathiri mtazamo wa hadhira lengwa.

Mawazo ya Hatim na Mason (kshj) na Venuti (kshj) yanashadidiwa na Baker (2014) ambaye anatambua kuwa tafsiri za leo zinaathiriwa na masuala kando na MC. Zinategemea hali na dhana nje ya MC ambazo ni pamoja na mtazamo na matarajio ya jamii kulingana na utamaduni wake. Anatoa mfano wa mtafsiri wa kazi zinazoangazia mwanamke Mwarabu ambapo uwakilishi katika tafsiri utafanywa kuambatana na imani na matarajio ya jamii. Tafsiri kama hizi zitamsawiri mwanamke huyu kama kiumbe aliyekandamizwa na kudhulumiwa kijinsia iwapo zinaandama itikadi ya kifeministi. Uwasilishwaji huu utategemea uteuzi wa lugha na dhana zinazotiliwa uzito na kupewa kipaumbele katika tafsiri.

Tymoczko (2003) ana msimamo kuwa itikadi ya tafsiri hupatikana sio katika matini iliyotafsiriwa, bali katika uteuzi na msimamo wa mtafsiri na uamilifu wake kwa hadhira inayolengwa. Dhana kuwa itikadi hubainika kutokana na uteuzi anaoufanya mtafsiri ni muhimu katika utafiti huu. Maswali yanayoibuka hapa ni kuhusu uteuzi aliofanya mwandishi na msimamo wake, pamoja na hadhira aliyoilenga. Aidha, ni muhimu kuchunguza uwakilishi wa uteuzi huu na mtazamo wa mwandishi, aliye pia mtafsiri wa MT1 na MT2 kwa kutambua kwanza hadhira iliyolengwa na MC, MT1

na MT2 mtawalia. Matumizi ya lugha ya Kikuyu katika kuandika MC ni ya kimakusudi kama Ngũgĩ (1981) alivyoeleza kuwa alijipa kibarua cha kuandika katika lugha hii ili kuthibitisha "imani" yake kuwa lugha za Kiafrika zina uwezo wa kutumika kuandaa kazi bunilizi pamoja na kueleza tajriba za Mwafrika. Imani hii ni sehemu muhimu katika kuueleza uteuzi alioufanya katika MC kwa kuhusisha na hadhira aliyoilenga. Aidha, kuambatana na ujelezi wa dhana itikadi uliotumiwa katika utafiti huu, ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha kwa Ngũgĩ wa Thiong'o ni zaidi ya mbinu ya kujieleza bali pia ni zao la imani na itikadi yake kuhusu lugha za Kiafrika na fasihi yake.

Azimio la kutafsiri MC kwa Kiswahili na Kiingereza kama walivyobainisha Cook & Okenimkpe (1997) lilikuwa la kimakusudi. Liliongozwa na hadhira iliyolengwa; Kiswahili kwa hadhira ya kitaifa na kieneo na Kiingereza kwa hadhira ya kimataifa. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa lugha alizotumia Ngũgĩ katika MC, MT1 na MT2 zinaingiliana katika mazingira asilia ya utunzi ambapo kuna wasemaji wa lugha zote tatu zilizotumika. Hivyo basi, mipaka ya hadhira iliyolengwa na matini katika lugha hizi si bayana kama Cook na Okenimpke (kshj) wanavyoisahilisha. Tukizingatia hali ya kiisimu nchini Kenya ambapo watu wengi wana umilisi wa uwililugha ama utatulugha, pana uwezekano hadhira ya MC ikawa tena ni hadhira ya MT1 na MT2. Kama Tymoczko (2003) anavyoeleza, hadhira ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa tafsiri hasa uteuzi wa lugha pamoja na uwasilishaji wa kiitikadi. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kwa utafiti huu kuchunguza ni kwa jinsi gani kuwepo

kwa hadhira tofauti kwa matini hizi kuliathiri uteuzi wake wa kiisimu na ni kwa jinsi gani uteuzi huu unasaidia kujenga utambulisho wa kibinafsi na hata wa kijamii.

Tafsiri nyingi zinahusisha zaidi ya lugha moja na hivyo zaidi ya utamaduni mmoja. Kutokana na hali hii, MT husheheni ushindani baina ya tamaduni zinazozalisha MC na MT zinazohusika. Ushindani huu aghalabu huhusisha utamaduni mmoja ambao ni babe na utamaduni usobabe. Kimapokeo, tafsiri zilifanywa pakubwa kutoka tamaduni babe kuelekea tamaduni zisobabe. Hali hii inadhihirika tunapotafakari kwa mfano tafsiri zilizofanywa katika kipindi cha ukoloni kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Suala la kuwepo kwa tamaduni mbili zilizo na uwezo tofauti zikikinzana ni mojawapo ya migogoro mikuu katika fasihi ya baadaukoloni na zinadhihirika katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* pamoja na tafsiri zake. Kimapokeo, kama anavyopendekeza Venuti (1992) katika kuangazia suala la itikadi katika tafsiri mtafsiri huibua ugeni katika MT na hulenga kuifanya matini anayoitafsiri kukubalika katika mazingira lengwa kwa kuiweka sawa na mahitaji na matarajio ya hadhira lengwa kiisimu, kitamaduni na kiitikadi. Ukubalifu wa tafsiri ni muhimu kwa kiwango sawa na usahihi. Kwa mfano, katika utamaduni wa Marekani, ni sawa kwa mtoto kumwita mzazi wake kwa jina lake la kwanza. Hata hivyo, katika utamaduni wa Kiafrika, tafsiri inayodumisha mtindo huo japo inaweza kuwa sahihi, si kubalifu na itaibua maana tofauti, kama vile, kwamba mtoto hana nidhamu. Hivyo suala la ukubalifu kitamaduni katika hali ya kawaida ni la kimsingi katika tafsiri.

Hata hivyo uwakilishi wa utamaduni babe, kutokana na itikadi ya baadaukoloni anayoandama mwandishi, unaegemea kukinzana na hali ya kimapokeo. Udumishwaji wa dhana za utamaduni chanzi katika tafsiri unafanywa kimakusudi kama mbinu ya kuukomboa dhidi ya utamaduni wa kikoloni. Ukinzani huu wa uwasilishaji wa dhana za kitamaduni ndicho kitovu cha udhihirikaji wa itikadi na ujengaji wa utambulisho ambao ndio kiini cha utafiti huu.

Baumgarten (2012) anfafanua dhana itikadi kwa namna pana kuwa ni mfumo wa mawazo unaoleta makundi mbalimbali pamoja ili kufikia malengo ya kibinafsi na ya kijamii. Hii ni tofauti ni ujelezi finyu kama vile wa Kimaksi unaotazama itikadi kuwa mtazamo uliovurugika wa ulimwengu ambapo mawazo ya matabaka tawala yanashinikizwa kwa matabaka ya chini ili kujenga utambuzi usio wa kihalisia. Katika tafsiri, hasa tafsiri za kibaadaukoloni, mielekeo yote miwili ni muhimu. Mitazamo ya wakoloni na mifumo yao ya kimawazo kwa upande mmoja imelazimishwa kwa watawaliwa ambao wanaishia kuwa na mtazamo wa ulimwengu usio na uasilia. Kwa upande wa pili, watafsiri na waandishi wa kibaadaukoloni wanafanya uteuzi maalum wa kuwakilisha ulimwengu wao kwa njia inayolenga kufikia malengo maalum ya kibinafsi na kijamii kama vile ukombozi.

Tukio lolote la tafsiri limejumuishwa katika muktadha maalum wa kijamii na kutawaliwa na mojawapo ya asasi katika tafsiri: kama vile mtafsiri, waanzilishi wa mradi au hata wachapishaji. Itikadi hivyo basi inaangazia nafasi wanayochukua watu au asasi maalum katika mifumo ya kiuwezo pamoja na kusaidia kubainisha maadili

na imani maalum zinazosaidia kuwa na fasili yenye muwala ya miktadha na dhima za matini. Hata hivyo, fasili yoyote ile inategemea sio dhima na muktadha wa tafsiri pekee, bali pia kwa kiwango kikubwa hutegemea mtazamo wa mfasili mwenyewe. Hivyo suala la itikadi haliwezi kupuuzwa katika uchanganuzi wa tafsiri au matini yoyote ile.

Aixela (1996) anaeleza kuwa tafsiri yoyote ile huhusisha juhudi za uandishi-upya. Aidha, uandishi-upya aghalabu hudhihirisha nia na itikadi za kipekee ambazo huifinyanga matini ili iihudumie jamii lengwa kwa namna fulani maalum, Bassnett & Lefevere (1995). Kutokana na maoni haya, utafiti huu ulichunguza juhudi za uandishi upya kwa kuzingatia dhana zinazofungamana na utamaduni pamoja na zile za kiitikadi katika tafsiri za *Caitaani Mutharaba-ini*. MT yoyote; iwe ya kifasihi au isiyo ya kifasihi hukubaliwa na wachapishaji wengi, wahakiki na wasomaji iwapo inasomeka kwa mtiririko kama matini nyingine yoyote katika lugha husika. Hata hivyo, mtiririko na ukubalifu wa MT hutegemea msomaji pamoja na dhana nyinginezo kama vile utamaduni.

Hatim (2001) katika kujadili mbinu za kushughulikia dhana ya utamaduni katika tafsiri anapendekeza mieleko kama vile ya udumishaji wa ugeni katika tafsiri pamoja na ubinafsishaji. Hata hivyo, tunapotafakari tafsiri za fasihi ya Kiafrika katika lugha za kimagharibi, mtindo wa udumishwaji wa ugeni unapendelewa zaidi. Hii ni kutokana na juhudi za Waafrika kujikomboa na kuzikomboa lugha zao na utamaduni wao pamoja na kujenga utambulisho wao dhidi ya utamaduni babe wa kimagharibi.

Katika kutafsiri fasihi, pana haja ya MT ya kifasihi inayozalishwa kudumisha sifa zake za kifasihi. Kama Aixela (1996: 52) anavyoeleza;

> ...Umuhimu wa kaida za kutafsiri fasihi unaweza kuelezewa kwa kuangazia vipengele viwili vikuu:
> 1. Kuwa na ubora wa kati ya fasihi katika lugha pokezi (LP) (yaani kuchukua nafasi inayofaa ama kujaza pengo la kifasihi katika mfumo wa LP).
> 2. Kuwa ni tafsiri (yaani ijumuishe uwakilishi wa matini nyingine iliyotangulia katika lugha chanzi (LC) na iliyokuwa sehemu ya mfumo wa fasihi katika lugha hiyo chanzi).
>
> (Ty)

Kutokana na mawazo haya, fasihi tafsiri inapaswa kusomeka kama kazi asilia ya fasihi na kwa wakati huo huo kusheheni mwangwi wa MC ndani mwake. Ili kufikia lengo hili mtafsiri sharti atumie mwelekeo mseto ambapo atachuja elementi za kimsingi katika MC na kuziandika upya kuambatana na lugha pokezi na utamaduni lengwa ili MT isomeke kama kazi asilia katika mfumo wake wa fasihi. Hata hivyo juhudi hizi hutegemea uwezo wa tamaduni husika kuingiliana pamoja na uwezo wa kuiunda upya itikadi ya mwandishi na ile mtafsiri ili kuibuka na kazi ya fasihi yenye muwala. Dhana hii ya uandishi-upya hasa katika ngazi ya kitamaduni ina umuhimu tunapoangazia umbali wa kitamaduni baina ya MC, MT1 na MT2 ambapo MC na MT1 zinakaribiana ikilinganishwa na MT2. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa, ubainishaji wa utamaduni hasa katika misingi ya MT1 na MT2 sio suala la moja kwa moja kutokana na athari za mwingiliano baina ya watumiaji wa lugha hizi.

Munday (2007) anaeleza kuwa, katika mawasiliano kupitia kwa tafsiri, ufasili na uwasilishaji wa itikadi ya mwandishi wa MC ni changamano. Hii ni kutokana na athari za washiriki wengine katika mchakato wa tafsiri kama vile; waanzilishi wa

mradi, mtafsiri na wachapishaji. Anazidi kueleza kuwa, licha ya kuwepo kwa mfanano au tofauti za itikadi kisiasa baina ya washiriki hawa, mtazamo wa mtafsiri kiisimu bila shaka hutofautiana na ule wa mwandishi wa MC. Katika utafiti huu, mawazo haya yanaibua maswali kama vile; inakuwaje wakati ambapo mwandishi wa MC ndiye mwanzilishi wa mradi na ndiye mtafsiri, na wachapishaji wa MC ndio wachapishaji wa MT1 na MT2? Majibu ya maswali haya na athari zake kiitikadi katika tafsiri yamebainishwa katika sura ya tatu kwa kuzingatia mawazo ya Fairclough (2001) kwamba uteuzi wa kiisimu na kisarufi wa mwandishi ndio huongoza ufasili wa matini. Aidha, matini hazizalishi itikadi bali humwelekeza msomaji kuzifasili kwa namna fulani na kwa jinsi hiyo kubainisha itikadi zilizomo.

## 2.5 Dhana ya Utambulisho

Utambulisho ni dhana telezi kuifafanua. Utambulisho unaweza kuwa wa kibinafsi au wa kijamii. Unadhihirika kwa kuangazia vipengele kama vile vya; kiisimu, kitamaduni, kisiasa, kidini, kikabila, kijinsia n.k. Hata hivyo, katika sehemu hii nimejishajiisha kuweka msingi kwa dhana ya utambulisho kama ilivyotumiwa katika utafiti huu. Utambulisho ni dhana inayohusu jinsi watu binafsi au vikundi vya watu "hujiona" na kujieleza ama jinsi watu wengine au vikundi vingine "huwaona" na kuwaeleza. Utambulisho hujengwa kutokana na mahusiano ya kijamii na athari za asasi mbalimbali katika jamii katika misingi ya maadili na imani zake. Dhana utambulisho inabainika katika misingi ya mfanano na misingi ya upekee wa ama mtu binafsi au kikundi na jamii mahususi.

Barth na Bailey katika Heller (2007) wanaeleza kuwa utambulisho kijamii unaweza kuangaziwa kwa kuchunguza jinsi mtu binafsi anavyojitambulisha ama jinsi jamii inavyomtambulisha mtu huyo. Hivyo basi, katika kutalii suala la utambulisho ni muhimu kutafakari: jinsi, wakati, pamoja na kwa nini watu hujinasibisha na kundi fulani. Tajfel (1982) anaeleza utambulisho wa kijamii kuwa ni ile sehemu ya mtu ambayo anaipata kutokana na kuwa mshiriki au mfuasi wa maadili au itikadi inayohusishwa na kikundi maalum. Aidha, ni muhimu kujiuliza maswali kama vile; Sisi ni nani? Tumetoka wapi? Malengo na maadili yetu ni yepi? Huwa tunafanya nini na kwa sababu gani?

Katika kutalii dhana ya utambulisho, ni muhimu kutambua kuwa inahusiana kwa karibu na kuathiriwa na itikadi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa itikadi mbalimbali huhusisha vipengele mbalimbali vikiwemo kile kinachobainisha ujumuishwaji katika kikundi maalum. Vipengele hivi hubainisha utambulisho wa kikundi husika na kwa njia hiyo popote kikundi kinapokuwa na itikadi maalum, itikadi hiyo inatumiwa kama kitambulisho chake. Katika riwaya zilizoshughulikiwa katika utafiti huu, itikadi zinazobainishwa kwenye riwaya zinasaidia kujenga utambulisho wa makundi mbalimbali yanayowakilishwa hadithini pamoja na utambulisho wa hadhira lengwa. Tunaweza kupanua hali hii na kudai kwamba, hali ni sawa hata katika ngazi ya kibinafsi kwa mujibu wa mwingiliano uliopo baina ya itikadi ya kibinafsi na utambulisho wa kibinafsi mtawalia.

Fanon (1963) anapojadili utambulisho anaeleza kuwa, utambulisho sio kitu maalum alichopewa mtu bali daima ni uzalishaji wa taswira za utambulisho na mageuzi ya wahusika katika kufikia utambulisho maalum. Maelezo haya yanaweza kupanuliwa na kumaanisha kwamba utambulisho, wa kibinafsi au wa kijamii ni zao la kijamii linalotokana na taswira za kiakili bali sio dhana yakinifu. Kwa mfano, utambulisho wa kibinafsi katika ngazi moja unatokana na jinsi watu wengine, katika kikundi mtu anamoshiriki, wanavyomtazama, kumweleza pamoja na kuhusiana naye. Utambulisho wa kijamii unawekewa msingi na itikadi zinazoileta jamii husika pamoja. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa, licha ya kuwa utambulisho wa kibinafsi na wa kijamii unaweza kubadilika, itikadi za kimsingi za kibinafsi au hata za kijamii husalia kama zilivyo kwa muda mrefu zaidi. Hata hivyo, dhana kama vile mitazamo ya kibinafsi au hata ya kijamii inaweza kubadilika kimakusudi kuafikiana na hali maalum ya kisiasa au hata kijamii. Mabadiliko haya ni sehemu ya uchangamano wa utambulisho wa mtu au kikundi chochote kile. Kwa mfano, tunapotafakari mitazamo ya Ngũgĩ wa Thiong'o kuhusu lugha, siasa na hata uchumi, tunatambua kwamba mabadiliko ya kijamii, hasa kielimu, pamoja na ya kisiasa yaliathiri mitazamo yake na itikadi zake kuhusu dhana mbalimbali kama inavyojitokeza kwenye mijadala katika sura zinazofuata.

Katika uchanganuzi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* pamoja na tafsiri zake; MT1 na MT2, utafiti huu unachanganua jinsi lugha ilivyotumiwa na jinsi matumizi haya yanadhihirisha utambulisho katika MC pamoja na ulivyohawilishwa katika

tafsiri, MT1 na MT2. Hali hii ni muhimu japo changamano kwa kuwa utambulisho, hasa katika mazingira ya sasa si bayana. Unadhihirika katika ngazi mbalimbali na unabadilika kulingana na muktadha na mtazamo. Kwa mfano, Ngũgĩ wa Thiong'o kupitia kwa matumizi yake ya lugha anatuelekeza kwa utambulisho tofauti katika muktadha wa kijamii, kieneo na kimataifa. Aidha, utambulisho huu unadhihirika katika ngazi tofauti tofauti kama vile matumizi ya lugha mbalimbali, imani ya mwandishi na mtafsiri kuhusu dhana mbalimbali katika jamii na hadhira 'anayoizungumzia'. Uelewa wa vichocheo vya utambulisho huu ni muhimu katika kuzielewa tafsiri zilizozalishwa pamoja na uteuzi wa kiisimu uliofanywa katika mchakato wa kuzizalisha tafsiri hizi.

### 2.5.1 Utambulisho katika Tafsiri

Tafsiri yoyote ile aghalabu huhusisha zaidi ya lugha moja na kwa hivyo jamii moja na utamaduni mmoja. Ufahamu huu ni wa kimsingi katika kutalii dhana ya utambulisho katika tafsiri. Ni muhimu kudadisi haja ya tukio la tafsiri kwa kutambua tofauti zilizopo baina ya MC yoyote ile na MT zake mtawalia katika msingi wa kijamii na kwa hivyo kiutambulisho. Lugha huweza kuihusisha jamii moja na jamii nyingine na wakati huo huo, kuitenga na kuibainisha jamii moja kutoka kwa nyingine. Hali hizi mbili ni muhimu katika ujengaji na ubainishaji wa utambulisho.

Tafiti nyingi zilizoangazia utambulisho katika tafsiri zimelenga kutambua dhima ya tafsiri katika kujenga utambulisho wa jamii mbalimbali, aghalabu jamii za wachache. Hali hii hufikiwa kwa kutafsiri fasihi na matini kutoka lugha zao hadi lugha

mojawapo ya ulimwengu. Hata hivyo, tafiti zilizojikita katika kuchunguza utambulisho katika tafsiri kwa misingi ya kibaadaukoloni ni chache mno. Gentzler (2008) ni miongoni mwa wasomi waliozamia suala hili la utambulisho katika tafsiri. Anaangazia hali ya tafsiri katika Bara la Amerika na kujadili nafasi yake katika kujenga utambulisho kiisimu na kiutamaduni. Ujumuishaji wa lugha na utamaduni kama vipengele vya utambulisho katika tafsiri ni hatua muhimu hasa katika utafiti huu ambapo tunalenga kuchanganua utambulisho katika misingi ya kiisimu, hasa dhana zinazofungamana na utamaduni mahususi, na jinsi zilivyoshughulikiwa katika tafsiri.

Tunapotekeleza tafsiri yoyote ile, msukumo hutokana na ama haja ya kujenga utambulisho mpya, kwa kuathiri jamii lengwa, au kudumisha utambulisho chanzi kwa kudumisha vipengele vya kiisimu-kitamaduni kwenye tafsiri zetu. Katika tafsiri za kibaadaukoloni, suala la utambulisho ni changamano kutokana na kuathiriana kwa tamaduni za watawala na watawaliwa kwa muda mrefu. Watawaliwa wanaparamia utamaduni wa watawala kwa lengo la kujinasibisha nao hali inayozalisha mkengeuko. Hali hii inaathiri utambulisho wao asilia.

Miongoni mwa vigezo vya kimsingi vinavyotumiwa kubainisha na kudhihirisha utambulisho huwa ni lugha na utamaduni. Katika tafsiri, mtafsiri hutwikwa jukumu la kuvusha mawazo kutoka MC hadi kwa MT kwa njia inayowezesha mawasiliano na kufikia athari sawa kwa hadhira lengwa. Hata hivyo, katika utekelezaji wa jukumu hili, suala la lugha na utamaduni, hasa katika muktadha wa tafsiri za

baadaukoloni, huwa na dhima ya ziada. Dhima hii inahusisha uhawilishaji wa vipengele vya utamaduni kupitia lugha kwa njia inayoipa tafsiri ladha ya utamaduni asilia na hivyo kuinasibisha na utamaduni chanzi. Suala la lugha kwa ujumla ni la kimsingi sana katika ujengaji wa utambulisho katika muktadha wa fasihi na fasihi tafsiri ya baadaukoloni.

## 2.6 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya baadaukoloni kama ilivyofasiliwa katika taaluma ya tafsiri kwa kuzingatia mawazo ya Bandia (2014) na kuhusishwa na mihimili ya nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi kwa mujibu wa Fairclough (1989/2001). Nadharia hizi mbili zilichangiana na kukamilishana katika kuongoza utafiti huu; kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti.

### 2.6.1 Nadharia ya Baadaukoloni

Dhana ya baadaukoloni imeangaziwa kwa misingi ya taaluma ya tafsiri. Katika mtazamo huu, vipengele vya kimsingi vya baadaukoloni kama vilivyoainishwa katika fasihi na Ashcroft na wenzake (2000) ndiyo nanga inayoshikilia mihimili yake katika tafsiri. Aidha, kuna utambuzi kuwa matukio yoyote ya matumizi ya lugha na mawasiliano husheheni mahusiano ya kiuwezo kama anavyoeleza Shamma (2009). Suala la ulazimishwaji na ukinzani ni la kimsingi katika mahusiano ya kimawasiliano yanayohusisha lugha mbili na tamaduni mbili tofauti kama ilivyo katika tafsiri; hasa tafsiri katika miktadha ya baadaukoloni. Licha ya mielekeo tofauti katika kuchunguza mwingiliano wa baadaukoloni na nadharia katika tafsiri,

utafiti huu umejikita kwa maelezo ya Bandia (2014).

Katika utafiti huu, mihimili iliyotumiwa ya mwelekeo wa baadaukoloni ni: lugha, utambulisho pamoja na itikadi. Mihimili hii kando na kuwa ni nguzo za kimsingi kwa utalii wa baadaukoloni vilevile inaoana vizuri na suala la utafiti, malengo pamoja na upeo wa utafiti huu. Katika kuitumia misingi hii ya baadaukoloni, utafiti umetambua kuwa mihimili hii inadhihirika katika utekelezaji wa tafsiri kupitia kwa mikakati ya tafsiri inayotumika. Katika muktadha wa utafiti huu, tumeihusisha mihimili hii na mikakati miwili ya tafsiri iliyopendekezwa na Venuti (1995); Ubinafsishaji na Uibuaji wa Ugeni.

#### 2.6.1.1 Baadaukoloni

Baadaukoloni ni dhana inayotumiwa kurejelea mwelekeo wa kifalsafa uliojitokeza kufikia katikati mwa karne ya ishirini. Katika fasihi umetumiwa kujadili kazi za waandishi kutoka mataifa yaliyotawaliwa na mkoloni au kazi zinazoangazia hali za ukoloni, (Ashcroft na wenzake 2002). Kama mwelekeo wa kinadharia wa kuhakiki fasihi, kuna vipengele anuwai ambavyo vinaweza kuangaziwa na ambavyo ni vya kimsingi katika uhakiki wowote kama vile: mahusiano baina ya mkoloni na mtawaliwa, suala la utofauti[6], elimu ya kikoloni, uhamaji[7], itikadi, utambulisho, hejimonia, lugha na umahuluti, miongoni mwa vipengele vingine.

---

[6] Kwa maana ya *Alterity*; hali ya kuwa tofauti, kisiasa, kitamaduni, kiisimu na hata kidini.

[7] Kwa maana ya *Diaspora;* uhamaji wa kujitakia au wa kulazimishwa kutoka nyumbani (taifa au hata bara).

Licha ya kuwa dhana hizi zinachangiana na kuingiliana kwa kiasi fulani, dhana za baadaukoloni zilizotiliwa mkazo katika taaluma ya tafsiri ni zile zinazofungamana na lugha na utamaduni. Hili ni tukio ambalo tunaweza kulihusisha na ukweli kwamba tafsiri ni mchakato unaotumia lugha na aghalabu unahusisha tamaduni mbili tofauti. Katika utafiti huu, dhana za lugha, itikadi, utambulisho na umahuluti zimetekeleza dhima muhimu katika kubainisha muktadha wa uchanganuzi kwa kila seti ya data iliyoangaziwa.

#### 2.6.1.2 Baadaukoloni katika Tafsiri

Katika tafsiri, mwelekeo wa baadaukoloni ulishamiri kuanzia miaka ya tisini ambapo mageuzi yaliyotokea katika taaluma ya tafsiri yalikinzana na misimamo ya hapo awali ya kutalii na kuchunguza tafsiri kwa misingi ya kiisimu na kimuundo. Tafsiri kabla ya mageuzi haya ilichukuliwa kuwa taaluma yenye mipaka bayana baina ya MC na MT, huku MC ikipewa hadhi zaidi ya MT. Mabadiliko yaliyotokea katika taaluma ya tafsiri, pamoja na fasihi za baadaukoloni, yaliibua masuala mbadala ya kuzingatiwa kama msingi wa taaluma ya tafsiri zaidi ya vipengele vya kiisimu vilivyoshamiri hapo awali. Masuala haya ni pamoja na jinsia, ukabila, sosholojia, utambulisho, siasa na itikadi.

Licha ya kuwepo kwa mawazo na mielekeo tofauti kuhusu baadaukoloni katika tafsiri, utafiti huu umejiegemeza kwa mawazo ya Bandia (2014). Hii ni kutokana na kina cha maelezo aliyoyatoa kuhusu mwelekeo huu wa kinadharia pamoja na misingi aliyoainisha. Isitoshe, misingi yake pakubwa imechangiwa na data kutokana na

tafsiri katika muktadha wa Bara Afrika kinyume na wataalamu wengine, kwa mfano, Tymoczko (1999, 2000) ambaye amejiegemeza kwa muktadha wa Amerika ya Kusini na Nirajana (1992) ambaye amejiegemeza kwa muktadha wa Kihindi. Aidha, Bandia ametambua uwezekano wa tafsiri za baadaukoloni katika muktadha wa Kiafrika kuweza kufanywa kutoka lugha mojawapo za kikabila hadi lugha ya kitaifa. Utambuzi huu ni wa kimsingi katika utafiti huu hasa tunapozingatia lugha za MC na MT1.

Licha ya tofauti za miktadha iliyoangaziwa, na wataalamu mbalimbali walioangazia baadaukoloni katika taaluma ya tafsiri, kuna vipengele vya kimsingi ambavyo vinajitokeza katika tafiti zao zote. Hii inajumuisha jinsi tafsiri imetumiwa na inaweza kutumiwa kama chombo cha ukombozi. Kwa mfano, Niranjana (1992) anadadisi suala la utafsiri-upya[8] kama dhana ya ukombozi hasa katika muktadha wa mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni huku akirejelea muktadha wa Wahindi.

Kwa mujibu wa Bandia (2014), misingi muhimu ya baadaukoloni inayoangaziwa katika fasihi tafsiri na ambayo imeunda sehemu ya msingi wa kinadharia katika utafiti huu ni:

i. Utambuzi wa uandishi wa Kiafrika kama tafsiri: uandishi wa Kiafrika aghalabu unahusisha uhawilishaji wa fasihi simulizi katika maandishi. Maandishi yanaweza kujitokeza katika lugha ya Kiafrika, kama ilivyo kwa MC ya utafiti huu ambapo tunatambua upekee wa kiisimu unadhihirika hasa

---

[8] Tafsiri yangu ya dhana *retranslation* aliyoitumia Nirajana (1992).

kutokana na kushamiri kwa vipengele vya fasihi simulizi katika riwaya hii. Dhana kama vile balagha, ufasaha wa kusema, ambao katika muktadha wa kiafrika inahusishwa na matumizi ya lugha ya kimafumbo, misemo na methali ni dhahiri. Katika uchanganuzi wetu wa tafsiri za MT1 na MT2, tunatambua upekee unaobainika katika MC na kuchanganua jinsi ulivyohawilishwa. Aidha, tunaangazia mikakati iliyotumiwa katika tafsiri hiyo mintarafu ya malengo ya utafiti.

ii. Upekee wa lugha ya fasihi ya Kiafrika, iliyoandikwa na iliyotafsiriwa: lugha ya fasihi ya Kiafrika inayowasilishwa katika lugha ya kigeni aghalabu hujumuisha ubunaji wa leksimu na ufinyanzi wa lugha za kikoloni ili kuwasilisha dhana za kitamaduni. Mkakati huu unazalisha lugha mseto yenye maneno ya lugha ya kikoloni ila maumbo na miundo ya lugha za Kiafrika. Katika utafiti huu, uhawilishaji wa dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi kutoka MC hadi katika MT2 ni suala la kimsingi, hasa katika kutalii uhawilishaji na utambulisho na ukiushi wa kiisimu wenye nia ya kukinza ubepari wa lugha ya kikoloni. Lugha inayozalishwa ni mahuluti na tunaweza kuihusisha na dhana ya msimbo wa tatu ambayo Bandia (2014) ameitumia kurejelea msimbo mseto unaojitokeza katika fasihi andishi ya Kiafrika ambao hauafiki lugha za kiasili wala za kigeni ila ni mchanganyiko wa leksimu, miundo na mitindo ya lugha zote husika. Utambuzi wa uchangamano huu kiisimu ni wa kimsingi na katika utafiti huu tunautambua kuwa ndio jukwaa la udhihirikaji wa utamaduni hasa katika MT2. Isitoshe, lugha hii mahuluti ni

msingi wa kutuwezesha kutalii mahusiano yanayojitokeza baina ya lugha na utamaduni wa mtawaliwa na lugha na utamaduni wa mkoloni. Utafiti umelinganisha uteuzi uliofanywa katika MT1 na katika MT na kubainisha tofauti zinazodhihirika kama msingi wa kubainisha itikadi na utambulisho.

iii. Uhusiano baina ya lugha ya mtawaliwa na lugha ya mkoloni:

Kwa kuchunguza uteuzi unaofanywa hasa katika ngazi ya msamiati na mkakati wa tafsiri; ubinafsishaji au uibuaji wa ugeni, tunaweza kubainisha iwapo tafsiri inaendeleza itikadi ya kikoloni; kwamba lugha na utamaduni wa mkoloni ni bora zaidi ama kuchangia ukombozi wa utamaduni na lugha ya jamii iliyotawaliwa mtawalia. Mahusiano ya kiuwezo baina ya lugha na utamaduni wa mkoloni na lugha na utamaduni wa mtawaliwa ni dhana ya kimsingi hasa katika kujadili uteuzi unaofanywa ama kimakusudi au kwa njia isiyo ya kimakusudi katika kuzalisha MT1 na MT2. Nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri inatambua kwamba uandishi wa fasihi ya Kiafrika katika lugha za kikoloni aghalabu hujumuisha mchakato wa uhawilishaji wa lugha ya kiasili na utamaduni wake kwa lugha ya kigeni ili kukiuka kanuni zake na kupinga ubabe wake. Kutokana na haya, utafiti ulichanganua jinsi uteuzi wa kiisimu ulivyotumiwa kimakusudi kukinza mahusiano yaliyoshabikiwa ya kukweza lugha na tamaduni za kigeni katika enzi ya ukoloni. Katika kufanya hivyo, tunadadisi itikadi inayodhihirika katika uteuzi husika na kuihusisha na ujengaji na udhihirikaji wa utambulisho kitaifa na kitamaduni.

Zaidi ya mihimili hii, ili kukamilisha uchanganuzi wa itikadi na utambulisho katika utafiti huu, tulitegemea nguzo za nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi. Nadharia hii ilikuwa muhimu katika kubainisha mipaka ya uchanganuzi wa data pamoja na kutoa kiunzi cha uchanganuzi wenyewe hasa tukizingatia kuwa data iliyotokana na matini zilizokwisha chapishwa.

### 2.6.2 Uchanganuzi wa Diskosi

Mwelekeo wa uchanganuzi wa diskosi ulitumiwa katika utafiti huu kwa kuwa uliwezesha kupanua muktadha wa kuchanganua uteuzi unaodhihirika katika matini zilizoshughulikiwa. Katika utafiti huu, dhana ya uchanganuzi wa diskosi imetumiwa kwa kuzingatia maelezo ya Gee, (1999). Tumerejelea maelezo yake ambayo yanatambua kuwa lugha zaidi ya kutuwezesha kuwasiliana pia hutusaidia kutenda na kuchukua nafasi mbalimbali (yaani lugha hutuwezesha kuwa vitu).

Kabla ya kueleza mihimili ya uchangnuzi wa diskosi iliyotumika katika utafiti huu, ni muhimu kueleza maana ya dhana tatu zifuatazo za kimsingi zilizotumika na jinsi zilivyotumika:

i. *Diskosi* – ni dhana ambayo imejadiliwa na kutolewa fasili mbalimbali na watalamu tofauti tofauti. Kwa mfano, Kamusi ya Cambridge (toleo la mtandaoni) inaeleza diskosi kuwa na maana ya mawasiliano kwa njia ya usemi au maandishi. Maelezo haya ni ya kimsingi zaidi na yanaibua hoja mbili muhimu katika kufafanua diskosi; suala la mawasiliano, ambalo pia tunaweza kulihusisha na matumizi ya lugha, pamoja na mbinu ya kutumia

lugha; usemi au maandishi. Hata hivyo, dhana ya diskosi inajumuisha zaidi ya hoja hizi mbili. Kwa mfano, Jorgensen na Phillips (2002) wanaeleza diskosi kuwa ni namna maalum ya kuongea kuhusu ulimwengu na namna ya kuuelewa ulimwengu au kipengele fulani cha ulimwengu. Kutokana na maelezo haya, suala la mtazamo wa ulimwengu na tajriba za wahusika linaibuliwa kama kipengele muhimu cha diskosi. Hivyo basi, utafiti huu umeifasili dhana ya diskosi kuwa ni jumla ya matumizi ya lugha, kwa njia ya usemi au maandishi, inayoelezea jambo, tukio, ulimwengu au kipengele cha ulimwengu katika mazingira maalum.

ii. *Uchanganuzi wa diskosi* - Brown and Yule (1983) kwa kujikita kwa mwelekeo wa kiuamilifu wanafafanua uchanganuzi wa diskosi kuwa na maana ya uchanganuzi wa lugha katika matumizi. Hivyo, uchanganuzi wa aina hii hauwezi kufungwa katika msingi wa kueleza maumbo ya kiisimu bila kuzingatia dhima na uamilifu wa maumbo hayo katika maisha ya binadamu. Katika utafiti huu, tumelenga kuchanganua matumizi ya lugha katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, pamoja na uteuzi na matumizi ya lugha katika uhawilishaji wa dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi katika tafsiri ya Kiswahili na Kiingereza. Ili kufanikisha juhudi hii, muktadha umepewa umuhimu mkubwa kama kipengele muhimu cha kutuwezesha kuelewa na kufafanua diskosi (matumizi ya lugha).

iii. *Muktadha* – kwa mujibu wa Gee (2011) dhana muktadha inajumuisha mandhari ya kiasili ambamo matumizi ya lugha yanatukia pamoja na jumla

ya yaliyomo katika mandhari na matumizi hayo ya lugha ikiwemo wahusika, miondoko ya mwili, (ma)tukio la matumizi ya lugha la awali ambalo limejenga ufahamu ambao wahusika wanashiriki ikiwemo ufahamu wa kitamaduni. Kutokana na ujelezi huu tunapendekeza kuwa muktadha unaweza kupanuliwa kujumuisha sio tu kinachosemwa au kuandikwa moja kwa moja bali pia unarejelea matukio ya awali ya matumizi ya lugha yanayotoa taarifa muhimu kwa tukio la sasa la matumizi ya lugha. Hivyo basi katika utafiti huu, ina maana kwamba, muktadha wa kufasili tukio la matumizi ya lugha – uteuzi uliofanywa katika MC, MT1 na MT2 – unaweza kujumuisha usemi (mihadhara na hotuba) au hata maandishi (tahakiki na maandishi ya fasihi) ya awali au hata ya baadaye ambayo yanamhusu mwandishi na mtafsiri anayerejelewa na yanahusiana na matini zinazorejelewa ili kuelewa kikamilifu tukio la matumizi ya lugha.

Kipengele alichozungumzia Gee (1999) cha matumizi ya lugha kama tukio linalomwezesha mtumiaji wa lugha kuchukua nafasi mbalimbali ni muhimu katika utafiti huu tunapolihusisha matumizi ya lugha kama kigezo cha kumwezesha mtu kupata utambulisho maalum. Utambulisho huu aghalabu humhitaji mtu kutumia lugha kwa namna fulani na hata kutenda kwa namna fulani maalum. Gee (kshj) aidha anaeleza kuwa ili kuelewa tukio la matumizi ya lugha kikamilifu tunahitajika kuelewa nani anasema nini na kile ambacho mtumiaji wa lugha analenga kutenda.

Gee ameainisha vipengele saba ambayo ni vya kimsingi katika utekelezaji wa uchanganuzi wa diskosi faafu. Vipengele hivi vimetegemezwa kwa vipengele sita vya uchunguzi ambavyo ni: *maana kimuktadha*, *lugha kijamii*, *lugha ya kitamathali*, *mwingiliano matini*, *diskosi* na *mazungumzo.* Ili kukamilisha uchanganuzi wa diskosi, ni muhimu kuuliza jinsi vipengele hivi vinahusiana na mihimili iliyoainishwa katika uchanganuzi wa diskosi kadri vinapotokea ifuatavyo:

a. Umuhimu – Katika kigezo hiki tunajiuliza jinsi vipengele vya; maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kuunda umuhimu kwa vitu na kwa watu katika muktadha maalum.
b. Desturi na utendaji – Hapa tunaangazia jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kuwezesha desturi na utendaji katika muktadha maalum.
c. Utambulisho – Kigezo hiki kinajikita kwa jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kuwezesha na kusawiri utambulisho mbalimbali wenye umuhimu kwa watu mbalimbali.
d. Mahusiano – Hapa mchanganuzi wa diskosi anatarajiwa kuchunguza jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha

vimetumika ili kuunda na kudumisha (kubadili au kuharibu) mahusiano ya kijamii.

e. Siasa – Kigezo hiki katika uchanganuzi wa diskosi kinajikita katika kupambanua jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kuunda, kusambaza au kuzuia malighafi ya kijamii au kuchukulia usambazaji fulani wa malighafi ya kijamii kuwa "Mzuri" au "Kubalifu" au kinyume chake.

f. Uunganifu – Katika kigezo hiki tunaangazia jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kufanya vitu na watu kuunganika au kuwa na maana kwa wahusika au kutokuwa na maana au kutounganika.

g. Mfumo wa ishara na ufahamu – Mchanganuzi wa diskosi katika kigezo hiki anatalii jinsi vipengele vya maana kimuktadha, lugha kijamii, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini, diskosi na mawasiliano katika tukio la matumizi ya lugha vimetumika ili kupendelea au kutopendelea mifumo fulani ya ishara (lugha, lugha kijamii na mifumo mingine ya ishara) na namna ya kufahamu.

Katika utafiti huu, tulijikita zaidi kwa mihimili mitatu katika kutekeleza uchanganuzi wa data. Kwa kila mhimili, vipengele vilivyotiliwa mkazo ni vile vya maana kimuktadha, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini na diskosi.

Mihimili ya uchanganuzi wa diskosi iliyotumika katika utafiti huu ni:

- *Utambulisho*
- *Mahusiano*
- *Siasa*

Kwa jinsi hii, mhimili wa utambulisho katika utafiti huu umetumika kueleza na kuchanganua jinsi maana kimuktadha, lugha ya kitamathali, mwingiliano matini na diskosi katika MC, na tafsiri za MT1 na MT2 zilivyotumika ili kuumba utambulisho maalum ambao una umuhimu katika muktadha wa baadaukoloni.

Katika kuangazia mahusiano, tumetumia mhimili huu kwa kujikita kwa lugha ya kitamathali, maana kimuktadha, mwingiliano matini na dhana ya diskosi kuchunguza jinsi tukio la matumizi ya lugha katika MC na katika MT1 na MT2 lilivyotumika kuunda na/au kudumisha mahusiano ya kijamii. Katika kutekeleza uchunguzi huu, dhana ya mahusiano katika muktadha wa baadaukoloni imetiliwa mkazo.

Mwisho, kipengele cha siasa katika utafiti huu kimetumika kama mhimili wa uchanganuzi kwa kuzingatia jinsi ambavyo tukio la matumizi ya lugha kama linavyodhihirika katika MC, MT1 na MT2 lilivyotumika katika kuunda, kumbaza au hata kuzuia malighafi ya kijamii kwa kuchukulia kuwa nzuri au kubalifu au kinyume chake. Uchanganuzi katika msingi huu vilevile umehusishwa na muktadha wa baadaukoloni ambapo malighafi ya kijamii ya mtawaliwa na usambazaji wake kama tukio la kukinza ubabe wa kikoloni ndio kiini cha uchanganuzi.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imejadili vipengele vya kimsingi katika uchanganuzi ulioendeshwa katika utafiti huu. Dhana ya tafsiri binafsi imejadiliwa kwa kuhusishwa na baadaukoloni huku utamaduni, itikadi na utambulisho ukiangaziwa kwa njia ya kipekee. Vipengele hivi vimejadiliwa kwa kina kwa lengo la kutoa taarifa za kiusuli kurahisisha uelewekaji wa uchanganuzi uliotekelezwa. Sura hii vilevile imejadili misingi ya kinadharia iliyouongoza utafiti huu na kwa jinsi hiyo kuelekeza uchanganuzi katika sura zinazofuata.

# SURA YA TATU

# UTAMADUNI KATIKA RIWAYA YA *CAITAANI MUTHARABA-INI* NA TAFSIRI ZAKE

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inafungamana na lengo la kwanza la utafiti huu. Sura imeweka usuli wa dhana hii ya utamaduni katika tafsiri kwa muhtasari kabla ya uchanganuzi wenyewe. Uchanganuzi katika sura hii umejikita kwa udhihirikaji wa dhana ya utamaduni katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* pamoja na jinsi dhana hii imeshughulikiwa katika tafsiri za *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross.*

## 3.1 Utamaduni katika Tafsiri

Suala la utamaduni katika tafsiri limeangaziwa na wasomi mbalimbali kama mojawapo ya dhana muhimu za kuzingatiwa katika utafiti wa fasihi tafsiri na katika taaluma ya tafsiri kwa ujumla hasa baada ya mageuzi ya miaka ya tisini

[9]Utamaduni ni jumla ya mitazamo ya watu kuhusu ulimwengu, kuhusu tamaduni nyingine na watu wengine pamoja na jinsi mitazamo hii inavyowasilishwa. Kwa jinsi hii, utamaduni unakuwa ni ufahamu ambao jamii fulani inashiriki: kile wanajamii wanatarajiwa kujua ili watende na kupokea tajriba maalum kwa namna sawa. Kipengele cha uwasilishaji katika kuielewa dhana hii ni cha kimsingi hasa tunapotafakari matini za kifasihi kama zilizorejelewa katika utafiti huu. Wataalamu kama vile Njogu na Chimerah (1999) wamejeleza fasihi kuwa ni kioo cha jamii kwa

[9] Hatim (2001) na Fairclough (1995)

maana ya kielelezo cha mipangilio, hali na tajriba za jamii rejelewa katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Utambuzi huu ni dhana muhimu tunapotafakari dhima ya utamaduni katika fasihi yoyote ile.

Tunapodhukuru tafsiri kuwa mchakato wa mawasiliano baina ya tamaduni mbili tofauti, tunajipata katika hali ya kutambua mtagusano, hasa wa lugha baina ya tamaduni hizi[10]. Aghalabu, tamaduni zinapochunguzwa kiulinganishi hubainika kuwa hazina uhusiano sawa; kuna utamaduni ulio babe kuliko mwingine. Haya ni baadhi ya masuala ya kimsingi katika kuchanganua mchakato wa mawasiliano baina ya lugha zaidi ya moja kama ilivyo katika tafsiri. Utafiti huu unatambua kuwa baina ya MC, MT1 na MT2 kuna tamaduni angalau tatu tofauti. Kutokana na mwingiliano na mtagusano unaodhihirika, panaibuka suala la kimsingi ambalo ni mojawapo ya malengo ya utafiti huu: je, vipengele vya utamaduni vimeshughulikiwa vipi katika tafsiri ya MC hadi MT1 na MT2. Lengo hili la kuchunguza kipengele hiki cha utamaduni linaweza kupambanuliwa kwa kuligawa katika maswali kadhaa ifuatavyo:

a. Je, tamaduni mbalimbali zinadhihirika vipi kupitia kwa lugha husika?
b. Je, kuna mipaka bainifu baina ya tamaduni hizi tofauti au kuna mwingiliano?
c. Mtafsiri ameshughulikia vipi tofauti au mwathiriano baina ya tamaduni mbalimbali anazokumbana nazo?
d. Athari za tamaduni hizi ni gani kwa ubora wa tafsiri zinazozalishwa kama matini huru, za kifasihi katika ngazi za mawasiliano, mshikamano na

[10] Said (2004)

muwala?

Katika kutafuta majibu kwa maswali haya utafiti uliangazia MC, MT1 na MT2 kiulinganishi kwa kurejelea vipengele mbalimbali vya kitamaduni katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake. Katika uchanganuzi ulioendeshwa, mikakati iliyotumiwa katika kuvishughulikia vipengele hivi ilibainishwa katika ngazi mbili: ubinafsishaji na uibuaji wa ugeni huku ikihusishwa na machukulio ya nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri kuhusu jinsi ya kushughulikia utamaduni babe na usobabe katika tafsiri kupitia kwa lugha, uteuzi wa leksimu na miundo ya tungo.

**3.2 Udhihirikaji wa Tamaduni mbalimbali Kupitia kwa Lugha Husika**

MC rejelewa katika utafiti huu; riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* ilikuwa ni zao la mtindo wa kimajaribio na wa kimakusudi wa kuandika riwaya katika lugha ya Kikuyu kama mwandishi mwenyewe alivyoeleza katika *Decolonizing the Mind (*1986*)* pamoja na katika sehemu ya utangulizi wa riwaya hii ya *Caitaani Mutharaba-ini.* Huenda ikawa ni kutokana na sababu hii ndipo riwaya hii ikawa ni mojawapo wa kazi za fasihi za Ngũgĩ wa Thiong'o zilizosheheni ukopaji mkubwa kutokana na fasihi simulizi ya jamii ya Gĩkũyũ na kwa jinsi hiyo ikawa na ukwasi wa vipengele vya kitamaduni katika utunzi wake.

**3.2.1 Tafsiri za Mitindo ya Ufunguzi na Utekelezaji**

Tukiangazia sehemu ya utangulizi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* tunapata mifano ya udhihirikaji wa utamaduni wa Gĩkũyũ katika uandishi wa Ngũgĩ kwa mfano:

**Mfano 1 (Kutoka sehemu ya Utangulizi)**

**MC**: *UGA IITHA*
**MT1:** *TEGA SIKIO*
**MT2: ******

Mfano huu ni dhihirisho la ukopaji wa moja kwa moja kutoka kwa kipera cha ngano za jamii ya Gĩkũyũ tukizirejelea. Hali hii inadhihirika kupitia kwa matumizi ya maneno *Uga Iitha* ambayo yanatokana na sehemu ya mtindo wa ufunguzi katika utambaji hadithi miongoni mwa jamii ya Gikuyu ambapo mtido kamili ni:

| | |
|---|---|
| Mtambaji hadithi: | *Ugaai iitha ndimuganire karugano* |
| Hadhira: | *Tuganire na utuganire keega* |

Uwepo wa sehemu hii ya utangulizi katika MC ni dhihirisho la fasihi ya baadaukoloni ya Kiafrika kusheheni uhawilishaji wa fasihi simulizi katika maandishi ama katika lugha ya Kiafrika au lugha ya kikoloni. Uhawilishaji huu ni kipengele cha kimsingi katika uimarishaji wa nafasi ya lugha na utamaduni asilia wa jamii ya Gĩkũyũ ambao ni mojawapo wa vichocheo vilivyomsukuma Ngũgĩ kuandika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* katika lugha ya Kikuyu. Msimamo huu unapata mashiko tukirejelea maelezo ya Ngũgĩ (1986) kuhusu lugha na fasihi ya Kiafrika kuwa:

> Naamini kuwa kwa kuandika katika lugha ya Kikuyu, lugha ya Kenya na ya Kiafrika, ni sehemu ya vita dhidi ya ubepari vinavyoendeshwa nchini Kenya na barani Afrika.
>
> (Ngũgĩ, 1986:28) *Ty*

Maelezo haya sio muhimu tu katika kuelewa falsafa na imani ya Ngũgĩ kuhusiana na lugha ila ni sehemu ya kimsingi ya jinsi lugha katika fasihi tafsiri ya baadaukoloni inavyoangaziwa. Yaani lugha ni chombo cha ukombozi na kila uteuzi unaofanywa ni

wa kimakusudi kuukweza utamaduni wa waliotawaliwa kupitia kwa lugha dhidi ya utamaduni uliofasiliwa kuwa babe; wa mkoloni na lugha yake. Katika muktadha wa mfano huu, japo MC imeandika kwa lugha ya Kikuyu, udhihirikaji wa vipengele hivi vya fasihi simulizi vinavyofungamana na utamaduni chanzi ni wa kimakusudi na mwandishi amefanya uteuzi huu kimakusudi ili kuonyesha ukwasi wa lugha hii ya Kikuyu. Tukiyahusisha maoni haya na mawazo ya wataalamu kama vile Berlin (1997) ambaye ana msimamo kuwa lugha ndiyo taswira ya mawazo na nafsi ya taifa au jamii na kwamba mawazo yetu hayawezi kujitenga na lugha zetu, uamuzi wa kuandika kwa lugha ya Gĩkũyũ unadhihirika kuwa sio wa kiajali ila ni wa kimakusudi kutokana na mwamko wa kiitikadi ndani ya mwandishi kwa lengo la kuwasilisha tajriba zake katika lugha yake asilia kinyume na kuchangia lugha ya kigeni, kwa mfano Kiingereza, kama alivyokuwa akifanya hapo awali.

MT1 katika utafiti huu ni tafsiri kwa Kiswahili; lugha ya Kitaifa na ya Kiafrika. Tukizingatia tafsiri iliyotolewa katika MT1 kwenye mfano 1; *Tega Sikio,* tunapata kwamba mtafsiri ametumia mtindo wa ubinafsishaji ambapo ametafuta visawe kwa kifungu hiki cha Kikuyu katika lugha na fasihi simulizi ya Kiswahili. Hata hivyo, tafsiri hii sio linganifu kiuamilifu kwa kuwa kuna mtindo wa ufunguzi katika utambaji hadithi kwa Kiswahili ambao huenda mtafsiri angekopa baadhi ya sehemu yake na kuutumia katika muktadha huu. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| Mtambaji hadithi: | *Hadithi hadithi.* |
| Hadhira: | *Hadithi njoo!* |

Ukopaji huu ungezidisha uasilia katika MT1 inaposomwa kama fasihi ya Kiswahili,

kinyume na ilivyo sasa ambapo mtindo uliotumiwa kushughulikia tafsiri hii unazalisha kifungu ambacho hakina uhusiano na fasihi simulizi na hivyo unapoteza baadhi ya umbuji uliotumiwa na msanii katika MC. Hata hivyo, uteuzi huu wa kutumia maneno *Tega sikio* katika MT1 kisemantiki unaafiki maana iliyomo katika MC. Huenda mtafsiri aliteua maneno haya ama makusudi kwa nia ya kusahilisha mawasiliano katika MT1 au akawa hana umilisi wa kutosha katika nadharia ya tafsiri kumwezesha kutafuta tafsiri faafu kimaana na kiuamilifu. Licha ya kuwa tofauti kiumbuji na kiuamilifu katika tafsiri iliyotolewa zinaibua changamoto kwa ubora katika uteuzi wa ubinafsishaji, mtafsiri anafanikiwa kuwasiliana na kuifanya MC kuwa na sura ya kiasilia katika MT1.

Uamuzi huu unaweza kueleweka katika misingi ya baadaukoloni tukiangazia nafasi ya lugha ya Kiswahili katika muktadha halisi wa mtunzi; Kenya, ambapo Kiswahili sio lugha tu ya Kiafrika bali ni lugha ya taifa inayowaleta pamoja wananchi ambao waliwahi kutawaliwa na mkoloni. Licha ya ukaribu wa kiuhusiano baina ya utamaduni wa jamii ya Wakikuyu na Waswahili, na ukuruba unaobainika baina ya jamii hizi kutokana na ukweli kwamba jamii zote mbili ni za Kibantu, mtafsiri kwa kubinafsisha tafsiri yake anafanikiwa kujinasibisha na hadhira lengwa ya Kiswahili. Katika kufanya hivi anafanikiwa kujitambulisha kama mmoja wa washiriki katika jamii husika. Ukuruba huu ni muhimu katika jamii za baadaukoloni ambazo aghalabu hulenga kujivunia lugha na tamaduni zake badala ya kukweza lugha za kikoloni.

Tukirejelea MT2 ambayo ni tafsiri ya Kiingereza; *Devil on the Cross*, tunapata kwamba sehemu nzima ya utangulizi inayojitokeza katika MC na MT1 haipo. Udondoshaji huu tunadai kwamba ni wa kimakusudi. Hii ni kutokana na uamilifu wake kimtindo na kimaudhui katika riwaya nzima. Ili kuipa MT2 mtindo sawa mtafsiri sharti angetafsiri sehemu hii kwa kuwa licha ya kuwa ndiyo inatanguliza masimulizi katika riwaya hii, inatoa msingi wa maudhui na matukio katika riwaya nzima. Utangulizi katika MC sio tu sehemu ambayo ingedondoshwa kama mkakati wa tafsiri bali sharti ilikuwa ni uamuzi wa kimakusudi. Udondoshaji kama mkakati katika utekelezaji wa tafsiri hutumika pale ambapo; hakuna kisawe cha kuwakilisha dhana husika katika mfumo lengwa kiisimu na kitamaduni. Hata hivyo, kanuni ya kimsingi kuzingatiwa katika kutumia udondoshaji ni kwamba sehemu inayodondoshwa sharti isiathiri ukamilifu wa ujumbe katika matini tafsiri. Tukiangazia hali ya utangulizi katika MC na kudondoshwa kwake katika MT2 tunapata kwamba hakuna msingi wa kinadharia katika tafsiri wa kudondosha sehemu hii. Hivyo basi tunahitimisha kwamba udondoshaji huu ulikuwa ni tukio la kimakusudi kwa kuwa ni katika utangulizi ambapo msimulizi anatoa maelezo ya kimsingi yaliyochochea uandishi katika lugha ya Kikuyu na mazingira halisi ya utunzi wa riwaya hii. Aidha, sehemu hii inatoa maelezo ya msingi wa masimulizi yanayofuata. Masuala haya ni ya kimsingi katika ukamilifu na uelewekaji wa riwaya hii hivyo udondoshaji wake katika MT2 ni wa kimakusudi na huenda ulitekelezwa ili kutobainisha dhahiri baadhi ya masuala yaliyolenga hadhira ya MC pekee na kwa kiasi fulani hadhira ya MT1; yaani Waafrika huku ikitenga hadhira ya MT2.

Tukiangazia mfano mwingine wa usharabu kutoka kwa fasihi simulizi hasa mtindo wa ufunguzi tukirejelea vitendawili kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

**Mfano 2**

**MC:** *Ndaathii uu Ndathii uu!* Muturi akiuga
*Njira cia ategi*. Wangari akiugira Wariinga
*Aaca!*
*Oya kigacwa*
Njira cia aturi! *Gwata riingi*!
*Ndaagwata*
Ndathii uu ndaathii uu!
Njira cia aturi
*Aaca. Reehe kigacwa*
Oya
Njira cia aruti-a-wira. Gwata o riingi
Ndaagwata
Ndaathii uu ndaathii ndoreete gwa ituika
Njira cia aruti-a-wira
*Ii na aaca. Reehe kigacwa na ndigukugaca muno ni wamenya menya*
*Oya*
Njira cia aregi…na no cio cia aruti-a –wira… (Ukurasa wa 67) (Msisitizo wangu)

**MT1:** *"Napitia hizi na zile!"* Muturi akasema.
*"Njia za msasi!"* Wangari akamtegulia Wariinga.
"*La!"*
*"Chukua zawadi*."
"Njia za Wahunzi!" *Kitendawili tena!"*
*"Tega."*
"Napitia hizi na zile."
"Msasi."
"*La! Lete zawadi*."
"Chukua."
"Njia za wafanya kazi. Kitendawili tena."
"Tega."
"Napitia hizi na zile kuelekea mpakani."
"Njia za wafanya kazi."
"*Ndiyo na siyo. Lete zawadi! Lakini si kubwa kwa kuwa umetambua kidogo."*
*"Chukua*."
"Njia za wakatavu…hizo hizo ndizo njia za wafanya kazi… (Ukurasa wa

72-73) (Msisitizo wangu)

**MT 2**: *"I walk this way and that way!"* Muturi said.
*"the ways of hunters."* Wangari answered for wariinga.
*"No!"*
*"Take a forfeit!"*
"The paths of builders! *Answer another riddle!"*
"I walk this way and that way!"
"The path of builders."
"*No. Give me a forfeit." It's yours."*
"The paths of workers. Answer another." "I will."
"I walk this way and that way towards a revolution"
"The paths of workers."
"*Yes and no. You owe me a forfeit, but I won't take everything, for you got half the answer." "I accept that"*
"The answer is the paths of resistance…and those are the paths made by workers." (Ukurasa wa 68-69) (Msisitizo wangu)

Katika mfano huu, mwandishi wa MC amechota kutokana na dafina ya fasihi simulizi hususan kipera cha vitendawili miongoni mwa jamii ya Gĩkũyũ na kutumia mtindo wake katika MC. Kwa kufanya hivi, mwandishi anafanikiwa kuipa MC uasilia zaidi kwa hadhira yake kwa kuipa ladha ya kiasili katika jamii ya Gĩkũyũ hali inayoafikiana na mawazo ya Okara (1963) kwamba waandishi wa mataifa yaliyowahi kutawaliwa hususan Afrika aghalabu hujihusisha katika zoezi la kuandika fasihi simulizi yao kila wanapoandika fasihi hasa kimtindo na kwa kutegemea zaidi fasihi simulizi ya jamii zao.

Mfano 2 unasheheni diskosi ambayo ni ya kipekee katika utamaduni chanzi wa Gĩkũyũ ambapo usemaji wa kutumia mafumbo na vitendawili ni dhihirisho la busara na ufasaha au ukomavu katika mawasiliano. Mtindo huu unaipa matini hii uasilia ambao hata unapotafsiriwa bado utasheheni vipengele vya utamaduni chanzi.

Aidha, kupitia matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika MC, mwandishi anafanikiwa kuiwasilisha fasihi simulizi ya jamii yake kwa hadhira pana kupitia uandishi na kwa wakati ule ule kuihifadhi. Uamuzi huu unaingiliana na msimamo wa baadaukoloni ambapo waandishi wa fasihi katika kipindi hiki wanaaminika kufanya maamuzi ya kimakusudi kukweza utamaduni wao asilia wa Kiafrika kwa kuuwasilisha katika maandishi na kwa jinsi hiyo kuusambaza kwa hadhira pana zaidi na kuuhifadhi.

Matumizi ya fasihi simulizi ya Kiafrika katika uandishi wa fasihi ya baadaukoloni yanatokana na maamuzi ambayo pakubwa huchochewa na misimamo ya kiitikadi. Watunzi kupitia kwa uandishi wa fasihi wanatumia vipawa vyao kuupa utamaduni wao asili; ambao awali ulichukuliwa kuwa duni, hadhi sawa na utamaduni wa mkoloni ambao awali ulichukuliwa kuwa babe na wenye hadhi zaidi. Juhudi kama hizi za kimakusudi ni sehemu ya juhudi pana za kutafuta kujikomboa kutokana na ubepari wa kiisimu na kitamaduni.

Tukiangazia jinsi mtindo huu wa kutoa vitendawili ulivyotafsiriwa kwa Kiswahili na Kiingereza katika MT1 na MT2 mtawalia, inabainika kuwa mtafsiri amedumisha uaminifu kwa mtindo asilia katika MC wa jamii ya Gĩkũyũ na kwa jinsi hiyo, mitindo inayodhihirika katika MT1 na MT2 ni zao la uibuaji wa ugeni ambapo matini tafsiri inakosa uasilia katika mfumo wa lugha na utamaduni lengwa.

Kwa mfano, tukiangazia sehemu ya tafsiri katika MT1:

**MC:** *Ndaathii uu Ndathii uu!*
*Njira cia ategi*

*Aaca!*
*Oya kigacwa*

**MT1**: Napitia hizi na zile!
Njia za msasi!
La!
Chukua zawadi

Katika tafsiri hii, tunapata kuwa mtafsiri amepuuza mtindo wa vitendawili katika Kiswahili ambao ni:

*Kitendawili*
*Tega…*

Badala yake amejaribu kutoa tafsiri sisisi kwa kitendawili kilichopo katika MC. Kwa jinsi hii, anaishia kuibua mtindo ambao si wa kawaida, mtindo wa kigeni, katika mfumo wa MT1.

Nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri inashikilia kuwa, katika kutafsiri fasihi iliyoandikwa kwa lugha za Kiafrika, aghalabu panazalishwa msimbo ambao hauna uasilia katika utamaduni na lugha lengwa. Mawazo haya, japo yalitolewa kurejelea lugha za kikoloni kama vile Kiingereza yanabainika hapa kuwa kweli kwa tafsiri iliyotolewa kwa Kiswahili kutokana na ukiushi unaodhihirika kimtindo. Inaelekea kuwa katika muktadha huu alichonuia mtafsiri, ambaye pia ndiye mwandishi wa MC, ilikuwa ni kuuhawilisha mtindo wa kigeni katika Kiswahili kwa lengo la kuibua ugeni na kumpa msomaji wa Kiswahili nafasi ya kutagusana na mtindo mbadala kutokana na jamii ya Gĩkũyũ. Uchukulio huu unapata mashiko tukizingatia maoni ya Schleiermacher (1992), kwamba katika zoezi lolote la tafsiri, hasa tafsiri ya matini ya kifasihi, mtafsiri aghalabu ana chaguzi mbili:

a. Ama mtafsiri asimtatize mwandishi kadri iwezekanavyo na amsogeze

msomaji wa MT karibu na mwandishi wa MC au,

b. Asimtatize msomaji wa MT na amsogeze mwandishi wa MC karibu na msomaji wa MT kadri iwezekanavyo.

Chaguzi hizi anazotoa zinafungamana na mielekeo ya Venuti (1995) ya uibuaji wa ugeni na ubinafsishaji mtawalia. Hata hivyo, katika kutafsiri fasihi, uchaguzi wa kudumisha uaminifu kwa mwandishi wa MC na hivyo lugha chanzi na utamaduni chanzi huelekea kupendelewa pakubwa. Hali hii ndiyo imesheni katika muktadha huu ambapo msomaji wa MT1 ameonjeshwa utamaduni chanzi kutokana na mwelekeo wa uibuaji ugeni uliotumiwa katika kutafsiri kifungu kilichorejelewa katika mfano 2.

Mbinu ya uibuaji ugeni iliyotumika hapa inaishia kumfanya msomaji wa MT1 kubaini moja kwa moja kuwa matini hii ama si asilia au mwandishi hana umilisi katika lugha ya Kiswahili na utamaduni unaoambatana na lugha hii.

Isitoshe, tukiangazia sehemu ya kitendawili ambapo aliyetegewa anakosea jibu:

**MC:** *Aaca!*
*Oya kigacwa*

**MT1:** La!
Chukua zawadi

Tafsiri iliyotolewa katika MT1 si linganifu kiuamilifu ila imetoa tafsiri ya moja kwa moja ya kisemantiki. Tukiangazia dhima za tafsiri kwa kuzihusisha na uainisho wa dhima aliotoa Merton (1968) wa: [11]uamilifu dhahiri na [12]uamilifu usodhahiri,

---

[11] Imetumika hapa kama tafsiri ya *Manifest function.*

ambapo uamilifu dhahiri wa tafsiri ni kuwezesha mawasiliano au kuwa daraja baina ya lugha mbili huku uamilifu wake usodhahiri ukiwa ni wa kiitikadi au kisiasa, kiuchumi na kitamaduni, huenda uteuzi uliofanywa ni wa kimakusudi kutokana na uamilifu usodhahiri wa kiitikadi. Vinginevyo, tafsiri mwafaka zaidi katika mfumo wa Kiswahili ingalikuwa ni:

*Nipe Mji*

Badala ya

*Chukua zawadi*

Uteuzi huu unibua masuala mawili;

a. Uibuaji wa ugeni kwa kukiuka mtindo asilia katika mfumo wa MT1 kutokana na,

b. Upungufu wa ubora, hasa kimawasiliano, katika tafsiri inayotolewa.

Msomaji wa MT1 anapokumbana na kipengele hiki iwapo ana umilisi katika lugha ya Kiswahili na fasihi simulizi ya Kiswahili bila shaka atahisi kuwa mtindo uliotumika hapa si wa kawaida ila una ukiushi unaovuruga mpangilio wa kawaida. Hali hii aghalabu itamfanya ama kutilia shaka umilisi wa mwandishi wa MT1 au kuwaza kwa nini hali hii ikatokea. Japo ubora wa tafsiri iliyotolewa unatiliwa shaka, hasa tukizingatia kuwa lugha husika si ya kikoloni ila ni ya Kiafrika na kitaifa katika muktadha wa matini hizi, ukiushi wa mtindo katika tafsiri hii unazalisha ugeni katika MT1 na kwa jinsi hiyo kupanua mawanda ya utamaduni wa MC.

[12] Imetumika hapa kama tafsiri ya *Latent function.*

Tukiangazia tafsiri iliyotolewa kwa kifungu katika mfano huu kwa Kiingereza katika MT2, hali ya uibuaji wa ugeni inadhihirika bayana.

**MC:** *Aaca!*
*Oya kigacwa*

**MT2:** *"No!"*
*"Take a forfeit!"*

Kwanza, mtafsiri hajazingatia mtindo wa utegaji wa vitendawili katika lugha na utamaduni wa Kiingereza na badala yake amejikita kwa tafsiri sisisi ya mtindo uliotumika katika MC. Tafsiri hii sisisi inaafikiana na maelezo ya wataalamu kama vile, Okara (1963) anayeeleza kwamba uandishi wa fasihi ya Kiafrika aghalabu husheheni matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi na kwamba uwasilishaji wa vipengele hivi katika lugha za kikoloni utafanikiwa tu iwapo utafanyika sisisi. Hii ina maana ya kutumia mbinu ya uibuaji ugeni katika kushughulikia dhana za kitamaduni kwenye matini za baadaukoloni ambapo watafsiri aghalabu hutoa tafsiri sisisi. Matokeo ya maamuzi haya ni uzalishaji wa lugha ambayo japo maneno ni ya lugha ya kikoloni, katika muktadha huu Kiingereza, yaliyomo bila shaka sio sehemu ya utamaduni wa lugha hii. Hivyo basi msomaji wa MT2, kama ilivyoelezwa kwa msomaji wa MT1, atakumbana na mtindo usio wa kawaida katika mfumo wa lugha yake na kwa jinsi hiyo kutambua na kufahamu mtindo tofauti wa kutega vitendawili ambao unatokana moja kwa moja na mtindo uliotumiwa katika MC.

Licha ya kuwa hali kama hizi huathiri ubora wa matini tafsiri na uwezo wake wa kuwasiliana, wanabaadaukoloni wanaamini kuwa kwa kudumisha mitindo ya

kitamaduni ya lugha chanzi za kiasili katika tafsiri zao kwa lugha za kikoloni, wanaisambaza na kuikweza kihadhi na kwa jinsi hiyo kuipa uwezo sawa na mitindo ya tamaduni babe za waliokuwa wakoloni. Aidha, tukizingatia maoni ya Benjamin (1923) kwamba tafsiri ni nyenzo ya kuhuisha MC, kuipa uhai zaidi kwa kupanua mawanda ya usomaji, tunaweza kudai kuwa MC katika muktadha huu riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* iliyoandikwa kwa lugha ya Kikuyu na kutegemezwa kwa utamaduni wa jamii ya Gĩkũyũ, inapata uhai mpya kwa kutafsiriwa katika lugha ya Kiingereza hali inayoiwezesha kuwafikia watu wengi zaidi na kusambaza vipengele vya kitamaduni vilivyomo katika matini kwa hadhira pana zaidi. Juhudi hizi zaidi ya kuhifadhi utamaduni wa LC katika maandishi zinasaidia kuusambaza na kuukweza kwa viwango vya juu zaidi ikilinganishwa na ilivyokuwa katika MC.

### 3.2.2 Tafsiri za Methali

Kipengele kingine cha utamaduni kinachojitokeza katika sehemu ya utangulizi na kwingine katika MC ni kipera cha methali. Kwa mfano:

**Mfano 3 (Kutoka sehemu ya Utangulizi)**

**MC:** *Kiambagio maai ni ihii nyene*

**MT1:** Mcheza kwao hutuzwa

**MT2: ******

Katika mfano huu, methali ya Kikuyu *Kiambagio maai ni ihii nyene* imetafsiriwa kwa Kiswahili kuwa *Mcheza kwao hutuzwa.* Hakuna tafsiri ya Kiingereza kutokana na kutokuwepo kwa sehemu nzima ya utangulizi katika MT2. Hata hivyo,

tukilinganisha methali ya MC na tafsiri yake katika MT1 inabainika kuwa kwa mara nyingine, mtafsiri amependelea mbinu ya ubinafsishaji kwa kutafuta methali linganifu kimaana na kiuamilifu katika mfumo wa lugha na utamaduni wa MT1 ikilinganishwa na methali katika MC. Uamuzi huu pakubwa unaweza kuelezewa katika ngazi mbili; ukaribu wa kitamaduni baina ya mfumo wa MC na MT1, pamoja na uamuzi wa kimakusudi wa mtafsiri kutaka kuifanya MT1 kuwa na uasilia wa kiisimu na kitamaduni hivi kwamba hadhira yake haitaweza kubainisha moja kwa moja kwamba matini hii ni tafsiri moja kwa moja.

Hata hivyo, tukiangazia methali nyingine katika MC na jinsi zilivyohawilishwa katika MT1 na MT2 kama vile;

**Mfano 4**

**MC:** *Mbeu ti ya Kinya kimwe, kaba kugarurira*. (Ukurasa wa 14)
**MT1:** Pombe si ya kitoma kimoja, badilisha! (Ukurasa 17)
**MT2:** *The seeds in a gourd are not all of the same type.* (Ukurasa wa 15)

Katika tafsiri hii, suala la ubora linapata utata kutokana na kuvurugwa kwa maana za methali. Methali hii imetumiwa katika muktadha ambamo Kareendi[13] anashauriwa na wenzake haja ya kuwa na mpenzi wa ziada, kando na Kamoongonye. Ushauri huu unalenga kumshawishi kukubali uhusiano na Boss Kihara japo hatua hiyo si ya busara na inatokana na wivu wanaomwonea Kareendi. Matumizi ya methali *Mbeu ti ya Kinya kimwe, kaba kugarurira* katika MC ni ya kipekee kwa kuwa yanalenga kuwasilisha ujumbe wa haja ya kutalii hali tofauti iwe ni kimapenzi au katika

[13] Ni mhusika kutokana na mojawapo ya masimulizi katika jamii ya Gikuyu.

miktadha mingine. Ujumbe huu umefumbatwa katika methali hii inayotokana na himizo kwa wakulima kwamba katika upanzi wa vitoma, wanapswa kubadili mbegu ili kupata iliyo bora zaidi badala ya kutegemea mbegu za kitoma kimoja tu.

Tafsiri inayotolewa katika MT1 kuwa *Pombe si ya kitoma kimoja, badilisha!* Inatekeleza dhima sawa na kuwasilisha maana inayokaribiana na maana iliyokusudiwa katika MC ila sio kwa ulinganifu kamili. Mtafsiri anabadili vipengele vya kitamaduni na vya kietimolojia vya methali kutoka kwa ukulima katika MC hadi kwa sherehe na unywaji pombe katika MT1. Hata hivyo, maana inayowasilishwa na methali hizi inakaribiana. Hali ni tofauti tunapoangazia tafsiri inayotolewa katika MT2 ambapo, licha ya kuwa maneno kama vile *Kinya (MC), Kitoma (MT1)* yametafsiriwa kwa njia sahihi katika MT2 kuwa *gourd*, maana inayowasilishwa katika tafsiri ya methali hii kwa Kiingereza *the seeds in a gourd are not all of the same type* inapotosha maana iliyokusudiwa katika MC. Hali hii inatokana na kosa la tafsiri kwa kutofasili vyema maana ya methali hii. Isitoshe, tafsiri hii, japo tunaweza kuiangazia kama jaribio la uibuaji ugeni, inakosa kuwasiliana kwa njia ipasayo na hivyo kuathiri ubora wa MT2 kimaana.

Tukifanya zoezi la tafsiri unyume kwa methali hii kutoka Kiingereza hadi Kikuyu, yaani;

| **Kiingereza** | **Kikuyu** |
|---|---|
| *The seeds in a gourd are not all of the same type* | *Mbeu cia kinya itihanaine ciothe* |

Maana msingi inayojitokeza katika Kikuyu ni tofauti na ile iliyodhamiriwa katika methali asilia katika MC. Kwa mintarafu hii, tafsiri iliyotolewa hapa haitoshelezi katika kiwango cha maana, uamilifu na hata mawasiliano.

Katika tafsiri za baadaukoloni, watafsiri wakati mwingine wanaelekea kuupa utamaduni chanzi mchomozo zaidi ya mawasiliano hivi kwamba uteuzi wanaofanya katika kuhawilisha dhana, hasa za kitamaduni, kutoka lugha chanzi hadi kwa lugha lengwa unaongozwa zaidi na itikadi zao na haja ya kuleta ukombozi wa kiisimu-kitamaduni zaidi ya kuumba upya matini ili iwasiliane. Katika fasihi aghalabu lengo kuu huwa ni kuhifadhi roho na ladha ya matini chanzi kiumbuji zoezi ambalo husheheni uandishi upya. Hata hivyo, katika mwelekeo wa baadaukoloni hali inabadilika ambapo lengo kuu, kama ilivyo katika muktadha wa matini zilizoshugulikiwa katika utafiti huu, ni kuukweza utamaduni chanzi kwa kuutafsiri sisisi kwa njia inayoibua ugeni.

Tukiangazia methali nyingine katika matini hizi kama vile:

**Mfano 5**

**MC:** *Kaihu gacangacangi gatigaga kwao gugithinjwo.* (Ukurasa wa 14)
**MT1:** Mtaka yote kwa pupa hukosa yote. (Ukurasa wa 17)
**MT2:** *A restless child leaves home in search of meat just as a goat is about to be slaughtered.* (Ukurasa wa 15)

Inabainika kuwa mtafsiri hakuwa na mwelekeo mmoja aliotumia katika kuzishughulikia methali katika matini hii. Kuna kuchanganya baina ya ubinafsishaji na uibuaji ugeni hali inayoathiri ubora wa tafsiri iliyotolewa katika baadhi ya

miktadha. Katika methali hii kwa mfano, *Kaihu gacangacangi gatigaga kwao gugithinjwo* ni methali inayotumiwa katika jamii ya Gĩkũyũ kusisitiza haja ya kuwa na subira. Maana msingi ya methali hii ni kuwa, nguchiro asiyetulia huondoka nyumbani kwao wakati mbuzi anachinjwa. Kimsingi, nguchiro ni wala nyama na wakati mnyama anachinjwa kuna nyama ndogondogo zinazosalia machinjioni na hivyo kuwa mlo kwao. Vinginevyo, nguchiro huishi kwa kusaka mchwa, ndege, panya, mizoga na wakati mwingine kuku. Tafsiri iliyotolewa katika MT1; *Mtaka yote kwa pupa hukosa yote* inaibua dhana ya ulafi. Hata hivyo, tunaweza kudai kwamba tafsiri hii inaafiki kiuamilifu hasa katika muktadha wa matumizi katika matini na ina uasilia katika lugha ya Kiswahili. Hivyo mtafsiri kwa kutumia ubinafsishaji amefanikiwa sio tu kuwasilisha maana iliyokusudiwa katika MC bali pia amedumisha usanii wake.

Tafsiri iliyotolewa katika MT2;

> *a restless child leaves home in search of meat just as a goat is about to be slaughtered,*

mtafsiri ametumia maelezo ili kuwasiliana. Japo kuna ulinganisho unaoibua dhana ya kitashbihi, maelezo haya ni ya kigeni katika utamaduni wa Kiingereza hasa tunaporejelea kipengele cha mbuzi kuchinjwa. Maelezo haya yanaafiki utamaduni na uhalisia wa jamii ya Gĩkũyũ zaidi ya utamaduni wa Mwingereza. Hata hivyo, licha ya ugeni katika ngazi hii, mtafsiri angalau amefanikiwa kuwasiliana na kudumisha maana iliyokusudiwa katika MC.

Kwa mfano, methali ifuatayo:

**Mfano 6**

**MC:** Nyamu ikuumagirira hari muumbire igeetikira *kugariurwo o uria iriigariurwo ni muumbire ta mutura wa ihii*. (Pg 47) (Msisitizo wangu)

**MT1:** Mnyama daima huwa mtumwa wa maumbile. (Ukurasa wa 51)

**MT2:** Animals stoop low before nature, allowing themselves to be turned this way and that by her, *just as sausages are turned casually in the fire by little boys.* (Ukurasa wa 48) (Msisitizo wangu)

Katika MC kuna matumizi ya methali katika sehemu iliyoandika kwa herufi za mlazo japo imepanuliwa. Methali kamili aghalabu huwa ni *Kugariura ta Mutura wa Ihii* na sana sana hutumiwa kurejelea hali ambapo mtu, kitu au hali inaathiri mtu, kitu au hali nyingine kwa kuikosesha utulivu na amani. Inatokana na utamaduni wa Gĩkũyũ ambapo wakati mnyama kama vile mbuzi anachinjwa, kuna nanma maalum ya kuandaa baadhi ya nyama kuunda kile wanaita [14]*mutura.* Zoezi hili huhitaji ustadi na haliachiwi wavulana wadogo (*ihii*) kwa kuwa watauharibu kwa kuugeuzageuza jambo linaloweza kusababisha kupasuka kwa mfuko wenye nyama na au kuzuia kuiva ipasavyo kwa utaratibu.

Katika MT1, mtafsiri ameepuka sehemu hii inayofungamana na utamaduni wa Gĩkũyũ kwa kuidondosha. Udondoshaji huu unaambatana na mahitaji ya mkakati wa undondoshaji kama sehemu ya utekelezaji wa tafsiri ambapo maana msingi haiathiriki. Hata hivyo katika MT2, mtafsiri ametumia dhana mbadala, *sausage*, katika utamaduni lengwa kama tafsiri ya dhana *mutura* kisha akaongezea maelezo kuwa hugeuzwa bila mpango na wavulana wadogo. Uteuzi wa dhana *sausage*

[14] Mfuko aghalabu wa utumbo wa ng'ombe ambao hujazwa nyama iliyosagwa na kukaangwa wakati mwingine ikichanganywa na damu.

unaweza kufasiliwa kuwa kisawe cha kiuamilifu katika utamaduni lengwa japo sio linganifu kikamilifu. Hata hivyo, katika muktadha huu wa matumizi, dhana hii kimaana na kimatumizi inaafiki japo inahitaji kutegemezwa kwa maelezo ya ziada yanayotolewa katika MT2.

Katika hali kama hii, mwandishi wa MC amerejelea utamaduni na matumizi ya lugha ya jamii ya Gĩkũyũ na kuwezesha mawasiliano yake bila tatizo. Hata hivyo anapata ugumu katika kutafsiri dhana na maana inayoambatana na dhana husika katika MT2 moja kwa moja. Kwa kutumia ubinafsishaji, maana haijitokezi bayana ila inahitaji maelezo ya ziada kwa kuwa dhana zilizotumiwa katika MC zimefungamana kwa karibu sana na utamaduni chanzi hivi kwamba haziwezi kupata visawe linganifu kileksia, kimaanana kiuamilifu katika utamaduni mwingine. Huenda ndio maana sehemu hii ikadondoshwa katika MT1 kwa kuwa hakuna kisawe cha ama dhana *mutura* wala *sausage* katika utamaduni wa Kiswahili. Iwapo mtafsiri angetaka kuwasilisha maana kikamilifu na kudumisha umbuji katika muktadha huu, uibuaji wa ugeni kwa kukopa dhana ya kigeni, *mutura* kisha akatoa ufafanuzi kwa kutumia tanbihi ingekuwa bora zaidi. Asingefanikiwa kuwasiliana tu bali angefanikiwa katika kuwasilisha utamaduni chanzi kwa njia iliyo bayana zaidi katika Kiingereza. Vinginevyo, angeitumia dhana ya *mutura* na kuiacha hivyo na kwa jinsi hiyo kumfikirisha msomaji wa kazi yake katika MT2. Hali hii hata hivyo, japo imejitokeza katika fasihi ya Kiafrika kama vile katika kazi za Chinua Achebe

anaporejelea dhana kama vile *iroko* bila kutoa ufafanuzi aghalabu inakwaza mawasiliano.

**Mfano 7**

**MC:** *Mwigerekanio wariire ciura matina*. (Ukurasa wa 6)
**MT1:** Njia mbili zilimshinda fisi. (Ukurasa wa 7)
**MT2:** *Aping others cost the frog its buttocks*. (Ukurasa wa 6)

Tukirejelea methali iliyoonyeshwa kwenye mfano 7, tunapata kwamba imetokana na ngano, hurafa, katika utamaduni wa MC. Kisa kinachosimuliwa ni cha jinsi mwana wa chura alivyopendezwa na fahali alivyokuwa mkubwa na mwenye misuli. Anaporejea nyumbani na kumsimulia mamaye mama anajidai kuwa ana uwezo wa kuwa mkubwa kumshinda fahali huyo. Alianza kujipulizia hewa na kujitanua hadi mwishowe akapasuka mkiani. Methali hii aghalabu hutumiwa kuonya dhidi ya kuiga tabia na mienendo ya wengine kiholela.

Katika muktadha wa matumizi kwenye MC, mwandishi ameitumia methali hii kuonya dhidi ya tabia alizokuwa nazo mhusika Wariinga za kuiga mitindo na tabia za kimagharibi kwa kukinai urembo na mitindo yake asili ya Kiafrika. Mkengeuko wa aina hii ni mojawapo ya migogoro inayoangaziwa katika baadaukoloni ambapo waliotawaliwa wanaiga tabia na mienendo ya watawala wao kilugha, kimavazi, kitamaduni na wakati mwingine hata wanajaribu kuiga rangi ya ngozi kwa kutumia dawa.

Kutojitambua na kuiga tabia za wengine kwa kuasi za mtu binafsi ndiko Waswahili walieleza kwa methali *Mwacha mila ni mtumwa.* Utumwa huu ndio mwandishi

anapinga kwa kutahadharisha madhara yanayoweza kutokana na uigaji bila kuchuja kwa kutumia methali iliyorejelewa katika mfano 7. Tafsiri inayotolewa kwa methali hii katika MT1, ya Kiswahili, si faafu hasa kiuamilifu na kimaana. Kama Baker (1992) anavyoeleza, mikakati faafu katika kutafsiri methali ni ule wa kutumia methali linganifu katika mfumo wa lugha lengwa ambayo inaafiki methali iliyotumiwa katika MC kimaana na kiuamilifu. Farahani na Ghasemi (2012) wanakubaliana na maoni haya ambapo wanaeleza mikakati inayopendelewa zaidi katika kutafsiri methali ni ama matumizi ya maelezo au kutafuta methali linganifu katika mfumo wa lugha pokezi. Hali hii ingefaa katika MT1 ambapo mtafsiri angetumia methali linganifu kimaana na kiuamilifu. Methali ya *Njia mbili zilimshinda fisi* inaibua maana tofauti na maana iliyokusudiwa katika MC. Katika MT1 maana msingi inayotokana na tabia hii ya fisi kutaka kufuata njia zote mbili ni ulafi. Hii ni kinyume na mkengeuko ambao unadhihirika kutokana na tabia ya kuwaiga wengine kiholela kama alivyofanya chura katika methali ya MC. Hata hivyo, kiumbuji, methali iliyotumiwa katika MC na ile iliyotumiwa katika MT1 zinafanana. Zote zina asili katika ngano za jamii husika. Kisa ambapo methali hii imetolewa kinasimulia kwamba siku moja fisi alikuwa akizurura akitafuta mlo kama ilivyokuwa kaaida yake. Alifuata harufu ya chakula iliyojaa hewa hadi alipofika njia panda. Kwa kuwa hakujua harufu ile ilitokea njia ipi, aliamua kuzifuata njia zote kwa pamoja, miguu miwili njia ya kulia na miguu miwili njia ya kushoto. Hali hii ilimshinda. Baadhi ya viishio vya kisa hiki huonyesha kwampa fisi alipasuka kutokana na tamaa yake. Licha ya kuwa methali ya *Njia mbili zilimshinda fisi*

hutumiwa kuonya dhidi ya tamaa na ulafi, katika muktadha huu wa matumizi, methali hii imefaulu kuakisi hali ya mkengeuko inayodhihirika miongoni mwa Waafrika waliotawaliwa na wakoloni ambapo wanajaribu kuiga Uzungu ilhali wao ni Waafrika. Njia hizi mbili hawawezi kuzimudu na zitaishia kuwadhuru.

Tukiangazia tafsiri ya methali hii katika MT2, mtafsiri ametumia mkakati wa tafsiri sisisi kutoka MC kupata *Aping others cost the frog its buttocks* kwa Kiingereza. Hali hii inaibua ugeni hasa katika ngazi ya asili ya methali husika. Inaelekea kuwa ni tafsiri sisi ya methali iliyotumiwa katika MC. Hali hii imejadiliwa na Bandia (2014:53) anapoeleza kuwa;

> Mitindo ya usimulizi ya kiasili kama vile matumizi ya methali na maelezo ya hali za kitamaduni pamoja na diskosi za kiethnografia na kitamaduni hutumiwa kama maudhui ya kimsingi katika fasihi ya baadaukoloni ili kuashiria ukiushi na uwakilishi wa kitamaduni…Kando na kuimarisha usanii wa riwaya ya Kiafrika na kuashiria upekee wake, matumizi ya usanii wa masimulizi huzalisha diskosi mseto ambayo huhitaji mkakati wa usomaji – kama-tafsiri… *(Ty)*

Katika nukuu hii, inabainika kuwa matumizi ya methali za Kiafrika katika fasihi ya baadaukoloni katika mazingira ya Kiafrika sio suala la kipekee ila ni la kawaida ambalo aghalabu hutumiwa kimakusudi. Tafsiri na uwakilishi ambao hufanywa katika lugha za kigeni kama vile Kiingereza katika muktadha wa MT2 hulenga sio tu kutoa ladha ya Kiafrika kwa matini zinazozalishwa bali pia kuzalisha kile kinachorejelewa hapa kama diskosi mesto, yaani matini ambayo haina uasilia katika lugha tafsiri licha ya kuwa inaandikwa kwa maneno ya lugha husika. Katika mfano huu, maneno *Aping others cost the frog its buttocks* ni ya Kiingereza. Hata hivyo,

jinsi yalivyotumiwa katika MT2 kama methali, hayana uasilia kama ilivyojadiliwa katika kubainisha chanzo cha methali hii katika utamaduni wa Gĩkũyũ.

Hali hii japo ya kimakusudi katika muktadha wa baadaukoloni, wakati mwingine inaishia kuathiri uelewekaji wa maana iliyowasilishwa. Kwa mfano, tunapoitafakari methali kama kifungu cha maneno kinachowasilisha ukweli fulani unaotokana na ama uhalisia wa kawaida au tajriba, aghalabu za kitamaduni kwa njia ya mafumbo, mfano uliotolewa hapa unapata ukweli wake kutokana na tajriba ya kitamaduni, hususan fasihi simulizi katika jamii ya Gĩkũyũ. Tafsiri iliyotolewa katika MT1 inaafiki maelezo sawa na haya. Hata hivyo katika tafsiri ya Kiingereza, hali hii haijadumishwa wala kutimizwa katika MT2 jambo linaloathiri uelewekaji wake na kuashiria kwamba ni kifungu kisichokuwa na uasilia katika muktadha wa Kiingereza na kwa jinsi hiyo ni cha kigeni. Ufasili wa methali iliyotumiwa katika MC na MT1 katika mazingira ya fasihi simulizi ya Gĩkũyũ na Kiswahili mtawalia unatoa muktadha wa uelewekaji wa ujumbe uliomo. Hali hii haipo katika MT2 na hadhira yake huenda isipate ujumbe uliofumbatwa katika methali hii kikamilifu.

### 3.2.3 Tafsiri za Maneno Yanayofungamana na Utamaduni

Tunaweza kuangazia lugha kama mfumo unaotumiwa kuunganisha mawazo ambayo hayawezi kuonekana, kugusika au kusikika kwa kutumia sauti nasibu zinazowakilishwa kupitia usemi au maandishi katika mawasiliano miongoni mwa kundi maalum la watu au jamii. Hii ina maana kuwa katika kila lugha, tunapata sauti tofauti zenye kubeba maana tofauti kabisa. Katika kutafsiri, mtafsiri aghalabu

hutwikwa jukumu gumu la kuhawilisha dhana zinazowakilishwa kwa kutumia lugha kutoka mfumo mmoja hadi mfumo mwingine wa pili. Zoezi hili kama anavyoeleza Jakobson (1959, 2001) haliwezi kufanikiwa kwa asilimia mia moja kimsingi kutokana na tofauti za kimfumo baina ya lugha na jamii. Licha ya uchangamano wa lugha, katika ngazi za kimsingi tunaweza kuanisha maneno ambayo huwasilisha maana dhahiri zinazojisimamia.

Kipengele cha kimsingi cha kuzingatia katika utekelezaji wa tafsiri ni maana. Maana hii aghalabu hutokana na maneno yaliyosukwa pamoja kuwasilisha maana moja kamilifu. Hivyo basi, japo hatutafsiri fahiwa za kimsingi za kila neno kila mara, fahiwa hizo ni muhimu katika zoezi lolote la tafsiri hasa kutokana na tofauti za kitamaduni na hivyo za kimatumizi zinazoshughulikiwa katika tafsiri.

Tukirejelea matini ya *Caitaani Mutharaba-ini* (MC) na tafsiri zake MT1 na MT2, tunatambua kuwa mwandishi ambaye pia ni mtafsiri alihitajika kuchakata matini yake katika lugha tatu, na hivyo tamaduni tatu, tofauti. Hivyo basi, suala la upekee wa baadhi ya maneno hasa yaliyofungamana na utamaduni wa MC ni la kimsingi katika kushughulikia tafsiri hizi na athari za kitamaduni katika tafsiri pamoja na jinsi tafsiri ilivyoshughulikia upekee wa kitamaduni wa dhana zinazowakilishwa na maneno husika. Kwa mfano:

**Mfano 8 (Kutoka sehemu ya Utangulizi)**

**MC:** *Ngaati*
**MT1:** *Wasaliti (Ngaati)*
**MT2:** ****

Neno *Ngaati* limetumika katika MC kwa maana hasi. Ni neno lililotumika na jamii

ya Gĩkũyũ kurejelea wenzao walioshirikiana na wakoloni katika jamii ya Gĩkũyũ. Neno hili limetokana na utohozi wa neno home guard ambayo ni dhana iliyotumiwa kurejelea polisi wa Kiafrika walioajiriwa na wakoloni kulinda miji yao. Tukiangazia muktadha wake kihistoria, polisi hawa walikuwa dhalimu na katili kwa Waafrika wenzao. Aidha, walitumika katika kukabiliana na wapiganaji wa Mau Mau pamoja na kutumika wakati mwingine kama majasusi katika utawala wa kikoloni na hivyo walichukuliwa kuwa wasaliti na maadui wa jamii iliyokuwa inadhulumiwa.

Matumizi ya neno *Ngaati* katika MC ni ya kimakusudi na yanalenga kuibua hisia za usaliti na ukosefu wa uzalendo kwa jamii na kwa taifa kwa ujumla. Mtazamo hasi wa wanajamii wazalendo dhidi ya wanajamii wasaliti walioshirikiana na utawala wa kikoloni ni kielelezo cha migogoro katika jamii za baadaukoloni. Historia ya vita vya Mau Mau hasa kutoka mtazamo wa wenyeji wa Gĩkũyũ imewasawiri wote waliokuwa *Ngaati* kama watu waliouza nchi yao, urithi wao na jamii yao kwa manufaa ya kibinafsi. Hivyo basi, neno hili linapotumika katika *Caitaani Mutharaba-ini*, linawasilisha maana hizi zote kwa hadhira lengwa. Kwa mintarafu hii, mtafsiri katika MT1 anapolitafsiri neno *Ngaati* kuwa *Wasaliti*, amefanikiwa kuhawilisha maana msingi iliyokusudiwa katika MC. Hata hivyo, kiwango cha usaliti na uzito wa hisia hasi dhidi ya wasaliti hawa si dhahiri. Neno wasaliti linakosa usuli wa kitamaduni na kihistoria wa neno *Ngaati* ambao ni muhimu katika kukamilisha maana iliyomo katika MC. Hali hii inaathiri ukamilifu wa ujumbe hasa katika kiwango cha athari kwa hadhira lengwa.

Licha ya baadhi ya misimamo ya wasomi kama vile Okara (1963) kuwa njia ya kipekee ya kufanikisha uhawilishaji wa dhana zinazofungamana na utamaduni kutoka lugha chanzi hadi lugha za kigeni ni kutoa tafsiri sisisi kwa dhana husika, katika muktadha wa mfano huu inakuwa vigumu kueleza uteuzi aliofanya mtafsiri katika MT1. Matumizi ya dhana *Ngaati* katika MT1 japo kwa mabano ikiandamana na tafsiri *Wasaliti* ni jaribio la kuhawilisha dhana ya kiasili kutoka Kikuyu hadi Kiswahili japo haichangii uelewekaji. Tunapozingatia kwamba hata katika lugha ya Kikuyu hii sio dhana ya kiasili ila imetokana na utohozi kutoka Kiingereza, inakuwa vigumu kufasirika katika Kiswahili na hivyo ujumuishwaji wake unachangia tu kuibua ugeni bali hauna thamani yoyote kimaana.

Baadhi ya maneno yaliyotumika katika MC yanarejelea dhana ambazo zinafungamana na utamaduni wa Gĩkũyũ hususan fasihi yake simulizi kwa mfano:

**Mfano 9**

**MC:** *Gĩcaandĩ* (Ukurasa wa 1)
**MT1:** *Gĩcaandĩ* (Ukurasa wa 4)
**MT2:** *Gĩcaandĩ* (Ukurasa wa 1)

*Gĩcaandĩ* kwa upande mmoja ni dhana inayotumiwa kurejela kipera cha fasihi simulizi katika jamii ya Gĩkũyũ kinachoakisi kilele cha ulumbi na balagha katika jamii hii. Aghalabu husheheni mafumbo na huwasilishwa kwa mtindo wa majibizano kama ilivyo kwa ngonjera. Wahusika, ambao huitwa waimbaji, hufumbiana mafumbo hadi wakati ambapo mmoja wao atashindwa kufumbua fumbo lililopo na hivyo mshindi kupatikana. Kwa


kawaida uiambaji wa *Gĩcaandĩ* huwa mrefu wenye beti zaidi ya mia moja hamsini kwa kutegemea umahiri wa waimbaji. Kwa upande mwingine, neno *Gĩcaandĩ* aidha linarejelea aina ya ala inayotumiwa katika utendaji/uimbaji. Ala hii huwa na sura ifuatayo:



**Picha 1 – *Gicaandi***

Kutoka *Gikuyu Centre for Cultural Studies* (https://mukuyu.wordpress.com/2016/08/30/gicandi/)

Picha 1 inaashiria mfano wa ala ya *Gĩcaandĩ* ambayo hutumiwa na mwimbaji katika kufanya mapigo maalum yanayoambatana na ushairi wake.



**Picha 2 – Michoro kwenye *Gicaandi***

Kutoka *Gĩkũyũ Centre for Cultural Studies*
(https://mukuyu.wordpress.com/2016/08/30/gicandi/)

Katika picha 2, tunaonyeshwa mfano wa michoro iliyochorwa kwenye *Gĩcaandĩ* sio tu kwa lengo la kuipamba ala hii bali pia michoro hii ilikuwa ishara zilizofungamana na shairi na mafumbo aliyowasilisha mwimbaji. Kutokana na wingi wa beti na mtindo wa kuhifadhi beti zote akilini, waimbaji waliweka ishara maalum za kuwakumbusha beti na mpangilio kwenye ala hii. Licha ya kuwa uimbaji wa *Gĩcaandĩ* ulikuwa ni usanii wa hali ya juu uliojaa mafumbo, kama ilivyo kwa sanaa yoyote ile, suala la burudani lilikuwa la kimsingi.

Ngũgĩ wa Thiong'o anapojilinganisha na mwimbaji wa *Gĩcaandĩ* kama inavyojitokeza katika MC ukurasa wa 1:

> *Niguo nyina wa Wariinga aarookire gwakwa ruoro rugitema, agiithaitha muno na maithori*:
> -*Muini wa Gĩcaandĩ, heana rugano rwa mwana ucio wakwa ndeendete muno.*
> -*Temania ciothe utheri-ini, o muundu atue ciira akimenyaga uria kurathii*.
> -*Muini wa Gĩcaandĩ, hithuria uria muhithe.*

Anafanikiwa sio tu katika kuiingiza fasihi simulizi ya Kikuyu katika riwaya yake bali pia ni zoezi changamano la kisanii linaloifanya riwaya nzima kuwa jazanda moja kuu. Kupitia usomaji tunatarajia kukumbana na maelezo marefu ya kisa cha Wariinga ambayo yatasheheni usanii, mafumbo na mdundo maalum kama ilivyo kwa uimbaji wa *Gĩcaandĩ* katika jamii ya Gĩkũyũ.

Okpewho (1992) anaeleza kuwa fasihi simulizi inapaswa iangaziwe katika lugha yake chanzi ili iweze kueleweka na thamani yake kubainika kwa uwazi zaidi na kwamba maana za vipera mbalimbali hudhirika bayana katika utamaduni wake chanzi. Kutokana na maelezo haya tunaweza kupanua jazanda hii na kuiangazia kama ushindani baina ya lugha ya Kikuyu na utamaduni wa Gĩkũyũ dhidi ya utamaduni babe wa mkoloni katika muktadha wa MC na MT2. Kwingineko, kutokana na mazingira halisi ya utunzi wa riwaya hii ambapo mwandishi aliiandika akiwa kizuizini, tunaweza kufasili jazanda hii kurejelea hali ya mwandishi kushindana na utawala dhalimu kwa kuwa anafanikiwa kuwasilisha ujumbe unaoeleza maovu ya jamii kupitia kwa mafumbo kama afanyavyo mwimbaji wa *Gĩcaandĩ*. Hivyo basi, matumizi ya neno *Gĩcaandĩ* sio ya kiholela bali yanaangazia kuwasilisha ujumbe mpana zaidi kwa wale wanaoelewa lugha na utamaduni wa Gĩkũyũ ambao ndio hadhira iliyolengwa na MC.

Tunapoangazia jinsi neno hili limeshughulikiwa katika tafsiri MT1 na MT2, tunapata kwamba mtafsiri alihamisha dhana ya *Gĩcaandĩ* kutoka Kikuyu hadi Kiswahili na katika Kiingereza. Hali hii ni dhihirisho la moja kwa moja la uibuaji ugeni ambapo

dhana ya kigeni inaingizwa katika lugha nyingine na hivyo kuashiria moja kwa moja kwamba matini inayorejelewa sio asilia katika utamaduni husika.

Kama anavyoeleza Bandia (2014), mwandishi wa fasihi katika mazingira ya baadaukoloni hutekeleza jukumu la kujenga daraja la kuvusha uhalisia na tajriba za kiasilia, katika muktadha huu za Gĩkũyũ, hadi kwa muktadha pana wa kitaifa na kimataifa ambako uhalisia huu unahuishwa upya. Hata hivyo, mkakati huu aliotumia Ngũgĩ huu pakubwa unakwaza mawasiliano ambapo tunapata kuwa msomaji wa MT1 na MT2 hatapata kuelewa maana ya dhana *Gĩcaandĩ*. Isitoshe, jazanda na usanii unaofungamana na matumizi ya dhana hii unakosa kujitokeza bayana katika MT1 na MT2.

Tunapotafakari dhima ya mtafsiri katika muktadha wa baadaukoloni, licha ya kutambua nafasi ya kipekee ya itikadi katika tafsiri hizi pamoja na kutambua kwamba lugha inatumiwa kama chombo cha kupigania ukombozi kiisimu na kitamaduni, suala la mawasiliano bado ni la kimsingi zaidi kama ilivyo kwa tafsiri nyingine yoyote ile. Maamuzi ya kuteua maneno yanayofungamana na utamaduni chanzi na kuyahamisha jinsi yalivyo katika tafsiri katika muktadha huu yanabainika kuwa ni ya lazima na ya kimakusudi. Ya lazima kwa sababu dhana hii haina kisawe linganifu katika tamaduni lengwa kwa jinsi ambavyo fani ya uimbaji *Gĩcaandĩ* inavyodhihirika katika utamaduni wa Gĩkũyũ. Japo inakaribiana kisifa na fani kama vile ngonjera na utenzi katika utamaduni wa Kiswahili, matumizi ya ala na uamilifu wa ala husika unaibua upekee. Uteuzi huu aidha unabainika kuwa wa kimakusudi

kwa kuwa mwandishi aliye pia mtafsiri anafahamu fika upana wa maana ya dhana *Gĩcaandĩ* katika muktadha wa matumizi kwenye riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na kwa jinsi hiyo hana budi kuidumisha katika matini yake. Licha ya kukwaza mawasiliano na pengine kupunguza usanii katika MT1 na MT2, mtafsiri amefanikiwa kuwasilisha dhana ambayo ni muhimu katika kuonyesha ustaarabu wa jamii ya Gĩkũyũ pamoja na kueleza baadhi ya vipengele vya kifalsafa na vya kifasihi vya jamii hii.

Kuna maneno mengine ambayo yametumika katika MC ambayo yameshughulikiwa kwa njia tofauti na mtafsiri katika MT1 na MT2. Japo huenda sio maneno yaliyosanifiwa katika utamaduni wa Gĩkũyũ, maana yake imefungamana na fasihi simulizi, matumizi na uhalisia wa jamii hii. Kwa mfano:

**Mfano 10**

**MC:** *Kamoongonye* (Ukurasa wa 14)
**MT1:** *Mchumbakijana* (Ukurasa wa 16)
**MT2:** *Kamoongonye* (Ukurasa wa 14)

Neno *Kamoongonye* katika *Caitaani Mutharaba-ini* limetumiwa kumrejelea kijana barobaro ambaye alipendwa na Kareendi. Neno hili limetokana na masimulizi katika fasihi simulizi ya Kikuyu. Masimulizi haya yanaelezea kisa cha msichana mmoja ambaye babaye alitaka kumwoza kwa Mzee aliyekuwa na mali (waigoko). Hata hivyo msichana alimpenda *Kamongonye* (kijana barobaro asiyekuwa na mali). Uhamisho huu wa majina ya wahusika kutoka kwa fasihi simulizi hadi fasihi andishi ni wa kimakusudi kwa kuwa unaafiki hali ambayo inaakisiwa tukiangazia Kareendi, Njooni na Boss Kihara pamoja na marafiki wa Kareendi. Kareendi amempenda

Njooni ambaye ni mwanafunzi wa chuo kikuu na hata anamsaidia kwa kugharamia mahitaji yake ya kimsingi. Boss Kihara ni mzee mwenye mali na anamtamani Kareendi ila hafanikiwi kumpata. Marafiki wa Kareendi wanamshawishi amkubali Boss Kihara kwa kusisitiza haja ya kuwepo mabadiliko.

Tukiangazia jinsi neno hili lilivyotafsiriwa katika MT1 tunaona kuwa mtafsiri amefanya ufasili na kutoa tafsiri sisisi kwa kubuni neno lisilokuwa sanifu katika lugha hii *Mchumbakijana* japo linaakisi maana iliyokusudiwa katika MC. Tafsiri hii inayohusisha ubunaji wa msamiati inaibua ugeni katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa japo neno hili linawasiliana, sio neno la kawaida kisarufi na hata kimatumizi. Ugeni huu unaashiria ugeni wa kitamaduni katika MT1. Aidha, uamuzi aliofanya mtafsiri katika MT1 unapoteza uamilifu wa fasihi simulizi katika muktadha huu.

Katika MT2 ya Kiingereza, neno *Kamoongonye* limedumishwa uamuzi ambao ni wa uibuaji ugeni moja kwa moja. Hata hivyo, kinyume na alivyoshughulikia dhana ya *Gĩcaandĩ* katika Mfano 9, katika muktadha huu mtafsiri anatumia tanbihi kwenye sehemu ya chini ya ukurasa kutoa muktadha wa kitamaduni unaomwezesha msomaji kuielewa dhana hii na hivyo kufanikisha mawasiliano. Uamuzi huu unaonyesha udhaifu katika mikakati ya tafsiri iliyotumiwa katika kushughulikia MC katika MT2 kwa kukosa msimamo hata pale mwelekeo wa uibuaji wa ugeni unapotumika. Hali hii inatufanya kujiuliza iwapo kweli mtafsiri wa kazi hizi alitambua athari ya maamuzi aliyofanya katika kushughulikia tafsiri za dhana mbalimbali au alifanya tafsiri hizi kiholela; bila kufuata kanuni zozote.

Tukiangazia mfano mwingine wa maneno yanayofungamana na utamaduni jinsi yalivyoshughulikiwa katika tafsiri, inabainika kuwa muhtasari unaotokana na matumizi ya neno moja linalowasilisha maana pana unaathiri mawasiliano na ukamilifu wa maana katika MT1 na MT2 hasa pale neno lilipotumika kijazanda. Kwa mfano:

**Mfano 11**

**MC:** *Tuhii tuu ni tukiri Ngwati naari*. (Ukurasa wa 17) (Msisitizo wangu)
**MT1:** Wana nini hawa? Maskini wa kupindukia! Hawa ni wa kuhurumiwa Tu! (Ukurasa wa 19)
**MT2:** *These boys, are they even circumcised?* (Ukurasa wa 17)

Katika mfano huu, neno *Ngwati* ambalo linafungamana na utamaduni wa Gĩkũyũ limetumika kwa maana msingi na kijazanda katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini.* Neno hili limejitokeza katika muktadha ambamo mwandishi anasimulia jaribio la Boss Kihara la kumfanya Kareendi kuwa mpenzi wake jambo ambalo Kareendi anakataa kwa kudai kwamba tayari ana mchumba. Kama inavyobainika kwenye kifungu kifuatacho kutoka kwa MC. (Ukurasa wa 17)

*Githi ndikwirire maguta makuru matiinaga rwimbo? Kareendi mugathi wakwa.*
*Nyaanya ya igaanjo. Ureetigira kii? Ni ha uroonera hinya?*
*Ndi na kamoongonye ka mwanake!*
*Ha! Ha! Ha! Tiga guuthekia Kareendi. Kai wi old fashioned atia?*
*Uroiga uhoro wa tuhii tutu tureetugiria twiigananagie na arume?*
*Tuhii tuu ni tukiri ngwati naari?* (Msisitizo wangu)

Katika kifungu hiki tunampata Boss Kihara akitumia maneno matamu ya kumrai Kareendi akubali ombi lake la kuwa mpenziwe japo anakataliwa. Hali hii inamfanya Kihara kuuliza iwapo Kareendi anamkataa kwa sababu ya kuwa na mchumba:

*Uroiga uhoro wa tuhii tutu tureetugiria twiigananagie na arume? Tuhii tuu ni tukiri ngwati naari?* – Unazungumzia hawa vijana wadogo wanaojigamba na kujilinganisha na wanaume? Vijana hawa hata wana *Ngwati?*

Katika mfano huu, neno *ngwati* ni la kimsingi katika kuelewa ujumbe unaowasilishwa na Boss Kihara. Kwanza, katika utamaduni wa Gĩkũyũ, wanaume wote (na katika miaka ya awali wanawake pia) walihitajika kupashwa tohara baada ya kufikia umri wa kubaleghe na kuvunja ungo mtawalia. Sherehe hii ya jando ilikuwa ya kimsingi na kando na uamilifu mwingine ilikuwa ishara ya kumvusha mvulana au msichana kutoka utotoni hadi utu uzima.

Tukiangazia tohara ya wavulana, kuna upekee wa jinsi inavyopashwa miongoni mwa jamii ya Gĩkũyũ hasa tukizingatia mafundisho yanayotolewa (*Kirira)*. Aidha, kuna upekee katika jinsi wanatahiriwa kitamaduni. Kuna sehemu kwenye uume inayoitwa *Ngwati*. Uamilifu wake unatofautiana kutoka kwa kumtambulisha “mwanamume kamili” hadi kwa ustadi wa kufanya mapenzi. Katika nukuu hii na muktadha ambamo neno *Ngwati* limetumika, kuna ulinganisho baina ya *Tuhii* na *arume.* Tuhii ni wingi wa neno *kahii* ambalo ni udogo wa neno *kihii*. Neno *kihii* linarejelea mvulana ambaye hajatahiri na aghalabu ana nafasi ya chini zaidi katika mpangilio wa kijamii. Utamaduni wa Gĩkũyũ unamtweza sana mvulana aliye katika hali hii kwa kuwa anaaminika kuwa mjinga, asiyeelewa taratibu, asiye na busara, asiyeweza kuweka siri na kadhalika; sifa ambazo ni kinyume kwa wanaume waliopashwa tohara, *Arume*. Mfano mzuri wa tofauti iliyopo baina ya *kihii* na *Mundurume*

unapatikana katika methali ya Kikuyu:

*Muici na Kihii akenaga kiarua –Anayeiba kwa ushirikiano na mvulana ambaye hajatahiri anafurahi mvulana huyo anapotahiri.*

Hii ina maana kuwa kupitia kwa tohara, mvulana anaasi mambo ya kitoto na hivyo kuelewa mpangilio wa jamii na kupata busara ikiwemo uwezo wa kuweka usiri. Wakati Boss Kihara anawalinganisha vijana na *tuhii*, pakubwa harejelei hali ile ya 'kukatwa' katika upashwaji tohara ila analenga busara na mafundisho pamoja na sifa wanazotarajiwa kuwa nazo wanaume ikiwemo ustadi katika kufanya mapenzi.

Tafsiri inayotolewa katika MT1 ya Kiswahili (Ukurasa wa 19):

> "Si nilikwambia mke wangu amekonga? Kalendi kipenzi cha moyo wangu. Waogopa nini? Ni yapi unayoyahofia?"
> "Nina mchumba wangu kijana!"
> Ha! Ha! Ha! Usinichekeshe Kalendi. Umekuwa *Old Fashioned*?
> *Yaani hawa vijana waliozaliwa juzi? Vijana wanaojikweza kujaribu kujitia katika tabaka za wanaume. Wana nini hawa? Maskini wa kupindukia! Hawa ni wa kuhurumiwa tu!"*
>
> (Msisitizo wangu)

Sehemu iliyosisitizwa kwa herufi za mlazo inaonyesha mbezo alionao Boss Kihara kwa vijana wa sasa. Anawaona kama wasio waume kamili kwa kuwa hawana mali. Katika MC, neno *arume* ndani mwake mna dhana ya mali kwa kuwa katika utamaduni wa Gĩkũyũ ilitarajiwa mwanamume awe na mali iliyojumuisha wake, watoto, mifugo na ardhi. Hivyo basi japo mtafsiri hapa ameifasili maana mojawapo iliyokusudiwa katika MC, ya kuwa wazee wana mali ilhali vijana ni maskini, dhana ya *Ngwati* ilivyotumiwa katika MC haijafasiliwa kwa ukamilifu. Mtafsiri amelenga

kuileta MC karibu na hadhira yake katika MT1 kwa kutumia dhana yenye uasilia katika lugha ya Kiswahili japo amedondosha maana ya kingono iliyopo kwenye MC.

Hali sawa inajitokeza tunapoangazia tafsiri katika MT2 ambapo msisitizo unawekwa kwa dhana ya tohara kinyume hata na mali. Kwa mfano sehemu iliyosisitizwa katika MC imetafsiriwa ifuatavyo katika ukurasa wa 17 wa MT2:

> *"Are you talking about one of those boys who pretend to be men? Those boys, are they even circumcised?"* (Msisitizo wangu)

Ukinzani baina ya vijana na wanaume unajitokeza dhahiri ila katika MT2 suala la mali halijaangaziwa. Aidha, kuwa mwanamume kunahusishwa na tohara. Tafrisi hii kando na kupoteza baadhi ya maana iliyokusudiwa katika MC imepungukiwa katika kuhawilisha dhana ya *Ngwati* kama ilivyodhamiriwa na kutumika katika MC. Tukirejelea jinsi neno *Ngwati* limeshughulikiwa katika MT1 na MT2, lugha ya kingono yenye uwazi hasa tukihusisha neno hili na muktadha wake wa matumizi katika MC haijitokezi dhahiri na kwa jinsi hiyo ukamilifu wa taswira ya tukio hili unakosekana katika MT1 na MT2 jambo linaloathiri usanii.

Katika kusoma riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake, kuna mifano mingine mingi ya maneno maalum yanayofungamana na utamaduni wa MC inayobainika. Maneno haya yameshughulikiwa katika tafsiri kwa mkakati wa ama ubinafsishaji au uibuaji ugeni kama ilivyojadiliwa katika mfano 8 hadi mfano 11. Hata hivyo, tunapoangazia maneno ambatano kama vile:

**Mifano 12**

**MC:** *Mbari ya Karianime* na *Mbari ya Karimi*. (Ukurasa wa 48)
**MT1**: *Wanyonyaji/vimelea* na *mafalahi/wafanyakazi*. (Ukurasa wa 53)
**MT2**: *The clan of parasites* na *the clan of producers.* (Ukurasa 50)

Tunapata kwamba mtafsiri amechanganya mielekeo anayotumia katika kuwasilisha maana ya kilichokusudiwa katika MT kwa kuwa MT1 imetokana na ufasili wa dhana iliyokusudiwa katika MC kisha kutafuta viwakilishi linganifu katika lugha ya Kiswahili, mtindo tunaoweza kuuhusisha na ubinafsishaji. Katika MT2 tunapata tafsiri mseto baina ya ubinafsishaji na uibuaji ugeni. Katika MT2, mtafsiri amedumisha uaminifu kwa MC na utamaduni wake kwa kutafsiri dhana *Mbari* moja kwa moja kuwa *Clan.* Suala la kuweka kundi la watu wenye tabia sawa katika mpangilio wa ukoo halina uasilia katika utamaduni wa Kiingereza bali ni la kawaida katika jamii za Kiafrika. Swali ambalo linaibuka hapa ni; kwa nini mtafsiri hakudumisha uaminifu kwa MC katika kutafsiri MT1 ilhali kuna ukuruba wa kiisimu na kitamaduni baina ya Kikuyu na Kiswahili?

Dhamira ya mwandishi katika muktadha huu inaelekea kuangazia suala la wachache dhalimu wanaotegemea na kunyonya jasho la walio wengi. Suala la utabaka kiuchumi ni la kimsingi kwa mwandishi na katika MC ambapo inaelekea walio wengi katika jumuia ya hadithini wanaumia huku wachache, wezi waliokongamana kwenye mashindano, wakiishi maisha ya kikwasi kwenye mitaa ya kifahari kwa kutumia hila na utapeli. Kwa kutumia neno *mbari* katika MC, mwandishi analinganisha muungano wa tabaka tajiri la wanyanyasaji wa wadhalimu na mpangilio wa familia. Katika

muktadha wa Gĩkũyũ, ukoo ni sehemu ya kimsingi ya mwanajamii yeyote. Kwa kugawa jamii katika ukoo wa wanyanyasaji na ukoo wa wazalishaji mwandishi anafanikiwa kuwafanya wasomaji kujisaili wao wapo katika ukoo upi. Kwa kufanya hivi anafanikiwa kuangazia suala lenye umuhimu kwa kutumia uhusisho wa kijamii na kwa jinsi hiyo kufanikisha mawasiliano.

Katika MT1, jamii inayolengwa, wasemaji wa Kiswahili, wengi ni wenyeji wa Afrika mashariki na uhalisia wao kitamaduni haujatengana sana na ule wa MC. Hata hivyo, mtafsiri anapuuza dhana ya ukoo katika tafsiri yake jambo ambalo halielezeki ila kwa kuliainisha kama upungufu wa uteuzi katika kutekeleza tafsiri ya kifungu hiki. Kulingana na uamuzi uliofanywa katika kushughulikia maneno yanayofungamana na utamaduni hapo awali, mtafsiri angefaulu zaidi katika kuteka hisia na kusisimua tafakuri ya hadhira yake kwa kutafsiri dhana *mbari* kuwa *ukoo* au hata *tabaka* badala ya kuipuuza.

Hali sawa na hii inabainika katika maelezo anayotoa mwandishi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* katika ukurasa wa 92 ambapo kuna matumizi ya dhana ya ukoo kurejelea watu wanene *(Mbari ya Mucuuha)* na kuwalinganisha na watu wembamba *(Mbari ya Waceke)*. Tafsiri inayotolewa kwa Kiingereza katika MT2, watu wanene *(clan of fatties)* na watu wembamba (*the clan of skinies*) katika ukurasa wa 94 imedumisha dhana ya ukoo kwa kutumia kisawe chake katika Kiingereza, *clan*. Hata hivyo, kama ilivyojadiliwa hapo awali, mpangilio wa jamii katika ukoo hauna uasilia katika jamii za kimagharibi ila ni dhana ya Kiafrika.

Suala ambalo halibainiki wazi hapa ni kwa nini mtafsiri katika MT1 alipuuza dhana ya ukoo katika tafsiri ya Kiswahili na kutumia dhana ya kawaida ya *kikundi* (Ukurasa wa 99) kuwarejelea wembamba na wanene. Kwa kupuuza dhana ya ukoo ambayo ni ya kisanii na imechota moja kwa moja kutokana na utamaduni wa Kiafrika, na imo katika utamaduni wa Kiswahili, mtafsiri anatufanya kukisia kwamba huenda hakutambua upekee wa neno hili na uamilifu wake kama lilivyotumika katika muktadha huu.

Upekee wa kufungamanisha makundi haya ya wezi na mpangilio wa kifamilia katika utamaduni wa Gĩkũyũ unadhihirka katika kuwatambulisha washindani katika shindano la wezi ambapo kwa mfano;

**Mfano 13**

> **MC**: Ni hangiatuthukire haaro riria Wamucuuha umwe aaniriire akiuga ati mundu
> Ucio ukwaragia ari muceke ota Ndaaya wa Kahuria. *Naake muuru wa Waceke*
> akiruuga na iguru riingi mikiha yoothe ya ngiingo na uthiu yuumiriite…
> (Ukurasa wa 92) *Msisitizo wangu*

> **MT1**: Vita vikali vilikuwa karibu kuzuka wakati mwizi mmoja alipopaza sauti
> akasema kuwa huyo mtu mwembamba alifanana na Mrefu wa kinyakuzi.
> *Huyu mtu mwembamba* naye akaruka akasimama akiwa na hasira nyingi…
> (Ukurasa wa 99) *Msisitizo wangu*

> **MT2:** *A fight almost broke out when one fatty said loudly that the man who had*
> *just spoken was as lanky as Ndaaya wa Kuraiha. The man who had been*
> *insulted stood up and demanded bitterly…*
> (Ukurasa wa 94) *Msisitizo wangu*

Kwa kurejelea sehemu iliyoandikwa kwa herufi za mlazo katika MC, mhusika aliyesimama kwa hasira anarejelewa kuwa *Muuru wa Waceke*. Kifungu hiki

kingetafsiriwa sisisi kwa Kiswahili kingekuwa ni *Bin/Mwanawe Waceke* huku kwa Kiingereza kikiwa *Son of Waceke*. Hata hivyo, matumizi ya kifungu hiki mkatika MC yamefungamana na utamaduni wa Gĩkũyũ ambapo mtu huhusishwa na ukoo wake. Hivyo, kifungu hiki kinamhusisha mhusika aliyesimama akiwa na hasira na ukoo wa watu wembamba. Hali hii inabainisha usanii ambao umepotea katika MT1 na MT2 kwa kuwa dhana ya uhusisho wa ukoo haipo kama inavyodhihirika katika sehemu zilizoandikwa kwa herufi za mlazo. Isitoshe, japo neno *Waceke* limetumiwa kurejelea watu wembamba katika muktadha huu, hili pia ni jina halisi linalotolewa kwa watoto wa kike katika utamaduni wa Gĩkũyũ. Hivyo kumhusisha msemaji aliyekuwa mwembamba na *Waceke* ni njia ya kuhusisha dhana ya *Waceke* kutoka kwa urejeleo wa watu wembamba na kuifanya kurejelea Mama.

Kinachobainika kutokana na tafsiri hizi katika muktadha wa mfano huu ni kwamba katika uandishi wa Kiafrika, baadhi ya waandishi wanachota kutoka kwa tamaduni zao na mipangilio yao ya kijamii kwa kiasi ambapo inakuwa vigumu kuzihawilisha dhana hizi katika utamaduni wowote mwingine uwe wa Kiafrika, kama ilivyo kwa Kiswahili, au wa kimagharibi, kama ilivyo kwa Kiingereza. Hivyo basi, majaribio ya kutoa ladha ya kiasili katika tafsiri za Kiingereza na lugha nyingine wakati mwingine hayafanikiwi kutokana na upekee na uchangamano wa mifumo ya kitamaduni ya lugha na tamaduni chanzi.

### 3.2.4 Tafsiri ya Misemo

Misemo inaweza kufasiliwa kuwa ni dhana yenye maana ya semi ambazo zinabeba ukweli wa kijumla ambazo hutumika kueleza mambo mbalimbali yanayokubali ukweli huo. Ukweli huu aghalabu hutokana na tajriba, mazingira na utamaduni wa jamii husika. Hivyo misemo ni baadhi ya udhihirikaji wa matumizi ya lugha ambao umefungamana na muktadha wa kijamii ambamo imezalishwa na kutumiwa. Kwa jinsi hii, ufasili na uhawilishaji wa misemo katika tafsiri pakubwa unafanikiwa kulingana na ufahamu alio nao mtafsiri kwa mazingira chanzi ambamo msemo husika unazalishwa na kutumika.

Tunaporejelea MC, tunapata kuwa mwandishi ametumia misemo ambayo pakubwa imefungamana na utamaduni wake chanzi, Gĩkũyũ, kama njia mojawapo ya kuimarisha usanii wake. Aidha, katika muktadha wa utafiti huu, hatuna budi kukisia kuwa huenda matumizi haya yana dhima zaidi ya ile ya usanii hasa tunapoangazia jinsi misemo mbalimbali inavyobainika na kutumika katika *Caitaani Mutharaba-ini*. Kwa mfano:

**Mfano 14**

**MC:** *Gĩkũyũ oigire kirira ni uura thoni*. (Sehemu ya Utangulizi)
**MT1:** Mafunzo hayaoani na haya wala woga. (Sehemu ya Utangulizi)

**MC:** *Muukabi ndatuuraga haria oimiriire.* (Sehemu ya Utangulizi)
**MT1:** Mambo hayawezi kuendelea vile vile kizazi baada ya kizazi. (Sehemu ya Utangulizi)

Katika mfano 14 hapo juu, kuna misemo miwili ambayo inatokea kwenye sehemu ya utangulizi ya MC na MT1. Kwa kuwa utangulizi wa *Caitaani Mutharaba-ini*

haukutafsiriwa katika *Devil on the Cross*, hatuna tafsiri ya misemo hii katika MT2. Tumeorodhesha misemo hii mwa pamoja kwa kuwa licha ya kutoka kwenye sehemu tofauti za utangulizi, na kuwa ina maana tofauti, mtafsiri katika MT1 ametumia mkakati sawa kuishughulikia katika tafsiri ya Kiswahili.

Tukirejelea msemo wa kwanza *Gĩkũyũ oigire kirira ni uura thoni* (msisitizo wangu) hasa sehemu niliyopigia msitari yenye maana ya *Gĩkũyũ alisema…* (tafsiri sisisi) ni dhahiri kwamba mwandishi amefungamanisha msemo huu na utamaduni wa jamii ya Gĩkũyũ kwa kuudokeza kuwa usemi wa moja kwa moja wa anayeaminika kuwa baba na mzazi wa kwanza wa jamii hii. Kwa kufanya hivi mwandishi anaupa usemi husika uasilia katika muktadha wa lugha ya Kikuyu pamoja na kwa hadhira inayolengwa. Mtindo huu wa uwasilishaji unaweza kuhusishwa na mtindo ambao Chinua Achebe anautumia katika uandishi wake kuwasilisha dhana inayofungamana na utamaduni wake ambapo kifungu cha maneno *Our people say* aghalabu hutumiwa kabla ya kutoa methali, msemo au hata urejelezi wa kitamaduni ambao unafungamana na utamaduni wake na hauwezi kutafsirika moja kwa moja katika lugha nyingine kama vile Kiingereza na ukawasiliana kikamilifu. Hali hii kama inavyoelezewa katika mazingira ya baadaukoloni ni ya kimakusudi kwa waandishi wanaotokea jamii zilizowahi kutawaliwa na wakoloni, kama vile Ngũgĩ wa Thiong’o katika muktadha wa Kenya.

Mtafsiri katika MT1 anatoa ufafanuzi wa maana iliyokusudiwa katika msemo unaobainishwa katika MC; kwamba, katika kutoa ushauri aibu haina nafasi kwani

kila jambo lazima lielezewe kinagaubaga. Ufafanuzi unadhihirika katika tafsiri iliyorejelewa kwamba *Mafunzo hayaoani na haya wala woga.* Ujumuishwaji wa dhana ya woga katika ufafanuzi katika MT1 umepanua maana iliyokusudiwa katika MC. Hii huenda ni jambo ambalo mtafsiri, ambaye pia ndiye mwandishi wa MC, alifanya kimakusudi kwanza kwa kujirejelea binafsi hasa tukizingatia mazingira halisi ya kisiasa ambamo riwaya hii iliandikwa. Pili, uamuzi huu huenda umefanywa kuhimiza haja ya ujasiri katika kuzungumzia masuala mazito ambayo huenda jamii na viongozi, hasa wa kisiasa, hawataki kuyasikia kama ilivyokuwa kwa mwandishi.

Tukirejelea msemo wa pili katika mfano huu; *Muukabi ndatuuraga haria oimiriire*, mwandishi ametumia msemo ambao ulikuwa wa kawaida katika kipindi ambacho mwandishi alikuwa akiitunga kazi yake. Msemo huu unaweza kutafsiriwa sisisi kwa Kiswahili kuwa; *Mmaasai daima haishi alikotokea.* Ni muhimu hapa kutambua kuwa licha ya kwamba huu ni msemo katika jamii ya Gĩkũyũ, urejelezi umefanywa kwa jamii ya Wamaasai. Hali hii inajitokeza katika lugha ya Kikuyu kutokana na ujirani baina ya jamii hizi mbili pamoja na mtagusano wa kijamii, kisiasa na kiuchumi kabla ya majilio ya wakoloni. Msemo huu hutumiwa kurejelea haja ya mambo kubadilika kama vile Wamaasai hubadili malisho katika kutekeleza ufugaji wao. Hali ya kuhama huwasaidia kupata lishe bora kwa wanyama wao na hivyo kuhakikisha afya ya mifugo wao.

Katika muktadha wa matumizi ya msemo huu, mwandishi anahimiza haja ya kuwepo kwa mabadiliko katika maarifa na ustaarabu wa jamii kitamaduni na hata

kisiasa na kiuchumi ili kulinda na kuhakikisha kwamba utamaduni husika unazidi kunawiri. Tunapozingatia mfano 14 kwa ukamilifu wake, mwandishi anahimiza haja ya mambo kubadilika ila katika mabadiliko hayo, watu wawe na ukakamavu, uwazi na ujasiri wa kukemea mabaya. Kwa mfano, katika MC sehemu ya utangulizi anatumia mfano kuhimiza haya anapoeleza;

> *Uguo ni kuuga ati kirira kiega ti kirira kiraahitha mauundu kuugaga ati muthuuri akimia nja muthenya barigici eeroreirwo ni ciana ni mucii ararathima. Muthuri ta ucio agiriirwo ni kuugirwo mbu ekunye gutu!*

Katika kifungu hiki, mwandishi wa MC ametoa taswira kali yenye uwazi na isiyozingatia tasfida kama kielelzo cha uwazi unaohitajika katika kukemea uovu katika jamii. Anaeleza kwamba mafunzo mazuri ni yale yasiyoficha mambo kwamba;

> *Mzee akinya paruwanja mbele ya wanawe asisemekane anabariki boma*
>
> (Tafsiri sisisi ya sehemu iliyopigiwa mstari).

Maelezo haya yamekiuka kanuni za tasfida za matumizi ya lugha ya Kikuyu. Uamuzi huu ni wa kimakusudi na unalenga kuibua ukakasi na kuleta fedheha katika kushadidia hoja anayoieleza. Hata hivyo katika tafsiri aliyoitoa kwa Kiswahili, mwandishi anarejelea matumizi ya lugha yanayozingatia tasfida kwa kutumia neno jumuisha la *tendo la fedheha.* Katika muktadha wa baadaukoloni ni kawaida kwa waandishi kutumia lugha kali yenye ukakasi katika ama kuizindua jamii au kukemea wakoloni, ukoloni na athari zake. Katika muktadha huu, mwandishi katika MC ametumia lugha isiyo na upole kimakusudi kufanikisha dhamira yake ilhali katika MT1 amerejelea matumizi ya lugha ya tasfida licha ya kuwa hata wasomaji wa

Kiswahili, jamii inayopatikana katika eneo la Afrika Mashariki na Kati, waliwahi kutawaliwa na wakoloni hivyo dhamira ilipaswa kuwa sawa.

**Mfano 15**

**MC:** *Ilmorog ni haaha riitho na iniuru*. (Ukurasa wa 25)
**MT1:** Kufumba na kufumbua mjione Ilmorog. (Ukurasa wa 28)
**MT2:** *Ilmorog is here, no further than the eye is from the nose*. (Ukurasa wa 26)

Kuna kisa kinachosimuliwa cha mhusika Mwaura ambaye ni dereva wa matatu ambayo imetumiwa kama mojawapo ya mandhari ya usimulizi. Msemo huu anautumia katika hali ya kuwarai watu kuingia katika gari lake *Matatu Matata Matamu*. Gari lenyewe limewasilishwa kuwa gari kuu kuu na hivyo ilikuwa vigumu kupata abiria. Kwa kutumia msemo *haaha riitho na iniuru* mwandishi amecheta kutoka kwa lugha yake ya Kikuyu kuashiria kwamba Ilmorog sio mbali. Ni karibu kama ilivyo baina ya jicho *(riitho)* na pua *(iniuru).* Uhawilishaji wa dhana hii katika MT1 ya Kiswahili umefanywa kwa kuzingatia mapendekezo ya wataalamu wa tafsiri kuwa tafsiri ya dhana zinazofungamana na utamaduni kama ilivyo kwa misemo itafanikiwa kwa kutafuta dhana sawia linganifu kimaana na au kiuamilifu katika utamaduni na lugha pokezi. Mtafsiri ametumia *Kufumba na Kufumbua* dhana ambayo ni ya kiasili katika Kiswahili na kwa jinsi hiyo amefanikiwa kuumba upya usanii aliotumia katika MC pasi na kuibua ugeni wowote. Juhudi hizi zinaifanya MT1 katika muktadha huu kuwa na uasilia kama matini yoyote ya Kiswahili kwa kuwa amechota moja kwa moja kutokana na utamaduni na lugha ya Kiswahili.

Hali ni tofauti tunapozingatia MT2 ya Kiingereza ambapo mtafsiri ametumia mseto wa tafsiri sisisi ikijumuishwa na maelezo. Huu ni mkakati wa kipekee ambao

haujatumika kufikia sasa katika matini hii. Awali tumetoa mifano ya miktadha ambamo mtafsiri katika MT2 ametumia ama tafsiri sisisi au akatumia maelezo ili kuhawilisha dhana zilizoko katika MC. Hii ndiyo mara ya kwanza naunganisha mikakati hii miwili kuibua mseto wa tafsiri sisisi na maelezo katika kuwasilisha dhana inayofungamana na utamaduni wa MC.

Katika kuelezea hali hii tunaweza kurejelea maoni ya Ashcroft na wenzake, (1989) katika *The Empire Writes Back* ambapo wanaeleza kuwa kuna mikakati miwili inayotumiwa na waliotawaliwa katika kutumia lugha za mkoloni:

> Kuna mikakati miwili inayotumiwa kupinga ubepari katika maandishi ya baadaukoloni: Kwanza ni kufumbia macho hadhi iliyopewa Kiingereza; kutenganisha lugha na watumiaji wake…*pili ni kuifinyanga lugha hii, kuiunda upya ili kuafiki matumizi mapya yaliyotengana na uhusisho wa lugha na ukoloni.*
> (Ashcroft na wenzake, 1989: 38) *Ty (Msisitizo wangu)*

Maamuzi ya kutumia lugha ya Kiafrika katika MC na kwa kiasi fulani katika MT1 yanatokana na haja ya kujiunga na Waafrika wengine katika juhudi za kupigania ukombozi kutokana na ubepari na ukoloni mamboleo. Tukiangazia mkakati wa pili wanaouzungumzia Ashcroft na wenzake, ulio katika herufi za mlazo, unadhihirika katika MT2, *Devil on the Cross,* ambayo licha ya kuandikwa kwa Kiingereza, inaakisi zaidi utamaduni na tajriba za Kiafrika. Lugha inayodhihirika inafanana na anayoitumia Achebe katika kazi zake ambazo zinatumia Kiingereza japo kama anavyoeleza katika *The African Writer and the English Language* kama alivyonukuliwa na Ngũgĩ (1986):

> … lugha ya Kiingereza ina uwezo wa kuhimili uzito wa tajriba za

> Mwafrika. *Hata hivyo, lazima kiwe Kiingereza kipya, kinachohusiana na asili yake ila kilichokarabatiwa kuafiki mazingira na muktadha wa Kiafrika.*
>
> (Ngũgĩ, 1986:8) *Ty (Msisitizo wangu)*

Mfano 15 ni dhihirisho la mkakati huu ambapo tafsiri inayotolewa;

*Ilmorog is here, no further than the eye is from the nose*.

Japo ni kifungu kilichoandikwa kwa Kiingereza, kinamwia msemaji mjua Kiingereza kuwa cha kigeni au kilichopotoka katika ngazi za uasilia. Kwa mfano, katika kifungu *Ilmorog is here* inaweza kufasiliwa ni kama *Ilmolog* ilikuwa imepotea au imejificha kisha msemaji akaipata na kueleza kuwa iko hapa. Maana iliyokusudiwa katika MC kwa kutumia neno *haaha (hapa)* haiwezi hufumbatwa katika kifungu hiki cha Kiingereza. Isitoshe, ulinganisho unaobainika katika maelezo yanayotolewa kuhusu umbali wa Ilmorog kutoka alikokuwa Mwaura hauna uasilia wowote katika Kiingereza. Unadhihirika moja kwa moja kuwa ni kifungu cha 'kigeni' katika lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi, mtafsiri katika MT2 anamwezesha mwandishi wa MC kuhawilisha dhana za kiasili katika MC kwenye mfumo wa Kiingereza. Tukio hili ndilo linarejelewa kama ufinyanzi wa Kiingereza kuibuka na lugha mseto, isiyo sanifu, ambayo inatumiwa kama jukwaa la ukombozi wa lugha za kiasilia za jamii zilizotawaliwa huku tamaduni zilizodhalilishwa zikiwasilishwa kwa kutumia lugha hii babe na kwa jinsi hiyo kuziwezesha. Hali sawa na hii inabainika katika tafsiri iliyotolewa kwa msemo ufuatao:

**MC:** *Moonire na kanua*… (Ukurasa wa 177)
**MT1:** Waliona kilichomtoa kanga manyoya. (Ukurasa wa 189)
**MT2:** *They all ended up seeing through their mouths instead of their eyes*.
(Ukurasa wa 179)

Kifungu hiki kimetokana na usemi wa Nditika wa Nguunji anapotoa ushuhuda wake. Anaeleza kwamba siku moja wafanyakazi wake walikuwa wamegoma wakidai waongezewe mishahara naye akawafuta bila kutoa ilani. Hali hii ndiyo iliwastaajabisha na kuwafanya *kuona na kanua* (kuona kwa midomo). Mojawapo ya dhana za zilizoathiriwa na maajilio ya ukoloni pamoja na mitagusano ya muda mrefu baina ya jamii za Kiafrika na wageni wa mataifa mengine kama vile ya Kiarabu pamoja na wakoloni ilikuwa ni suala la imani za kidini.

Nchini Kenya, ujio wa wakoloni, walowezi na wamishenari haukuweza kutofautishwa na wenyeji. Katika jamii ya Gĩkũyũ paliibuka msemo wa:

*gutiri muthuungu na Mubia*

Kwa maana ya, hakuna tofauti baina ya mkoloni na padre. Miongoni mwa athari za ujio wa wageni wa Kiingereza kwa jamii ya Gĩkũyũ ilikuwa ni pamoja na kuingizwa kwa dini ya Kikristo ambayo ilichukua nafasi ya imani za kiasili.

Utaratibu wa kijamii hususan kwa masuala yanayohusiana na imani za kiungu katika jamii zilizotawaliwa na wakoloni ziliathiriwa pakubwa na watawala hao. Kama anavyoeleza Muriuki (1969) katika tasnifu yake inayoangazia historia ya jamii ya Gĩkũyũ ni kwamba, mabadiliko yaliyoletwa na wageni hawa yaliyumbisha imani za kiasili na tabia za wanajamii jambo lilioishia kwa mageuzi katika jamii nzima. Aidha, mipangilio ya kijamii kuhusu masuala kama vile ndoa, baraka na laana yalibadilika. Katika jamii ya Gĩkũyũ kwa mfano, sawia na katika baadhi ya jamii nyingine za

Kiafrika, suala la baraka kwa mtoto liliaminiwa kwamba ni baba tu ndiye mwenye uwezo wa kumbariki mwana wake. Utoaji wa baraka ulikuwa ni tambiko kuu ila kulikuwa na mchakato sahili wa kumbariki mwana au mtu yeyote uliohusisha anayetoa baraka kumtemea mate kifuani. Hali hii ndiyo mwandishi wa MC anarejelea ambapo anaeleza ifuatavyo:

**Mfano 16**

**MC:** *Magigituira mata githuri…* (Ukurasa wa 138)
**MT1:** Wakamwombea Mungu ambariki… (Ukurasa wa 147)
**MT2:** *They prayed…* (Ukurasa wa 140)

Kifungu hiki kimetumika katka usimulizi wa jinsi wazazi baada ya kuachiliwa toka kizuizini mnamo 1960 walikokuwa wameishi tangu mwaka wa 1954, wakapata ardhi yao ishauziwa wasaliti walioshirikiana na serikali ya kikoloni. Mwanao Wariinga amejiunga na shule na wanamwombea afanikiwe katika masomo yake wakiwa na imani kuwa huenda atawaauni kutokana na minyororo ya umasikini. Kama ilivyokuwa ada katika jamii ya Gĩkũyũ, wazazi, hususan baba, anatemea mate kifuani kama ishara ya kutoa baraka kwa mwanawe. Katika kuhawilisha dhana hii kwa Kiswahili, mtafsiri katika MT1 ametumia maelezo ambayo yanaashiria kwamba alielewa kilichomaanishwa katika MC. Anafumbata dhana zote mbili za maombi na baraka katika ufafanuzi wake kama ilivyobainishwa katika Mfano 16 MT1. Anaongeza dhana ya Mungu katika ufafanuzi wake pengine kwa kuwa katika utamaduni wa Kiswahili, maombi huwasilishwa kwa Mungu ambaye anayatimiza. Hata hivyo, katika MT2, mtafsiri anatumia dhana ya maombi pekee kama

kiwakilishi cha *Gutuira mata githuri* (kutemea kifua mate). Hali hii haifumbati kikamilifu maana iliyokusudiwa katika MC na inabainika kuwa ni tukio la ubinafsishaji ambapo mtafsiri anatumia dhana ya maombi kwa ujumla ambayo inatekeleza umailifu sawa na ule uliokusudiwa katika MC.

Tukio hili la ukosefu wa mtiririko katika mikakati aliyotumia mtafsiri hasa katika MT2 linazidi kuibua swali la iwapo mtafsiri ambaye pia ndiye mwandishi wa MC alielewa uzito na au dhima ya baadhi ya uteuzi aliofanya katika kushughulikia tafsiri za dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi. Mkanganyiko huu ni suala la kawaida kwa waandishi wa baadaukoloni hasa kutokana na utamaduni mseto ambamo wanashiriki na kuandikia. Kwa mfano, Ngũgĩ japo anashadidia suala la matumizi ya lugha za kiasili katika utunzi wa fasihi ya Kiafrika, tangu miaka ya themanini hadi sasa bado anaishi kwa [15]Wazungu ambao lugha yao na matendo yao ndiyo yalidhalilisha lugha yake na utamaduni wake. Aidha, hata katika uandishi wake katika lugha ya Kikuyu inaelekea kwamba huenda yeye hutekeleza tafsiri kutoka Kiingereza kama ilivyojadiliwa katika sura ya nne.

### 3.2.5 Tafsiri ya Nyimbo

Nyimbo katika jamii za Kiafrika zina uamilifu muhimu katika mahusisano ya wanajamii, namna wanavyosherehekea na jinsi wanavyoyawasilisha matukio muhimu ya kihistoria katika jamii husika. Aghalabu nyimbo katika jamii za Kiafrika huwa ni sehemu muhimu ya sherehe mbalimbali kama vile ndoa, kusherehekea mwana

[15] Dhana hii hapa imetumiwa kwa maana wa Waingereza na Wamarekani.

kuzaliwa pamoja na kusherehekea hatua mbalimbali kama vile utoaji wa jina, sherehe za jando na unyago, na hata kifo. Kama anavyoeleza Mbaegu (2015), suala la nyimbo katika jamii za Kiafrika limefungamana na utamaduni wao na maisha yao ya kila siku. Takriban sherehe zote katika jamii za Kiafrika, hasa sherehe zinazofungamana na utamaduni wa jamii husika, huanza na husheheni nyimbo na ngoma. Huenda matumizi ya nyimbo yamekithiri katika jamii za Kiafrika kwa kuwa zilikuwa na historia ndefu ya ustaarabu uliohifadhiwa katika masimulizi ikiwemo nyimbo.

Miongoni mwa jamii ya Gĩkũyũ, nyimbo ni sehemu ya kimsingi ya utamaduni wake na sherehe zake. Kwa mfano, Gakaara (1988) katika utangulizi wa kitabu chake *Nyimbo Cia Mau Mau: Iria Ciarehithirie Wiyathi* ambacho ni mkusanyiko wa nyimbo zilizoimbwa wakati wa kupigania uhuru hasa na wapiganaji wa Mau Mau anaeleza kwamba;

> Nyimbo za Mau Mau ziliimbwa wakati tulikuwa tunapigania uhuru wa Kenya na ndio maana zinaitwa nyimbo za uhuru. Ndani mwake mna historia ya tangu mwaka wa 1948 hadi 1964 tulipoipeperusha bendera ya Kenya. Nyimbo hizi zilitungwa kulingana na matendo yaliyofanywa wakati ule na maneno katika kila wimbo yanaonyesha hivyo wazi…(*Ty)*

Kutokana na kifungu hiki, ni bayana kwamba hata wakati maisha yalikuwa magumu kutokana na makabiliano baina ya jamii hii na wakoloni, nyimbo bado zilikuwa na nafasi yake na uamilifu wake ni dhahiri. Hivyo basi sio ajabu Ngũgĩ katika kuandika riwaya yake *Caitaani Mutharaba-ini* ametumia nyimbo kupamba masimulizi yake na kuakisi hali ya kijamii pamoja na kuweka bayana kipengele hiki cha utamaduni wa jamii hii. Katika utunzi wa MC, mwandishi ametumia nyimbo za aina mbalimbali

kwa dhima tofauti tofauti. Katika sehemu hii, tutaangazia lugha katika baadhi ya nyimbo hizi kwa lengo la kuonyesha jinsi dhana zinazofungamana na utamaduni wa MC zilivyohawilishwa katika MT1 na MT2. Mifano zaidi ya nyimbo, hasa kwa kuzingatia uchanganuzi wa ujumbe na dhamira zake utaangaziwa katika sura ya nne.

**Mfano 17**

**MC:** *Kwa Ngai kuungiri hakuhi,*
*Maraaya twathii ciira na inyui*
*Kiindu mwaheirwo ni mwathani*
*Mbaga ici muukwendia kibaau!* (Ukurasa wa 25)

**MT1:** Kwa Mungu kungalikuwa karibu
Tungekwenda kesini na kahaba
Mlipewa bure na Mungu
Majura sasa mwadai manoti! (Ukurasa wa 28)

**MT2:** *If God's kingdom were near,*
*I would take you whore to court.*
*Something given you free by the Lord*
*You now sell for twenty shillings!* (Ukurasa wa 26)

Huu ni wimbo ambao, Mwaura ambaye ni dereva wa matatu anaimba kuwavutia abiria kwa gari lake kuu kuu. Uhalisia unaosawiriwa hapa sio wa jamii ya Gĩkũyũ katika mazingira yake ya kiasili ila ni wa jamii hii katika mazingira ya jijini ambako wanajamii wametangamana na mambo mengi ya kigeni na kwa jinsi hiyo dhana kama vile za ukahaba zinabainika.

Uhalisia katika jamii ya Gĩkũyũ katika miaka ambayo mtunzi anaisawiri ni kwamba wanaume wengi katika jamii hii walihamia mijini kusaka riziki na kuwaacha wake na wana wao katika sehemu za mashambani. Licha ya hayo, kutokana na ukosefu wa ajira, baadhi ya wasichana walijiingiza katika biashara ya ukahaba kama njia ya kujipa riziki. Hali hizi hivyo basi tunaweza kuzihusisha sio na utamaduni asilia wa

Gĩkũyũ ila kwa uhalisia wa kijamii unaodhihirika katika miji kutokana na athari za ukoloni na maingiliano ya kitamaduni baina ya jamii mbalimbali. Neno kama vile *maraya* sio neno asilia la Kikuyu ila limetoholewa kutoka neno la Kiswahili ‘malaya’.

Ucheshi anaoibua Mwaura kwa kusaili kwa nini kahaba wanauza sehemu ya mwili ambayo walipewa bila malipo na Muumba unawavuta watu kwake. Bei ya kushiriki ngono inaelezwa kuwa ni *Kibaau* msimu unaorejelea shilingi ishirini mbazo kwa wakati huo zilikuwa pesa zenye thamani kubwa na hivyo ile haikuwa bei rahisi. Katika MT1 mtafsiri amedumisha lugha ya ucheshi na upotovu wa nidhamu iliyotumiwa katika MC na katika kutafsiri bei, ametumia neno *Manoti* kuonyesha kuwa ni pesa nyingi wanazodai makahaba hao.

Tuikiangazia tafsiri katika MT2, suala la upole limekiukwa kama ilivyo kwa MT1 na MC, hata hivyo mtafsiri anatoa tafsiri sisisi kwa dhana ya *Kibaau* na kiwasilisha kuwa ni *Twenty Shillings.* Kutokana na tofauti za kitamaduni baina ya hadhira ya MC na ile ya MT2, suala la gharama kuwa juu halibainiki wazi. Tofauti za kitamaduni zinazowasilishwa katika nyimbo alizotumia mwandishi katika MC zinaweza kubainika tunapozingatia mfano ufuatao:

**Mfano 18**

**MC:** *Uri kuuga wega*
*Uri kuuga wega*
*Iingiuma na iria*
*Ndaguitiriria* (ukurasa wa 34)

**MT1:** Umesema kweli
Umesema kweli
Ningalikuwa na maziwa
Ningalikunywesha! (Ukurasa wa 38)

**MT2:** *You have said well.*
*You have said well.*
*If I had milk*
*I would wash you in it.* (Ukurasa wa 36)

Katika mishororo miwili ya mwisho, mwandishi wa MC anawasilisha ujumbe aliokusudia kwa kutumia msemo. *Ingiuma na iria ndaguitiriria* (Tafsiri sisisi: ningalikuwa na maziwa ningalikumwagia). Katika jamii ya Gĩkũyũ, maziwa na pombe ni vinywaji viwili vilivyokuwa na umuhimu katika matambiko yao. Miviga ya kubariki wana na jamii ilitegemea pombe *(njoohi)* au mchanganyiko sawa na ule wa kuunda pombe ya kiasili ila haujachacha *(Ngogoyo).* Usemi ningalikuwa na maziwa ningalikumwagia ulitumiwa kukiri kupendezwa na jambo au kitendo alichofanya mtu kiasi cha kutaka kumtambua rasmi kwa kumwagia maziwa kama ilivyokuwa katika utamaduni wa Gĩkũyũ.

Dhana hii na uamilifu wa kifungu hiki umepotoshwa katika tafsiri inayotolewa katika MT1 na katika MT2. Jaribio la kuhawilisha dhana hii katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza limeishi kupotosha ujumbe. Aidha, tafsiri zinazotolewa zinakosa uasilia katika lugha husika na kwa jinsi hiyo zinaashiria ugeni wa namna fulani kutokana na hali ya kawaida ya matumizi ya lugha katika mifumo husika la lugha. Licha ya ugumu unaotambuliwa katika kutafsiri ushairi, zikiwemo nyimbo, tunatambua kuwa katika mazingira ya baadaukoloni, tafsiri sisisi kama ilivyo katika MT2 ni za kimakusudi licha ya kuwa zinapoteza uhalisia wa ‘nafsi’ ya wimbo katika

lugha chanzi. Hali kama hii inatufanya kuangazia upya haja ya kung'anga'nia kuibua ugeni hata pale ugeni huu unapoleta hali ya kupotoka kwa ujumbe, wakati mwingine hakuna mawasiliano kabisa.

### 3.2.6 Tafsiri ya Misimu

Msanjila na wenzake (2009) wanaifafanua misimu kuwa ni aina ya misemo katika lugha ambayo huzuka na kutoweka. Wanaendelea kusema kuwa kuzuka kwa misimu hutegemea mahitaji ya kikundi hicho kwa wakati huo na mara mahitaji hayo yanapokwisha, basi na misimu hiyo nayo hutoweka. TUKI (1990) wanaelekea kukubaliana na maelezo haya kuhusu dhana ya misimu. Kwa mujibu wa ufafanuzi wao, misimu ni mitindo ya lugha ambayo huzuka katika kipindi fulani na kutumiwa na kundi fulani la watu. Kutokana na fafanuzi hizi, suala la mabadiliko ya misimu baada ya muda ni la kawaida. Hata hivyo, tukiangazia suala la kwa nini misimu hutokea, tunapata kuwa misimu hutegemea mahitaji ya kikundi husika. Katika muktadha wa tasnifu hii, tunaeleza kuwa baadhi ya masuala yanayochochea uibukaji na matumizi ya misimu ni mabadiliko ya kiisimu, kijamii na kitamaduni ambayo tunayahusisha na athari za kikoloni. Kwa mfano, mtagusano baina ya jamii ya Gĩkũyũ na wakoloni ulizalisha maneno ambayo yalitumika wakati ule ila hayatumiki tena kwa sasa au hata yanapotumiwa, yamepata maana tofauti na iliyokuwepo awali. Kwa mfano, neno *Ngaati* katika MC lilitumiwa kwa maana ya Wakenya walioshirikiana na wakoloni. Leo hii, neno hili wakati mwingine hutumiwa kurejelea mtu mkali na mgumu kwa mali yake.

Katika MC, kuna baadhi ya misimu iliyotumiwa na inayofungamana na utamaduni chanzi kiasi kwamba tafsiri yake ama haiwezekani au inapofanywa inatukia kama tafsiri sisisi inayoibua ugeni katika matini tafsiri na kuathiri uelewekaji huku ikifungamana na utamaduni chanzi. Ni rai yetu hapa kuwa mwandishi wa MC aliitumia kimakusudi sio tu kuipamba lugha katika riwaya yake, bali pia alifanya hivi kimakusudi kuakisi uwezo na unyumbufu wa lugha yake asili. Kwa mfano:

**Mfano 19**

**MC:** *Mahua Kareendi* (Ukurasa wa 11)
**MT1:** Maua Kaledi (Ukurasa wa 13)
**MT2:** *Mahua Kareendi* (Ukurasa wa 11)

Katika mfano huu, dhana *Mahua Kareendi* inaweza kufasiliwa kuwa ni nomino ambatano. Ni jina analopewa mhusika wa kike ambaye ni kiwakilishi cha wasichana kama Wariinga jijini Nairobi na kwa upana wake katika jamii inayoangaziwa kwa ujumla. Amepewa jina la kimajazi lililo na sehemu mbili; *Mahua* neno lenye maana ya maua. Neno hili limetumiwa likiambatana na neno *Kareendi*. Neno hili ni simo iliyotumiwa katika kipindi kile kurejelea msichana mrembo. Katika matumizi ya kawaida neno hili ni *Reendi*. Katika muktadha wake wa matumizi limeambishwa kiambishi awali *ka*- ambacho katika lugha ya Kikuyu kinatumiwa kwa maana mbili: kwanza kuonyesha hali ya udogo na pili kuonyesha sifa ya uzuri.

Katika muktadha wa *Kareendi* katika MC, kiambishi *ka*- kinafasiriwa kwa maana zote mbili kwa kuwa, warejelewa ni wasichana ambao hawajakomaa kiumri, msichana wa kidato cha pili, na wasichana hawa katika mazingira yanayowasilishwa

kwenye riwaya ni wa kupendeza hasa kwa wavulana wa umri wao na hata kwa wanaume wa umri wa juu kama inavyojitokeza katika mahusiano baina ya Wariinga na Boss Kihara.

Tukiangazia jinsi dhana hii imehawilishwa katika MT1 tunapata kwamba, mtafsiri ametafsiri dhana ya maua na kudumisha dhana ya *Reendi* japo ameifanyia marekebisho ili isomeke kama dhana asili ya Kiswahili kuwa *Kaledi.* Maendelezo haya yametegemea fonolojia ya Kikuyu ambapo sauti /r/ huwa haitamkiki ila wasemaji wazawa wa lugha hii hutumia sauti iliyo baina ya /r/ na /l/. Aidha, herufi [n] na [d] zinapotumiwa katika mazingira sawa kama ilivyo katika neno *karee<u>nd</u>i* katika lugha ya Kikuyu sauti hii /nd/ hubainika kama sauti /d/. Licha ya kuzingatia kanuni za kiisimu za lugha chanzi, mtafsiri katika MT1 hajafanikiwa kuhawilisha dhana iliyofumbatwa katika simo *Kareendi* kama ilivyotumiwa katika MC. Tafsiri inayotolewa inakosa uasilia katika mfumo wa lugha ya Kiswahili na hivyo ni dhana ya kigeni. Kando na haya, mtafsiri anapoteza usanii wa majazi yaliyotumika katika MC.

Katika MT2, mtafsiri ameamua kudumisha dhana iliyotumiwa katika MC. Hali hii inaibua maneno ya kigeni katika mfumo wa Kiingereza. Uteuzi huu unakwaza mawasiliano na kupoteza maana na usanii unaobainika katika MC. Huenda mtafsiri katika MT2 alipata ugumu wa kutafsiri dhana hii kwa Kiingereza kutokana na tofauti za kitamaduni na za kitajriba katika ulimwengu halisi baina ya lugha hizi mbili. Mtafsiri angeweza kwa mfano kuumba upya dhana aliyolenga kuhawilisha kwa

kutumia simo linganifu katika lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa awali, katika mazingira ya baadaukoloni, uzalendo wa waandishi kwa lugha na tamaduni zao wakati mwingine hupendelewa wanapojieleza kwa lugha za kikoloni hata pale uamuzi huo unakwaza mawasiliano.

Mtindo huu wa kutafsri dhana zinazofungamana na utamaduni, hususan misimu, sisisi imedhihirika kwingineko katika MC, MT1 na MT2. Kwa mfano:

**Mfano 20**

**MC:** *Nguhiuuha ngithii-kuu* (Ukurasa wa 16)
**MT1:** Nataharuki kwenda wapi (Ukurasa wa 19)
**MT2:** *no-destination-why-should-I-hurry?* (Ukurasa wa 17)

Katika mfano huu, kifungu kinachorejelewa kimetumiwa na mwandishi wa MC katika kutoa maelezo ya vishawishi ambavyo Boss Kihara anatumia kumrai Kareendi amkubalie awe mpenzi wake. Anaorodhesha bidhaa za kifahari ambazo angemnunulia iwapo angekubali kuwa mpenzi wake. Samani na vyombo ataagiziwa kutoka ughaibuni, nguo na viatu mtawalia. Katika muktadha huu, mwandishi anachota kutokana na matumizi ya simo katika lugha ya Kikuyu kuelezea aina moja ya viatu ambavyo ni virefu kwa kutumia dhana ya *Nguhiuha-ngithii-kuu.* Dhana hii ikitafsiriwa sisisi ina maana ya *Nakimbia nikienda wapi?* Hii ni dhana inayotokana na mtindo wa matembezi ambao wasichana hutumia wanapovaa viatu hivi. Hawawezi kutembea kwa kasi kutokana na urefu wake na kwa jinsi hiyo huonekana kama wasio na haraka ya kufika wanakokwenda.

Mtafsiri katika MT1 ameitafsiri dhana hii kwa undani zaidi na kupotosha maana yake. Kwa kutumia neno *nataharuki*, maana iliyokusudiwa kutokana na taswira na tajriba aliyotumia mwandishi katika MC inapotezwa. Neno taharuki linaibua maana ambayo haikukusudiwa katika MC na kwa jinsi hiyo maana jumla ya kifungu kizima inavuka mipaka ya kimaana kama inavyobainika katika MC. Tunaweza kuhusisha hali hii na ukosefu wa umilisi wa mtafsiri wa kufasili MC kwa kuzingatia muktadha wake kiisimu na kitamaduni. Katika MT2, mtafsiri ametumia tafsiri sisisi na akazingatia maendelezo ya neno hili kwamba japo ni kifungu cha maneno, kinafasiliwa kama nonimo ambatano inayorejelea aina ya kiatu. Hata hivyo, ugeni unaoibuliwa na tafsiri hii ni dhahiri katika Kiingereza kwa kuwa hakuna kiatu ambacho kimepewa lakabu hii katika utamaduni wa Kiingereza. MT2 kwa ukalifu imeeleza kifungu hiki ifuatavyo:

> *When you step out in those shoes which you people have nicknamed*
> *'no-destination-why-should-I-hurry?...*

Maelezo haya japo yanatokea kwa lugha ya Kiingereza moja kwa moja yanaashiria kuwa jamii na utamaduni unaorejelewa sio wa Kiingereza. Hivyo mtafsiri katika MT2 anazalisha matini ambayo japo maneno yapo kwa Kiingereza, ujumbe wake na mandhari yake kijamii na kitamaduni hayafungamani na Kiingereza hata kidogo. Hii ni mojawapo ya sifa za kimsingi za matini za baadaukoloni zilizondikwa na Waafrika katika lugha za kikoloni kama vile Kiingereza (Bandia, 2014).

Licha ya sifa za baadaukoloni zinazodhihirika bayana kufikia sasa, bado suala la iwapo mtafsiri alifahamu athari za uteuzi wake katika kushughulikia MT1 na MT2 ni la mjadala. Kwa mfano:

**Mfano 21**

**MC:** *Ureenda gutwara uria ungi Ngong'u ni ki?* (Ukurasa wa 31)
**MT1:** Kwa nini wataka kumpeleka mwenzetu Ngong? (Ukurasa wa 34)
**MT2:** *Why are you taking this one to Ngong?* (Ukurasa wa 32)

Tukiangazia sehemu ya MC *…gutwara uria ungi Ngong'u…* imetumiwa hapa kama msimu wenye maana ya kuhatarisha maisha ya mtu. Ni matumizi yaliyopata umaarufu kutokana na mauaji ya mwanasiasa J. M. Kariuki ambaye mwili wake ulipatikana kwenye msitu wa Ngong'. Katika muktadha huu wa matumizi kwenye MC, Mwaura alimesimamisha gari lake kwa ghafla nusura amrushe mmmoja wa abiria wake. Muturi ndiye anayetumia maneno haya kulalamikia tabia hii ambayo inahatarisha maisha ya abiria yule. Suala la kumpeleka mtu Ngong' lina msingi wake katika mazingira ya Kenya ikiwemo katika utamaduni chanzi wa Gĩkũyũ kwani, J. M. Kariuki alikuwa ni mmoja wa viongozi waliovuma sana katika miaka ya sabini miongoni mwa wenyeji wa eneo la kati la Kenya. Tafsiri anayoitoa mtafsiri katika MT1 haina ufafanuzi wowote unaolenga kutoa muktadha wa kijamii wa matumizi ya kifungu hiki. Hii huenda ni kutokana na ukweli kwamba wasomaji wa MT1 ambayo ipo kwa Kiswahili hawana haja ya kuelezewa etimolojia ya kifungu hiki. Katika mawazo ya mwandishi aliye pia mtafsiri wa MT1, Kiswahili kimefasiliwa kama lugha ya kitaifa na hivyo haiangaziwi kwa uhalisia wake kimatumizi kama inavyobainika katika *Decolonizing the Mind* na katika *Detained.*

Ukosefu wa msimamo katika kushughulikia tafsiri ya dhana zinazofungamana na utamaduni wa MC katika MT2 unazidi kudhihirika. Tukizingatia mfano huu, mtafsiri ametumia mkakati wa tafsiri sisisi ila anatumia tanbihi kutoa maelezo yanayobainisha muktadha wa kijamii wa ufasili wa kifungu hiki. Kwa mujibu wa wanabaadaukoloni akiwemo Ngũgĩ wa Thiong'o matukio haya ya uibuaji wa ugeni katika mifumo ya lugha za kigeni yanayotokana na tafsiri sisisi ni ya lazima kutokana na haja ya kueleza tajriba za kiasili na tamaduni asili katika uandishi wa Kiafrika. Hii ni njia ya kipekee ya kuzipa lugha na tamaduni hizi za kiasili mchomozo na kuziwezesha katika mazingira jirani na lugha za kipebari ambazo awali ziliangaziwa kuwa zenye uwezo na mamlaka zaidi. Kwa jinsi hii, tafsiri hizi zinakuwa ni jukwaa la mapambano ya lugha na tamaduni za kiasili dhidi ya lugha na tamaduni babe za kikoloni kwa lengo la kuzikomboa na kuziwezesha.

Kutokana na mifano hii inayoangazia jinsi misimu iliyotumiwa katika MC imeshughulikiwa katika MT1 na MT2, ni dhahiri kwamba licha ya kudumisha uaminifu kwa mwelekeo wa baadaukoloni katika tafsiri zake, mtafsiri anaelekea kukosa uhakika wa ama adumishe uaminifu kwa itikadi yake ya ukombozi wa lugha na tamaduni chanzi dhidi ya tamaduni babe za lugha za kigeni katika MT2 au afanikishe mawasiliano. Ukinzani wa mikakati inayotumiwa katika mifano tofauti huenda umetokana na uchangamano wa mchakato wa tafsiri wenyewe hata bila kuzingatia mahitaji ya baadaukoloni.

### 3.2.7 Tafsiri ya Majazi

Wamitila (2003:106) anaifafanua dhana ya majazi kuwa ni:

> Mbinu ya kuwapa wahuska majina ambayo yanaakisi au yanatuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Jina la mhusika linakuwa kielekezi cha tabia yake. Majazi huhusisha pia majina ya mahali, mandhari, n.k. *Mbinu hii ina uzuri wa kuwa inamsaidia msomaji kuweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi sana.* Pili, mwandishi anaweza kuitumia mbinu hii kuuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima.
> *(Msisitizo wangu)*

Kutokana na maelezo haya, ni bayana kuwa hii ni mbinu ya kisanaa ambayo inatekeleza dhima muhimu katika uandishi wa fasihi. Uamilifu wa majazi katika kazi ya fasihi hasa tunapoangazia majazi katika kiwango cha majina ya wahusika unapata umuhimu hasa kutokana na dhima ya wahusika katika kazi yoyote ile ya fasihi. Maelezo kwamba waandishi hutumia majazi kutoa maoni yao kuhusu wahusika au hata kutoa misimamo yao kuhusu hadithi nzima pia ni muhimu hasa katika muktadha wa baadaukoloni na kwa jinsi hiyo katika MC ya utafiti huu. Takriban wahusika wote wamepewa majina ya kimajazi ambayo yanatekeleza dhima mbalimbali. Aidha, majazi haya yamefungamana na utamaduni wa lugha chanzi na kwa jinsi hiyo hatuna budi kuchanganua uhawilishaji wake katika tafsiri hasa tukizingatia umuhimu ambao Wamitila (2003) anaeleza kuwa:

> *Mbinu hii ina uzuri wa kuwa inamsaidia msomaji kuweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi sana.*

Uchanganuzi wetu wa dhana hii unalenga kudadisi maswali kadhaa ikiwemo: Je, majazi yametafsiriwa vipi katika MT1 na MT2? Pili, tunalenga kujibu swali la: Je, uhawilishaji uliofanywa katika MT1 na MT2 una athari gani kwa uelewekaji na

ubora wa matini hizi katika mifumo husika kilugha na kitamaduni? Katika uchanganuzi huu, tunatoa muktadha chanzi ambapo majazi haya yametumika katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* pamoja na katika muktadha wa jamii ya Gĩkũyũ kabla ya kuangazia jinsi ulivyotafsiriwa kwa Kiswahili na Kiingereza mtawalia.

**Mfano 22**

**MC:** *Mithita Mugwate* (Ukurasa wa 37)
**MT1:** *Mr. Mugwate* (Ukurasa wa 41)
**MT2:** *Mr. Mugwate* (Ukurasa wa 39)

Kifungu hiki kinatokana na masimulizi ya Wangari akielezea jinsi alivyokamatwa na polisi pale hotelini alikokuwa ameenda kusaka kibarua. Ana uchungu kwamba mtu mweusi kama yeye ndiye anayemsaliti na kumtoa kwa polisi, ambao ni watu weusi kama yeye. Maneno haya yanasemwa na Mzungu mwenye hoteli ile ambaye anampongeza Bwana Mugwate kwa "kazi nzuri." Jina la kimajazi *Mithita Mugwate* katika MC linaashiria tabia yake katika ngazi mbili na kuibua ucheshi kwa wakati huo huo. Kwanza, tukiangazia neno la kwanza; *Mithita*, linabainika kuwa ni utohozi wa neno *Mister* la Kiingereza ambalo halina kisawe cha moja kwa moja katika lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, tukiliangazia kama neno asilia la Kikuyu, neno hili linapata maana tofauti ya kuwa ni uume katika hali ya wingi. Huenda mwandishi hakukusudia kuibua maana hii kwa kutumia neno hili. Hata hivyo, tukihusisha matukio katika kifungu hiki na hali ilivyokuwa kwa Wangari alipoenda kwa duka la mtu mweusi kusaka ajira:

> …Nduka iraari ya muundu muiru, Ngoro yaakwa iraathera haniini. Ndiraamuumburira mathiina maakwa moothe. Hi! Araagwa na mitheko!

> Araanjiira *wira uria aangihee no wa gutaaganura maguru*, ati atumia aria aitikaangu maai haniini ni o mooi wira usio muno. (MC; Ukurasa wa 37)

Kifungu hiki kinaelezea aliyokumbana nayo kwamba mzee mwenye duka anamwambia kazi ambayo anaweza kumpa ni ya *kupanua miguu pekee*. Urejelezi huu wa kingono huenda ndio unaomfanya mwandishi kutohoa neno *Mister* katika Gĩkũyũ kuwa *Mithita* akifahamu fika kwamba litaibua utata wa kimaana kwenye aya inayofuata. Hata hivyo, neno la pili; *Mugwate* ndilo la kimajazi na linalooana na tabia ya mhusika anayerejelewa. Yeye ni meneja katika hoteli ile na Wangaria katika pita pita zake akitafuta ajira anaishia kurudi katika hoteli ile. Bwana *Mugwate* anamkaribisha kiti na kumwarifu atulie ndipo apige simu kuulizia kazi mahali alikokuwa na uhakika Wangari angefaidika. Badala yake, anawapigia polisi ambao wanakuja na kumtia Wangari mbaroni kuwa ni mshukiwa wa wizi.

Neno *Mugwate* katika lugha ya Gĩkũyũ lina maana ya *Mateka* kwa Kiswahili na *Hostage* kwa Kiingereza. Kwa kurejelea muktadha ambamo neno hili limetumiwa katika MC, tunapata aina mbili za mateka; kwanza mhusika *Bwana Mugwate* mwenyewe ni mateka japo ana mamlaka. Amekengeuka kiasi cha kumdharau mtu mweusi mwenzake ambaye amefika pale kuomba kazi. Anabainika kuwa ni mtumwa wa mkubwa wake ambaye ni Mzungu. Hali hii katika muktadha wa baadaukoloni ni ya kiukoloni mamboleo ambapo tunapata mtu aliyewahi kutawaliwa japo yu huru bado angali mtumwa kimawazo na kiitikadi. Tukio la pili la *Mateka* ni hali ambayo Wangari anajipata. Anasingiziwa wizi na kukamatwa na baadaye kushtakiwa mahakamani. Baadaye analazimishwa kurejea kwao *Ilmorog* ili kusaidia serikali

kuwakamata wezi. Hali hizi zote zinahusu Wangari kufanya mambo ambayo hakujitakia ila analazimika kuyafanya kutokana na uhalisia katika maisha yao.

Tafsiri inayotolewa katika MT1 na MT2 inaibua ugeni kwa kudumisha jina la mhusika huyu kuwa *Mr. Mugwate* katika Kiswahili na katika Kiingereza. Kwanza, matumizi ya *Mr.* kwa Kiswahili hayawezi kuelezewa kwa kuwa kuna kisawe faafu ambacho kingewasilisha maana hii; *Bwana.* Ucheshi unaotokana na *Mithita* katika MC hauwezi kuhawilisha katika MT1 au MT2 na kwa hivyo mtafsiri angejifunga kwa maana halisi ya neno hilo na kulitafsiri kisemantiki hasa kutokana na uamilifu wake kama utambulisho wa mtu. Neno *Mugwate* katika Kiswahili huenda kwa kuwa hakuna namna ya kulitafsiri na kudumisha usanii wa kimajazi uliomo ndani. Hata hivyo uamuzi huu unapoteza usanii huu kwa kuwa haufasiriki katika Kiswahili. Katika MT2, *Mithita* linatafsiriwa kuwa *Mr.* Hii ni tafsiri sahihi kimaana ila haiwasilishi ucheshi na maana zinazojitokeza katika MC kama ilivyojadiliwa hapo awali. Kwa kudumisha neno *Mugwate,* mtafsiri kama alivyofanya katika MT1, anapoteza usanii wa kimajazi. Ugeni anaoibua unachangia kuipa MT2 “ladha” ya kigeni na kuashiria kwamba huenda MT2 sio matini asilia katika mfumo wa lugha na utamaduni wa Kiingereza.

Katika *Caitaani Mutharaba-ini* takriban wahusika wote wakuu wamepewa majina ya kimajazi. Hii huenda ni kutokana na majukumu ambayo wamepewa katika kuiendeleza riwaya hii pamoja na uwakilishi wa kimajii katika riwaya husika. Kwa mfano;

**Mfano 23:**

**MC:** Wangari (Ukurasa wa 32)
**MT1:** Wangari (Ukurasa wa 36)
**MT2:** Wangari (Ukurasa wa 33)

**MC:** Muturi (Ukurasa wa 33)
**MT1:** Muturi (Ukurasa wa 36)
**MT2:** Muturi (Ukurasa wa 34)

**MC:** Gatuiria (Ukurasa wa 32)
**MT1:** Gatuiria (Ukurasa wa 35)
**MT2:** Gatuiria (Ukurasa wa 33)

Majina ya wahusika katika mfano huu yanadumishwa katika tafsiri za MT1 na MT2 kama yalivyowasilishwa kwenye MC. Tukiangazia uamilifu na nafasi za wahusika hawa katika MC na tukayahusisha na utamaduni ambao umewazalisha tunapata kwamba; *Wangari* ni mhusika wa kike mwenye umri wa juu akilinganishwa na wahusika wengine katika riwaya hii. Jina *Wangari* tunaweza kulifasiri kama la kimajazi kutokana na dhima anayotekeleza kama mzazi wa kike. Aidha, mhusika huyu ni kiwakilishi cha masaibu yanayowapata wananchi licha ya kujinyakulia uhuru.

Katika utamaduni wa Gĩkũyũ, *Wangari* ni mmoja kati ya wasichana wa Gĩkũyũ na Mumbi ambao wanaaminika kuwa ndio wazazi wa jamii hii. *Wangari* anaaminika kuwa alikuwa mwana wao wa tatu baada ya Wambui na Wanjiru. Kwa kupewa jina Wangari mhusika anayerejelewa amepewa dhima ya mama katika riwaya hii. Anatekeleza jukumu la mzazi kwa wahusika kama vile Gatuiria na Wariinga. Katika simulizi ya asili ya jamii ya Gĩkũyũ, Wangari ndiye mama wa ukoo wa *Angari*

ambao pia wanaitwa *Aithe Kahuno* kwa maana ya mwana aliyezaliwa kabla ya wakati wake. Huenda mwandishi aliteua jina *Wangari* kati ya majina kumi ya wasichana wa Gĩkũyũ na Mumbi kwa sababu hii. Kwa upande mmoja, anamtumia kama kiwakilishi cha jinsi watu waliowahi kutawaliwa na wakoloni wanakumbana na changamoto katika nchi zao wenyewe na kwa upande wa pili yeye ni kiwakilishi cha uthabiti ambao watu hawa wako nao katika kukabiliana na changamoto hizi pamoja na juhudi zao za kupigania haki na usawa. Mhusika *muturi* ni kiwakilishi cha wafanyakazi ambao daima wanadhulumiwa na walio na uwezo. Ni mfanyakazi na kiongozi wa wafanyakazi ambao wanapigania haki zao. Jina hili ni la kimajazi kwa kuwa muturi katika jamii ya Gĩkũyũ inarejelea mhunzi. Katika jamii ya Gĩkũyũ, wahunzi walikuwa watu wa kuheshimiwa kutokana na kazi waliyotekeleza ya kutengeneza ala za kulimia mashamba pamoja na za kupigana vita na maadui waliovamia jamii yao.

Gatuiria katika MC amesawiriwa kama kijana aliye na elimu ya kisasa. Ni msomi ana anafanya kazi katika chuo kikuu. Anaonekana kuwa aliyekengeuka kutokana na athari za kigeni kwa utamaduni asilia na lugha yake ya Kikuyu. Akilalamikia hali hii anaeleza ifuatavyo:

> Thiomi cia bururi witu ciathiire ku? Mari ha mabuku maandike na ndemwa cia thiomi cia bururi witu? Kirira giitu kiri ku riu? Uugi wa maithe maitu wi ha? Uthamaki wa maithe maitu wi ha? Booi wa bururi witu ni watharirio, mwaki ukihorio, njung'wa ikinyugutwo kiara iguru, nganatha nayo ikimomorwo, aanake a bururi magivuuria matimu nango makumbi-ini. Wuui tutituirie ha kwirutira moohoro ma teme na bururi witu i! *Mwana utari na aciari a Kumutaara ri, ni ki kiingigiria ahahate mai ma mugeni eeciriitie ni rukuri araamonjora?*
>
> (MC – Ukurasa wa 53) (Msisitizo wangu)

Katika kifungu hiki, Gatuiria analalamikia hali ya kutoweka kwa ustaarabu, historia na mafundisho ya kiasili. Anahitimisha kwa kuuliza swali ambalo likitafsiriwa sisisi litakuwa na maana ya:

> *Mwana asiye na wazazi wa kumpa wosia, nini kitamzuia kuyaokota mavi ya mgeni na kuyala akidhani ni chakula kitamu anafurahia?*

Gatuiria amepewa kazi ya kudadisi kama vile kitenzi *tuiria* katika lugha ya Kikuyu linavyomaanisha. Isitoshe, katika chuo kikuu, yeye ni mmoja wa wanafunzi wanaotafitia tamaduni za kiasili. Yeye ni kiwakilishi cha ufufuo wa tamaduni, lugha na ustaarabu wa kiasili uliotawaliwa na tamaduni babe za mkoloni. Majina ya wahusika hawa; Wangari, Muturi na Gatuiria yamedumishwa katika MT1 na katika MT2. Uamuzi huu unatokana na uchangamano wa majazi yaliyotumiwa katika MC kama ilivyoelezwa hapo juu. Hata hivyo, licha ya kuashiria utamaduni wa kigeni katika MT1 na MT2, uhamishaji wa dhana hizi jinsi zilivyo katika mfumo wa Kiswahili na Kiingereza unatatiza maana, uelewekaji na mawasiliano kwa ujumla ya matini tafsiri za Kiswahili na Kiingereza mtawalia.

Msomaji wa MT1 au MT2 ambaye hana ufahamu wa lugha na utamaduni chanzi wa MC anapata ugumu kufasili majina haya kama majazi yaliyo na maana ya ndani. Kama alivyojirejelea mwandishi wa MC kuwa ni mwimbaji wa *Gĩcaandĩ* katika sehemu ya utangulizi, anatumia usanii kama majazi kuwasilisha maana changamano zaidi kama afanyavyo mwimbaji wa *Gĩcaandĩ* kwa kutazama alama zilizopo kwenye ala yake. Hali hii aya kukwaza mawasiliano kwa kuibua ugeni unaotokana na udumishaji wa dhana za kimajazi katika MT1 na MT2 kutoka MC unashuhudiwa

tena tunapoangazia majina ya wezi wanaotoa ushuhuda wa ubabe wao wa wizi kwenye pango. Kwa mfano:

**Mfano 24:**

**MC:** Robin Mwaura (Ukurasa wa 31)
**MT1:** Robin Mwaura (Ukurasa wa 34)
**MT2:** Robin Mwaura (Ukurasa wa 32)

**MC:** Gitutu wa Gataanguru (Ukurasa wa 95)
**MT1:** Gitutu wa Gataanguru (Ukurasa wa 102)
**MT2:** Gitutu wa Gataanguru (Ukurasa wa 97)

**MC:** Kihaahu wa Gatheeca (Ukurasa wa 105)
**MT1:** Kihaahu wa Gatheeca (Ukurasa wa 112)
**MT2:** Kihaahu wa Gatheeca (Ukurasa wa 107)

**MC:** Mwireri wa Mukiraai (Ukurasa wa 159)
**MT1:** Mwireri wa Mukiraai (Ukurasa wa169)
**MT2:** Mwireri wa Mukiraai (Ukurasa wa 162)

**MC:** Nditika wa Nguunji (Ukurasa wa 176)
**MT1:** Nditika wa Nguunji (Ukurasa wa 187)
**MT2:** Nditika wa Nguunji (Ukurasa wa 178)

Majina ya wahusika hawa wote yanatokana moja kwa moja na sifa zao au maumbile yao kama yanavyoelezewa kwenye riwaya. Robin Mwaura ambaye ni dereva wa matatu ambamo matukio ya awamu ya kwanza ya riwaya yanatokea anabainika baadaye kuwa ni tapeli na mwizi. Anaweka pesa mbele ya utu kama inavyobainika Wangari anapoeleza kuwa hana nauli. Tukiangazia jina lake, la kwanza *Robin* linakaribiana kimatamshi na neno *Robbing* kwa Kiingereza ambalo linarejelea hali ya kuiba kwa kutumia mabavu. Jina la pili *Mwaura* tunaweza kulihusisha na kitenzi cha Kikuyu *Kwaura*, ambacho katika lugha isiyo rasmi kina maana ya kuiba.

Gituutu wa Gataanguru ni jina la kimajazi ambalo linaunganisha majina mawili: *Gitutu* ambalo lina maana ya *funza mkubwa* na jina *Gataanguru* ambalo lina maana ya *Minyoo* katika hali ya udogo. Funza na minyoo ni vimelea na hunyonya wanyama wengine. Hii ni sifa ambayo inadhihirika katika ushuhuda anaotoa. Inabainika kwamba yeye amepata utajiri kwa kuwanyanyasa wafanyakazi; kuwanyonya damu na jasho lao, kama kimelea. Mwandishi zaidi ya kutumia majazi katika jina la mhusika huyu, anatumia utamaduni wa LC katika kuendeleza jina ambapo anatumia jina la mzazi kama ilivyo kaida katika jamii ya Gĩkũyũ. Kwa mfano, mwandishi wa MC mwenyewe anaitwa Ngũgĩ wa Thiong’o yaani ni Ngũgĩ mwana wa Thiong’o. Vivyo hivyo, Gitutu *wa Gataanguru* lina maana ya Gitutu mwana wa Gataanguru. Uhusisho huu wa mwana na baba unadhihirika katika majina ya wezi wote wanaorejelewa. Kwa mfano; *Kihaahu wa Gatheeca* ambaye jina lake ni la kimajazi. Taswira tunayochorewa na maelezo ya mwandishi ni kwamba mhusika huyu ni mrefu na mwembamba. Sifa hii inahusiana moja kwa moja na jina la baba *Gatheeca* ambalo linaweza kuhusishwa na kitenzi *Gutheeca* chenye maana ya kudunga. Jina lake *Kihaahu* limetokana na kitenzi *Hahura* chenye maana ya kutia wasiwasi. Maelezo yake katika kutoa ushuhuda wa jinsi alivyo bingwa wa wizi ni dhihirisho tosha. Kwa mfano, anajieleza ifuatavyo:

> *Ni nii nderi iria ireraga riera-ini huungu ikoorira itara-ini* hii ina maana ya *Mimi ndiye tai ambaye humfanya mwewe kukimbilia kiotani.*

Tukiangazia kifungu hiki, Kihahu wa Gatheeca anajifananisha na tai ambaye ni mkali kiasi cha kumtia mwewe wasiwasi na kumfanya kukimbia na kujificha.

Kwingineko, Kihaahu wa Gatheeca anajidai kuwa anapenda kushiriki mapenzi haramu na wake za watu kiasi cha kuwafanya waachane na waume zao. Majazi yanatokea katika hali ya kumithilisha kitendo cha ngono na kitendo cha kudunga kama jina lake la pili linavyoashiria.

*Mwireri wa Mukiraai* naye ni mmoja wa wezi wanaoshindana pale pangoni. Hata hivyo ushuhuda wake hauwaridhishi walioko pale kwa kuwa “hajafikia kiwango” kilichowekwa na watangulizi wake kuhusu mali waliyo nayo. Anawatuliza kwa kuwaambia kuwa: *Nguuguni iireagira ruku-ini na ikaaya kuigana*kwa maana ya kunguni hujitunza akiwa kwenye ukuni hadi akawa mkubwa. Mwireri wa Mukiraai anajitokeza kama mhusika ambaye anaamini katika kujiimarisha; *kwirera-kujilea*, katika wizi kwa kutegemea itikadi.

*Nditika wa Nguunji* naye amepewa jina la kimajazi linalooana na tabia zake. Jina lake linatokana na maneno mawili ya Gĩkũyũ *Tindika* – kitenzi chenye maana ya kusukuma na *Kuunja* – kitenzi chenye maana ya kunja. Ushahidi wake unaashiria jinsi anavyowanyanyasa wafanyakazi wake na kutumia uwezo wake kupata chochote atakacho. Unyanyasaji huu unawasukuma wafanyakazi wake kuwa masikini zaidi. Aidha anaamini katika unyakuzi wa mali ya umma kama anavyoeleza mwenyewe katika ushuhuda wake (MC, Ukurasa wa 178):

> Rekeei andu aitu turiganirwo ni mauundu maathirire. Icio ciari irooto njuru…mahahura-toro. Rekeei riu tugwatanire mauundu matatu: *kuhuria, Gukuunja na Gutitika.* Utatu Mutheru. *Huria Kuunja, Titika* uroreetie na gwaku.
> (Msisitizo wangu)

Maneno yaliyo katika herufi za mlazo yana maana ya *Kunyakua, Kukunja na Kubeba.* Anarejelea hali hizi tatu kuwa utatu mtakatifu wa wizi wa kisasa. Maneno haya yanaoana na jina alilopewa na kwa jinsi hiyo jina lake ni la kimajazi.

Tukiangazia jinsi majina haya ya kimajazi yameshughulikiwa katika MT1 na MT2, tunapata kwamba majina yamedumishwa jinsi yalivyo katika MC. Shirinzadeh na Mahadi (2014) wanaeleza kwamba katika kutafsiri nomino za pekee kama vile majina ya wahusika, mielekeo inayopendelewa sana ni ile ya uhawilishaji wa jina jinsi lilivyo kutoka LC na kulitafsiri jina husika kuafiki mfumo wa LP. Mtafsiri wa MT1 na MT2 katika muktadha wa utafiti huu alidumisha majina haya jinsi yalivyotumiwa katika MC. Huenda hali hii ilichangiwa pakubwa na ukweli kwamba majina haya ni ya kubuni; hayapo katika utamaduni halisi wa jamii ya MC, isipokuwa jina Mwaura na Robin. Isitoshe, uamuzi wa kuyadumisha jinsi yalivyo huenda ulichangiwa na haja ya kuwasilisha majazi ambayo hayangeumbika upya katika mifumo ya MT1 na MT2 mtawalia. Uamuzi huu hivyo basi unaishia kuibua ugeni katika matini hizi na kuashiria kuwa hazina uasilia katika mifumo ya Kiswahili na Kiingereza.

Kwingineko, kuna majina ya kimajazi ambayo yameshughulikiwa kwa njia tofauti katika MT1 na MT2. Kwa mfano:

**Mfano 25:**

**MC:** Professor Kimenyiugeni (Ukurasa wa 56)
**MT1:** Profesa Kijuaugeni (Ukurasa wa 61)
**MT2:** Professor Kimenyiugeni (Ukurasa wa 58)

Hili ni jina la mmoja wa wahadhiri katika chuo kikuu ambako Gatuiria anafanya kazi. Profesa mrejelewa amepagazwa jina la kimajazi *Kimenyiugeni* kutokana na ujuzi wake wa historia ya kigeni kama anavyoeleza Gatuiria katika MC, Ukurasa wa 56:

> "*I Professor Kimenyiugeni?"*
> *"Ucio ni wa Ruhoonge rwa Moohoro-ma-Tene. No we ooi o moohoro-ma-tene ma Ruraaya tu."*

Jina lake hivyo ni la kimajazi moja kwa moja kutokana na ufahamu wake wa historia ya kigeni. Jina hili limetafsiriwa katika MT1 sisisi kuwa *Profesa Kijuageni.* Hali hii inazalisha hali ile ile ya kimajazi katika mfumo wa MT1 kama ilivyo katika MC. Uteuzi wa kutumia tafsiri sisisi kushughulikia jina la profesa anayerejelewa katika Kiswahili unaashiria ukosefu wa muwala katika mikakati anayotumia mtafsiri wa MT1 kwa kuwa ni kinyume na uhawilishaji wa moja kwa moja anaotumia katika kushughulikia majina ya kimajazi ya wezi wanaoshindana pale pangoni. Aidha, udumishaji wa majina ya kimajazi ya wahusika kama vile Wangari, Muturi na Gatuiria yanaweza kuelezwa kuwa yanadumishwa kwa kuwa ni majina halisi katika utamaduni chanzi wa MC. Hata hivyo, majina ya wezi pamoja na ya Profesa *Kimenyiugeni* si majina halisi katika utamaduni wa Gĩkũyũ ila ni majina ya kubuni yanayotokana na ubunifu na usanii wa mwandishi wa MC mwenyewe. Licha ya kuwa hakuna mkakati mmoja uliotumiwa kuyashughulikia huenda uamuzi anaofanya mtafsiri wa MT1 na MT2 unaishia kuwa na athari hasi kwa ubora na wepesi wa kimawasiliano wa matini hizi mbili kwa hadhira lengwa. Hata hivyo, uamuzi huu unafanikisha juhudi za mwandishi aliye pia mtafsiri wa MT1 na MT2 za kuhawilisha utamaduni wa MC kama njia mojawapo ya kuuimarisha kwa kuupa uhai

mpya katika mifumo ya Kiswahili na Kiingereza.

### 3.3 Mwingiliano baina ya tamaduni: Ithibati za Kiisimu katika MC

Miongoni mwa athari kuu za ukoloni kwa jamii zilizotawaliwa zinazobainishwa na wasomi wa baadaukoloni ni mwathiriano baina ya tamaduni za watawala na watawaliwa pamoja na lugha zao. Mwathiriano huu hudhihirika katika fasihi kupitia kwa lugha ambayo huwa na mchanganyiko wa kimfumo, kimsamiati na kitamaduni baina ya tamaduni na mifumo ya kiisimu ya jamii iliyotawaliwa na jamii iliyotawala. Tukiangazia uandishi wa baadaukoloni hasa katika ngazi ya lugha, tunapata ithibati za madai ya Bandia (2010) kuwa uandishi wa Kiafrika ni zoezi la tafsiri hasa ya kisemiotiki ambapo ngano na masimulizi huwasilishwa katika maandishi. Kwa waandishi wa Kiafrika wanaoandika katika lugha za kikoloni kama vile Kiingereza, lugha inayotumika ina msingi wake katika utamaduni chanzi wa Kiafrika licha ya kutumia maneno ya Kiingereza. Hali hii ndiyo inayochangia mawazo ya wasomi kama vile Ngũgĩ wa Thiong'o (2009) ambaye anajadili suala la tafsiri miongoni mwa waandishi wa Kiafrika. Anaeleza kwamba ili kuwaelewa vyema waandishi hawa, pana haja ya kutafakari tafsiri kama zoezi la uhawilishaji wa maana kutoka lugha na utamaduni mmoja hadi mwingine na kwa wakati huo huo kuiangazia dhana ya uandishi kama mchakato wa tafsiri unaotokea katika kiwango cha akilini hasa kwa waandishi wa Kiafrika. Hali hii ya tafsiri akilini inatokana na uhalisia wa waandishi hawa kutagusana na tamaduni zao asili na utamaduni wa kikoloni. Aidha, masimulizi yao aghalabu huangazia masuala ya jamii zao asilia ila wanayawasilisha

katika lugha ya kigeni. Udhihirikaji wa tafsiri halisi, yaani tafsiri baina ya lugha mbili tofauti, aghalabu unazalisha mwingiliano baina ya tamaduni mbili au zaidi na kwa jinsi hii husheheni lugha ambayo haina uasilia tunapoifungamanisha na utamaduni unaowakilishwa.

Kwa mujibu wa Klinger (2015) mwathiriano baina ya lugha na tamaduni hizi unatokea sio tu katika uhawilishaji wa maana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine ya pili bali pia hutokea katika mazingira ya hadithini. Kwa mintarafu hii, suala la lugha mseto katika tafsiri linachangia ujengaji wa mtazamo wa mwandishi kuhusu ulimwengu wake na ulimwengu anaousawiri katika maandishi yake na kwa wakati huo huo huashiria hisia za mwandishi kwa lugha husika. Madai haya ni muhimu hasa tunapoyaweka katika muktadha wa utafiti huu ambapo masuala la lugha, utamaduni, itikadi na utambulisho ni ya kimsingi. Katika kuchanganua mwathiriano uliopo baina ya tamaduni katika sehemu hii, ni muhimu kuweka wazi kuwa mwathiriano huu unabainika kupitia kwa mwathiriano kilugha baina ya Kikuyu, Kiswahili na Kiingereza mtawalia. Ngũgĩ wa Thiong'o anaweka bayana vichocheo vyake vya kutumia lugha ya kiasili kuandikia fasihi yake ambapo katika kitabu chake, *Detained: A Writer's Prison Diary* anaeleza ifuatavyo:

> Mawazo huru kwenye karatasi shashi! Nilikuwa nimejipa kibarua kigumu makusudi. Nilikuwa nimeamua kutumia lugha ambayo kufikia sasa haikuwa na riwaya ya kiasasa. Changamoto kwangu binafsi na kama njia mojawapo ya kuthibitisha imani yangu katika uwezekano wa kutumia lugha zote za Kenya ambazo maendeleo yake kama nyenzo ya kupambana na ubepari yalikuwa yamedumazwa na utawala wa kikoloni wa Uingereza pamoja na utawala wa ukoloni mamboleo wa Kenyatta na washiriki wake katika KANU.
>
> (Ngũgĩ, 1981:8) *Ty*

Nukuu hii inaeleza wazi imani ya Ngũgĩ kuwa lugha zina uwezo wa kutumiwa kama zana za kujikomboa dhidi ya ubepari wa kikoloni. Katika kuzungumzia uamalifu wa lugha katika *Decolonizing the Mind* anaeleza ifuatavyo:

> Lugha kama mawasiliano na kama utamaduni hivyo basi ni mazao yanayozalishana. Mawasiliano hujenga utamaduni: utamaduni ni mbinu ya mawasiliano. Lugha hubeba utamaduni, na utamaduni hubeba, hasa kupitia kwa masimulizi na fasihi, mfumo mzima wa maadili ambao huisaidia jamii kujitambua na kutambua nafasi yake ulimwenguni. (Ngũgĩ, 1981: 15-16)

Kutokana na nukuu hii ni wazi kuwa kwa mtazamo wake, suala la lugha ni la kimsingi katika kudumisha, kuwasilisha na kujenga utamaduni na utambulisho wa jamii na hata wa mtu binafsi. Katika kujibu wahakiki wake anaeleza kwamba:

> Ninaamini kuwa kuandika kwa lugha ya Kikuyu, lugha ya Kikenya, lugha ya Kiafrika, ni sehemu ya juhudi za Wakenya na Waafrika za kupinga ubepari. (Ngũgĩ, 1981: 28).

Uwezo uliopo katika lugha ambao anazungumzia ndicho kichocheo kikuu cha yeye kuiandika MC katika Kikuyu. Hata hivyo, mawazo yake yanaelekea kudokeza uwepo wa lugha ya kiasili ambayo ni sanifu na iliyojitenga na athari za ubepari na ukoloni inayoweza kutumika kama kiwakilishi cha juhudi za kukabiliana na mahusiano ya kiuwezo yasiyo sawa yanayoshuhudiwa katika mazingira ya baadaukoloni. Tunapodadisi maamuzi na uteuzi kiisimu anaoufanya katika uandishi wa MC tunapata ishara na dalili za kuwa lugha kama hii haipo kamwe. Baadhi ya uteuzi anaoufanya unaashiria athari za lugha ya kigeni, utamaduni wa kigeni na hata itikadi za kigeni. Kwa mfano:

**Mfano 26:**

**MC:** *Caitaani Mutharaba-ini* (Anwani ya MC)

Anwani ya MC *Caitaani Mutharaba-ini* ni kiashiria cha ugeni katika lugha ya Kikuyu. Maneno haya mawili yanarejelea dhana ambazo ni za kigeni na zinazotokana na athari za mtagusano wa kitamaduni, kijamii na kiisimu baina ya Kikuyu, Kiswahili na hata Kiingereza. *Caitaani* ni neno linalorejelea "kiumbe" anayeaminika kuwa ni mwovu katika muktadha wa imani ya Kikristo. Dhana hii haipo katika utamaduni wa Gĩkũyũ na ndiyo maana neno *Caitaani* linahusishwa na neno la Kiswahili *Shetani* ambalo lina asili ya Kiingereza[16] *Satan.* Dhana inayorejelewa na *Caitaani* inaaminika kuwa ni pepo ambaye anawafanya wanadamu kutenda maovu.

Katika utamaduni wa Gĩkũyũ, pepo wana jina la kiasili la *Ngoma.* Kisha wanagawika katika makundi mawili; *Ngoma Njega* - pepo wazuri, na *Ngoma Njuru* –pepo wabaya. Hivyo, kiwakilishi chenye asili ya kigeni *Caitaani* kimetumika hapa kama kisawe cha *Ngoma Njuru.* Ugeni huu katika MC, japo unaonekana kama dhana ya kawaida kutokana na mwathiriano baina ya jamii ya Gĩkũyũ na imani ya Kikristo, ni ishara ya athari za ubepari wa kitamaduni, kiimani na hata kilugha unaotokana na mtagusano baina ya jamii tawaliwa (Gĩkũyũ) na jamii tawala (Mkoloni Mwingereza). Japo mwandishi anatumia maneno anayoamini yanatokana na lugha ya Kikuyu, udadisi wake unaonyesha kuwa matumizi haya hayachangii ukombozi kutokana na

[16] Pia tunaweza kuhusisha neno hili na imani ya Kiislamu ambapo neno *Iblis* au *Shaitan* linatumiwa kumrejelea kiumbe huyu. Asili ya neno hili katika Kiingereza na Kiarabu inaaminika kuwa ni Kihebrania.

ubepari wa kikoloni. Badala yake yanaashiria jinsi athari za kikoloni zimefumbatwa katika tamaduni na lugha za watawaliwa.

Hali sawa inabainika tunapoangazia neno *Mutharaba-ini* ambalo ni kivumishi kutokana na uambishi wa kiambishi tamati *–ini*. Kivumishi hiki kinatokana na nomino *Mutharaba* ambayo ni dhana linganifu kwa neno la Kiswahili *Msalaba*. Kama ilivyo kwa *Caitaani*, dhana hii ina asili yake katika imani ya Kikristo na kwa jinsi hiyo haina uasilia katika utamaduni na lugha ya Kikuyu. Matumizi ya dhana za kigeni katika MC kwa upande mmoja yanatufanya kukisia uwezekano wa kuwa mwandishi alihusika katika zoezi la tafsiri ya kiakili katika uandishi wake.

Baadhi ya maneno anayotumia yanaelekea kuashiria kwamba huenda hadithi chanzi, iliyokuwako akilini, haikuwa katika lugha ya Kikuyu. Madai haya japo hayana ithibati ya moja kwa moja hatuwezi kuyapuuza tukizingatia kuwa hapo awali mwandishi alikuwa akiandika bunilizi zake kwa Kiingereza, hii ndiyo riwaya ya kwanza katika lugha ya Kikuyu. Mtindo wa masimulizi aliotumia katika uandishi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* umezingatia mtindo wa masimulizi katika jamii ya Gĩkũyũ. Kwa mfano, uradidi katika matumizi ya methali zenye maana sawa, matumizi ya vyanzo na viishio vya masimulizi ya ngano katika jamii hii miongoni mwa mbinu nyingine.

Ukinzani huu baina ya lugha asilia na lugha ya kigeni pamoja na matumizi ya mtindo wa masimulizi ulioegemezwa zaidi kwa fasihi simulizi ya jamii ya Gĩkũyũ tunaweza kuufasili kuwa ni ishara ya athari za tamaduni za kigeni, ikiwemo mfumo

wa imani, mfumo wa elimu na hata mfumo wa maisha kwa ujumla, kwa jamii hii. Hali hii inamfanya mwandishi kutumia lugha mahuluti ambayo haina uasilia katika mfumo wa LC. Maneno kama vile *yunibaciti* kwa maana ya chuo kikuu, *ceekeretari* kwa maana ya mhazili, *injinia* kwa maana ya mhandisi ni baadhi tu ya maneno yanayoashiria utofauti wa kitamaduni unaotokana na mtagusano wa jamii hii na wakoloni jambo linalobainika kupitia kwa lugha.

Athari za mkoloni zinazalisha uhalisia mpya katika jamii ya watawaliwa. Hali hi inaibua dhana zisizo na uasilia na hivyo mwandishi anapoziwasilisha katika MC hana budi kutohoa maneno kwa kukosa dhana asilia katika mfumo wa LC. Hata hivyo, kuna mazingira ambapo mwandishi anatumia maneno mkopo licha ya kuwa na maneno ya kiasili katika LC. Maneno haya pakubwa yamekopwa kutokana na lugha ya Kiingereza. Kwa mfano:

**Mfano 27:**

**MC:** *Hicitoria/kirira, Ndiramu*

Katika mfano huu, neno *Hicitoria* limetumika pamoja na neno *Kirira* kwa maana ya Historia. Matumizi haya yanadhihirisha hali ambapo mwandishi wa MC anatumia mifumo miwili katika uandishi wake. Mfumo mmoja unaashiria uandishi kwa kuzingatia mfumo wa LC; matumizi ya neno *kirira* ambalo ni la kiasili katika lugha ya Kikuyu. Mfumo wa pili, matumizi ya neno, *hicitoria*, unaashiria utata wa kilugha ambao mwandishi anakumbana nao akilini mwake. Neno hili ni usharabu wa moja kwa moja kutoka lugha ya Kiingereza. Huenda uamuzi wa kusharabu unatokana na


ukweli wa matumizi ya lugha miongoni mwa hadhira lengwa ya MC ambapo maneno asilia katika lugha hii yamepuuzwa na badala yake maneno mkopo yanatumiwa zaidi. Hali hii katika mazingira ya jamii zilizotawaliwa inaweza kuhusishwa na vichocheo vya kiisimu jamii (Cherono, 2018). Usharabu kutoka lugha ya Kiingereza unaweza kuhusishwa na uwezo wa lugha hii ya Kiingereza kutumiwa kutimiza haja ya mawasiliano katika miktadha mbalimbali pamoja na hadhi ambayo lugha hii imepewa miongoni mwa jamii za Kiafrika ikiwemo lugha ya Kikuyu.

Tukiangazia mfano wa neno *Hicitoria*, tunaweza kudadisi kuwa mwandishi akiwa mzawa wa Kenya kama walivyo Wakenya wengi ana umilisi wa lugha angalau tatu: lugha ya mama, Kikuyu, Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, licha ya imani yake katika matumizi ya lugha za kiasili na Kiafrika kujikomboa kutokana na ubepari wa kiisimu na kitamaduni, anapata ugumu wa kukopa maneno ya Kiswahili anapopungukiwa katika lugha yake ya Kikuyu kutokana na ukweli kwamba hata lugha ya Kiswahili yenyewe imekopa kutoka kwa lugha ya Kiingereza. Hali hii inatufanya kutambua kinaya kilichopo katika kutafakari uwezekano wa kutumia lugha za kiasili dhidi ya ubepari wa Kiingereza, kwa mfano, huku tukikopa maneno kutoka kwa Kiingereza chenyewe. Uhalisia wa mwathiriano baina ya tamaduni na tajriba asili za Kiafrika na tajriba ngeni za Kiingereza katika mazingira ya Kenya ni suala ambalo hatuwezi kulipuuza. Wasemaji wazawa wa lugha za Kiafrika baada ya majilio ya elimu ya kimagharibi wana mazoea ya kusharabu kutoka kwa Kiingereza

ambacho kinatumiwa katika utoaji wa mafunzo na hivyo ni rahisi kwa wasemaji hawa kuelewa neno *Ndiramu* ambalo limetoholewa kutokana na neno *drum* la Kiingereza badala ya kutumia neno asilia la Kikuyu kurejelea dhana hii, *ibuuba.*

### 3.4 Athari za Utamaduni katika Ubora wa Tafsiri; MT1 na MT2


Matini yoyote ile husukwa na kusimbwa kwa kutumia lugha ambayo ni sehemu ya utamaduni maalum. Lugha hivyo basi huwa ni sehemu ya utamaduni na ni kiwakilishi cha utamaduni kwa wakati ule ule. Tunapozingatia tafsiri, mtafsiri ana jukumu la "kubeba" maana zilizomo katika matini chanzi, iliyoandikwa kwa lugha chanzi na hivyo iliyo sehemu na inayowakilisha utamaduni chanzi, na kuzihawilisha katika mfumo wa lugha na utamaduni pokezi. Katika muktadha wa utafiti huu, mtafsiri wa MC analenga kuhawilisha yaliyomo katika MT1 na MT2 kwa njia iliyo sahihi na inayokubalika. Newmark (1981, 1988) katika kujadili dhana ya ulinganifu katika tafsiri anaangazia suala la mawasiliano kuwa la kimsingi. Mawasiliano katika muktadha wa tafsiri tukiyaangazia kwa kuyalinganisha na mawasiliano ya kawaida yanabainika kuwa ni changamano mno. Kwa mfano, tukiangazia kielelezo kilichotolewa kuhusu mawasiliano timilifu tunapata kwamba:




**Mchoro 2 – Kielelezo cha Mawasiliano Sahili**

Kutoka; Ogechi (2002:7)

Mtoa ujumbe hutuma ujumbe wake kwa kutumia nyenzo anayohisi ni faafu kwa mpokea ujumbe ambaye huufasili na kutoa mwitikio. Katika kufanya hivi kuna kelele ambazo huchachawiza mawasiliano haya. Mtoa ujumbe ana jukumu la kuhakikisha kuwa kelele hizi haziathiri ujumbe wake. Kielelezo hiki kinaashiri kile tunaweza kueleza kuwa ni mawasiliano katika misingi ya kawaida. Mawasiliano ambayo huhusisha wahusika wawili (mwasisi ujumbe na mpokeaji) ambao huwasiliana kupitia kwa mbinu maalum (maandishi, mazungumzo; ana kwa ana, kuwezeshwa kwa vifaa kama vile simu n.k. au hata kutumia ishara kando na lugha). Tunapoangazia mawasiliano katika mazingira ya tafsiri, tunapata kuwa huu unakuwa ni mchakato changamano zaidi ambao tunaweza kuuwakilisha ifuatavyo:




**Mchoro 3 – Kielelezo cha Mawasiliano katika Tafsiri**

Tukiangazia mchoro huu, tunapata kuwa washiriki wa moja kwa moja katika mchakato wa mawasiliano katika mazingira tafsiri ni watatu. Mwasisi ujumbe, katika muktadha wa utafiti huu Mwandishi, Mtafsiri, katika Kiswahili na katika Kiingereza, na hatimaye tuna msomaji wa ama MT1 au MT2. Usawazisho baina ya

kusudi la mwandishi, imani zake, mtazamo wake wa ulimwengu na kusudi la mtafsiri sio jambo rahisi. Mtafsiri anaweza kufumbata maana msingi ya maneno lakini akakosa kuwasilisha maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, katika mazingira ya kutafsiri MT1 na MT2, kuna dhana za kitamaduni alizotumia mwandishi ambazo ama hazikutafsiriwa au zilitafsiriwa visivyo na kwa jinsi hii kuathiri maana ya matini.

Tukiangazia ubora kwa misingi ya uwezo wa MT1 na MT2 kuwasiliana na kuibua athari sawa ikilinganishwa na MC, tunapata kuwa mtafsiri anapungukiwa katika kufanikisha zoezi hili kama ilivyojadiliwa kwenye sehemu ya 3.1. Mtanziko uliopo kwa mtafsiri wa matini za baadaukoloni ni ama adumishe ukiushi wa kiisimu na uibuaji wa ugeni unaochangia kupinga athari za kibepari au azingatie mawasiliano na kupuuza baadhi ya ukiushi uliofanywa makusudi na mwandishi wa MC na kwa jinsi hiyo kutofikia lengo la kuibua ugeni. Maamuzi pakubwa yatategemea itikadi ya mtafsiri kama inavyojadiliwa katika sura inayofuata.

**3.5 Hitimisho**

Sura hii imeangazia dhana ya utamaduni na kuchanganua jinsi dhana za kiisimu na za kisanii zinazofungamana na utamaduni chanzi uliowakilishwa katika MC zilivyohawilishwa katika MT1 na MT2. Inabainika kuwa mwandishi wa MC ametegemea dafina ya LC na fasihi simulizi ya Kikuyu ili kurutubisha riwaya yake pamoja na kuipa ladha ya kiasili katika mfumo wa Kikuyu. Tafsiri ya dhana hizi katika MT1 na MT2 imechanganya baina ya mbinu ya ubinafsishaji na mbinu ya

uibuaji ugeni. Vilevile inabainika kwamba mtafsiri hakuwa na mkakati maalum jambo linaloashiria ukosefu wa uthabiti wa kinadharia katika utekelezaji wa tafsiri hizi.

Uteuzi wa kiisimu umeangaziwa kama ishara ya mwathiriano wa kitamaduni baina ya tamaduni zote tatu husika. Umahuluti wa lugha unabainika katika MC kama ishara ya athari za kikoloni kwa lugha na utamaduni wa Gĩkũyũ. Hali hii inaibua maswali kwa uwezekano wa kutumia LC kama lugha 'safi' ya kukabiliana na ubepari wa lugha ya kikoloni. Isitoshe, suala la tafsiri kama mawasiliano na jinsi mchakato huu ulivyo changamano limeangaziwa huku ikibainika kwamba ubora wa tafsiri kimawasiliano na uteuzi wa kiisimu unaolenga kuibua ukiushi na ugeni ni hali mbili zinazoibua utata kwa mtafsiri. Uamuzi wa nini kipewe kipaumbele baina ya mawasiliano au juhudi za ukombozi kiisimu na kitamaduni unategemea itikadi ya mtafsiri na uamilifu wa tafsiri husika kama inavyojadiliwa katika sura ya nne.

# SURA YA NNE

# ITIKADI NA UTAMBULISHO KATIKA

# *CAITAANI MUTHARABA-INI* NA TAFSIRI ZAKE

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia dhana mbili ambazo ni za kimsingi katika utafiti huu; itikadi na utambulisho kuambatana na lengo la pili na la tatu la utafiti huu. Dhana hizi zimejadiliwa kwa pamoja kwa kuwa zinategemeana na kujengana. Aidha, utambulisho umechanganuliwa kwa msingi wa baadaukoloni na uchanganuzi wa diskosi. Sura hii imeanza kwa kuweka usuli wa uchanganuzi ambapo imetambua dhima na nafasi ya kipekee ya utamaduni na lugha katika kujadili dhana za itikadi na utambulisho. Baadaye, dhana za itikadi na utambulisho zimejadiliwa kwa ujumla kisha kuchanganuliwa kwa mifano mahususi kutoka kwenye matini teule za utafiti huu.

## 4.1 Dhima ya Utamaduni na Lugha katika Kubainisha Itikadi na Utambulisho

Utamaduni ni kipengele cha kimsingi katika kujenga na kubainisha utambulisho wa mtu au jamii. Mtagusano baina ya tamaduni mbili tofauti au zaidi huibua ukinzani baina ya ‘sisi’ na ‘wao’ vipengele ambavyo katika muktadha wa tafsiri, hasa kama ilivyo katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini,* ni vya kimsingi katika kuielewa tafsiri iliyotekelezwa. Tunapotalii mitagusano ya kitamaduni katika tafsiri tunapata msingi wa kutalii dhana za utambulisho, mfanano na tofauti. Hata hivyo, utamaduni katika matini aghalabu hudhihirika kupitia kwa lugha. Uteuzi wetu na matumizi yetu ya lugha kwa pamoja hutoa mwanga wa imani zetu, mila na desturi pamoja na

mitazamo yetu kuhusu hali mbalimbali za maisha kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Lugha hivyo basi inakuwa ni jukwaa muhimu katika kutalii dhana za utambulisho na itikadi kwa kuwa ni kupitia kwa maamuzi tunayofanya katika matumizi yetu ya lugha ndipo dhana hizi zinadhihirika na kubainika.

Silverstein (2004) anaeleza kwamba dhana za kitamaduni huweza kubainika na tunaweza kutagusana nazo kupitita kwa nyenzo ya lugha katika matumizi. Hii ina maana kwamba katika matumizi yetu ya lugha, zaidi ya kuwasilisha maana msingi zinazotokana na maneno tunayotumia, huwa tunawasilisha pia dhana za kitamaduni na hata za kiitikadi kupitia kwa uteuzi wetu wa lugha. Hofstede (2001) naye anafafanua dhana ya utamaduni kuwa ni utaratibu wa jumla wa kiakili ambao hutofautisha baina ya washiriki wa kikundi kimoja au kategoria moja na kikundi au kategoria nyingine.

Kutokana na maelezo haya, tunabainisha dhana ya kimsingi; kwamba kupitia kwa utamaduni, suala la utofauti baina ya watu au washiriki tofauti katika jamii linabainika. Katika muktadha wa utafiti huu, utofauti huu tunaufasili kuwa msingi wa utambulisho ambao ni dhana ya kimsingi katika sura hii. Aidha, maelezo haya ni muhimu hasa tukiyahusisha na ujelezi anaotoa Minkov (2013) kwa dhana ya utamaduni kuwa; utamaduni ni jumla ya vipengele kama vile maana mbalimbali, miviga, miiko, mipangilio ya kijamii, maadili na kaida, imani, mitazamo na tabia. Suala la imani na mitazamo ni muhimu katika muktadha wa utafiti huu, hasa katika sura hii kwa kuwa dhana hizi tumezihusisha na dhana kuu ya itikadi.

Dhana hizi mbili za itikadi na utambulisho ndizo msingi wa sura hii ambapo tumechanganua jinsi matumizi ya lugha ya mwandishi wa MC yanabainisha itikadi yake pamoja na jinsi anavyoitumia lugha hii kujenga utambulisho wake binafsi na utambulisho wa kijamii. Aidha, sura hii imejadili namna dhana ya itikadi inavyosaidia katika kujenga utambulisho katika MC na jinsi itikadi na utambulisho huu ulivyoshughulikiwa katika MT1 na katika MT2 mtawalia.

**4.2 Itikadi katika Caitaani Mutharaba-ini**

Dhana itikadi ni changamano na ina fasili mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi, uwanja unaohusika pamoja na kile kinachoangaziwa. Katika utafiti huu, dhana itikadi imetumika kwa maana pana kurejelea imani, msimamo, mtazamo wa mtu binafsi au wa jamii fulani kwa ujumla kuhusu jambo, mtu au kikundi cha watu au hali fulani, ambao aghalabu unadhihirika kupitia kwa matumizi ya lugha. Katika sura hii, tulichunguza na kuchanganua uteuzi wa lugha aliofanya mwandishi wa MC kwa kuuweka katika muktadha wake kimatumizi na muktadha kijamii. Kuambatana na maelezo ya Van Djik (1998) kwamba nadharia ya uchanganuzi wa itikadi inaakisi masuala matatu makuu; jamii, diskosi na utambuzi, uchanganuzi ulizingatia vipengele hivi vitatu kama dira ya kutuwezesha kutimiza malengo yetu katika sehemu hii. Katika kufanya hivi, vipengele hivi vilichunguzwa kwa msingi wa uchanganuzi wa diskosi hasa kwa kujikita kwa vipengele vya utambulisho, mahusiano na siasa.

Katika uchanganuzi, utafiti ulitia maanani kuwa dhana ya jamii aliyokusudia Van Djik (1998) ilidhamiriwa kwa upana wake unaojumuisha muktadha wa kitamaduni pamoja na tajriba zinazohusiana na itikadi inayotawala jamii husika. Dhana hii ya jamii katika utafiti huu inafasiliwa kupitia kwa sajili zinavyoeleweka kwa mwandishi na au mtafsiri, hali ambayo inampa uwezo wa kufanya maamuzi na uteuzi wa kibinafsi licha ya mazingira ya kijamii na kitamaduni anamojipata. Uteuzi huu wa kibinafsi ndio mojawapo ya msingi wa uchanganuzi katika sura hii. Aidha, tulitambua kwamba matini teule ni sehemu ya diskosi ya mwandishi aliye pia mtafsiri. Hivyo basi, katika kuchanganua dhana za itikadi na utambulisho, tulichanganua diskosi hii kwa kuiweka katika muktadha wake ili kubaini maana kimuktadha. Katika kufanya hivi, tulihusisha matini teule na matini nyingine za mwandishi kwa kuangazia utalii wa mwingiliano matini kama sehemu ya kukamilisha uchanganuzi wa diskosi.

### 4.2.1 Lugha katika MC na Udhihirikaji wa Itikadi

Tunapoangazia dhana ya itikadi, tunaweza kuanzia kwa kuichunguza katika kiwango cha chini cha uteuzi wa kiisimu na kisarufi. Katika muktadha wa utafiti huu, hatuna budi kutalii jinsi lugha imetumiwa katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* kama msingi wa kuchunguza udhihirikaji wa itikadi. Itikadi aghalabu hudhihirika kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika kazi anuwai za mwandishi. Hata hivyo, katika utafiti huu tunahoji kwamba, itikadi hudokezwa kupitia kwa uteuzi na maamuzi anayofanya mtumiaji lugha kila mara anapotumia lugha. Hii ndiyo hali ambayo

tulichunguza kwa kuangazia uteuzi aliofanya mwandishi katika kuiandika MC. Tunapata kuelewa mtazamo wake na msimamo wake wa maisha na kwa jinsi hiyo kupata kufahamu maana zilizokusudiwa katika ujumbe anaowasilisha. Uteuzi huu ni sehemu ya mtindo wa kibinafsi ambao unatekeleza dhima muhimu katika kuitambulisha itikadi ya mwandishi na au mtafsiri wa matini husika.

Tukirejelea riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, tunaifasili matini hii kama matini chanzi. Hata hivyo, tunatambua kuwa matini hii ni zao la mchakato changamano ambao unahusisha tafsiri ya kiakili na hivyo tunaweza kudai kwamba matini hii ni "matini tafsiri." Yaani, ni dhihirisho la kimaandishi la masimulizi yaliyo akilini mwa mwandishi. Uchukulio huu unatokana na mawazo ya Bandia (2014) kuhusu uandishi wa fasihi ya Kiafrika kuwa ina msingi wake katika tafsiri hasa kutokana na masimulizi ya kiasilia na fasihi simulizi ya jamii husika. Hivyo basi, tunaiangazia MC kama zao la usanii wa mwandishi na kwa wakati huo huo kama dhihirisho la tafsiri (ya kisemiotiki) ya hadithi chanzi iliyokuwa akilini mwa mwandishi. Mtazamo huu ni wa kimsingi katika utafiti huu kwa kuwa mwandishi aliyeangaziwa katika utafiti huu awali aliwasilisha sanaa yake kwa lugha ya Kiingereza kisha akafanya maamuzi ya kimakusudi kuanza kuiwasilisha sanaa hii kwa lugha ya Kikuyu. Uamuzi huu tunauchukulia kuwa ulichochewa na misingi ya kiitikadi. Hivyo basi matumizi ya lugha, na kwa jinsi hiyo, uteuzi anaofanya katika uwasilishaji wa hadithi yake ni wa kimsingi katika kuelewa itikadi yake. Kwa mfano tukirejelea sehemu nzima ya utangulizi:

Sehemu ya utangulizi katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* ni ya kimsingi kwa usomi wa riwaya hii. Umuhimu wake ni bayana kwa utalii wa kimtindo na hata kwa zoezi la uhakiki wa kijumla. Katika utafiti huu, uwepo wa sehemu ya utangulizi katika MC sio tukio la kisadfa. Ni uamuzi wa kimakusudi ambao unalenga kutekeleza dhima mahususi. Ili kueleza dhima hii, hatuna budi kuangazia suala la kimsingi katika sehemu hii ambalo ni; uteuzi wa kiisimu uliofanywa, uteuzi wa kisanii na dhamira ya sehemu hii kwa kuihusisha na matini nzima ya *Caitaani Mutharaba-ini*. Mwandishi ametumia utangulizi wa riwaya hii kuhamasisha hadhira yake kuhusu masuala anayohisi kuwa ya kimsingi na ambayo yanaangaziwa japo sio kwa njia ya moja kwa moja katika riwaya nzima. Kwa mfano:

**Mfano 28:**

> **MC:** Kiambagio maai ni ihii nyene. Niingi ngemi ciumaga na mucii. Tutaangikuria thiomi ciitu cia giikenya ri ithui eene cio ri, ni mugeni uriku uungiuma na njira ooke acikurie? …Gute thiomi ciitu tukaruugira cia ageni, no undu umwe ne kuruma Ngai! O Mukeenya haandu aaruma, aagirirwo ni gukorwo ari njoorua ya thiomi igiri; rwa ruuriri rwake (hari ithui Agikuyu ni Gikuyu) na rwa bururi ni ruo Githweri. Andu matari thiomi ciao ni ngoombo, makiria mwena-ini wa kirira. *(Ukurasa wa kwanza wa utangulizi)*

Nukuu hii kutoka sehemu ya utangulizi inaangazia suala la lugha za kiasili. Mwandishi anauliza swali la kimsingi ambalo ni: je, tusipokuza lugha zetu za kiasili nchini Kenya, ni mgeni yupi tunatarajia aje kuzikuza hasa kimatumizi? Swali hili ni la kimsingi katika muktadha wa baadaukoloni ambapo mahusiano baina ya lugha ya mtawala na ile ya mtawaliwa pamoja na tamaduni zinazohusika ni suala la kimsingi. Kipengele cha siasa katika uchanganuzi wa diskosi kwa mujibu wa Gee (1999)

kinahusu jinsi matumizi ya lugha yalivyotumika kuunda, kusambaza au hata kuzuia malighafi ya kijamii kwa kuchukuliwa kuwa kubalifu au kinyume chake. Katika mfano huu, swali analouliza mwandishi katika sehemu hii ya utangulizi linaangazia matumizi ya lugha za kiasili, malighafi ya jamii iliyotawaliwa, badala ya kutumia lugha za kigeni. Swali kuhusu ukuzaji wa matumizi ya lugha za kiasili za Kenya linalenga kuhimiza haja ya kuimarisha matumizi na kwa jinsi hiyo kukweza lugha na utamaduni asilia badala ya kuchangia kongoo za lugha za kigeni. Swali hili aidha ni la kiitikadi ambapo tukichukulia vipengele vya mtazamo, msimamo na imani kama baadhi ya vijenzi vya itikadi, basi swali hili linatuelekeza kwa dhana ya itikadi ya mwandishi kuhusu lugha.

Nukuu katika mfano 28 pia inadai kwamba; *Gute thiomi ciitu tukaruugira cia ageni, no undu umwe ne kuruma Ngai!* Hapa mwandishi anaeleza kuwa kuzitelekeza lugha zetu za kiasili ni sawa na kumtukana Maulana, ni kufuru! Umithilisho huu huenda umechangiwa na hoja kwamba, Maulana katika utamaduni wa Gikuyu ndiye mwanzilishi wa yote. Jamii hii inaamini kuwa *Ngai* aliwaumba na kuwabariki wazazi wao *Gikuyu* na *Mumbi*. Hivyo basi kuna mantiki kuchukulia kwamba lugha ya jamii hii pia ilitoka kwa Mungu (*Ngai).* Kuipuuza lugha hii kimatumizi ni sawa na kumkosoa Maulana na kwa jinsi hiyo kumvunjia heshima. Sehemu ya utangulizi vilevile imetumiwa na mwandishi kueleza maoni yake na msimamo wake kuhusu lugha nchini Kenya ambapo tukiangazia sehemu ya mwisho ya nukuu katika mfano 28:

> *O Mukeenya haandu aaruma, aagiririwo ni gukorwo ari njoorua ya thiomi igiri; rwa ruuriri rwake (hari ithui Agikuyu ni Gikuyu) na rwa bururi ni ruo Githweri. Andu matari thiomi ciao ni ngoombo, makiria mwena-ini wa kirira.*

Mwandishi anaeleza kuwa popote pale alipo Mkenya anapaswa kuwa na umilisi katika lugha mbili; lugha ya jamii (kabila) yake – kwa jamii ya Gikuyu ni Kikuyu – na lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili. Anazidi kueleza kuwa watu wasio na lugha zao asilia ni watumwa, hasa kwa upande wa historia, elimu na ustaarabu.

Suala la utumwa ni la kimsingi hasa katika kuangazia mahusiano baina ya mtawala na mtawaliwa. Masuala haya ya kisiasa na kiitikadi yameandikwa dhahiri katika MC na kutafsiriwa sisisi katika MT1. Hata hivyo sehemu nzima ya utangulizi imedondoshwa katika MT2. Uamuzi wa kudondosha sehemu hii katika MT2 tunadai ni wa kimakusudi kwa kuwa ujumbe uliopo katika sehemu hii ulikusudiwa hadhira maalum ya Kikuyu na Kiswahili pekee.

Isitoshe, kama anavyoeleza Van Dijk (1998), matini na matumizi yetu ya lugha hayaathiriwi tu na muktadha ambamo matini husika au matumizi ya lugha yanabainika bali huathiriwa pakubwa na mifumo ya kimuktadha ya mtumiaji lugha. Yaani, matumizi ya lugha yanategemea sio tu muktadha halisi ambamo lugha inatumika au matini husika inazalishwa bali pia hutegemea tajriba za mtumiaji lugha katika matukio ya awali ya matumizi ya lugha. Katika muktadha wa utafiti huu tunaweza kudadisi kuwa, maamuzi ya kiisimu anayofanya Ngũgĩ katika kusimulia hadithi yake yanategemea muktadha halisi ambamo matini hii inazalishwa pamoja na tajriba zake za awali kijamii, kisiasa na hata kiitikadi. Hivyo basi katika kuchanganua

uteuzi anaofanya kiisimu katika sehemu ya utangulizi wa MC hatuna budi kutalii muktadha ambamo MC inazalishwa pamoja na kuhusisha muktadha huu na tajriba za awali za mwandishi kwa kurejelea yaliyomo katika sehemu hii.

Tukimrejelea Simpson (1993), mtumiaji lugha anapofanya uteuzi wowote kiisimu, aghalabu huwa hafanyi uamuzi pasi mapendeleo ila huwa anatawaliwa na kuongozwa na misimamo yake ya kijamii, kitamaduni na kiitikadi. Isitoshe, muktadha wa mtumiaji lugha kijamii pamoja na tajriba zake katika ulimwengu halisi huchukua nafasi muhimu katika uteuzi wake kiisimu. Katika MC, mwandishi, licha ya kuwa anazalisha matini katika lugha yake chanzi akilenga wasomaji kutoka kwa jamii yake, ametumia lugha kimakusudi ama kuchora taswira au kueleza mitazamo yake kuhusu hali na matukio mbalimbali katika jamii ya hadithi anayosimulia. Miongoni mwa matumizi ya lugha ambayo ni ya kimakusudi na ambayo ni muhimu katika kuelewa jinsi itikadi imebainishwa na jinsi imechangia utunzi wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* ni yale yanayodhihirika katika sehemu ya utangulizi. Mwandishi anatoa taarifa za kiusuli kuhusu mazingira halisi ya utunzi wa hadithi hii pamoja na taarifa za kiusuli kumhusu mwandishi mwenyewe ifuatavyo:

**Mfano 29**

> *Rugano ruuru ni rwa kiiriu. Ndaarwandikire ndi Njeera nene ya Kamiti Mwaka-ini wa Ngiri Ikumi cia Magana kenda ma Miroongo mugwanja na inyaanya, 1978 riria ndaathamiirio kuo ni undu wa kunyiitanira na arimi-anyinyi na aruti-a-wira ithaako-ini ri ngerekano, Ngaahika Ndeenda, riria riathaakagirwo Kamirithu Limuru, 1977. (Ukurasa wa Kwanza wa Utangulizi)* (Msisitizo wangu)

Taarifa hizi za kiusuli zinatoa mwanga wa hali ya kisaikolojia pamoja na mazingira halisi ambamo MC ilizalishwa. Licha ya kuwa kuna usimulizi unaoelezea matukio halisi wakati wa utunzi, mwandishi anaamua kimakusudi kueleza sababu za kukamatwa na kutiwa korokoroni kama inavyojitokeza katika sehemu iliyoandikwa kwa herufi za mlazo-

> *ndaathamiirio kuo ni undu wa kunyiitanira na arimi-anyinyi na aruti-a-wira ithaako-ini ri ngerekano, Ngaahika Ndeenda*
> (nilifungwa gerezani kwa kushirikiana na wakulima wadogo na wafanyakazi katika kuigiza mchezo uitwao *Ngaahika Ndeenda* - Nitaolewa Nikipenda)

Msisitizo wa vyombo vya dola, serikali, polisi na jela, kutumiwa "kumdhulumu" mwananchi anayeshirikiana na wakulima wadogo na wafanyakazi katika kufanya igizo linaloakisi hali zao za maisha ni dhihirisho la vita vya kiitikadi ambavyo mwandishi anaamini alikuwa akipigana kwa niaba ya wasiokuwa na uwezo. Maelezo haya yanahusiana kwa karibu na mitazamo ya Kimaksi ambayo mwandishi amehusishwa nayo (Tazama Paolo Abis, 2011). Aya ya kwanza ya riwaya hii inaanza kwa maneno haya na kwa jinsi hii tunadadisi kwamba huenda uteuzi huu ni wa kimakusudi na unasaidia katika kueleza msimamo wa mwandishi tangu mwanzo kuhusu hali za maisha kijamii na kisiasa. Anajinasibisha na wazalishaji na wafanyakazi wanaokandamizwa kwa kutekeleza mojawapo ya haki za kimsingi, kueleza hisia zao kupitia kwa mchezo wa kuigiza.

Mojawapo ya vipengele vya kimsingi katika utalii wa baadaukoloni ni suala la utamaduni na suala la lugha. Mwandishi wa MC anajitosa moja kwa moja katika

kueleza msimamo wake na mtazamo wake kuhusu uhusiano uliopo baina ya lugha na utamaduni, ikiwemo historia, ya watawala wa kikoloni kwa upande mmoja na lugha, utamaduni na historia za watawaliwa waliojinyakulia uhuru kwa upande wa pili. Hata hivyo, suala la umahuluti wa kitamaduni na kiisimu haliwezi kupuuzwa. Ngũgĩ katika kuandika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* anaweka wazi mtazamo wake na uchukulio wake ambao unaongozwa na misingi yake ya kiitikadi kuhusu mahusiano yaliyokuwepo, yaliyopo na yanayofaa kuwepo baina ya ustaarabu wa Mwafrika-Mkenya, na ustaarabu wa watawala wa Kikoloni - Mwingereza na mataifa mengine ulimwenguni yaliyo na uwezo kiuchumi na kisiasa.

Kwa kutumia kigezo cha historia, lugha na utamaduni wa wazawa wa Kenya, Ngũgĩ anaweka wazi dhamira yake katika utunzi wa riwaya hii. Aidha, anabainisha itikadi iliyochochea uzalishaji wa MC pamoja na kuiumba kuwa jinsi ilivyo. Kwa mfano, katika sehemu ya utangulizi wa MC, anaeleza ifuatavyo:

**Mfano 30:**

**MC:** Ndithii wa Kiambuu, agitunyana marua ma uthaaki wa ithaako riu, oigire ati ni riaragia cararuku uhoro wa Njaamba cia Mau Mau, Ngaati na Uuthukumu. Mauundu ta Macio ati Magiriire o kuriganira ta kirooto kiuru, kihahuratoro. No riiri, twahota atia kuriganirwo ni hiicituri iitu? Tutaangimenya kuria tuoimire ri, twamenya atia haria turi, naharia turoreete ruuciu? Ni kio o nandi ruo-ini rwa Njeera nene, ni ndaatuire na ngoro ati no muhaka thii na mbere na wandiki wa ruthiomi rwitu, ruthiomi rumwe rwa ingi nyiingi cia bururi witu…O Muukenya haandu aaruma, aagiriirwo ni gukorwo ari njoorua ya thiomi igiri; rwa ruuriri rwake (hari ithui Agĩkũyũ ni Gĩkũyũ), na rwa bururi ni ruo Githweri. Andu matari thiomi ciao ni ngoombo, makiria mwena-ini wa kirira. Ruthiomi ni ruo mwiri wa kirira kia ruuriri. Kirira kiega ni kio ngoro ya ruuriri.

(Kutoka Sehemu ya Utangulizi)

**MT1:** Mkuu wa wilaya ya Kiambu, katika mkoa wa Kati, Kenya, alitupokonya kibali cha kuigiza mchezo huo, alisema ya kuwa mchezo wenyewe ulizungumzia kwa udhahiri sana vitendo vya Mashujaawa Mau Mau, Wasaliti (Ngaati) na ubeberu wao. Aliendelea kusema kuwa inabidi tuyasahau mambo hayo kwani yalikuwa kama ndoto mbaya – jinamizi. Lakini twawezaje kuisahau historia yetu? Tusipojua tulikotoka, tunawezaje kujua tulipo na tunakokwenda? Ndipo nilipokata shauri kwa moyo wa dhati, nilipokuwa katika mateso gerezani, kuendelea kuandika kwa lugha yetu ambayo ni miongoni mwa lugha nyingi za taifa letu…Mkenya yeyote popote alipo yambidi ajimudu katika lugha mbili: lugha ya kabila lake na lugha ya Kiswahili. Watu wasio na lugha zao ni watumwa. Hawawezi kabisa kufahamu mafunzo yanayohusu utamaduni wao. Lugha ni Kioo cha taifa cha kujitazama. Lugha ni msingi thabiti wa taifa ambao kwao taifa huimarisha mafunzo ya utamaduni wake.

(Kutoka Sehemu ya Utangulizi)

**MT2:** **** (Sehemu ya utangulizi haipo)

Tukirejelea mfano huu, masuala kadhaa ya kiitikadi yanabainika. Kwanza, kwa kuzingatia historia ya taifa la Kenya, mwandishi anarejelea mchezo wa kuigiza aliouandika kwa ushirikiano na Ngũgĩ wa Mĩriĩ, *Ngahika Ndeenda – Nitaolewa Nikipenda*, kuonyesha jinsi waliochukua hatamu za uongozi baada ya mkoloni kuondoka walivyoishajiisha kukomesha juhudi zozote za ukombozi wa kiakili. Mwandishi anaeleza kuwa mkuu wa wilaya anapobatilisha kibali cha kuigizwa kwa mchezo huu, anatoa kauli kwamba masuala ya vita vya uhuru, mashujaa wa Mau Mau pamoja na wasaliti wa taifa wakati wa ukoloni hayapaswi kurejelewa wala kuangaziwa kwa njia iliyo dhahiri kama ilivyokuwa katika mchezo uliokuwa ukiigizwa. Hali hii inaashiria juhudi za walio mamlakani kuzidi kuwakandamiza wananchi kwa kupotosha ukweli kwa manufaa yao ya kibinafsi. Mwandishi anasisitiza haja ya kuielewa historia ya taifa kwa ukamilifu na ukweli ili kuelewa

mahali taifa lilipo na kwa jinsi hiyo kuliwezesha taifa kupiga hatua kuelekea linakotaka kufika.

Jambo la pili la kimsingi linalobainishwa katika mfano huu na ambalo lina chembechembe za itikadi ndani mwake ni msimamo wa mwandishi kuhusu lugha na utamaduni. Ngũgĩ anashikilia kwamba lugha za kiasili ni zana ya kimsingi katika kulipa taifa uhai mpya na utambulisho. Kwa maneno yake mwenyewe, anatafsiri mawazo yake aliyoyaeleza katika MT1 kuwa:

> Ndipo nilipokata shauri kwa moyo wa dhati, nilipokuwa katika mateso gerezani, kuendelea kuandika kwa lugha yetu ambayo ni miongoni mwa lugha nyingi za taifa letu…Lugha ni kioo cha taifa cha kujitazamia. Lugha ni msingi thabiti wa taifa ambao kwao taifa huimarisha mafunzo ya utamaduni wake.

Mawazo haya ni dhihirisho la kichocheo cha kwa nini akaamua kuiandika MC kwa lugha ya Kikuyu na pengine kwa nini akaitafsiri kwa Kiswahili. Isitoshe, mawazo haya yanatupa mwanga wa mtazamo, imani na kwa jinsi hiyo itikadi ya mwandishi katika suala la lugha ambapo, anaiangazia lugha kama kioo cha taifa ambapo linaweza kujitazama. Aidha, anaeleza kuwa lugha ndiyo msingi thabiti wa taifa ambao kwao taifa linapata kuimarisha mafunzo na utamaduni wake. Mjadala huu wa lugha za kiasili na uamilifu wake ni mojawapo ya migogoro inayojitokeza na inayojadiliwa katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*.

Katika muktadha wa baadaukoloni, suala la utamaduni, hasa mahusiano ya kiuwezo yaliyopo baina ya utamaduni wa mtawala na ule wa mtawaliwa ni la kimsingi. Uhuru wa kisiasa pasi na ukombozi wa kitamaduni na kisaikolojia sio uhuru kamili. Haya ni

mawazo ambayo mwandishi anayaeleza kama msingi wa imani yake. Mhusika Gatuiria anaelekea 'kubeba' mtazamo huu kwa niaba ya mwandishi ambapo kwa mfano katika MC ukurasa wa 53, anadadisi suala la lugha za kiasili, historia na mafundisho ya kiasili, falsafa, hekima ya wazee, utamaduni na hata fasihi simulizi ya kiasili. Maswali anayoyauliza ni ya balagha na ni ya kumfikirisha msomaji na kumfanya kujisaili na kwa jinsi hiyo kumfanya azinduke na kutambua kwamba ufufuo na matumizi ya lugha za kiasili, ustaarabu pamoja na utamaduni wa kiasili ndio msingi wa uhuru wa kweli. Uhuru unaomrejeshea msemaji mzawa wa lugha fulani na utamaduni fulani hadhi yake na kumkweza na kufanya mahusiano baina yake na aliyekuwa mtawala wake kuwa yenye usawa. Aidha, kwa kuzitumia lugha za kiasili, inakuwa rahisi kwa waliotawaliwa na kisha kujinyakulia uhuru kudumisha utambulisho wao kiisimu na kwa kiasi kikubwa kitamaduni.

Masuala haya yote tunaweza kuyahusisha na mhimili wa utambuzi anaobainisha Van Djik (1998) kama kipengele cha kimsingi katika utalii wa dhana ya itikadi. Hii ina maana kwamba, katika usimulizi wake, Ngũgĩ anajihusisha katika uteuzi wa kimakusudi unaoafikiana na utambuzi wake, imani na itikadi zake kuhusiana na masuala ya lugha, utamaduni na ustaarabu wa kiasili. Uingizwaji wa maneno yanayoturejesha kwa mjadala kuhusu lugha katika muktadha wa fasihi ya baadaukoloni na hata kwa jamii ya baadaukoloni kwa ujumla ni wa kumakusudi. Ni madai yetu kuwa uamuzi huu unalenga kusisitiza haja ya ufufuo wa kitamaduni pamoja na uimarishaji wa tamaduni hizi ili kukabiliana na ubabe wa lugha na

tamaduni wa watawala wa kikoloni. Msimamo huu ni dhahiri kutoka kwa mwandishi wa riwaya iliyorejelewa katika utafiti huu hasa katika maandishi yake yasiyokuwa ya kifasihi.

Ngũgĩ wa Thiong'o kando na kuwa mwandishi mashuhuri wa fasihi ikiwemo riwaya, tamthilia na hata hadithi fupi, yeye pia ni mmoja wa waandishi wanaotambulika katika kuandikia masuala ya kiuhakiki, kifalsafa na ya kinadharia katika fasihi ya Kiafrika. Maandishi yake pakubwa yanajiegemeza kwa masuala ya lugha, ukoloni na ukoloni mamboleo, utamaduni, ukombozi wa kiakili pamoja na haja ya kudumisha utambulisho wa kiasili wa Mwafrika. Yeye ni miongoni mwa wasomi wa awali wa Kiafrika kujadili mawazo ya baadaukoloni. Mengi ya machapisho ambayo yanatambulika zaidi ni yale aliyochapisha baada ya kuasi kuandika fasihi yake kwa Kiingereza na badala yake akaamua kuandika kwa lugha yake asili ya Kikuyu. Uamuzi huu umekuwa msingi wa mijadala na tafiti nyingi za kitaaluma. Katika utafiti huu, tunatambua kuwa huu ndio ulikuwa msingi wa Ngũgĩ kujitosa katika tafsiri ambapo kazi anazozalisha kwa lugha ya Kikuyu ama amezitafsiri binafsi au zimetafsiriwa na wengine katika lugha nyingine za ulimwenguni. Uchunguzi wetu unaangazia matokeo ya uamuzi huu katika jinsi fasihi anayoizalisha inavyoandikwa kwa Kikuyu; hususan uteuzi wa kiisimu, pamoja na jinsi matini hizi zinavyohawilishwa katika tafsiri ama kwa Kiswahili au Kiingereza.

Suala la lugha, utamaduni na mahusiano ya kiuwezo baina ya makundi mbalimbali katika jamii zilizotawaliwa, jamii tawala au hata baina ya jamii tawala na tawaliwa

zimekuwa nguzo muhimu katika fasihi ya Ngũgĩ wa Thiong'o. Mbali na kuitumia migogoro hii na tajriba zinazotakana na migogoro hii kama malighafi ya kuumba fasihi yake, Ngũgĩ pia ameandikia hali hizi na kujieleza kwa uwazi zaidi katika machapisho mengine ambayo si ya kifasihi. Kwa mfano katika sehemu ya utangulizi ya; *Detained: A Writer's Prison Diary* Ngũgĩ anaeleza ifuatavyo:

> Katika ukoloni mamboleo, wageni wenye uwezo kwa ushirikiano na tabaka tawaka fisadi hujawa na kiburi kiasi cha kuchopeka vidole vyao machoni na ndani ya mapua ya wananchi waliodhalilishwa na kuwakemea: 'Niondokee kinyangarika wee!' Nikubalie mimi pekee ninyonye jasho la wafanyakazi wako. *Wananchi wachache wanapolalamikia hali hii, wanaomiliki nyenzo za uzalishaji kama vile au wawakilishi wao hujifanya kuumia wakiuliza: "Mbona wengine wenu mko hivi? Tunabuni nafasi za ajira kwa watu wenu.* ***Bila sisi watu wa New York, London, Bonn, Paris, Rome, Stockholm na Tokyo,*** *mngekuwa wapi nyinyi?" Kwa bahati mbaya, baadhi ya Wakenya hutazama hali ya maisha kwa jicho la mabepari wanyanyasaji na hawako radhi kufanya chochote kuhusu hali hii hata wanapoona hatari iliyopo kwa manufaa ya nchi yao.*
>
> Ty. *Msisitizo wangu (1981: XV)*

Tunaporejelea nukuu hii na kuichunguza kwa jicho pekuzi, ndani mwake tunapata maneno maalum, niliyoyapigia mstari, yanayofungamana na itikadi maalum, ya Kimaksi. Suala la utabaka, ubepari na unyonyaji wa jasho la wafanyakazi kwa manufaa ya walio wachache ni la kimsingi hasa tunaporejelea MC na tafsiri zake. Maisha ya wahusika kama vile Muturi, Wangari, Wariinga ni dhihirisho la masaibu wanayopitia wafanyakazi mikononi mwa tabaka tawala linalohodhi nyenzo za uzalishaji mali. Aidha, tukihusisha mawazo haya na nukuu kutokana na ushahidi wa baadhi ya wezi wanaoshindana pale pangoni kuanzia sura ya nne hadi sura ya saba ni dhihirisho la jinsi mwandishi ametumia maneno, lugha, kuwasilisha chembechembe za kiitikadi katika usimulizi wake. Kwa mfano;

**Mfano 30:**

**MC:** UIRA WA KIHAAHU WA GATHEECA (Ukurasa wa 105 – 115)

Katika ushahidi anaotoa mhusika Kihaahu wa Gatheeca, anadhihirisha hila zinazotumiwa kuwanyanyasa wananchi kisiasa kwa kuingilia demokrasia ambayo inapaswa kuwa nguzo ya utawala bora. Hata hivyo, inabainika kuwa hata katika demokrasia hii, wenye uwezo na mali wanapata njia ya kuwatapeli wananchi ama kwa kutumia hila au kwa kutumia fujo. Hila kama anazotumia katika kuwatapeli wananchi kuwapeleka wana wao katika shule yake anayoipa jina na maelezo ya kigeni ili kuwashawishi wale wanaopenda kujihusisha na tabaka tawala la wakoloni ni mojawapo wa nyenzo ambazo zinatumiwa kunyonya jasho la wananchi na wafanyakazi wa taifa. Aidha, kutumia fujo katika kupigania uongozi wa *Iciciri County Council* dhidi ya wapinzani wake ni kielelezo cha matumizi ya uwezo wa dola kukabiliana na wachache wanaojaribu kupingana na tabaka tawala.

Kwa kurejelea nukuu iliyoandikwa kwa herufi za mlazo na kukolezwa rangi kutokana na kitabu cha *Detained: A Writer's Prison Diary,* mwandishi amerejelea miji mikuu ya baadhi ya mataifa yenye uwezo kiuchumi kama kielelezo cha wanyanyasaji wa kiuchumi wa mataifa yaliyowahi kutawaliwa. Vielelezo hivi ni viwakilishi vya ukoloni mamboleo ambao mwandishi anakemea katika MC. Tukiangazia baadhi ya uteuzi wa kiisimu aliofanya katika uandishi wa riwaya yake, tunapata kwamba vielelezo hivi vinajitokeza hasa katika maelezo ya mavazi ya wezi kwenye pango

**Mfano 31**

> Mitwe-ini yaao mehuumbiite ngubia ciahaanaga thuumbi. Na o thuumbi yaari na tucuma mugwanja twekoonjeete ta hia na twhenagia muno hakuhi guzina maitho. Thuumbi niciahanaine tiga ati ya mutoongoria yaari nenanene. Niingi o karuhia ga thuumbi geekoonjeete ruuri rwa kuria o Mugeni oimiite. Nguo kana thuuti ciao no cio ciari na utiganu. Ya mutoongoria yatumiitwo na taama wa manooti ma ndoora ($); ya Muungeretha yatumiitwo na taama wa manooti ma mabaaundi (£); ya Muunjirimaani na taama wa manooti ma Ndoicimaki (DM); ya Muubaraanja na taama wa manooti ma Buraniki (Fr); ya Muucikandinibia na taama wa mannoti ma Korona (Kr); Muitariani na ma Riira (lr); na Muunjabaani na ma Yeeni (Yen). O Thuuti yagemeetio na Mbaanji nyiingi ta iria ciikiragwo ni thikaahiti. O mbaanji yaari na gacuuma kaamenamenukaga gakamurika riandiko riria riari mbaanji-ini, gagacooka gakahora gaikaraanga haniini gakamenuka riingi, o uguo o uguo, ta imenyithia cia mataawa wa thiitima. O mbaanji yanagirira undu umwe kana meeri ta uu: WORLD BANKS; COMMERCIAL BANKS; WORLD'S EXPLOITATION BANKS; MONEY SWALLOWING INSURANCES, INDUTRIAL GOBBLERS OF RAW MATERIALS, CHEAP MANUFACTURERS FOR EXPORT ABROAD; TRADERS IN HUMAN SKINS; LOANS FOR A PROFIT; AID WITH IRON STRINGS; ARMS FOR MURDER; MOTOR VEHICLE ASSEMBLIES FOR VANITY FAIR AT HOME & BIGGER PROFITS ABROAD; ALL PRODUCTS LOVELY AND FAIR TO KEEP FOOLS IN DEPENDANT CHAINS OF SLAVES; SLAVE FOR COMFORT, DEAL WITH ME; na imenyithia ingi nyiingi ta icio… (MC: Ukurasa wa 86-87).

Maelezo anayoyatoa ya jinsi vitambaa vya suti za wageni wa heshima vilivyotengenezwa kwa pesa za taifa ambapo kila mgeni alitoka yanaelekea kuoana na maneno anayotumia katika nukuu iliyoandikwa kwa herufi za mlazo na kukolezwa rangi na kurejelea miji mikuu ya mataifa kama vile Marekani, Uingereza, Ufaransa, Italia, Uswizi na hata Japani. Maneno yaliyoandikwa kwenye beji za wageni hawa ni kiashiria cha mtazamo wa mwandishi kuhusu mahusiano yaliyopo baina ya mataifa haya na mataifa yaliyotawaliwa, kama vile Kenya, katika misingi ya kiuchumi na hata kisiasa. Baada ya ukoloni kufika kikomo, mataifa mengi yaliyokuwa yakiendeleza mahusiano ya kikoloni yalitafuta mbinu za kurudi katika mataifa yaliyokuwa koloni

zao kwa mlango wa nyuma. Kisiasa, katiba na sheria zilitungwa kwa msingi wa ubabe wa kibepari uliotukuza ustaarabu wa kimagharibi dhidi ya ustaarabu wa mataifa yaliyotawaliwa. Suala la ukandamizwaji na unyonyaji wa kiuchumi ni la kimsingi katika MC na kwa mwandishi. Taswira anazowasilisha kuhusu hali hii ya mahusiano ya ukoloni mamboleo yanaashiria msimamo wa mwandishi. Masimulizi yanayolenga "kumsulubisha Shetani" ambaye ni kiashiria cha ukoloni mamboleo kwa ushirikiano na "wasaliti" katika nchi huru yanaakisi mageuzi ambayo anayatamani. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kupata mwao kuhusu itikadi ya mwandishi hasa katika kushughulikia uhuru wa kiuchumi wa mataifa yaliyotawaliwa.

Katika kushadidia imani hii, mwandishi ametumia nukuu mbalimbali kutokana na Biblia, ambayo ni kielelezo cha dini iliyoletwa na wageni. Inaelekea kwamba Ngũgĩ anaiona dini hii kama njia mojawapo iliyotumiwa na mkoloni kumtawala Mwafrika kimawazo na kiimani. Nukuu za Biblia alizotumia pakubwa zimefanyiwa mageuzi ya maneno na kupewa uamilifu wa kuonyesha jinsi ambavyo mkoloni alitumia hila kuendeleza utawala wake kiuchumi na kitamaduni hata baada ya kutoa "uhuru" wa kisiasa kwa mataifa yaliyotawaliwa. Kwa mfano:

**Mfano 32:**

> **MC:** *Gicuunji Gia Kana* (Ukurasa wa 77-81)
> **MT1:** Sehemu ya Nne (Ukurasa wa 83 – 88)
> **MT2:** Chapter Four (Ukurasa wa 79 – 83**)**

Mwandishi anamithilisha hila za mkoloni dhidi ya Mwafrika aliyetawaliwa na simulizi zinazotolewa katika Biblia Takatifu kwa kuzifanyia mageuzi ya kisanii ili

kuafiki hali anayolenga kujadili; utabaka na unyanyasaji wa kiuchumi. Nukuu ifuatayo kutoka MC imetumia mtindo sawa na nukuu kutoka Biblia ya Kikuyu:

> … *uthamaki wa mawara ma guuku thi no uhaananio na* … (MC, Ukurasa wa 77)
> … *uthamaki wa iguru uhaana ta*… (Biblia ya Kikuyu; Mat 13:44)
> … *uthamaki wa iguru ungihaananio na*… (Biblia ya Kikuyu; Mat 13:33)
>
> …ufalme wa hila humu duniani unaweza kufananishwa na… (MT1, Ukurasa wa 83)
> …ufalme wa mbinguni unafanana na … (Biblia ya Kiswahili; Mat 13:44)
> …ufalme wa mbinguni unafanana na … (Biblia ya Kiswahili; Mat 13:33)

Mwandishi ametumia mfumo sawa na ule uliotumiwa katika kurekodi simulizi za Yesu katika Biblia anapotoa mifano ya kulinganisha ufalme wa mbinguni. Kwa kuyageuza maneno; ‘ufalme wa mbinguni’ yaliyotumiwa katika Biblia na badala yake kutumia maneno ufalme wa hila za humu duniani katika uandishi wake, mwandishi anafanikiwa kuchokoa mawazo ya msomaji, hasa mfuasi wa dini ya Kikristo, na kumfikirisha kudadisi imani yake na itikadi yake ya kidini.

Zaidi ya nukuu hii, kuna matumizi mengine ya nukuu kutokana na Biblia ambayo yametumiwa na kufanyiwa mageuzi ama ya kimatumizi au ya ufasili ili kumsaidia mwandishi kutimiza azma yake. Kwa mfano:

**Mfano 33:**
**MC**

> Mugunda-ini ucio eegwaka Kanitha kana o Muthigiti kuriingana na ndini ya andu acio…o kiumia o kiumia andu acio mariihunjagirio na makoonithio ati gutahwo thithino, gukamwo thakame, na kuriio toombo, - ni tuuge o rimwe kuiyo hinya na uugi wao – ati uguo ni guo wendi wa Ngai, na ati kuriinganiite na mibaango ya uhonokanio wake. O ta uria ati kwandikitwo atiri: gukena ri, ni aria mari na kieha, ni gukorwo ni makaniinirwo kieha. Gukena ri, ni aria mahuutaga na makanyootera uthiingu ni gukorwo ni makahuunio. Gukenari, ni aria mateeciiragiria mundu o na u uuru, toondu ni makoona Ngai. Gukena ri ni ngoro

> iria yaathikagira maathani maria ati: Ndukaanoragane, Ndukaanaheenanie, Ndukaanaiye, Ndukaanacuumikire indo ciene… tondu ngoro iyo ni yo ikaagaya utoonga wa matu-ini.
>
> (Ukurasa wa 189-190)

**MT1**

> Katika shamba hilo atajenga kanisa kubwa sana au msikiti mkubwa sana kutegemea imani ya watumwa wake…Kila Jumapili watu hao watahubiriwa kuwa kunyonywa damu, kunyonywa jasho na kukamuliwa mabongo – hebu tuseme kwa jumla, kuibiwa ujuzi wao – ati hayo ndiyo mapenzi ya Mungu, na kuwa mambo hayo yanaambatana vizuri na wokovu wake. Kama ilivyoandikwa katika misahafu: Heri weye huzuni, maana watafarijika. Heri wenye njaa na kiu, maana wao watashibishwa. Heri wenye moyo safi, maana watamwona Mungu. Heri watu wazingatiao amri hizi: Usiue, Usidanganye, Usiibe, Usizionee kijicho mali za mwingine kwani mtu kama huyo ndiye atakayerithi ufalme wa mbinguni…
>
> (Ukurasa wa 200-201)

Nukuu hii inatokana na Sauti ambayo inamsemeza Wariinga katika juhudi za kuyafumbua macho yake kuona hila wanazofanya [17] *Kimeenderi* ili kudumisha udhalimu wao wa kuwakandamiza na kuwanyonya jasho wafanyakazi. Mwandishi anatoa nukuu kutokana na Biblia Takatifu (Mathayo 5: 3-12), na kuitumia kuonyesha jinsi dini na itikadi nyingine za kigeni zilizotokana na mkoloni zilivyotumiwa kuathiri mtazamo wa Mwafrika aliyetawaliwa na kumpumbazwa ili azidi kunyanyaswa. Matumizi haya ya nukuu kutokana na Biblia si ya kisadfa ila yametumiwa makusudi kuashiria unafiki na undumakuwili wa dini ya mkoloni ambayo imetumika pakubwa kumlainisha Mwafrika anayetawalia ili asizinduke na kudai haki yake.

Kwa kuangazia msisitizo unaotolewa kwa haja ya waliokandamizwa kuridhika na hali zao za uchochole na kunyanyaswa kwa ahadi za maisha bora baada ya kifo, mwandishi anaazimia kumfikirisha msomaji na kudadisi itikadi hii ya kidini. Stadi hii

[17] Jina *Kimeenderi* ni nomino inayotokana na kitenzi *Meendeera/monda* chenye maana ya kubonda.

japo haijitokezi kama umbuji moja kwa moja, hasa kwa wasomaji wasioelewa imani Kikristo, imemwezesha mwandishi kueleza mtazamo wake kwa imani za kigeni, za kidini na jinsi zilivyosukwa kwa manufaa ya mtawala.

Ukopaji wa dhana za kiimani na kiitikadi kutokana na dini kwa ajili ya kuziumba upya kuwasilisha uhalisia anaozungumzia mwandishi, unajitokeza bayana anapojadili suala la unyanyasaji; unyonyaji wa damu na ulaji wa nyama ya binadamu, kama wanavyofanya watawala na matapeli wenye uwezo kwa kuwakandamiza wafanyakazi na wananchi wasiokuwa na uwezo. Mwandishi anatoa nukuu kutokana na Biblia ifuatavyo:

**Mfano 34:**

Mugaambo: Jacinta…kai hiihi uriganiirwo ati ucio niguo urutani wa kanitha cianyu…?
Wariinga: Atia…?
Mugaambo: I ati urii andu na unyui wa thakame ya andu ni undu muraathime iguru
na thi? Mwiriingariingaga maita atatu mukoiga atia?
*Agnus Dei, quitollis pecca'ta mundi:*
*Misere're nobis*
*Agnus Dei, quitollis pecca'ta mundi:*
*Dona nobis pacem*
Wariinga: Aaca…Aaca…uguo ti guo kuri!
Mugaambo: Tiguo atia? Ririkana thakaramendi iria wee Wariinga wariiaga wi *Holy Rosary* Naikuru? Baaba wa kanitha ucio wanyu aakuneengagira gicuunji kia mugate akoiga:
*Ecce Agnus Dei,*
*Ecce qui tollit pecca'ta mundi…*
Agacooka niingi agakwira ati uhiingagie uria Njiicu ooigire gwikagwo:
Ria uyu ni mwiri wakwa
Mwikage uguo nginya ngooka…
Ningi Baaba o ucio agacooka ho agakuneengereria ndibei nduune agakwira unyue, o ta uria ati Njiicu aathanire gwikagwo:

Nyua, ino ni thakame yaakwa
Mwikage uguo nginya riria ngaacooka…

(MC, Ukurasa wa 191-192)

Katika mfano huu, mwandishi amekopa baadhi ya dhana zinazotokana na imani ya Kikristo hasa dhehebu la Kikatoliki ambalo lilikuwa miongoni mwa madhehebu ya awali kuingizwa Kenya. Anamithilisha ulaji wa mkate ambao unaaminiwa kuwa ni mwili wa Yesu, unywaji wa divai, ambayo inaaminiwa kuwa ni damu ya Yesu, na unyanyasaji wa kidhalimu wa jasho, na damu ya wafanyakazi. Licha ya kuwa hakuna uhusisho wa moja kwa moja, ulinganisho huu unaashiria jinsi ambavyo dini iliyoletwa na wageni kwa Mwafrika ilivyoanzisha matambiko yasiyo ya kawaida na yanayokiuka utamaduni wa Kiafrika.

Ulaji wa nyama ya binadamu na unywaji wa damu ya binadamu ni taswira ambazo mwandishi ametumia kama jazanda ya jinsi ubepari ulioanzishwa na wakoloni ulivyotumiwa kuwakandamiza wananchi na wafanyakazi. Ukakasi unaotokana na taswira hii inayoibua zoezi ambalo ni mwiko katika jamii unatumiwa kimakusudi kumzindua msomaji ili kujisaili na kutathmini imani yake hasa kuhusu masuala ya imani ya kidini na athari zake kwa mahusiano katika jamii kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kando na dini, mwandishi pia amedadisi mfumo wa elimu ulioletwa na mkoloni. Anadai kuwa mfumo huu umepangwa makusudi kumdhalilisha Mwafrika, utamaduni wake na ustaarabu wake na kumfanya kutamani kuwa kama mkoloni. Kwa mfano anaeleza ifuatavyo:

**Mfano 35:**

> Ndaakwira atia o riu? Ati muri na matu na mutiiguuaga. Muri na maitho na mutionaga. Githoomo giaku gikuinamaniitie wonage ati *Thi* ni kuo *Iguru* nakuo *Iguru* ni kuo *Thi;* wonage ati Uiru ni guo Weu na Weru ni guo *Uiru; wega* ni guo *Uuru* na *Uuru* ni guo *Wega…* (MC, Ukurasa wa 187)
>
> Nimekwambiaje sasa hivi? Kuwa mna masikio na hamsikii. Mna macho na hamwoni. Elimu yako imekupindua mpaka mbinguni unakuona ndiko duniani na duniani unakuona ndiko mbinguni. Weusi unauona ndio weupe na weupe ndio weusi. Wema ukauona ndio uovu na uovu ndio wema… (MT1, Ukurasa wa 198)
>
> What did I tell you just now? That you have eras and you can't hear; you have eyes and you can't see. Your kind of learning has turned you upside-down. You have come to believe that the clouds are the earth and the Earth is the clouds; that black is white and white is black; that *good is evil and evil is good.*
> (MT2, Ukurasa wa 189)

Kutokana na vifungu hivi, masuala kadhaa yanayohusiana na dhana za kiitikadi yanabainika. Kwanza, kuna suala la elimu ya Kimagharibi ambayo mwandishi anadai ndicho chanzo cha mkengeuko na kutojielewa kwa Mwafrika. Maelezo yake yanadai kuwa elimu hii ndiyo imemgeuza Mwafrika kiasi cha kuyaona mambo kinyume. Pili, suala la elimu limehusishwa na suala la utambulisho japo si kwa njia ya moja kwa moja. Wakati mwandishi anaeleza kuwa elimu inamfanya Mwafrika kuona weusi kuwa ndio weupe na weupe kuwa ndio weusi, maneno haya yana maana ya ndani. Japo nyeupe na nyeusi ni rangi tu, katika muktadha wa riwaya hii, na katika muktadha wa baadaukoloni kwa jumla, dhana za weupe na weusi ni za kimsingi katika kubainisha utambulisho wa mkoloni na mtawaliwa. Aidha, ina umuhimu katika kubainisha mahusiano ya kiuwezo yaliyopo baina ya makundi haya mawili. Kwa kuihusisha elimu ya kimagharibi na kukanganyikiwa kwa mwafria kuhusu dhana za weusi na weupe, mwandishi kwa undani analaumu mfumo wa elimu ulioetwa na

wakoloni kuwa ni kichocheo cha kutoweka kwa utambulisho asili wa Kiafrika pamoja na kukengeuka kwa Mwafrika na kwa jinsi hiyo kudhalilisha elimu na maarifa yake huku akikweza yale ya kigeni.

### 4.3 Itikadi katika Uteuzi wa Lugha katika MC na Tafsiri za MT1 na MT2

Munday (2015) akifafanua mawazo ya Van Djik (1998) kuhusu nadharia ya itikadi anaeleza kwamba dhana hii katika lugha aghalabu hutokea katika ngazi mbili kuu; kiwango pana na kiwango finyu cha ubainikaji. Katika kiwango pana, itikadi inatambuliwa kuwa ni zao la muktadha wa utamaduni katika jamii na hudhihirisha mahusiano ya kiuwezo katika jamii kupitia kwa diskosi. Aidha kiwango hiki huhusishwa na muktadha wa hali au sajili ambapo mtazamo wa jumla wa mwandishi kwa kuuhusisha na muktadha wa tafsiri hutumiwa kubainisha itikadi kwenye matini husika. Tukiangazia kiwango finyu cha itikadi kwa mujibu wa Munday (2015), suala la msamiati na sarufi hasa kupitia kwa uteuzi wa kimakusudi na ule usio wa kimakusudi wa msamiati na tungo, hutuwezesha kuelewa mtazamo wa mwandishi na maana alizokusudia kuwasilisha.

Katika utafiti huu, dhana hizi mbili; kiwango pana na kiwango finyu cha udhihirikaji wa itikadi ni za kimsingi katika kuelewa jinsi mwandishi wa MC alivyoiwasilisha itikadi yake na kutathmini jinsi itikadi hii ilivyohawilishwa katika MT1 na MT2 na kwa jinsi hiyo kubaini athari yake kwa maana na mawasiliano ya matini husika. Kiwango pana kwa pakubwa kimehusishwa pakubwa na dhana ya muktadha kitamaduni. Kwa hivyo hatuwezi kuelewa itikadi ya mwandishi wa MC kwa

kuzingatia kiwango pana. Badala yake, kiwango finyu ambacho kinaangazia uteuzi wa kileksia na uteuzi wa tungo kwa njia ya kimakusudi au isiyo ya kimakusudi ndicho kitakachotuwezesha kuchanganua itikadi ya mwandishi aliye pia mtafsiri wa matini zilizorejelewa katika utafiti huu. Kwa kumhusisha mwandishi wa MC na mwelekeo wa baadaukoloni, hatuna budi kuangazia jinsi mtazamo wake binafsi pamoja na uteuzi wake wa maneno unavyosaidia kudhihirisha na kuiwasilisha itikadi yake katika kuandika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na baadaye jinsi uteuzi huu unavyoshughulikiwa katika tafsiri za MT1 na MT2. Kwa mfano:

**Mfano 36:**

**MC:** *Caitaani Mutharaba-ini*
**MT1:** Shetani Msalabani
**MT2:** *Devil on the Cross*

Mfano huu umetokana na anwani za riwaya zilizorejelewa. Uteuzi wa anwani hii ni wa kimakusudi na ni madai yetu kwamba unasheheni dhana za kiitikadi ndani. Madai haya yanashadidiwa tunapozingatia vipengele vya diskosi hasa kwa kujikita kwa maana kimuktadha, lugha ya kitamathali na mwingiliano matini. Mwandishi katika MC, licha ya kuwa hii ndiyo riwaya ya kwanza kuandika katika lugha ya Kikuyu, anateua dhana ambayo haina uasilia katika utamaduni asilia wa Kikuyu. Hii ni licha ya kuwa dhana anayoirejelea ina kiaswe chake katika utamaduni wa Gĩkũyũ. Neno *Caitaani* kama lilivyotumiwa ni neno mkopo kutokana na neno la Kiswahili *Shetani* ambalo pia asili yake ni Kiarabu. Neno hili, *Caitaani*, limetumika kama kiwakilishi cha kisababishi cha maovu yote miongoni mwa binadamu. Katika lugha ya Kikuyu, imani na utamaduni wake ulitumia dhana ya *Ngoma* kwa maana ya *Mzimu*. Iliaminika

kuwa kuna mizimu mizuri, *Ngoma Njega* na mizimu miovu, *Ngoma Njuuru*. Dhana ya *Caitaani* iliingizwa katika utamaduni wa Gĩkũyũ kutokana na majilio ya dini ya Kikristo. Dini iliyoletwa na wamishenari, ambao kwa misingi ya baadaukoloni wanaaminika kuwa walitekeleza dhima muhimu katika kufanikisha ukoloni.

Hivyo basi, uteuzi anaofanya Ngũgĩ wa kutotumia dhana ya kiasili katika anwani ya riwaya yake na badala yake anateua dhana yenye asili ya kigeni pakubwa ni uteuzi wenye msingi wa kiitikadi. Dhana hii imetumiwa kijazanda kama kiwakilishi cha mkoloni na asasi za kigeni zinazoendeleza ukoloni mamboleo. Aidha, kwa kuwa dhana *Caitaani* ni ya kigeni, tunaweza kuifasili kama jazanda na kiwakilishi cha athari hasi za mgeni kwa jamii iliyotawaliwa kiimani, kijamii, kisiasa na hata kiuchumi.

Uchukulio huu unaambatana na itikadi ya mwandishi na hata ya jamii iliyotawaliwa kuhusu mkoloni na asasi za kigeni zinazodhibiti na kuathiri mifumo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hivyo basi, kutokana na uteuzi huu, mwandishi anaashiria kuwa uovu uliomo katika jamii una asili ya kigeni bali si wa kiasili. Isitoshe, neno hili *Caitaani* limetumiwa pamoja na dhana nyingine yenye asili ya kigeni kutokana na dini ya Kikristo, *Mutharaba*. Hili ni neno ambalo limekopwa kutokana na neno la Kiswahili *Msalaba* ambalo pia halina uasilia katika Kiswahili. Maelezo yametolewa kuhusu maana ya nenO msalaba kama vile[18]:

1. Alama inayowakilisha kusulubiwa kwa Bwana Yesu Kristo.

---

[18]TUKI (2019)

2. Ishara ya wokovu au msamaha wa dhambi kwa Wakristo.

Kwa kutumia kitomeo hiki kwa mujibu wa kamusi hii, uteuzi wa Ngũgĩ wa kutumia dhana ya *Caitaani Mutharaba-ini* kama anwani ya riwaya yake unakuwa wa kinaya hasa tunapofahamu kuwa aliyekuwa msalabani ni Yesu ambaye ni ishara ya wema na wokovu. Hata hivyo, kwa kumtundika Shetani msalabani katika riwaya hii, Ngũgĩ anaonyesha jinsi ambavyo uovu na wanaosababisha uovu huo wanapaswa kusulubiwa ili walionyanyaswa wapate kujikomboa. Suala la ugeni wa dini ya Kikristo pamoja na mafundisho yake ambayo mwandishi ametumia kudhihaki ustaarabu wa kigeni linaibuliwa kimakusudi kwa lengo la kubainisha mtazamo na msimamo wa mwandishi kuhusu dhana hii ya dini ya kigeni. Maisha ya mwandishi katika ulimwengu halisi yanadhihirisha kwamba yeye alitangamana na dini ya Kikristo kwa karibu sana hasa tunaposoma kitabu chake *In the House of The Interpreter* (2012). Mitazamo yake binafsi kuhusu imani ya Kikristo imeelezwa vyema katika tafiti mbalimbali na maandishi yake mwenyewe. Yeye aliasi dini ya Kikristo kiwango cha kuacha kutumia jina la "*Kikristo/la Ubatizo"* na badala yake akarejelea mtindo asilia unaozingatia mfumo wa majina ya jamii ya Gĩkũyũ na kujiita Ngũgĩ wa Thiong'o kwa maana ya Ngũgĩ mwana wa Thiong'o.

Katika tafsiri za MC kwa Kiswahili na kwa Kiingereza, dhana *Caitaani* imetafsiriwa moja kwa moja kwa kutumia visawe vyake; *Shetani* na *Devil* mtawalia. Uamuzi huu unadumisha kinaya kilichomo katika MC. Hata hivyo, undani wa uelewa wa kiitikadi unaodhihirika katika MC huenda haubainiki kwa kiwango sawa hasa katika MT2

kutokana na umbali wa kitamaduni pamoja na uasilia wa dhana ya *devil* katika imani ya Kikristo. Uteuzi wa kileksia kama kigezo cha udhihirikaji wa itikadi ni dhana ambayo mwandishi ameitumia kujieleza kwa njia ambayo wakati mwingine inabainisha kwa uwazi zaidi jinsi anavyochukizwa na athari ya kikoloni. Kwa mfano:

**Mfano 37:**

> **MC**: *Kimuthuungu kimwe* (Ukurasa wa 138)
> **MT1:** Mzungu mmoja (Ukurasa wa 147)
> **MT2:** European (Ukurasa wa 140)

Katika mfano huu neno *Kimuthuungu* lililotumika katika MC linaibua hisia hasi dhidi ya anayerejelewa. Tukiangazia muundo wa neno hili, limetokana na neno *Muthuungu* katika hali ya kawaida. Hata hivyo, jinsi lilivyotumika hapa, limeambishwa kiambishi *ki* ambacho katika lugha ya Kikuyu aghalabu hutumiwa kuibua maana mbili; maana ya ukubwa na kwa wakati huo huo kuibua hisia hasi za kutopendeza. Alomofu ya kiambishi *ki* ambayo ni *gi* kama vile katika *gikaari* ambalo linaweza kuwa na maana ya gari kubwa au gari kuukuu/bovu. Matumizi ya uambishaji katika muktadha huu yanatuwezesha kuelewa mtazamo wa mwandishi kuhusu wazungu. Maelezo kamili ya nukuu ambamo neno hili limetumika ni;

> Wariinga…aarotaga na caitaani ari na gikonde kieru cua to gia *kimuthuungu* kimwe kinoru muno Wariinga oonire rimwe hakuhi na Rift Valley Sports Club
> (Ukurasa wa 138)

Katika muktadha huu, Mzungu anayerejelewa hapa anapewa sifa za kutopendeza kutokana na unene wake. Isitoshe, Wariinga katika muktadha huu alikuwa akiota na katika ndoto yake alimwona shetani akiwa anafanana na *kimuthuungu*… Ulinganisho

huu wa Mzungu anayerejelewa na shetani unashadidia hoja kuwa kuna ukakasi fulani ambao unaibuka kutokana na uambishaji uliofanywa. Aidha, uambishaji huu unaitoa nomino hii kutoka kwa ngeli ya binadamu – Mundu/Andu, Muthuungu/Athungu (A-Ma) – katika lugha ya Kikuyu na kuiingiza katika ngeli ya vitu visivyo hai. Udunishwaji huu sio wa kisadfa ila tunautambua kuwa dhihirisho la uteuzi wa kimakusudi uliochangiwa na itikadi ya mwandishi.

Hata hivyo, tunapoangazia tafsiri ya Kiswahili na hata ile ya Kiingereza haidumishi ukakasi huu. MT1 na MT2 zimetumia neno la wastani ambalo haliibui hisia/sifa hasi kwa mrejelewa; *Mzungu* na *European* mtawalia. Hali hii inajitokeza kama upotoshi wa itikadi ya mwandishi katika tafsiri jambo linaloathiri uwasilishaji wa maana kikamilifu. Hali sawa na hii inajitokeza tunapotafakari mfano ufuatao:

**Mfano 38:**

**MC:** *Njaanji oima Muthuungu wi na gikoonde gituune ta Nguruwe. Iniuru riake riigucunukaga nguuci ta mwiri wa njagathi…* (Ukurasa wa 38)

**MT1:** Hakimu alikuwa Mzungu aliyekuwa na ngozi nyeupe kama ya nguruwe. Pua lake refu lilikuwa limebambuka na magamba yalitokeza kama ya mjusi… (Ukurasa wa 42)

**MT2:** *The judge was a European with a skin that was red like a pig's. His nose was peeling like a lizard's body …* (Ukurasa wa 39)

Katika mfano huu, mwandishi vilevile ametumia ulinganisho ili kuibua hisia hasi dhidi ya Mzungu ambaye ni kiwakilishi cha mkoloni. Anaeleza kuwa ngozi ya hakimu ambaye alikuwa akiendesha kesi dhidi ya Wangari ilikuwa sawa na ngozi ya nguruwe. Kumithilisha ngozi ya hakimu huyu na ngozi ya nguruwe ni tukio la kimakusudi lenye lengo la kuibua hisia hasi dhidi ya mrejelewa. Maana ya neno

nguruwe kimuktadha inaeleweka tunapoangazia utamaduni wa Gĩkũyũ ambapo nguruwe ni mnyama aliye na sifa hasi zikiwemo; uchafu na kuwa na umbo/sura mbaya, pamoja na ulafi. Kwa kutumia ulinganisho huu, mwandishi anafaulu kuitweza hadhi iliyowekewa rangi ya ngozi ya Mzungu kiasi cha kuwafanya baadhi ya watu weusi kutumia dawa za kugeuza rangi za ngozi yao nyeusi ili ikaribiane na ya Mzungu.

Uhawilishaji wa dhana hii ya *nguruwe* katika tafsiri za MT1 na MT2 unaibua masuala kadhaa. Katika MT1, mtafsiri ametumia dhana ya nguruwe ambayo ni tafsiri linganifu kisemantiki na dhana iliyotumiwa katika MC. Hata hivyo, maana iliyo muhimu zaidi hapa ni maana kimuktadha kama tulivyoeleza hapo juu. Katika ngazi hii, dhana nguruwe katika Kiswahili haiibui ukakasi sawa na dhana *nguruwe* katika Kikuyu. Katika msingi wa dini ya Uislamu ambayo inaweza kuhusishwa na lugha ya Kiswahili kihistoria, nguruwe ni mnyama haramu. Ni marufuku kumla. Hata hivyo katika jamii pana ya Waswahili, suala la uhasi wa mnyama nguruwe halijitokezi moja kwa moja. Kwa mfano kuna methali inayosema “ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona”.

Katika MT2, neneo *nguruwe* limetafsiriwa kwa mtindo sawia, sisisi, kuwa *pig.* Dhana hii katika utamaduni wa Kiingereza haiibui ukakasi wowote. Nguruwe ni mnyama ambaye anapendwa na wasemaji wazawa wa Kiingereza (Uingereza na Marekani). Nyama yake ni mlo mtamu kwao. Hivyo dhana hasi zinazohusishwa na mnyama huyu katika utamaduni chanzi zinakosa kuhawilishwa kwa njia linganifu katika MT1 na MT2. Uteuzi huu unaathiri ubainikaji wa itikadi ya mwandishi dhidi ya ukwezwaji wa

rangi ya ngozi ya Mzungu dhidi ya ile ya Mwafrika. Mwandishi anatumia maneno, *gikoonde gituune* kurejelea rangi ya ngozi ya hakimu. Hii ni kinyume na inavyoelezwa katika MT1 ambapo neno *nyeupe* linatumiwa huku Kiingereza kikidumisha maana ya MC kwa kutumia neno *red.* Suala la rangi ya ngozi ni la kimsingi katika mahusiano ya kiuwezo hasa katika muktadha wa baadaukoloni. Mwandishi katika MC anaamua kimakusudi kuiwakilisha rangi hii kama nyekundu bali si nyeupe. Uamuzi huu ni kinyume na hali ya kawaida ambapo rangi ya Mzungu imehusishwa na weupe ambao zaidi umehusishwa na mambo mazuri huku rangi nyeusi ikitumiwa kurejelea ngozi ya mwafrika na ikihusishwa na uovu. Huenda hali hii ndiyo iliyomchochea mwandishi sawia na mtafsiri wa MT2 kuenda kinyume na mazoea kwa kutumia rangi nyekundu badala ya nyeupe. Hata hivyo, tunapoangazia MT1 tunapata kuwa kuna utofauti ambapo rangi ya ngozi ya hakimu inaelezwa kuwa ilikuwa nyeupe. Uteuzi huu unafuata maelezo ya kuikweza rangi ya ngozi hii jambo ambalo ni kinyume na hali katika MC na MT2.

Maelezo ya ziada yanatolewa kuhusu ngozi hii. Uteuzi anaofanya mwandishi katika MC wa kutumia neno *Nguuci* kwa maana ya magamba ni wa kimakusudi. Taswira inayochorwa ya sura ya hakimu haipendezi. Taswira hii ambayo imeumbwa na kuwasilishwa kupitia kwa lugha imetumiwa kimakusudi. Hii ni kuambatana na mtazamo wa mwandishi ambaye tunadai kuwa analenga kuidhalilisha rangi ya Mzungu na kwa jinsi hiyo kujaribu kuathiri mahusiano ya kiuwezo baina ya Mzungu na Mwafrika.

Itikadi kupitia kwa uteuzi wa kiisimu haipo tu katika uteuzi wa kileksia bali pia inajitokeza katika miundo ya tungo ambapo mwandishi anayapanga maneno kimakusudi ili kuwasilisha mtazamo wake kuhusu makundi ya watu, hali au masuala mbalimbali katika jamii. Kwa mfano:

**Mfano 39:**

**MC:** Wendani ndoonire kuo
Wa ciana na atumia
Mbooco yaagwa thi
Tukeenyurana …

Nayo ngwataniro ya Ngaati na Thukumu yaaringithagia rwimbo atiri;

Kwiyeenda na kwendia andu
Gwa thaata cia bururi
Mbooco twaiya andu
Tugatharana…

Wee iyo ya ngaati na Thukumu yaari ngwataniro ya uunyamu:
ati kuna kaba muundu aikie ciana na cionje riiko akiguthukira matigio na matahiko na Thukumu?
Ya Mau mau yaari ya Umuundu, toondu muundu aarutaga muoyo wake agitire ciana na cionje.
Ya ngaati ya kwendia bururi: ya Mau Mau yaari ya kugitira bururi!

(Ukurasa wa 33- 34)

**MT1:** Mapenzi niliyoyaona huko
Ya watoto na wanawake
Haragwe likianguka chini
Watu hao hugawana.

Nao wasaliti na wabeberu walikuwa wakiimba wimbo wa namna hii;
Kujipenda na kuwauza watu
Kwa utasa wa nchi
Tukiwaibia watu haragwe
Tunanyang’anyana.

Ushirikiano wa wasaliti na wabeberu ulikuwa wa kinyama kwani haukujali

Utu. Haukujali watoto na wasiojiweza. Wasaliti walipokimbilia kuramba

> makombo ya wabeberu, waliwapiga pembe watoto, wanawake na wasiojiweza. (Ukurasa wa 37)

Katika mfano huu, mwandishi katika MC ameviweka vipashio vinavyokinzana katika mazingira jirani ili kushadidia utofauti uliopo baina ya makundi mawili; wazalendo dhidi ya wasaliti. Utukiaji wa mawazo haya katika mazingira jirani unatusaidia sio tu kuelewa tofauti iliyopo bali pia tunapata mwao wa mtazamo wa mwandishi. Kwa kulinganisha vitendo vya upendo na huruma vya wanawake na watoto waliotiwa kizuizini na wakoloni; kugawana haragwe likianguka dhidi ya ulafi na ubinafsi wa wasaliti wa taifa walioshirikiana na wakoloni; wanawapiga pembe wasio na uwezo wakikimbilia makombo ya wakoloni, mwandishi anafanikiwa kuonyesha tofauti za kiitikadi baina ya makundi hayo mawili. Analipa kundi la wazalendo sifa ya utu huku akilipatia kundi la wasaliti wa taifa sifa za unyama.

Wasaliti wa nchi, yaani walioshirikiana na wakoloni katika kuendeleza utawala wao dhalimu wanapewa utambulisho wa *thaata cia bururi* katika MC. Uteuzi huu unapowekwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii ya Gĩkũyũ unatekeleza dhima muhimu ya kuonyesha nafasi ya watu kama hawa katika jamii. Kwa mfano, wanawake tasa katika utamaduni wa Gĩkũyũ walichukuliwa kuwa hawana maana, waliwekwa katika kundi la chini zaidi katika jamii. Kwa kukosa wana, hawakugawiwa shamba, hasa pale ambapo mume alikuwa na wake wengi, jina lao "lilipotea". Dhana hii ya jina kupotea ni tafsiri sisisi kutoka lugha ya Kikuyu. Kutokana na mfumo wa utoaji majina katika jamii ya hii, mwanamke tasa hakuwa na mwana wa kuendeleza jina lake na kwa jinsi hiyo jina lake halikuendelezwa kwa

kukosa mwana wa kuliendeleza. Hivyo basi wanawake kama hawa hawakuthaminiwa kwa njia yoyote katika jamii. Kwa kutumia maneno haya kuwarejelea walioshirikiana na wakoloni, mwandishi anahawilisha uhalisia wa mwanamke tasa katika jamii ya Gĩkũyũ na kuupachika kwa watu hawa. Kwa jinsi hii, anafanikiwa kuwatweza na kuwadhalilisha kwa kutumia malighafi ya utamaduni wake asilia. Uteuzi wa neno *thaata* hivyo basi ni wa kimakusudi unaotokana na mtazamo na imani ya mwandishi kisiasa na kitamaduni. Angetumia neno kama vile *Thũ* kwa maana ya *adui* lingewasiliana ila tu kwa kuwasilisha maana moja. Neno *Thaata* katika muktadha huu, hivyo basi, linatekeleza dhima muhimu kando na kuonyesha utovu wa uzalendo miongoni mwa wasaliti hawa.

Ngũgĩ katika kuumba MC, amefanya uteuzi mwingi wa kimakusudi katika lugha aliyotumia. Kufikia sasa, tumeangazia baadhi ya uteuzi aliofanya kama vigezo vya kitamaduni na au vya kiitikadi. Hata hivyo, zaidi ya kuwa lugha imetumiwa kwa dhima hizi katika MC, tunatambua kwamba kama ilivyo kwa ujumla, lugha ni mfumo ambao kupitia kwake mtumiaji huwasilisha maana fulani, akajenga uhalisia kutokana na tajriba zake katika ulimwengu halisi ama wa kufikirika na muhimu zaidi ni kwamba, kupitia kwa lugha, mtumiaji huweza kujinasibisha na mtu, wazo au hata kundi fulani la watu na kwa jinsi hiyo kujenga utambulisho. Edwards (2009) anaeleza kwamba katika kuitumia lugha, bila kukusudia, aghalabu huwa tunatangamana na dhana za kitamaduni ambazo ni sehemu ya matumizi ya lugha. Hivyo basi matumizi yetu ya lugha hufungamana na huathiriwa na uwezo wa lugha kutumiwa kama

kiwakilishi cha dhana za kitamaduni, kihistoria na hata utambulisho wa kijamii. Hali hii ndiyo iliyoangaziwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.4 Utambulisho katika *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake MT1 na MT2

Gumperz (1982) katika kujadili suala la utambulisho anatambua kuwa, katika ulimwengu wa sasa, utambulisho unafasiliwa katika vigezo vya jinsia, kabila na tabaka. Vilevile, anaeleza kwamba katika kuelewa masuala yanayohusiana na utambulisho na jinsi yanavyoathiri na kuathiriwa na mpangilio wa kijamii, kisiasa na kikabila, sharti tutalii michakato ya kimawasiliano ambamo masuala haya yanaibuliwa. Katika mazingira ya utafiti huu, dhana hizi za jamii, siasa na kabila ni muhimu katika kutalii utambulisho hasa katika muktadha wa baadaukoloni. Utambulisho hasa wa kikabila, katika muktadha huu wa Kiafrika, ni nyenzo ya kuibua msaada wa kisiasa na kijamii katika harakati za kufikia malengo ya jamii pana kama vile mahusiano sawa ya kiuwezo baina ya mtawala wa kikoloni na mtawaliwa kilugha, kitamaduni, kisiasa, kiuchumi na hata kimahusiano kwa ujumla.

Katika muktadha wa baadaukoloni, suala la utambulisho ni mojawapo ya vipengele vya kimsingi. Hata hivyo, utambulisho katika mazingira ya baadaukoloni unakuwa dhana changamano kwa kuwa aghalabu unadhihirika kwa umahuluti kutokana na athari za utamaduni, lugha na tajriba za kigeni. Klinger (2013) anafafanua mikakati ambayo imebainishwa kwamba inatumiwa katika kubainisha umahuluti ikiwemo: ubadilishaji msimbo, ubunaji wa istilahi mpya pamoja na kujumuisha dhana za kimasimulizi katika uandishi.

Katika kushughulikia dhana ya utambulisho katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, hatuna budi kuangazia jinsi lugha ilivyotumiwa kama kigezo cha ubainishaji huu.

**Mfano 40:**

**MC**: *Gĩkũyũ ooigire ati muruga igiri ndaagaga imwe iriicura* (Ukurasa wa 42)
**MT1**: Wahenga walisema kuwa mwangaza mbili moja humponyoka (Ukurasa wa 46)
**MT2:** *Gĩkũyũ said that no one can cook two pots of food simultaneously without burning the contents of one of them* (Ukurasa wa 43)

Katika mfano, tunapata kwamba kuna urejelezi wa dhana ya *Gĩkũyũ*. Huyu anaaminika kuwa ndiye baba wa jamii ya *Gikuyu*. Katika mfano huu anahusishwa na usemi unaofuata. Kwa kutumia neno hili katika MC, mwandishi anafanikiwa katika kuonyesha utambulisho wa matini hii kitamaduni na kwa jinsi hiyo anajenga utambulisho wake binafsi na kikabila. Aidha, katika tafsiri ya Kiingereza, dhana hii ya *Gĩkũyũ* inahawilishwa jinsi ilivyo. Zoezi hili linadhihirika kama ubadilishaji msimbo katika MT2 hali ambayo inaashiria umahuluti wa kiisimu katika matini hii. Uamuzi huu ni wa kimakusudi hasa tunapozingatia hoja kwamba, licha ya MT2 kuwa ni tafsiri binafsi ya mwandishi wa MC, mtazamo wake kuhusu mahusiano ya kiisimu na kitamaduni baina ya lugha ya asilia, Kikuyu¸ na lugha ya kibepari (Kiingereza) ni wa kujaribu kuleta usawa. Kwa jinsi hii, matini ya Kiingereza inahusishwa moja kwa moja na utamaduni wa Gĩkũyũ sio tu kama zoezi la kiitikadi bali pia ili kuipa utambulisho mahuluti na kuihusisha moja kwa moja na utamaduni chanzi.

Kwingineko katika MC, mwandishi ametumia maneno ya kigeni ambayo ama yamesharabiwa moja kwa moja au yameendelezwa kwa kuzingatia lafudhi inayoonyesha ugeni wake katika mfumo wa Kikuyu. Kwa mfano:

**Mfano 41:**

**MC:** …*nguundi waka Mithita Mugwate, nguundi waka*… (Ukurasa wa 37)
**MT1:** …*Good work, good work Mr. Mugwate, good work*… (Ukurasa wa 41)
**MT2:** …*Good work, Mr. Mugwate, good work*… (Ukurasa wa 39)

Maneno haya yalivyoendelezwa katika MC yanazinagatia mofolojia ya lugha ya Kikuyu licha ya kuwa haya ni maneno ya kigeni. Yanasemwa na Wangari akieleza jinsi Mzungu alivyokuwa akimpongeza meneja Mwafrika kwa kuwaita polisi kumkamata. Maneno haya yametumiwa kimakusudi kuonyesha athari za lugha ya kigeni hata kwa wale wasioimudu. Hii ni hali ambayo inaashiria athari za lugha ya Kiingereza kwa lugha ya Kikuyu. Maneno yanayotumiwa hapa, licha ya kuashiria athari za kigeni kiisimu yametumiwa pia kuonyesha jinsi ambavyo utamaduni wa kigeni umewateka nyara Waafrika ambao wamo mbioni kung'ang'ania kufanana na wageni wa kikoloni. Huenda ndiyo maana Mwafrika anayerejelewa hapa amepewa jina la kimajazi *Mugwate* ambalo lina maana ya aliyetekwa nyara. Katika MT1 na katika MT2, maneno haya ya Wangari yanabainika kama Kiingereza sanifu hali ambayo inapotosha maana na utambulisho unaojitokeza katika MC. Hata hivyo, neno *Mugwate* linadumishwa kwa mhusika wa Kiafrika anayemsaliti Wangari.

Katika kujadili suala la umahuluti wa utambulisho kupitia kwa lugha, ubadilishaji msimbo aghalabu umetumiwa kama kigezo cha kuonyesha athari hasi za utawala wa

kikoloni kwa lugha na tamaduni asili za watawaliwa. Hali hii katika matini zilizorejelewa imetumiwa zaidi kwa wahusika ambao ni viwakilishi vya wasomi katika jamii. Wametumiwa kuonyesha jinsi elimu yao ya kimagharibi imewakengeusha kutokana na lugha na tamaduni zao asilia. Kwa mfano:

**Mfano 42:**

**MC:** "*Even mine, I mean,* o na ciakwa *forget it, sorry, I mean,* riganirwo ni cio," …Gatuiria ni acoonokaga ni gutukania kiingenu na GiiGĩkũyũ no ni aageragia muno kwaga gwika uguo… (Ukurasa wa 32)

**MT1:** "*Even mine, I mean,* hata zangu, forget it, *Sorry I mean,* zisahaulie mbali," …Gatuiria aliona haya kuchanganya Kiingereza na Kiswahili lakini alikuwa akijaribu sana asifanye hivyo… (Ukurasa wa 36)

**MT2: '***Even mine…I mean, Mine also, forget it – sorry, I mean,* forget about my share.'…Gatuiria was always ashamed of mixing English and Gĩkũyũ words, and he tried hard not to do it… (Ukurasa wa 34)

Katika mfano huu, suala la ubadilishaji msimbo limejitokeza bayana katika maneno ya mhusika Gatuiria katika MC na katika MT1. Kinyume na waandishi wengine[19] ambao waliwahi kutumia mbinu hii kuashiria mkanganyiko wa utambulisho kwa Waafrika waliowahi kutawaliwa, Ngũgĩ anatoa ufafanuzi wa moja kwa moja kuonyesha jinsi athari za kigeni zinavyoathiri umilisi wa kimawasiliano katika lugha asilia. Hii huenda ni kutokana na msimamo wake kuhusu lugha za kigeni kwa ujumla. Matumizi ya Kiingereza katika MC na katika MT1 ni kielelezo cha utofauti na utabaka unaobainika baina ya Waafrika waliopata elimu na wasiopata elimu. Ukilinganisha Kizungu cha Gatuiria katika MC (mfano 42) na kile cha Wangaria katika MC (mfano 41), inabainika kwamba kuna tofauti za kiumilisi baina ya

[19] Tazama Chinua Achebe (1974, 1960) *No Longer at Ease*, *Arrow of God* na Okara (1973) *The Voice.*

wahusika hawa wawili. Hata hivyo, katika MT2, dhana hii ya ubadilishaji msimbo haijitokezi bayana ila inabainika tu kupitia kwa maelezo ya mtafsiri (mwandishi). Hali hii japo inafanikiwa kueleza kile ambacho mwandishi katika MC alilenga kuwasilisha, inapungukiwa kiumbuji kwa kuwa maneno yote, ya Kiingereza na ya Kikuyu, yanawasilishwa kwa Kiingereza. Katika MT1 vile vile, utambulisho unabadilishwa kabisa ambapo sasa Gatuiria anasemekana kuwa ni msemaji asilia wa Kiswahili. Maelezo ya mwandishi katika MT1 ni kuwa:

> Gatuiria aliona haya *kuchanganya Kiingereza na Kiswahili* lakini alikuwa akijaribu sana asifanye hivyo… (ukurasa wa 32) (Msisitizo wangu)

Hali hii inaibua utata wa kiutambulisho kwa mhusika huyu ambapo ana jina la Gĩkũyũ ambalo ni la kimajazi (lenye maana ya mtu anayedadisi mambo) ila anatambulishwa kuwa ni msemaji wa lugha ya Kiswahili. Utata huu huenda unatokana na utata wa kiutambulisho ambao mwandishi aliye pia mtafsiri wa kazi hii anapitia au ukawa ni upungufu katika tafsiri kwa kulenga kuipa MT1 uasilia kama matini ya Kiswahili licha ya kusheheni vipengele vya utamaduni tofauti. Kwa kutumia lugha ya Kikuyu, mwandishi anadumisha uzalendo wa kikabila na kushadidia imani yake katika uwezekano wa kutumia lugha za Kiafrika kuumba fasihi. Hata hivyo, tafsiri ya Kiswahili anaieleza kama hatua muhimu hasa kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya kitaifa na kieneo. Kwa jinsi hii, Ngũgĩ katika kutafsiri *Caitaani Mutharaba-ini* kwa Kiswahili analenga kujinasibisha na taifa na eneo mahususi ambamo Kiswahili kinatumika. Licha ya azma hii, MT1 inapochanganuliwa katika

mazingira ya baadaukoloni inakosa sifa kama vile za uibuaji wa ugeni, au hata ubadilishaji msimbo kama mbinu ya uibuaji wa utambulisho mahuluti.

Suala la utambulisho, hasa utambulisho wa Kiafrika, limeibuka kuwa la kimsingi hasa kutokana na maelezo ya mwandishi katika MC. Wahusika ambao ni viwakilishi vya makundi mbalimbali ya Kiafrika wameelezewa jinsi walivyojitambua mwanzoni mwa riwaya na utambulisho wao unafuatwa hadi mwisho. Kwa mfano, tukimwangazia Wariinga ambaye ni kiwakilishi cha mwanamke wa kisasa aliyepata elimu ya wastani na aliyetangamana na utamaduni wa kigeni, anaelezwa ifuatavyo mwanzoni mwa riwaya:

**Mfano 43**

**MC:** Waaringa aatuuraga eciiragia ati muumbire wake ni guo wari gitina kia mathiina makaake. Eerora, eeyonaga ari njong'i muno. Kiriaaamenete munoni uiru wake. Ni eethuukagia mwiri muno na ndaawa iria icinaga ikoonde ta *ambi*, na *Snowfire*, akariganirwo ati wairire ndakeeruha. Wmiri wake riu wari na icigo njeru na njiru ta ngaanga. Njuiri nayo yaatuikaangite na igatuuniha ta guoya wa huko ni kumuundagio na icanuri cia cuuma kaingi. Kiria kiingi ameneete ni magego make. Magego make maari mathitu haniini; matiari meru cua, ta uria angiendire makorwo mahuana… No riria Wariinga akeneete, akariganirwo ni uthitu wa magego kana uiru wa gikoonde, agatheka na ngoro yaake yoothe, mitheko iyo yaheheenjaga andu kuheheenja. Aari mugaambo wa maguta. Maitho mahenagia ta njata utuku. Kiuga giake kiari gia kwirorerwo. Kaingi na kaingi agikinyukia njira-ini eeriganiirwo nyoondo ciake ikiinainaga ta matuunda meeri makiinainio ni karuhuuho Wariinga ni aatumaga aanake moinike ngiingo. (Ukurasa wa 5)

**MT1:** Wariinga daima alifikiri kuwa sura yake mbaya ndiyo ilikuwa chanzo cha taabu zake. Aliudharau weusi wake. Alikuwa akiiharibu ngozi yake kwa madawa ya *Ambi* na *Snowfire* ati akitaka kuiondolea mbali hiyo rangi yake nyeusi. Alisahau kuwa mweusi hawezi kuwa mweupe. Mwili wake, kwa sababu ya madawa hayo, ulikuwa na mapakupaku meusi na meupe kama kanga. Nywele zake nazo zilikuwa zimekatikakatika na kubadilika rangi, zikionekana kama za fuko kwa sababu ya kuchanwa mara kwa mara kwa vitana vya moto vya chuma. Kitu kingine alichokichukia ni meno yake.

Hayakuwa meupe sana kama angalivyotaka. Yalikuwa na rangi ya hudhurungi iliyochujuka…wakati Wariinga alipokuwa katika kilele cha furaha na kucheka, akasahau hali mbaya ya meno yake na weusi wake, kicheko chake kiliwavutia watu wengi. Sauti yake ilikuwa kama ya kinanda kizuri. Macho yake yalimetameta kwa furaha kama nyota. Umbo lake kwa jumla lilivutia ajabu. Mara nyingi Wariinga akiwa njiani akitembea, akiwa mchangamfu, na matiti yake kifuani yakiyumbayumba kwa mwendo wake wa madaha, kama matunda mawili yaliyoyumba huku na huko kwa mvumo wa upepo, aliwavunja wanaume shingo.

**MT2:** Wariinga was convinced that her appearance was the root cause of all her problems. Whenever she looked at herself in the mirror, she thought herself very ugly. What she hated most was her blackness, so she would disfigure her body with skin-lightening crams like Ambi and Snowfire, forgetting the saying; that which is born black will never be white. Now her body was covered with light and dark sports like the guinea fowl. Her hair was splitting, and it had browned to the colour of moleskin because it had been straightened with red-hot iron combs. Wariinga also hated her teeth. They were a little stained; they were not as white as she would have liked them to be…But when Wariinga was happy and forgot to worry about the fading whiteness of her teeth and about the blackness of her skin and laughed with all her heart, her laughter completely disarmed people. Her voice was as smooth as perfume oil. Her eyes shone like stars in the night. Her body was a feast for the eyes. Often, when she walked along the road without self consciousness, her breasts swaying jauntily like two ripe fruits in a breeze, Wariinga stopped men in their tracks.

Wariinga katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* ni mhusika mkuu. Anawakilisha jamii iliyonyanyaswa, masaibu yake na mwisho ukombozi wa jamii hii. Hivyo basi tunaweza kueleza kwamba taswira inayotolewa hapa katika nukuu hii kuhusu umbo lake na jinsi alivyojitazama ni kielelezo cha jinsi jamii hii inavyojichukulia. Maelezo ya mwandishi yanaangazia pande mbili za mhusika huyu. Kwa upande mmoja, mwandishi anasimulia kuhusu msichana ambaye anaichukia sura yake mwenyewe. Kila kitu kinamchukiza, rangi yake nyeusi, meno yake yasiyokuwa meupe kabisa na hata nywele zake za singa alizozichoma kuzilainisha kiasi cha kuzigeuza kuwa mithili

ya ngozi ya fuko. Anatumia dawa za kuchoma ngozi lakini matokeo ni mapakupaku meupe na meusi usoni. Taswira hii tunaihusisha na utambulisho wa Mwafrika. Anajitizama kuwa duni na hafai. Ngozi yake inayompa utambulisho wake haimfurahishi ila anatamani kuwa na ngozi kama ya Mzungu. Nywele zake za singa anazilainisha kwa vitana moto vya chuma ili inyooke kama ya Mzungu. Hali hii inaashiria mkengeuko wa kuasi utambulisho asilia na kutamani kufanana na Mzungu. Hata hivyo, maelezo ya matokeo ya majaribio ya kujibadilisha ni kielelezo cha msiba unaotokana na mkengeuko huu. Kama anavyoeleza mwandishi mwenyewe, kilicho cheusi hakigeuki kuwa cheupe.

Kuhusudu sura ya Kizungu na kudharau sura asili ya Mwafrika kunaishia kusababisha madhara yanayoharibu sura kabisa. Tukitumia taswira hii kama jazanda ya utambulisho, tunapata kwamba Mwafrika alikuwa na utamaduni wake, mila na desturi ikiwemo lugha. Hata hivyo, mkoloni anapofika, baadhi ya Waafrika wanatamani kuiga Uzungu lakini matokeo yake ni kukanganyikiwa. Husuda ya kufanana na Mzungu kisura na kitabia ni mojawapo ya masuala yanayoangaziwa na kupingwa na wanabaadukoloni. Kuukweza utamaduni wa mkoloni na kuufanya ule wa mtawaliwa kuonekana duni ni hali inayochangia kuendelezwa kwa mahusiano yanayopendelea mkoloni hata baada ya uhuru.

Kwa upande wa pili, mwandishi anaeleza kuwa, wakati ambapo Wariinga anajikubali, urembo wake unabainika dhahiri. Anaeleza kuwa urembo wake uliwafanya wanaume “kuvunjika shingo”. Isitoshe, tukirejelea maelezo ya Wariinga baada ya kujitambua

katika sehemu za mwisho mwisho wa riwaya, tunapata maelezo ya mtu anayejithamini na aliyejikubali alivyo. Mwandishi analeza ifuatavyo

**MC:** Wariinga uyu ni atigire kumuundagia njuiri yaake na icanuri cia thigiingi nduunihie ni mwaki… Matuku maya nguo ciake ciothe iraamwagirira. Matuku maya Wariinga atumithagia, kana akagura nguo, kuriingana na mwiri wake. Mwiri wake riu niguo ukoragwo ukimwatha mwikire no ti miiri ya andu angi…Maitho make mairu makeengeete giutheri kia muundu uumiririe ngoro…Wariinga thaka nyakairu. (Ukurasa wa 220-221)

Maelezo haya ni kwamba Wariinga sasa hana haja kuiga Uzungu, amejikubali alivyo. Mavazi yake anayachagua kuambatana na mwili wake bali sio kuambatana na watu wengine. Haya yote yanaashiria kujithamini na kujitambua. Tukimtumia Wariinga kama kiwakilishi cha jamii iliyotawaliwa, basi maelezo haya yanatuelekeza kwa jamii inayojithamini jinsi ilivyo. Haina haja ya kuiga jamii nyingine. Mwandishi anarejelea ngozi nyeusi ya Wariinga kwa kutumia neno *Nyakairu* ambalo linaibua hisia chanya. Kukweza ngozi nyeusi ni tukio la kukweza utambulisho wa Mwafrika.

Kwingineko tukiangazia suala hili la utambulisho hasa kwa kuzingatia rangi ya ngozi na sura, tunapata kwamba mwandishi anapendelea uasilia wa Kiafrika dhidi ya ugeni wa kikoloni. Kwa mfano tukiangazia maelezo hapo juu kuhusu Wariinga na kuyalinganisha na maelezo kuhusu hakimu aliyesikiliza kesi ya Wangari:

**Mfano 45**

**MC:** *Njaanji oima Muthuungu wina gikoonde gituune ta Nguruwe. Iniuru riake riigucunukaga nguuci ta mwiri wa njagathi* (Ukurasa wa 38)

**MT1:** Hakimu alikuwa Mzungu aliyekuwa na ngozi nyeupe kama ya nguruwe. Pua lake refu lilikuwa limebambuka na magamba yalitokeza kama ya mjusi

Ni dhahiri kutokana na maelezo haya kuwa ngozi ya Mzungu haina tena utukufu ambao mkoloni alilenga kujenga. Rangi yake ya ngozi inalinganishwa na nguruwe ambaye ni mnyama aliye na sifa hasi katika utamaduni chanzi. Kwa kufanya hivi, mwandishi anatweza utukufu wa rangi hii ya ngozi. Maelezo anayotoa kuhusu pua ya hakimu huyu; kwamba ilikuwa imebambuka magamba kama mjusi, yanatoa taswira isiyo ya kupendeza.

Ukinzani huu hasa wa rangi ya ngozi; nyeupe dhidi ya nyeusi, unazidi kudhihirika tunaporejelea mfano ufuatao unaoeleza picha zilizokuwa imetundikwa kanisani:

**Mfano 46:**

**MC:** *Thiingi Maria na njiicu na Araika a Ngai maari eeru ta athuungu, no Caitaani na araika aake maari airu ci.* (Ukurasa wa 137-138)

**MT1:** Mtakatifu Maria, Yesu, na malaika wa Mungu walikuwa weupe kama wazungu; lakini shetani na wafuasi wakewalikuwa weusi kama makaa. (Ukurasa wa 146)

**MT2:** *The Virgin Mary, Jesus and God's angels were white, like Europeans; but the Devil and his angels were black.* (Ukurasa wa 140)

Suala la rangi ya ngozi ni la kimsingi katika utambulisho wa mtu au hata jamii. Tangu enzi ya ukoloni na maajilio ya dini ya Kikristo, taswira nyingi za wema; ikiwemo Mungu, malaika na mbinguni, aghalabu huwasilishwa kuwa zenye weupe wa namna fulani. Kinyume chake ni kuwa uovu, shetani na jehanamu huwasilishwa kuwa zenye weusi wa giza. Hali hii ndiyo mwandishi anaiangazia hapa ambapo anadadisi uwakilishi huu. Tukirejelea maelezo ya Fanon (1967) katika *Black Skin, White Masks*:

> Je, si weupe ni ishara ambayo daima katika Kifaransa inahusishwa na Haki, Ukweli, Ubikira? Nilijuwa mtu mmoja wa Anttillea ambaye alimwambia mwenzake, "Mwili wake ni mweusi, lugha yake ni nyeusi, roho yake sharti

iwe nyeusi pia." Mantiki hii inatumika katika Maisha ya kila siku na Mzungu. Mtu mweusi ni ishara ya Uovu na Sura ya kutisha. (Ty)

Nukuu hii inaelekea kushadidia suala la uwakilishi wa wema dhidi ya uovu ambao unawasilishwa katika riwaya kwa kuuhusisha na weupe dhidi ya weusi. Kwingineko Fanon (1967) anaeleza kuwa weusi ulihusishwa na dhambi, giza na uovu/ukosefu wa uadilifu. Hali hii ya ukinzani baina ya weupe na weusi, Mzungu na Mwafrika ndiyo iliyoshikiliwa na kuhimizwa na ubepari wa kikoloni. Utwezaji na kudharau utambulisho wa Mwafrika; rangi ya ngozi, mila, desturi na hata lugha yake ulikuwa wa kimakusudi huku utambulisho wa Mzungu; rangi yake ya ngozi, lugha yake, desturi na mila zikikwezwa kuwa bora. Mwandishi katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na tafsiri zake MT1 na MT2 anapinga ubabe huu wa utambulisho wa Mzungu. Hili linadhihirika tunapoangazia maelezo ya Mzungu dhidi ya Mwafrika kama ilivyobainishwa katika mfano 45 na katika maelezo yaliyotolewa katika ufuatao:

**Mfano 47**

**MC:** Thiingi maria na njiicu na Araika a Ngai maari eeru ta athuungu, no Caitaani Na araika aake maari airu ci. Utuku ni aarootaga mahahuratoro ni undu wa mbica icio. No haandu ha kuroota na Njiicu akiambwo, *aarootaga na Caitaani ari na gikoonde kieru cua ta gi kimuthuungu kimwe kinoru muno Wariinga oonire rimwe hakuhi na Rift Valley Spoerts Club*, akimabwo mutharab-ini ni andu atarukaangire – ta aria oonaga Bondeni ... (Ukurasa wa 137-138)

**MT1:** Mtakatifu Maria, Yesu, na malaika wa Mungu walikuwa weupe kamawazungu; lakini shetani na wafuasi wakewalikuwa weusi kama makaa. Usiku alikuwa akishikwa na jinamizi kwa sababu ya mapicha hayo. Lakini badala ya kuota Yesu msalabani, *alikuwa akimwota shetani mwenye ngozi nyeupe kabisa kama ya Mzungu mmoja, jitu la miraba minne, aliyekuwa amemwona karibuna Rift Valley Sports Club*, akisulubiwa na watu waliovaa

matambara – kama wa watu aliowaona katika majengo ya Bondeni… (Ukurasa wa wa 146 -147)

**MT2:** The Virgin Mary, Jesus and God's angels were white, like Europeans; but the Devil and his angels were black. At night Wariinga would have a recurrent nightmare. Instead of Jesus on the Cross*, she would see the Devil, with skin as white as that of a very fat European she once saw near the Rift Valley Sports Club*, being crucified by people in tattered clothes – like the ones she used to see in Bondeni … (Ukurasa wa 140)

Maelezo yanayotolewa katika mfano huu kuhusu ndoto ya Wariinga, yakifuata maelezo yaliyotolewa kuhusu picha za Maria Mtakatifu, Yesu, malaika na Mungu wakiwa weupe huku shetani na wafuasi wake wakiwa weusi, yanalenga kugeuza mtazamo wa kibepari kuhusu utambulisho wa watu weusi.

Katika jinamizi yake, Wariinga anaeleza kwamba alikuwa akimwota shetani akiwa;

*mwenye ngozi nyeupe kabisa kama ya Mzungu mmoja, jitu la miraba minne, aliyekuwa amemwona karibuna Rift Valley Sports Club*.

Katika kufanya hivi, mwandishi kimakusudi anakinza hali iliyobainishwa na mfumo wa kibepari kuwa weusi ndio ishara ya uovu. Anachora taswira ya shetani akifanana na Mzungu. Taswira hii ni muhimu hasa tukizingatia kwamba ndoto hii, utundikwaji wa shetani msalabani ndio anwani ya riwaya hii na hivyo ni tukio la kimsingi katika ukamilifu wa ujumbe katika riwaya hii.

Ugeuzaji wa uwakilishi wa wema na uovu kwa kutumia rangi ya ngozi ni tukio la kimakusudi ambalo tunaweza kueleza linalenga kubadili kasumba kuhusu utambulisho wa Mwafrika, mwenye ngozi nyeusi. MT1 na MT2 zinawasilisha maelezo haya kwa njia linganifu kisemantiki na kiumbuji kuashiria udhati wa

ujumbe uliomo katika kifungu hiki. Tukio hili linaafikiana na maelezo ya wanabaadaukoloni kwamba fasihi kando na kuwasilisha uhalisia katika jamii pia hutumiwa kama nyenzo ya "kujikomboa" kwa kwenda kinyume na mawazo ya kibepari.

Athari nyingine ya ukoloni kwa utambulisho wa jamii zilizowahi kutawaliwa ni suala la majina ya kuwaitia watu. Utawala wa kikoloni na maajilio ya dini ya Kikristo ni matukio mawili ambayo yanafungamana. Dini hii ya Kikristo ilizalisha uhalisia mpya kwa utambulisho wa jamii zilizotawaliwa hasa mfumo wa majina. Mwandishi katika MC anagusia suala hili la majina kama kigezo cha utambulisho na tafsiri zinaliangazia kwa ulinganifu katika MT1 na katika MT2 ambapo suala hili limejitokeza bayana ifuatavyo:

**Mfano 48**

**MC:** ...akamuuria riitwa riake *ria guciarwo* na *ria kiingenu*… (Ukurasa wa 13)
**MT1:** …anapomwuliza jina lake la *ubatizo* na la *ukoo*… (Ukurasa wa 16)
**MT2:** …he asks her what her names are, *the one she was given at birth* and *her acquired English one*… (Ukurasa wa 13)

(Msisitizo wangu)

Tukiiweka nukuu hii katika muktadha wake, hali kitamaduni, hasa sehemu zilizoandikwa kwa herufi za mlazo, suala la umuhimu wa jina kama sehemu ya utambulisho linabainika dhahiri. Kwa mfano, katika jamii ya Gikuyu, utambulisho wa familia hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa mfumo wa utoaji majina. Mvulana wa kwanza anapewa jina la baba ya baba. Mvulana wa pili anapewa jina la baba ya mama. Msichana wa kwanza anapewa jina la mama ya baba

huku msichana wa pili akipewa jina la mama ya mama. Watoto wanaozaliwa baada ya hapa wanapewa majina ya ndugu za wazazi; wa kiume na wa kike, kuanzia yule mzee hadi mchanga, mmoja kwa upande wa baba na anayefuata kwa upande wa mama. Kwa mfano, mwendesha utafiti huu ni mwana wa pili wa kiume katika familia yake. Hivyo basi amepewa jina la baba ya mama yake.

Mtindo huu wa utoaji majina kando na kubeba utambulisho wa familia, aidha hutumiwa kuingiza wageni katika familia. Kwa mfano wageni waliotekwa nyara kutoka jamii jirani na kufanywa kuwa sehemu ya jamii ya Gikuyu, wakimbizi na hata wake walioolewa kutoka jamii tofauti. Jina katika muktadha wa jamii ya Gikuyu, hivyo basi, sio tu neno la kumwitia mtu bali linatekeleza dhima muhimu katika kumtambulisha. Aidha, mfumo wa utoaji majina unaaminika kuwaunganisha watu wa vizazi mbalimbali, waliopo na hata walioaga dunia katika mzunguko wa ukamilifu wa maisha. Inaaminika pia kwamba, mtoto anapopewa jina, hasa la mtu aliyeaga dunia, roho ya mfu huyo hupata uhai mpya katika maisha ya mtoto anayepewa jina lake. Hivyo basi jina sio utambulisho wa mtu pekee bali ni kiungo muhimu katika mfumo wa utambulisho wa familia, ukoo, rika na hata jamii nzima. Mfumo huu ni kama anavyoeleza Katama Mkangi katika tamthilia yake *Ningekuwa na Uwezo.*

> Kwetu sisi Waafrika,
> Jina si jina tu!..
> Jina ni uzi…wa kutungia ushanga
> Wa ukoo;
> Kutoka jadi
> Mpaka leo… (2009: 7-8)

Katika mfano 48, sehemu ya nukuu iliyoandikwa kwa herufi za mlazo ni ya kimsingi katika kuelewa ukinzani wa utambulisho unaodhihirika katika muktadha wa baadaukoloni.

> MC…*ria guciarwo* na *ria kiingenu*
> MT1…*la ubatizo* na la *ukoo*
> MT2…*the one she was given at birth* and *her acquired English one*

Majina yanawekwa katika kategoria mbili: jina la kiasili na lile la kigeni. Katika MC, mwandishi ametumia dhana ya *ritwa ria guciarwo*. Tafsiri yake sisisi ni *jina la kuzaliwa.* Hii ni dhana ya kimsingi katika utamaduni chanzi ambapo jina lina umuhimu katika utambulisho wa mtu. Linamfanya kuwa sehemu ya familia na jamii. “Linamzaa” katika mfumo maalum wa kitamaduni. Jina la pili ni la *kiingenu*. Huu ni msimu unaotumiwa kurejelea dhana ya kigeni hasa ya kuhusishwa na Uzungu. Tafsiri ya MT2 inaakisi mtazamo wa mtafsiri aliye pia mwandishi kwa jina hili la kigeni; *her acquired English one.* Swali linaloweza kuibuliwa hapa linahusu uamilifu wa kupata jina la Kizungu. Iwapo jina la kiasili “linamzaa” mtu katika mfumo wa jamii yake, je la Kizungu “linamzaa” katika mfumo upi?

Katika MT1, mtafsiri anahusisha jina hili la kigeni na ubatizo. Dhana hii ya ubatizo inahusishwa na dini ya Kikristo ambayo katika mfumo wa jamii chanzi, ni imani ya kigeni. Hata hivyo, suala la jina “kumzaa” mtu linajitokeza pia hapa kwa sababu tukiangazia Biblia Takatifu, ubatizo unamithilishwa na kuzaliwa upya (Tazama Yohana 3:1-5). Kuzaliwa upya kutokana na kupewa jina, au matambiko yanayoambatana na kupewa jina husika, ni suala la kimsingi tunapojadili suala la utambulisho katika muktadha wa baadaukoloni.

Jamii zilizowahi kutawaliwa zinajipata katika hali ambapo mfumo wake wa kitamaduni, ambao ulikuwa na namna ya kipekee ya kumpa wanajamii utambulisho, umevurugwa na athari za kigeni. Hali hii inaathiri utambulisho wa wanajamii asilia. Tafsiri zilizotolewa katika MT1 na MT2, japo hazikutumia mkakati sawa, MT1 imetumia mkakati unaoangazia uamilifu, huku MT2 ikitumia mkakati unaolenga tafsiri sisisi, zinafanikiwa kuwasilisha suala hili la jina na utambulisho kama lilivyokusudiwa katika MC.

**4.5 Hitimisho**

Sura hii ya tasnifu imechunguza vipengele vya itikadi na utambulisho katika MC na katika MT1 na MT2. Hii ni kuambatana na lengo la pili na la tatu la utafiti huu. Dhana hizi zimeshughulikiwa katika sura moja kutokana na kuingiliana kwa vipengele hivi katika matini teule. Baada ya kutanguliza dhana ya itikadi, sura imetumia mifano mahususi kuichunguza kwa kujikita kwa uteuzi wa kiisimu uliofanywa na mwandishi na mtafsiri. Mwandishi amerejelea matini nyingine, hasa za kidini, na kutumia malighafi ya kiumbuji katika kuwasilisha ujumbe wake. Kipengele cha utambulisho kimebainishwa kuwa cha kimsingi katika MC kutokana na matumizi ya dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi. Aidha, ukinzani baina ya utambulisho wa kibepari na utambulisho wa mtawaliwa umedhihirika, suala ambalo linabainisha kwamba, tukio hili ni mgogoro wa kimsingi katika fasihi na tafsiri za baadaukoloni. Matokeo ya uchanganuzi uliofanywa katika sura hii yameelezwa katika sura inayofuata.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ya tasnifu ni hitimisho kwa utafiti uliofanywa. Hivyo basi, inatoa muhtasari wa tasnifu nzima na kueleza matokeo ya uchanganuzi uliofanywa katika utafiti huu. Matokeo haya yamewasilishwa kuambatana na malengo yaliyoongoza utafiti huu. Aidha, sura hii imetoa mahitimisho ya mtafiti kuhusu mada iliyoangaziwa kisha ikatoa mapendekezo ya utafiti huu ikijikita kwa matokeo yaliyobainishwa, tafiti za baadaye pamoja na nadharia.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu katika sura ya kwanza ulijadii usuli kwa kuangazia hali halisi ya taaluma ya tafsiri ulimwenguni, barani Afrika na nchini Kenya. Katika sehemu hii, utafiti ulijikita kwa upeo wa taaluma ya tafsiri kinadharia na kiutekelezaji. Suala la mageuzi ya kinadharia na kimwelekeo katika taaluma ya tafsiri limeangaziwa na kubainishwa kuwa la kimsingi katika upanuzi wa taaluma ya tafsiri na kuwezesha tafiti mbalimbali katika uwanja huu ikiwemo utafiti ulioendeshwa katika tasnifu hii. Usuli aidha umeangazia suala la tafsiri binafsi na kutalii uamilifu wake katika muktadha wa baadaukoloni kama njia ya kuweka msingi kwa utafiti huu. Ni katika sura hii pia ambapo suala la utafiti malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu yameelezwa. Isitoshe, sura hii imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada hasa kwa kujikita kwa hali ya tafsiri kwa Kiswahili kiupeo na kimwelekeo ambapo

ilibainishwa kwamba utafiti wa aina hii haukuwa umeshughulikiwa hasa katika kiwango cha mwelekeo uliotumika. Sura ya kwanza ilikamilika kwa kujadili misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu kwa kujikita kwa nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri pamoja na nadharia ya uchanganuzi wa diskosi, na kueleza mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

Sura ya pili imejadili dhana za kimsingi katika utafiti huu; utamaduni, itikadi na utambulisho na kuibuka na ufafanuzi ambao ndio msingi wa uchanganuzi katika sura ya nne na ya tano. Dhana hizi zimejadiliwa kwa kuzihusisha na kipengele cha matumizi ya lugha, hasa uteuzi wa kiisimu. Katika sura hii pia, dhana hizi za utamaduni, itikadi na utambulisho aidha zimejadiliwa kwa kuzihusisha na mwandishi na mtafsiri wa riwaya zilizoshughulikiwa katika utafiti huu. MC, MT1 na MT2 zimetolewa muhtasari kabla ya kuchanganua data kutokana na matini hizi katika sura ya tatu na ya nne.

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu umetekelezwa katika sura ya tatu na sura ya nne. Katika sura ya tatu, utafiti ulichanganua vipengele vya utamaduni vilivyotumika katika MC na jinsi vilivyohawilishwa katika MT1 na MT2 katika msingi wa baadaukoloni. Uchanganuzi huu ulilenga kushughulikia lengo la kwanza la utafiti huu na kwa wakati huo huo lengo la nne. Vipengele vinavyofungamana na utamaduni chanzi na fasihi simulizi ya utamaduni chanzi vinafafanuliwa kwa undani ili kuweka bayana nafasi yake na athari zake katika MC, MT1 na MT2. Katika sura ya nne, utafiti unajikita kwa uchanganuzi wa vipengele vya itikadi na utambulisho.

Vipengele hivi vimeshughulikiwa katikasura moja kutokana na mwingiliano uliopo baina ya dhana hizi kama ilivyojadiliwa katika tasnifu hii. Uchanganuzi katika sura hii umejikita kwa lengo la pili na lengo la tatu la utafiti huu na kwa wakati huo huo kuangazia lengo la nne ambalo limefungamana na uchanganuzi ulioendeshwa.

### 5.2 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii ya tasnifu inatoa maelezo kamili kuhusu matokeo ya utafiti huu. Hii ni kutokana na uchanganuzi ulioendeshwa katika sura ya tatu na sura ya nne katika tasnifu hii. Matokeo haya yameelezwa kwa kujikita kwa vigeu vilivyoangaziwa katika utafiti huu na kuwasilishwa kuambatana na malengo mahususi ya utafiti huu ifuatavyo:

#### 5.2.1 Utamaduni katika MC, MT1 na MT2

Lengo la kwanza la utafiti huu lilihusu uchanganuzi wa jinsi dhana ya utamaduni inavyodhihirika katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*, na katika tafsiri zake; *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross*. Katika kushughulikia lengo hili la utafiti huu, mifano mbalimbali ya vipengele vya utamaduni vilibainishwa na kujadiliwa katika sura ya tatu ya tasnifu hii. Utamaduni ulichunguzwa kwa kujikita kwa vipengele viwili vikuu: fasihi simulizi-vipera vyake, na maneno maalum yanayofungamana na utamaduni chanzi. Kipengele cha fasihi simulizi kilibainishwa kuwa cha kimsingi katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini.* Utafiti ulibainisha kuwa mwandishi, katika kuandika MC, alitumia mtindo maalum wa ufunguzi wa utambaji hadithi. Mtindo huu unajitokeza katika sehemu ya utangulizi wa MC.

Uamuzi huu tumeubainisha kuwa wa kimakusudi. Unaipa riwaya hii ufasili wa simulizi moja kuu. Mtindo huu aidha ukiwekwa katika muktadha wa baadaukoloni unaafiki madai kuwa uandishi wa Kiafrika aghalabu huhusisha tafsiri ya kisemiotiki ambayo inajumuisha uhawilishaji wa masimulizi kutoka mbinu ya usemi hadi maandishi. Hali sawa na hii katika MC inadhihirika kupitia kwa mtindo uliotumika katika uwasilishaji wa fumbo lililoangaziwa katika mfano 2. Mbinu ya uwasilishaji aliyotumia mwandishi inatokana moja kwa moja na mtindo wa uwasilishaji wa vitendawili katika utamaduni chanzi. Hali hii, kando na kuipamba riwaya na kuikolezea ladha kiumbuji, imechangia kuakisi uhalisia wa kitamaduni ambao awali uliwasilishwa kimasimulizi kama sehemu ya fasihi simulizi ya jamii ya Gikuyu. Hapa, mtindo unapata kuandikwa na umetumiwa kuakisi dhana ya kimsingi sana katika riwaya hii; changamoto wanazopitia wafanyakazi, wajenga nchi.

Katika kutafsiri mitindo hii ya ufunguzi kwenye MT1, mtafsiri alipendelea kutumia tafsiri sisisi. Mbinu hii ya tafsiri inaibua ugeni ambao unazalisha udhihirikaji wa tafsiri. Yaani, matini tafsiri inaonekana wazi kwamba ni matini ya kigeni isiyo na uasilia katika mfumo wa lugha na utamaduni pokezi. Kutokana na haya, utafiti ulibainisha kwamba, licha ya kuwa nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri iliangazia ugeni kama dhana inayodhihirika katika fasihi inayohusisha lugha ya kikoloni, ugeni aidha unaweza kubainika katika ngazi ya lugha ya kiasili na ya kitaifa au kieneo kama ilivyo Kiswahili. Hali hii inatufanya kusaili uwezekano kwamba uibuaji wa ugeni katika tafsiri kwenye mazingira ya baadaukoloni ni dhana isiyoepukika bila

kujali lugha iliyotumika. Tunaweza kuhusisha uhalisia huu na dhana ya uzalendo wa kijamii ambao unapiku uzalendo wa kitaifa. Mwandishi au mtafsiri katika muktadha wa baadaukoloni ni mtumwa wa lugha chanzi, matini chanzi na utamaduni chanzi.

Kwenye MT2, inabainika kuwa mtafsiri aliandama mkondo sawa na ilivyo kwa tafsiri katika MT1. Mitindo ya ufunguzi ilitafsiriwa sisisi kama ilivyojadiliwa katika mfano 2. Uamuzi huu, kando na kuibu ugeni, unafanikiwa kuvusha utamaduni wa lugha chanzi kwenda mfumo wa Kiingereza. Kwa jinsi hii mtafsiri kimakusudi anawasilisha dhana za kigeni bila kutafuta visawe katika mfumo wa lugha na utamaduni pokezi. Tukio hili tumehitimisha linaukweza utamaduni chanzi na kuupa hadhi unapoangaziwa kando na utamaduni wa Kiingereza.

Kipengele kingine cha fasihi simulizi kilichoangaziwa katika kuchunguza utamaduni kilikuwa ni methali. Uchanganuzi ulibainisha methali zinazofungamana na utamaduni chanzi wa MC na jinsi zilivyotumiwa kupamba na kukamilisha riwaya hii. Matumizi ya methali katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* yamedhihirisha kuwa fasihi ya Kiafrika husheheni diskosi za kimzunguko ambapo mambo husemwa kwa njia ya mafumbo na kimzunguko. Kutosema mambo kwa njia ya moja kwa moja ni sifa ya ulumbi inayothaminiwa na ni kiashiria cha busara ya mnenaji. Isitoshe, methali hizi zimetumiwa kuwasilisha maana za ndani kama ilivyojadiliwa katika mfano 3 hadi mfano 7. Dhana muhimu kama vile mkengeuko zimewasilishwa kupitia kwa methali kama ilivyojadiliwa katika mfano 7.

Tafsiri ya methali hizi katika MT1 na katika MT2 zimetumia mbinu mseto. Katika MT1, mtafsiri ametumia tafsiri ya kimawasiliano ambayo inampa uhuru wa kutafuta maneno mbadala yanayowasilisha ujumbe na kuibua athari sawa kwa hadhira lengwa. Mbinu hii inabainika katika mfano 4, 5 na 7. Katika mifano hii, mtafsiri ametumia methali mbadala katika mfumo wa lugha na utamaduni wa Kiswahili kuwakilisha methali zilizotumiwa katika MC. Kwingineko, kama ilivyo katika mfano 6, mtafsiri alitumia maelezo yanayoweka bayana ujumbe fiche uliokuwepo katika methali kwenye MC. Mbinu hizi zinaafiki mbinu ya ubinafsishaji ambapo mtafsiri anaipa MT uasilia katika mfumo wa lugha na utamaduni pokezi. Uamuzi huu ni kinyume na mbinu zilizotumiwa kushughulikia mitindo ya ufunguzi.

Ukosefu wa usawa kimkakati unaashiria mambo mawili. Kwanza, huenda mtafsiri katika MT1 hakuwa na msukumo wa kimakusudi wa kuibua ugeni. Pili ni kwamba, huenda kutokana na ukuruba wa kiisimu na kitamaduni baina ya Kikuyu na Kiswahili, ilikuwa rahisi kwa mtafsiri kupata visawe vya kimawasiliano na kiuamilifu. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa mbinu ya ubinafsishaji haikufanikiwa kikamilifu katika kuhawilisha dhana kutoka MC hadi MT1 kama ilivyobainishwa katika mfano 7.

Tukiangazia MT2, methali zote zilizoangaziwa zimetafsiriwa kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi. Ugeni unaoibuliwa unafanikiwa katika kuikosesha MT2 uasilia katika mfumo wa Kiingereza. Hivyo basi, msomaji wa MT2 hana budi kusaili sababu za ugeni huu na kutaka kujua asili yake. Hali hizi ndizo msingi wa tafsiri za

baadaukoloni ambapo ubabe wa lugha na utamaduni wa kibepari unakinzwa huku utamaduni na lugha asilia za mtawaliwa ukikwezwa.

Uteuzi wa maneno yanayofungamana na utamaduni katika uandishi wa MC ulibainishwa kuwa wa kimakusudi na kimkakati. Kwa mfano, dhana *Ngaati* katika sehemu ya utangulizi imetumiwa kubainisha tangu mwanzo kuwa kuna mgawanyiko katika jamii zilizotawaliwa; walioshirikiana na watawala na waliopinga watawala. Hali hii ya ukinzani ni muhimu katika muktadha wa baadaukoloni na husaidia katika kusaili mahusiano ya kiuwezo na athari zake kwa jamii husika. Neno *Gicaandi* limebainishwa kuwa muhimu kimtindo. Limeangaziwa katika ngazi mbili; ala na kipera cha fasihi simulizi katika jamii ya Gikuyu. Matumizi ya neno hili yamejadiliwa kama jazanda kuu katika MC kama ilivyobainishwa katika mfano 9.

Matumizi ya maneno yanayofungamana na utamaduni mahususi yanaipa MC uasilia. Aidha, matumizi haya yanaashiria ukwasi wa kitamaduni wa lugha chanzi na utamaduni chanzi. Matumizi ya dhana hizi kiumbuji ni dhihirisho la kwamba lugha na utamaduni wa mtawaliwa una uwezo wa kubuni na kuwasilisha fasihi pevu sawia na lugha za kikoloni.

Tafsiri ya maneno yanayofungamana na utamaduni katika MT1 imeandama mtindo uliobainishwa wa mbinu mseto ya kuchanganya uibuaji ugeni na ubinafsishaji kupitia kwa tafsiri za kimawasiliano. Kwa mfano, dhana *Gicaandi* inadumishwa katika MT1 lakini neno *Kamoongonye* linatafsiriwa kuwa *Mchumbakijana.* Hali hii ya kuchanganya mbinu na mikakati inaleta ugumu wa kueleza tafsiri iliyotekelezwa

katika MT1 kikamilifu. Inaelekea kwamba MT1 haikulenga kuibua ugeni wala kujenga ubinafsishaji.

Kinyume na hivyo, tafsiri katika MT2 imetumia mbinu ya tafsiri sisisi na ukopaji wa dhana. Katika ukopaji, maneno yanayofungamana na utamaduni chanzi yaliwasilishwa jinsi yalivyo. Kutokana na mbinu hii, ugeni unaibuliwa na kuashiria kuwa MT2 sio matini asilia katika utamaduni wa Kiingereza. Hata hivyo, dhana zinapokopwa, mtafsiri amechanganya mbinu za kuzihawilisha. Kwa mfano, neno *Gicaandi* limetumika katika MT2 bila kufafanuliwa. Hata hivyo, neno *Kamoongonye* linapotokea katika MT2 kwa mara ya kwanza linatolewa maelezo katika tanbihi iliyo kwenye ukurasa wa 14 wa *Devil on the Cross.* Licha ya maelezo yanayotolewa, kimsingi dhana hizi zinaisawiri MT2 kama matini yenye msingi wa kitamaduni katika mfumo tofauti na lugha iliyotumika.

Vipengele vingine vya utamaduni vilivyoshughulikiwa kama vile misemo katika MC ilichangia kukita mizizi ya MC katika mfumo wa lugha na utamaduni wa Gikuyu. Hali sawa inabainika tunapoangazia nyimbo na hata misimu. Tafsiri zake katika MT1 na MT2 zimefuata mbinu na mikakati sawa na ilivyojadiliwa awali katika sehemu hii.

### 5.2.2 Itikadi katika MC, MT1 na MT2

Kipengele cha itikadi kilikuwa mojawapo ya dhana za kimsingi zilizochanganuliwa katika utafiti huu. Lengo la pili la utafiti huu liliangazia uchunguzi wa dhana ya itikadi inavyodhihirika kupitia kwa lugha katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini*

na jinsi inavyowakilishwa katika tafsiri za *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross.*

Utafiti ulibainisha kwamba, kutokana na sehemu hii mwandishi aliweka msingi wa kiitikadi kuhusu lugha. Kwa mfano, kwa mwandishi, kutelekeza lugha za kiasili na badala yake kutukuza lugha za kigeni ni sawa na kumtukana Mungu. Ilibainika kwamba, kupitia kwa uteuzi uliofanywa, mwandishi ameweka msingi wa mtazamo wake kuhusu lugha iliyotumika pamoja na kubainisha muktadha wa kijamii na wa kitamaduni wa MC na wa MT1. Ni dhahiri kwamba mwandishi anashabikia matumizi ya lugha za kiasili; za kijamii na kitaifa. Utafiti unahoji kwamba upekee huu katika kurejelea lugha ya Kikuyu na lugha ya Kiswahili katika sehemu ya utangulizi, kama zilivyotumika katika MC na katika MT1 mtawalia, ndio sababu mojawapo ya kutotafsiriwa kwa sehemu ya utangulizi kwa Kiingereza katika MT2.

Utangulizi aidha umeweka wazi vichocheo vya dhamira iliyotawala MC. Hii ni riwaya ambayo njia mahususi imeendeleza imani na msingi wa utunzi wa mwandishi. Masimulizi ya matukio halisi kihistoria wakati wa utunzi ni suala la kimsingi katika kuelewa hali ya kisaikolojia na hata mazingira halisi ya utunzi wa MC. Kwa kujikita kwa uchanganuzi ulioendeshwa, utafiti ulifanikiwa kuzichunguza hali hizi na mwelekeo wa kinadharia ulio na itikadi ya Kimaksi inayojitokeza katika riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* na kuihawilisha katika tafsiri za *Shetani Mslabani* na *Devil on the Cross.*

Kwa kujikita kwa msingi wa baadaukoloni, utafiti pia uliweza kuchanganua kiulinganishi utamaduni na ustaarabu wa kiasili dhidi ya ule wa kigeni (kikoloni).

Ilidhihirika kwamba mwandishi kwa njia ya kimakusudi anakata shauri kwenda kinyume na hali iliyowekwa tayari ya kutukuza ubepari; lugha, utamaduni na hata fasihi, ya kikoloni na badala yake anafanya juhudi za kimakusudi kuukweza utamaduni, ustaarabu na lugha za kiasili katika fasihi yake. Hatua hii ya kimakusudi tumehitimisha kwamba ni zao la imani ya kiitikadi. Msingi wake upo katika imani kwamba mkoloni, lugha yake, utamaduni wake na ustaarabu wake sio babe ukilinganishwa na lugha, utamaduni na ustaarabu wa kiasili. Kwamba lugha ya kiasili kama vile Kikuyu, inaweza kutumiwa kuandikia riwaya ya kisasa yenye uwezo wa kushughulikia masuala ya dhati kama vile *Caitaani Mutharaba-ini*, sawia na ilivyo katika lugha za kikoloni.

Hata hivyo, kutotafsiriwa kwa sehemu ya utangulizi katika MT2 ambayo inaweka msingi kwa riwaya nzima kumebainishwa kuwa na athari hasi kwa ukamilifu wa ujumbe na uelewekaji wa uteuzi uliofanywa katika riwaya yenyewe. Katika kuchunguza kipengele cha utambulisho, imebainika kwamba mwandishi wa MC alikuwa makini kudumisha utambulisho wa mfumo wa utamaduni chanzi. Anatumia dhana nyingi zinazofungamana na utamaduni huo katika uandishi wake jambo linaloipa riwaya hii ladha asilia.

Ilibainika kwamba mwandishi alizamia suala la ukoloni mamboleo katika kazi hii. Katika kufanya hivi, ameangazia suala la athari hasi za mahusiano baina ya serikali na uongozi wa jamii zilizotawaliwa na mkoloni, na mataifa yenye uwezo na ushawishi mkubwa duniani. Kwa kutumia viwakilishi vya pesa za mataifa haya,

mwandishi anafanikiwa kuyahusisha mataifa haya na wizi na dhuluma katika nchi zilizotawaliwa na mkoloni. Utafiti ulibainisha kwamba, viwakilishi vya unyonyaji huu ni vya kimakusudi na vimepiga darubini suala la uhusiano wa kiuwezo; kijamii, kiuchumi na hata kisiasa baina ya waliokuwa wametawaliwa, mabwanyenye walio viongozi katika mataifa haya, watu wanaowatumikia mabwanyenye na kuwezesha utekelezaji wa sera zao, pamoja na uhusiano na mataifa yenye uwezo na ushawishi ulimwenguni. Uhusiano huu unamwezesha mwandishi kukuza itikadi za kimaksi; kisosholisti na kijamaa, dhidi ya itikadi ya kibepari katika riwaya hii. Katika tafsiri za MT1 na MT2, dhana za kiitikadi zimebainishwa kwamba pakubwa zilihawilishwa kwa njia ya moja kwa moja ila katika MT2, lugha ilitumiwa makusudi kupunguza makali. Utafiti huu ulihusisha hali hii ya kupunguza makali na suala la kuwepo na ukubalifu wa riwaya ya *Devil on the Cross* miongoni mwa hadhira yake ya kimataifa.

Mtafsiri anajihusisha katika zoezi la udhibiti wa kibinafsi[20] katika uteuzi wake wa lugha hasa katika MT2 na kwa kiasi kidogo katika MT1. Kwa kujikita kwa mazingira halisi ya kihistoria ya uzalishaji wa MC, tunapata kwamba iliandikwa na Ngũgĩ wa Thiong’o akiwa kizuizini, ambapo alikuwa ametiwa na serikali kutokana na kazi zake kama mwanafasihi. Akiwa kizuizini ndipo akaandaa mswada wa *Caitaani Mutharaba-ini*. Kutokana na ukweli huu, inakuwa si ajabu mambo yafuatayo yanadhihirika katika MC, MT1 na MT2 mtawalia:

---

[20] Udhibiti wa Kibinafsi ni dhana iliyotumika kama tafsiri ya dhana ya Kiingereza ya *Self Censorship.*

a. MC imesheheni matumizi mengi ya methali na mafumbo. Riwaya nzima ni jazanda moja kuu. Hali hii tunadadisi kwamba huenda kando na sababu za kiumbuji na kisanaa zinazotokana na mtindo huu, pia kuna uwezekano mkubwa kwamba mtindo huu ulitumiwa na mwandishi kimakusudi ili kujilinda dhidi ya utawala. Hivi kwamba, hata kama karatasi shashi alizotumia kuandaa mswada asilia zingepatikana, ingekuwa vigumu kumhukumu mwandishi kutokana na mafumbo na jazanda zilizotumiwa na zinazotoa ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Aidha, mafumbo yaliyotumiwa yanaweza kufasiliwa kwa njia tofauti na ni katika wingi wa fasili ambapo mwandishi anajilinda.

b. Licha ya MC kutumia lugha kali na ya matusi dhidi ya viwakilishi vya ubepari na udhalimu, MT1 na MT2 zimedhibiti ukali huu. Udhibiti unabainika kuwa wa dhati hasa katika MT2 ambapo sehemu kama ile ya utangulizi wa riwaya inadondoshwa kabisa licha ya uamilifu wake katika kuwekea riwaya hii msingi. Hali hii tunahoji huenda ni kutokana na haja ya mtafsiri kujilinda dhidi ya mitazamo hasi ya hadhira ya MT1 na MT2 jambo ambalo tunalihusisha na suala la mauzo ya kitabu hiki hasa MT2 na kwa jinsi hiyo anadhibiti lugha ili kulinda kipato.

c. Kwa mwandishi wa MC, hii ndiyo ilikuwa riwaya ya kwanza kuandika katika lugha ya Kikuyu. Katika riwaya hii, mwandishi anaangazia dhana za baadaukoloni waziwazi kwa kutumia lugha kali. Licha ya kuwa maandishi ya awali aliyozalisha katika Kiingereza yalifuata dhamira sawa, katika *Caitaani*

*Mutharaba-ini* Ngũgĩ wa Thiong'o anajitosa katika kushambulia ukoloni mamboleo na usaliti wa mabwanyenye na mabwanyenye uchwara unaotekelezwa kwa manufaa ya kibinafsi. MC inafuatiwa na maandishi mbalimbali yanayoendeleza mawazo haya kwa mfano: *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature* (1986) na *Detained: A Writer's Prison Diary* (1981).

Kwa ujumla, itikadi katika MC ya utafiti huu ilibainishwa kuwa dhana yenye umuhimu hasa katika uteuzi wa lugha na uwakilishi wa vipengele mbalimbali. Tafsiri za MT1 na MT2 zilijizatiti kudumisha vipengele vya kiitikadi ila mtafsiri wakati mwingine alikwepa baadhi ya dhana au hata kutumia lugha yenye kupunguza makali kwa ajili ya kujilinda na kuilinda kazi yake.

### 5.2.3 Utambulisho katika MC, MT1 na MT2

Lengo la tatu la utafiti huu lilijikita katika kutalii jinsi utambulisho umeumbwa katika MC na namna ambavyo mtafsiri wa *Shetani Msalabani* na *Devil on the Cross* alivyoushughulikia utambulisho huu.

Utafiti ulitambua ngazi za jamii, siasa na kabila kama vigezo vya kimsingi katika kubainisha utambulisho huku utambulisho wa kikabila ukibainishwa kama nyenzo ya kuibua msaada wa kisiasa na kijamii katika harakati za kufikia malengo ya jamii pana. Mifano ni, mahusiano sawa ya kiuwezo; kilugha, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi katika mazingira ya baadaukoloni.

Uchanganuzi wa dhana ya utambulisho katika MC ulibainisha kwamba, riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* imetungwa kwa njia ambayo inajikita katika utamaduni maalum wa jamii ya Gikuyu. Katika kufanya hivi, mwandishi amesawiri uasilia wa utambulisho kijamii na kikabila na kwa wakati huo huo akaakisi uhalisia wa utambulisho mahuluti katika mazingira ya baadaukoloni. Anafanya hivi kupitia kwa matumizi ya lugha za kigeni kama vile Kiingereza kama ilivyojitokeza katika mfano 41. Matumizi ya maneno ya kigeni katika MT1 na MT2 yamebainishwa kuwa zoezi la kimakusudi ambalo linazipa matini hizi msingi wa utamaduni wa lugha chanzi na hivyo kuibua utambulisho wa ugeni katika mifumo ya fasihi na ya lugha za Kiswahili na Kiingereza mtawalia.

Suala la utambulisho mahuluti katika mazingira ya baadaukoloni limeangaziwa katika MC kupitia kwa wahusika kama vile Gatuiria na Wariinga. Gatuiria ametumiwa kuwakilisha uhalisia wa kiisimu katika jamii zilizowahi kutawaliwa na mkoloni. Uchanganyaji na ubadilishaji msimbo ni suala la kawaida katika matumizi ya lugha ya jamii hizi kama inavyobainishwa katika mfano 42. Uhalisia huu ni mojawapo ya athari hasi kwa utambulisho wa jamii zilizotawaliwa.

Hata hivyo, ubainishwaji wa ubadilishaji msimbo katika MT1 umefuata mtindo wa ubinafsishaji ambapo lugha ya Kikuyu imebadilishwa na kuwa lugha ya Kiswahili. Huenda hali hii ni kutokana na ukweli kwamba jamii zinazosema Kiswahili pia zilipitia hali sawa kikoloni na jamii ya Gikuyu. Katika MT2, mtafsiri ametumia maelezo kuashiria suala hili la ubadilishaji msimbo ambao haubainiki wazi. Hii ni

kwa sababu katika MT2, maneno ya Gikuyu yamedondoshwa kama ilivyobainishwa katika mfano 42. Suala la utambulisho mahuluti kupitia kwa lugha halibainiki wazi katika tafsiri kama lilivyoangaziwa katika MC.

Mahusiano ya kiuwezo yamehusishwa na utambulisho ambapo dhana ya weupe na weusi zimetumika kama viwakilishi vya uzungu na wema kwa upande mmoja na Uafrika na uovu kwa upande wa pili mtawalia. Inabainika kuwa Mwafrika aliyetawaliwa akiwakilishwa na Wariinga katika MC, anajichukia na kutamani Uzungu. Utambulisho wa rangi ya ngozi umebainishwa kuwa dhana ya kimsingi katika ukombozi wa Mwafrika aliyewahi kutawaliwa. Mwandishi kupitia kwa mhusika huyu anafanikiwa kulinganisha mtazamo wa Mwafrika aliyetawaliwa (kisiasa, kiuchumi na kiakili) na Mwafrika aliyejikomboa kupitia kwa dhana ya weusi na weupe.

Kuiga Uzungu kwa kutamani weupe wa ngozi na kuchukia weusi ni hali ambayo inaashiria mtazamo duni kwa utambulisho unaohusishwa na ngozi nyeusi. Hata hivyo, kama ilivyo mojawapo ya azma za fasihi ya baadaukoloni, kuelekea mwishoni mwa MC mwandishi anaonyesha mabadiliko ya kukumbatia ngozi nyeusi na kujivunia utambulisho wake. Weupe unavuliwa "utukufu" ambao umekuwa ukihusishwa nao kupitia kwa maelezo ya rangi hii ya ngozi. Kwa mfano, ngozi nyeupe inalinganishwa na nguruwe, huku pua la hakimu aliyekuwa Mzungu likilinganishwa na mjusi anayebambuka magamba.

Ulinganisho huu katika mazingira ya utamaduni wa MC unatoa taswira hasi kutokana na jinsi nguruwe wanavyofasiliwa pamoja na mjusi. Taswira hasi vilevile inadumishwa katika MT1 kupitia kwa ulinganisho huu. Hata hivyo katika MT2, uhusisho wa rangi ya Mzungu na nguruwe na kubambuka kwa mjusi tunahoji kuwa huenda hakukutoa taswira hasi kama ilivyo kwa MC na MT1 hasa kutokana na tofauti za kitamaduni.

Suala jingine tulilohusisha na utambulisho lilikuwa jina. Mwandishi katika MC ameangazia suala la jina moja kwa moja na kimajazi kupitia kwa majina ya wahusika kama njia ya kubainisha utambulisho. Mwandishi katika kubainisha utambulisho kwa msingi wa jina, amejadili athari za dini inayohusishwa na ukoloni katika mfumo wa utoaji majina. Katika MC, anabainisha aina mbili za majina; kile anaita "ritwa ria guciarwo" (jina la kuzaliwa) na "ritwa ria kingenu" (jina la Kiingereza). Uhusisho wa jina na kuzaliwa ni dhana muhimu katika kubainisha utambulisho wa mtu kama ilivyojadiliwa katika mfano 48. Kuwepo kwa jina la Kiingereza ni zao la ukoloni na mabadiliko ya kijamii yanayofuata ikiwemo dini.

Katika tafsiri ya Kiswahili, jina la kiasili linahusishwa na ukoo. Dhana ambayo inaafiki maana inayojitokeza katika MC. Hata hivyo, jina la kigeni linahusishwa na ubatizo. Uhusisho huu unapunguza uhasi wa kimtazamo dhidi ya majina haya ya kigeni ambao unadhihirika katika MC. Hata hivyo, katika tafsiri ya Kiingereza, mtafsiri anafanikiwa katika kuonyesha tofauti za kihadhi zilizopo baina ya majina ya kiasili na yale ya kigeni katika kumtambulisha mtu. Anaeleza kuwa jina la kiasili

mtu hupewa anapozaliwa. Ndio utambulisho msingi wa mtu husika tangu anapozaliwa. Jina la kigeni (Kiingereza) analieleza kuwa ni jina mtu analopata baadaye. Hivyo haliwezi kuwa na hadhi sawa kiutambulisho na lile la kiasili. Kuchukua jina la kigeni kwa maoni ya mwandishi ni sehemu ya kuvuruga utambulisho uliokuwepo wa Kiafrika na ni sehemu ya juhudi za kumtumikisha Mwafrika kwa utamaduni na utawala wa kibepari.

Hali hii ni msisitizo wa uhalisia wa maisha ya mwandishi ambapo aliacha kutumia jina la Kiingereza, James, mnamo 1977 na badala yake akatumia jina, lake la Gikuyu, *Ngũgĩ* na kulihusisha na familia yake kwa kujitambulisha kuwa mwana wa babake, *wa Thiong'o.* Jina linabainika kuwa ni dhana ya kimsingi katika kubainisha utambulisho. Mawazo haya yanafungamana na itikadi ya mwandishi kama inavyobainika katika kitabu chake *Decolonizing the Mind* sehemu inayoangazia dhana ya "Cultural Bomb."

## 5.3 Mahitimisho ya Utafiti

Kupitia kwa utafiti huu, ilibainika kuwa dhana ya utamaduni ni ya kimsingi hasa katika uumbaji wa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini.* Utamaduni ulidhihirika katika riwaya hii kupitia kwa dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi pamoja na vipengele vya fasihi simulizi ya utamaduni chanzi. Vipengele vya kitamaduni vilitumiwa katika kuimarisha umbuji wa kazi hii hasa vipera vya fasihi simulizi ya jamii ya Gikuyu. Isitoshe, ilibainika kuwa kando na thamani ya kiumbuji, vipengele vya kitamaduni hasa vilivyowasilishwa kwa njia ya mafumbo na jazanda vilitekeleza

dhima muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui na kukamilisha dhamira ya mwandishi. Riwaya hii ya *Caitaani Mutharaba-ini* ilitumia baadhi ya dhana za kitamaduni kimakusudi kama njia ya kumlinda mwandishi dhidi ya utawala wa wakati wa utunzi hasa kwa kuzingatia mazingira halisi ya utunzi ambayo yalikuwa kizuizini.

Katika kutafsiri dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi, ilibainika kwamba mtafsiri katika *Shetani Msalabani* alipendelea zaidi mbinu ya ubinafsishaji katika kuzihawilisha dhana hizi. Yaani, mtafsiri alizitafsiri dhana hizi kimawasiliano au akatafuta vibadala linganifu katika mfumo wa utamaduni na lugha pokezi ya Kiswahili. Tunahusisha uteuzi huu na ukuruba wa kitamaduni na wa kiisimu baina ya lugha ya Kikuyu na ile ya Kiswahili, pamoja na uhalisia wa baadaukoloni wa jamii zinazotumia lugha hizi mbili, kwamba ziliwahi kutawaliwa na mkoloni. Licha ya hayo, mtafsiri katika baadhi ya matukio alitumia mbinu ya uibuaji ugeni katika kutafsiri MC kwa Kiswahili. Hali hii inaafikiana na mapendekezo ya nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri kuwa katika uandishi na tafsiri za baadaukoloni aghalabu panaibuka lugha ambayo haina uasilia kitamaduni. Hata hivyo, hali hii hapo awali imeaminika kuwa hutokea pale ambapo lugha za kigeni, zisizo za Kiafrika, zinatumika. Matokeo ya utafiti huu kwa kujikita kwa MT1 yanaelekeza kuwa, pana uwezekano wa lugha isiyo na uasilia kitamaduni kutokea katika fasihi ya baadaukoloni inayohusisha lugha za Kiafrika kama ilivyo kwa Kiswahili katika utafiti huu.

Tafsiri ya Kiingereza; *Devil on the Cross* imebainishwa kupendelea matumizi ya mbinu ya uibuaji ugeni katika kuhawilisha dhana za kitamaduni kutoka kwa MC. Mapendeleo haya yanaafikiana barabara na mapendekezo ya mihimili ya nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri. Kutokana na tafsiri hii, inabainika kwamba, katika muktadha wa baadaukoloni, uteuzi wa kiisimu aghalabu huchochewa na sababu zaidi ya haja ya kuwezesha mawasiliano kama ilivyo kwa tafsiri za kawaida. Katika MT2, dhana zinazofungamana na utamaduni wa Gikuyu zilihawilishwa jinsi zilivyo. Dhana hizi zilijumuisha maneno yanayorejelea vipengele vya mila na desturi za jamii ya Gikuyu, majina ya watu miongoni mwa nyingine.

Kwa kuandama mbinu ya uibuaji ugeni kwa dhati, mtafsiri kwa kiasi kikubwa anakwaza mawasiliano kamilifu katika MT2 hivi kwamba, kwa msomaji wa tafsiri hii ambaye hana umilisi au ufahamu wowote katika lugha na utamaduni wa Gikuyu, inakuwa vigumu kupata ujumbe kwa njia kamilifu. Ilibainika pia kwamba, huenda msisitizo wa kuibua ugeni alioandama mtafsiri ulikuwa juhudi ya kimakusudi ila kuna matukio kadhaa ambamo alitoa kipaumbele kwa mawasiliano. Mfano ni, matumizi ya tanbihi kufafanua dhana zinazofungamana na utamaduni chanzi katika MT2.

Katika kiwango cha itikadi, utafiti ulibainisha kwamba, katika mazingira ya baadaukoloni, dhana hii ni ya kimsingi kwa uandishi wa fasihi na hata tafsiri yake. Uteuzi wa lugha unafanywa kwa njia ya kimakusudi kwa msingi wa kiitikadi ili kufanikisha dhamira ya mwandishi wa MC. Kuanzia kwa anwani ya riwaya, kwenda

kwenye sehemu ya utangulizi na hata katika sehemu mbalimbali tulizorejelea ambazo zilikuwa muhimu katika kuipa riwaya hii msingi wa kiitikadi, mwandishi alitia bidii kuhakikisha kwamba dhana hizi zinabainika wazi. Itikadi hasa katika kiwango cha uteuzi wa kiisimu imebainika kwa kujikita kwa nadharia ya uchanganuzi wa diskosi. Kutokana na haya, pana haja ya kupanua mwelekeo wa nadharia ya baadaukoloni katika tafsiri kwa kutambua uamilifu wa uchanganuzi wa diskosi katika ufafanuzi wa baadhi ya vipengele kama vile itikadi na utambulisho kwa undani. Itikadi katika MC ilibainika katika kiwango dhahiri na kiwango kisicho dhahiri. Katika kiwango dhahiri, utafiti ulibainisha maelezo ya mwandishi ambayo yaliweka bayana misimamo na mitazamo yake kuhusu lugha, utamaduni na mahusiano ya kiuwezo baina ya mtawala na mtawaliwa. Katika kiwango kisicho dhahiri, mwandishi kupitia kwa wahusika na maudhui yanayoangaziwa anadokeza misingi ya kiitikadi kama vile ya Kimaksi. Utafiti huu hata hivyo ulijikita zaidi kwa itikadi katika kiwango dhahiri.

Kutokana na uchanganuzi wa MT1 na MT2, ilibainika kuwa pakubwa mtafsiri alifanikiwa kuhawilisha vipengele vya kiitikadi ambavyo vilikuwa vimebainishwa katika MC. Mafanikio haya ni kutokana na ukweli kwamba MT1 na MT2 ni mazao ya tafsiri binafsi. Aidha, matini hizo zote; MC, MT1 na MT2, zilizalishwa katika kipindi kifupi cha miaka miwili baina yake huku MC ikichapishwa mnamo 1980 na MT1 na MT2 zikichapishwa mnamo 1982. Kutokana na ufupi wa kipindi hiki, kuhitimisha kuwa dhamira iliyoongoza uandishi wa MC bado ilikuwa inakumbukwa

wazi wakati wa kutafsiri riwaya hii kwa Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, ilijitokeza kwamba mtafsiri hasa katika MT2 aliteua lugha ambayo ilipunguza makali ya lugha iliyotumika katika MC katika kushughulikia masuala dhati ya kiitikadi. Hali hii tumehitimisha kwamba ilichangiwa na haja ya kuilinda MT2 na kwa jinsi hiyo kuhakikisha mauzo kwa kuwa hii ndiyo nakala iliyolenga soko pana zaidi. Aidha, huenda uteuzi huu ulikuwa wa kimakusudi kwa ajili ya mwandishi mwenyewe kujilinda binafsi dhidi ya tuhuma kutoka magharibi.

Dhana ya utambulisho ilichanganuliwa ili kubaini jinsi ilivyowasilishwa katika MC na kisha kuhawilishwa katika tafsiri za MT1 na MT2. Ilibainika kwamba, mwandishi alitilia makini sana suala la utambulisho hasa kwa kutumia vipengele vya kitamaduni. Anafanikiwa kuipa riwaya ya *Caitaani Mutharaba-ini* uasilia katika lugha na utamaduni wa Gikuyu. Hata hivyo imebainshwa kuwa mafanikio haya hayakuwa bila changamoto zake kutokana na mtagusano na tamaduni na lugha nyinginezo kama zao la ukoloni. Matumizi ya uchanganyaji msimbo na ukopaji wa maneno katika MC yamebainishwa. Hali hii inatufanya kuhitimisha kwamba, ni vigumu kuzungumzia lugha asilia ya Kikuyu katika mazingira ya sasa kutokana na mwingiliano baina ya jamii hii na jamii nyingine kitaifa na kilimwengu. Mwandishi pia aliweza kuangazia vipengele anuwai vinavyochangia ubainishaji wa utambulisho ikiwemo dhana ya jina na ile ya rangi. Tafsiri ya dhana hii ya utambulisho katika MT1 na MT2 kwa kiasi kikubwa imefanikiwa ila baadhi ya maana zinazofumbatwa katika majina, hasa ya kimajazi haikueleweka vyema katika MT1 na katika MT2.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Kupitia kwa utafiti huu, upeo wa utafiti katika taaluma ya tafsiri umepanuliwa. Kwa kuvuka mipaka ya kuangazia ulinganifu na ubora, ni matumaini yetu kwamba utafiti katika taaluma ya tafsiri, hasa kwa Kiswahili umepiga hatua kiupeo. Mwelekeo uliotumiwa kuchunguza dhana ya utamaduni, pamoja na ujumuishwaji wa vipengele vya itikadi na utambulisho katika uchanganuzi ni nyongeza muhimu kwa taaluma ya tafsiri kwa jumla na hasa kwa taaluma ya tafsiri kwa Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu, kando na kusaidia kuwafahamisha wasomi na watafiti katika uwanja huu yanatazamiwa kuwa msingi wa kutalii dhana hizi, hasa ile ya itikadi, sio tu katika uwanja fasihi ya baadaukoloni bali pia katika tafsiri kwenye nyanja nyinginezo kama vile kisiasa, kisheria na hata kiuchumi. Aidha, mwelekeo wa mwingiliano taaluma uliotumika katika utafiti huu utakuwa wa manufaa katika tafiti za baadaye hasa kinadharia. Isitoshe, upeo wa utafiti huu; kujikita kwa tafsiri binafsi katika lugha tatu, unatoa umaizi wa kipekee katika kushughulikia tafsiri binafsi.

Kwa kuwa tasnia ya tafsiri hasa tafsiri ya fasihi kutoka lugha za Kiafrika kwenda lugha za kigeni imezidi kushika kasi, kama inavyoshuhudiwa baina ya Kiswahili na Kiingereza, baadhi ya masuala yaliyoangaziwa na kuibuliwa katika utafiti huu, kama vile dhana za itikadi na utamaduni, zitakuwa za manufaa kwa watafsiri wa kazi za fasihi na wahariri wa matini za fasihi zilizotafsiriwa. Kwa wasomi katika taaluma ya tafsiri, utafiti huu na matokeo yake ni nyongeza tunu kwa kongoo iliyopo katika uwanja huu hasa kwa Kiswahili.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na utafiti huu upeo; mwelekeo na matokeo yake, ninapendekeza masuala kadhaa ya kiusomi ifuatavyo:

a. Pana haja ya kutalii tafsiri binafsi kwa undani zaidi hasa katika lugha za Kiafrika. Tafiti za baadaye zinaweza kushughulikia hali hii katika tanzu nyingine za fasihi kando na riwaya pamoja na kuangazia lugha tofauti kando na Kikuyu, Kiswahili na Kiingereza.

b. Pana haja ya kupanua mielekeo ya kinadharia katika taaluma ya tafsiri hasa kupitia tafiti za mwingilianotaaluma kando na mielekeo ya kimapokeo inayojikita kwa ulinganifu.

c. Pana haja ya juhudi za kimakusudi kuziandikia lugha za kiasili ikiwemo kuandaa othografia kwa lugha ambazo hazina othografia maalum. Maandishi katika lugha za kiasili yanaweza kukuzwa kimakusudi kwa kuandika katika lugha hizi au kupitia kwa tafsiri ambapo matini kutoka lugha nyingine zitatafsiriwa katika lugha hizi.

d. Tafiti nyingine zinaweza kuendeshwa kwa kuangazia vipengele vilivyoshughulikiwa katika utafiti huu ila katika muktadha tofauti, au kwa kutumia mielekeo tofauti na ule uliotumiwa katika tasnifu hii.

Ninatoa mapendekezo yafuatayo katika ngazi ya utendaji:

a. Kadri inavyowezekana, pana haja ya kukuza tafsiri za matini zilizoandikwa kwa lugha za kiasili au hata kwa Kiswahili kwenda Kiingereza. Isitoshe, ni

muhimu kuweka vichocheo vya kuwezesha tafsiri baina ya lugha za Kiafrika.

b. Kadri inavyowezekana, sera ya lugha nchini Kenya itekelezwe kikamilifu ili kuimarisha uwezekano wa kila Mkenya kupata taarifa anayohitaji, hasa kutoka kwa serikali na asasi zake.

## MAREJELEO

Abis, P. (2011). *Class Struggle, Elistism and Social Collectivism in Ngugi wa Thiong'o's Devil on the Cross: A Marxist Approach.* (MA Thesis). Dalarna University. Sweden.

Achebe, C. (1975) "The African Writer and the English Language." *Morning Yet on Creation Day.* Anchor Books.

Aixela, J. F. (1996). Culture-Specific Items in Translation. In. Alvarez, R & Carmen-Africa Vidal, M. (Whr.). *Translation, Power, Subversion*. Clevedon: Multilingual Matters.

Alvarez, R. & Vidal, C. (1996). *Tranlation, Power, Subversion.* Clevedon/Philadelphia: Multilingual Matters.

Amoko, A. O. (2010). *Postcolonialism in the wake of the Nairobi Revolution: Ngũgĩ wa Thing'o and the Idea of African Literature.* New York: Palgrave Macmillan.

Ashcroft, B. n.wnzk (Whr.) (2000). *Post-colonial Studies: The Key Concepts.* London/New York: Routledge.

Ashcroft, B. n.wnzk (Whr.). (1995). *Post-Colonial Studies Reader*. London/New York: Routledge.

Baker, M. (1992). *In Other Words: a coursebook on translation*. London: Routeledge.

Baker, M. (2014). "The changing Landscape of Translation and Interpreting Studies". In. Bermann, S. (Mhr). *A Companion to Translation Studies.* Offord: Wiley Blackwell.

Bandia, P. F. (2003). "Postcolonialism and Translation: the dialectic between theory and Practice." Linguistica Antverpiensia, New Series – *Themes in Translation Studies*, 0 (2). Retreived from https://lans-tts.uantwerpen.be /index.php/ LANS-TTS/article/view/81/36

Bandia, P. F. (2008). *Translation as Reparation: Writing and Translation in Postcolonial Africa.* Manchester: St. Jerome Publishing.

Bandia, P. F. (2010). "Postcolonial Literatures and Translation." In. Gambier, Y & Doorslaer, L (Whr.). *Handbook of Translation Studies.* (Vol. 1).

Bandia, P. F. (2014). *Translation as Reparation: Writing and Translation in Postcolonial Africa.* New York: Routledge.

Bandia, P. F. (2002). African European-Language literature and Writing as Translation: Some Ethical issues. Retrieved from, http://www.soas.ac.uk /literatures/satranslations/Bandia.pdf on 20th July 2015, 9.14 pm.

Bandin, E. (1993) *The Role of Self-Translation in the Colonization Process of African Countries.* Estudios Humanísticos. Filología. 35. 10.18002/ehf. v0i26.2661.

Bassnett, S. & Lefevere, A. (1990). *Translation, History and Culture.* London: Printer Publishers.

Bassnett, S. (2013) "The self-translator as rewriter". In Cordingley, A. (Mhr) *Self Translation: Brokering Originality I Hybrid Culture.* London/New Delhi/New York/Sydeny: Bloomsbury Publishing Plc.

Baumgarten, S (2012). "Ideology and Translation." In. Gambier, Y (Mhr). *Handbook of Translation Studies.* (Vol. 3) Amsterdam/ Philadelphia: John Benjamins Publishing.

Ben-Ari, H. (2008). "Popular Mass Production in the Periphery? Socio-Political tendencies in Subversive translation". In. Pym, A. Shlesinger, M & Simeni, D (Whr.) *Beyond Descriptive Translation Studies: Investigations in Homage to Gideon Toury.* Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing.

Benjamin, W. (2000). The Task of the Translator. In L. Venuti (Mhr), *The translation Studies reader* (pp.15-25). London: Routledge

Bermann, S & Peter, C (Whr.). *A Companion to Translation Studies.* Malden/Oxford: Wiley Blackwell.

Blommaert, J (2005). *Discourse.* Cambridge: Cambridge University Press.

Boehmer, E. (2005). *Colonial and Postcolonial Literature: Migrant Metaphors.* Oxford: Oxford University Press.

Brown, G. & Yule, G. (1983).*Discourse Analysis.* Cambridge: Cambridge University Press

Catford, J.C. (1965). *A Linguistic Theory of Translation.* Oxford: Oxford University Press.

Cherono, N. J. (2018). *Msamiati Mkopo katika Kikipsigis: Uchanganuzi wa Kimofofonemiki na Kiisimujamii.* Unpublished M.A Thesis. Moi University.

Cook, D. & Okenimkpe, M. (1997). *Ngũgĩ: An Exploration of His Writings.* (2nd Edition). New Hampshire: Heinemann.

Cook, D. & Okenimkpe, M. (1997). *Ngũgĩ: An Exploration of his Writings.*Oxford: Heinemann Education Books.

Cordingley, A. (Ed). *Self-Translation: Brokering Originality in Hybrid Culture*. London, New York, New Delhi: Bloosmbury Publishing Plc.

Cronin, M. (2006). *Translation and identity*. London: Routledge.Eagleton, T (1991). *Ideology: An Introduction.* London/New York: Verso.

Cronin, M. (2003). *Translation and globalization*. London: Routledge.

Edwards, J (2009). *Language and Identity.* New York: Cambridge University Press

Fairclough, N (1995). *Critical Discourse Analysis: The critical study of language.* New York: Longman Group Ltd.

Fanon, F (1963). *The Wretched of the Earth.* (C. Farrington, Trans.). New York: Grove Press.

Fanon, F (1967). *Black Skin White Masks.* (C. L. Markmann.). New York: Grove Press.

Farahani na Ghasemi (2012) "The Naturalness in Translation of Idioms and Proverbs: The Case of a Persian Translation of Pinocchio" In. *Journal of Language and Translation.* Vol 3, Number 1 PP. 17-22, 2012.

Fawcett, P. (1998). " Ideology in Translation." Katika. Baker, M. (Mhr) *Routledge Encyclopaedia of Translation Studies.* London: Routledge.

Fuertes, E. B. (2004). "The role of self-translation in the colonisation process of African countries". *Estudios humanísticos. Filología*, (26), 35-54.

Gakaara, W. (1988). *Nyimbo Cia Mau Mau: Iria Ciarehithirie Wiyathi*. Karatina: Gakaara Press Ltd.

Gee, J. P. (1999). *An Intorduction to Discourse Analysis: Theory and Method.* New York/ London: Routledge.

Gee, J. P. (2011). "Discourse Analysis: What Makes it Critical?" Katika Rogers, R. (Mhr). *An introduction to critical discourse analysis in education*. New York: Routledge.

Gentzler, E. (2008). *Translation and Identity in the Americas: New Directions in Translation Theory.* Oxon/ New York: Routledge.

Gikandi, S. (2009). *Ngũgĩ wa Thiong'o.* New York: Cambridge University press.

Glodjović, A. (2010). “Translation as a Means of Cross-Cultural Communication: Some Problems in Literary TextTranslations” Linguistics and LiteratureVol. 8, No 2, 2010, pp. 141 – 151.

Goduwala, D. (2007). “Postcolonial Desire: Mimicry, Hegemony, Hybridity". In. Kuortti, J. na J Nyman, J. *(Whr.). Reconstructing Hybridity: Post-Colonial Studies in Transition.* Amsterdam/New York: Rodopi.

Gumperz, J. J. (1982). (Ed). *Language and Social Identity.* United Kingdom: Cambridge University.

Hadjivayanis, I. (2011). Norms of Swahili Translations in Tanzania: An Analysis of Selected Translated Prose. Phd Thesis. School of Oriental and African Studies: University of London.

Hatim, B & Munday, J (2004). *Translation: An Advanced Resource Book.* London/ New York: Routledge.

Hatim, B. & Mason, I. (1990). *Discourse and the Translator.* London/ New York:Routledge.

Hatim, B. & Mason, I. (1997). *The Translator as Communicator.* London/New York: Routledge.

Hatim, B. (2001). *Teaching and Researching Translation.* Harlow: Longman.

Heller, M. (2007). *Bilingualism: A social approach*. London: Palgrave MacMillan.

Hiwarkar, R. P. (2012).” Post colonialism: A Substabtial Contribution of English to the Study of Literature and Culture. Katika. *Translation* (pp.165-207). Ithaca, London: Cornell UP.

Hofstede, G. (2001). *Culture’s consequences*: *Comparing values, behaviors, institutions and organizations across nations.* 2nd ed. Thousand Oaks, CA: Sage Publications.

Holmes, J (1972). *The Name and Nature of Translation Studies*, unpublished manuscript, Amsterdam, Translation Studies section, Department of General Studies, reprinted in Toury, G. (ed.) (1987). *Translation Across Cultures*, New Delhi, Bahri Publications.

House, J. (2016). *Translation as Communication across Languages and Cultures.* London/New York: Routledge.

Klinger, S. (2013). Translated Otherness, Self-translated in-betweenness: Hybridity as Medium versus hybridity as object in Anglophone Afican Writing. In

Klinger, S. (2015). *Translation and Linguistic Hybridity: Constructing World-View*. New York: Routledge.

Kuortti, J. & Nyaman, J. (2007) (Whr.). *Reconstructing Hybridity: Postclonial Studies in Transition.* Amsterdam/ New York: Rodoppi.

Lefevere, A & Bassnet (1995). *Translation, History, Culture: A Sourcebook.* London/New York: Routledge.

Macharia, M. (2002). The aesthetics of the Gĩkũyũ Language in Ngũgĩ wa Thiong'o's Caitaani Mutharaba-ini. Unpublishd MA Thesis. University of Nairobi.

Marais, K. (2014). Translation Theory and Development Studies: A Complexity Theory Approach. London/New York: Routledge.

Marais, K. (2018). *A (Bio) Semiotic Theory of Translation: The Emergence of Social-Cultural Reality.* London/New York: Routledge.

Mbaegu, C. C (2015). The effective Power of Music in Africa. In. *Open Journal of Philosophy.* http://file.scirp.org/pdf/OJPP_2015032617174798.pdf. Last accessed 24th Sepetember 2020 1.40 PM.

Merton, R. K. (1968b*). Manifest and latent functions in Social Theory and Social Structure*. Free Press: New York.

Minkov, M. (2013). *Cross-cultural analysis. The science and art of comparing the world's modern societies and their cultures*. Thousand Oaks, CA: Sage.

Mkangi, K. (2009). *Ningekuwa na Uwezo.* Nairobi: Oxford University Press.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimujamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mugambi, P. J. M. (2001). "Language Conflict in Literary Translation: Imbuga's *Betrayal In the City* (Usaliti Mjini). Ktk. Shitemi, N. L; Noordin, M.M. Opija, A. O na Mukuria D. M. (Whr). *Kiswahili A Tool for Development: The Multidisciplinary Approach.* Eldoret: Moi University Press.

Muigai, M.N (2005). Ubunifu wa Mtafsiri: Tamthilia ya Masaibu ya Ndugu Jero. Unpublished M.A Thesis. Kenyatta University. Nairobi.

Muriuki, G. (1969). *A History of the Kikuyu upto 1904*. PhD Thesis. University of London.

Mwansoko, H. J. M. et al (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI

Newmark, P. (1981). *Approaches to Translation* Oxford / New York: Pergamon Press

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation.* New York, London: Prentice Hall.

Nida, E. (1964). *Toward a science of translation*. Leiden: Brill.

Niranjana, T. (1992). *Sitting Translation: History, Post-structuralism, and the Colonial Context.* California: California University Press.

Nord, C. (1990). Functionalism and loyalty: some considerations around the translation of titles. *Proceedings of the II Complutense Meetings on Translation*, 153-162.

Nord, C. (1997). *Translation as a Purposeful Activity: Fuctionalist Approaches Explained.* Manchester/New York: St. Jerome Publishing

Ogechi, N. O. (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili.* Moi University Press: Eldoret.

Okara, G. (1963). "African Speech. English Words," *Transition.* 3, 15-16.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds Character and Community*. Bloomington: Indiana University Press.

Parikh, P. (2001). *The Use of Language.* CSLI Publications: California.

Puurtinen, T. (2003). Genre-specific features of translationese? Linguistic differences between translated and non-translated finnish children's literature. *Literary and linguistic computing*, 18(4), 389---406.

Pym, A. (1993). *Epistemological Problems in Translation and its Teaching. A Seminar for Thinking Students.* Calaceit (Teruel), Spain: Edicions Caminade.

Reiss, K. & Vermeer, J. (1984). *Towards a General Theory of Translational Action Skopos Theory Explained.* Manchester: St. Jerome Publishing.

Schaffner, C. (2007). " Politics and Translation". In. Kuhiwczak, P & Littau, K (Whr.). *A Companion to Translation Studies.* Clevedon/Buffalo/Toronto: Multilingual Matters.

Schleiermacher, F. (1992). "On the Different Methods of Translating." Katika. *Theories of Translation,* Ed. Rainer, S. & Biguenet, J. trans. Bartscht, W, 36-54. Chicago: University of Chicago Press.

Serem, S. J. (2018). Uhakiki Linganishi wa Fani Katika Tafsiri Mintarafu ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali* (Madumulla, 1999). Unpublished PhD thesis. Moi University.

Shamma, T. (2009). Postcolonial Studies and Translation Theory. MonTI. Monografias de Traduccion e Interpretatcion, (1), 183-196. ISSN 1989-4178. Disponible en: https://www.redalyc.org/articulo.oa?id=265119728014

Shirinzadeh, S. A & Mahadi T. S (2014). "Translating Proper Nouns: A Case study of English Translation of Hafez's Lyrics. In. *English Language Teaching.*Vol 7, No. 7. Canadian Centre of Science and Education.

Shitemi N.L (1997). Uaminifu katika Tafsiri: Uhakiki wa Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili; Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka. Unpublished Dphil Thesis. Moi University. Eldoret

Silverstein, M. (2004). "Cultural" Concepts and the Language-Culture Nexus. *Current Anthropology, 45*(5), 621-652. doi:10.1086/423971.

Simpson, P. (1993). *Language, Ideology and Point of View.* London & New York: Routledge.

Snell-Hornby, M. (2006). *The turns of translation studies. New paradigms or shifting viewpoints?* Amsterdam: John Benjamins.

Tajfel, H. (Mhr) (1982b). *Social Identity and Intergroup Realations.* London: Cambridge University Press

Toury, G. (1995). *Descriptive Translation Studies and Beyond.* Amsterdam / Philadelphia: John Benjamins Publishing Company

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam.

Tymoczko, M. (1999). *Translation in a Pots-colonial Context: Irish literature in English Translation.* Manchester: St. Jerome Publishing.

Tymoczko, M. (2000). Translations of Themselves: theContours of Postcolonial Fiction." Katika. Simon, S. & Paul St Pierre (Whr.). *Changing the Terms: Translating in The Postcolonial Era.* Ottawa: University of Ottawa Press.

Tymoczko, M. na Gentzler, E. (2002). *Translation and power*. Amherst: University of Massachusetts Press.

Van Djik, T. (2000). *Ideology and Discourse: A Multidisciplinary Introduction.* Barcelona. OUC.

Van Djik. T. (1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach.* London/Carlifornia/New Delhi: Sage Publications.

Venuti, L. (1995). *The Translator's Invisibility: A History of Translation.* London & NewYork: Routledge.

Venuti, L. (Mhr), (1992). *Rethinking Translation. Discourse, Subjectivity, Ideology*. NewYork: Routledge.

Verschueren, J. (2011). *Ideology in Language Use Pragmatic: Guidelines for Empirical Research.* Cambridge University Press. Cambridge/New York.

Vidal, M. C (Whr.) *Translation Power Subversion.* Clevedon/ Philadelphia/ Adelaide: Multilingual Matters.

Vincent, A. (1995). *Modern Political Ideologies*. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Wa Thiong'o, N. (1981). *Detained: A Writer's Prison Diary.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Wa Thiong'o, N. (1986). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African literature.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Wa Thiong'o, N. (2009) 'Translated by the author: My life in between languages', *Translation Studies* 2(1): 17–20.

Wa Thiong'o, N. (2012). *In the House of the Interpreter: A memoir.* New York: Pantheon Books.

Williams, J. & Chesterman R. (2002). *The Map: A Beginners Guide to Doing Research in Tarnslation Studies.* Manchester: St. Jerome.

Williams, P. (1999). *Ngũgĩ wa Thiong'o*. Manchester: Manchster University Press.

Zaja, O.J. (2011). *Literary Translation in Kiswahili: Locating Text, Context, Culture and pedagogy in cultural transfer.* Lambert Majestic Publishing.

Zaja, O.J. (2011). Siting, Text, Culture, Context and Pedagogy in Literary Translation: A Theorization of Translation in Cultural Transfer with Examples from Selected Texts in Kiswahili. Unpublished PhD thesis. Kenyatta University.

*www.https://publishingperspectives.com* downloaded 25/02/2018 at 15.00 hrs

https://www.theguardian.com/books/2018/mar/12/Ngũgĩ-wa-thiongo-wrestling-with-the-devil-interview Accessed on 30th April 2018 at 5.38 a006D